Al-Islam.org
Ahlul Bayt Digital Islamic Library Project
Published on *Books on Islam and Muslims* | *Al-Islam.org* (https://www.al-islam.org)

Haki za Wanawake Katika Uislamu

Author(s):

Ustadh Shahid Murtadha Mutahhari [3]

Publisher(s):

Al Itrah Foundation [4]

Mahitaji ya zama zetu hizi yanamlazimisha kutathmini maswali mengi yenye umuhimu na sio kuridhika na tathmini zake za awali. Mfumo wa haki za ndoa na majukumu ya kifamilia ni miongoni mwa masuala haya.

Suala la msingi kabisa juu ya kifamilia, ni iwapo mfumo wa ndoa unajitegemea na hautangamani na mifumo mingine yote ya kijamii na una vigezo na mantiki take maalum, au ni moja tu ya mifumo mingi ya kiajmii na kuwa vigezo na falsafa zile zile zinazotumika kulishugulikia suala hili kama ilivyo kwa mifumo mingine ya kijamii.

Translator(s):

Aziz Njozi [5]

Category:

Women [6]

Topic Tags:

Haki [7]
Wanawake [8]

Historia [9]
Kifamilia [10]

Person Tags:

Imam Khomein [11]
Bibi Fatima (as) [12]
Imam Ali (a) [13]

Neno La Mchapishaji

Kitabu kilichoko mikononi mwako, ni tarjuma ya kitabu cha Kiingereza, kwa jina la: ***"Woman and her rights."*** Sisi tumekiita: ***"Haki za Wanawake Katika Uislamu*** **."**

Kitabu hiki, **" *Haki za Wanawake Katika Uislamu*"** ni matokea ya utafiti wa kielimu uliofanywa na Mwanachuoni wa Kiislamu, **Allamah Murtaza Mutahhari.**

Allamah Murtaza Mutahhari, mwandishi wa kitabu hiki ameichambua historia ya maisha ya mwanamke katika nchi za Magharibi na Mashariki (Asia) na mifumo yao ya ndoa. Mwandishi amerejea vyanzo vya wanasaikolojia na wanasosholojia wa Magharibi ili kuthibitisha hoja zake. Madhumuni yake ni kutaka kuthibitisha kwamba Uislamu una mfumo mzuri wa ndoa na haki za wanawake, kinyume na wanavyoamini watu wa Magharibi na wengine waliokuwa na kasumba ya umagharibi.

Inakubaliwa na kila rafiki na adui kuwa Qur'ani Tukufu ilifufua haki za wanawake. Hata maadui wanakiri angalau kwamba Qur'ani wakati wa kuteremshwa kwake ilichukuwa hatua kubwa katika kuboresha hali ya mwanamke na kurejesha haki zake za binadamu. Qur'ani ilifufua haki za mwanamke kama mwanadamu na kama mwenzi wa mwanaume katika utu na haki za binadamu lakini haikupuuza jinsia yake wala jinsia ya mwanaume.

Kwa maneno mengine Qur'ani haikupuuza maumbile ya mwanamke. Ndio maana kuna kuwafikiana kikamilifu kati ya kanuni za maumbile na kanuni za Qur'ani. Mwanamke katika Qur'ani ni sawa na mwanaume katika maumbile. Vitabu hivi viwili vikubwa vya kimungu (Qur'ani na maumbile), kimoja kikiwa kimeumbwa na kingine kikiwa kimekusanywa, vinakubaliana na kuafikiana kabisa. Nia ya kitabu hiki ni kuangazia na kuelezea kuafikiana huku.

Kitabu hiki ni chenye manufaa sana, hususan wakati huu wa maendeleo makubwa ya elimu katika nyanja zote. Kutokana na ukweli huu, Taasisi yetu ya ***'Alltrah Foundation'*** imeona ikitoe kitabu hiki kwa lugha ya Kiswahili, kwa madhumuni yake yale yale ya kuwahudumia Waislamu, hususan wazungumzaji wa Kiswahili, ili kuongeza ujuzi wao katika masuala ya dini na ya kijamii.

Tunamshukuru ndugu yetu, **Aziz Njozi** kwa kukubali jukumu hili la kukifanyia tarjuma kitabu hiki. Vilevile tunawashukuru wale wote walioshiriki kwa njia moja au nyingine hadi kufanikisha kuchapishwa kwa kitabu hiki.

Mchapishaji:
Alltrah Foundation
S. L. P. 19701
Dar es Salaam, Tanzania.

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَٰنِ الرَّحِيمِ

Kwa
Fatima Zahra
Binti anayeheshimika wa Mtukufu Mtume wa Uislamu,
na kiigizo cha wanawake wa Ulimwengu.

Mwandishi

Ayatullah Murtaza Mutahhari, alizaliwa mwaka wa 1920, na alikuwa ni miongoni mwa wanazuoni wa Kiislamu hodari sana na waandishi mashuhuri wa zama hizi. Alikuwa amezama sana katika kujifunza kimapokeo (*traditional learning*) na alivutiwa na watetezi wa masomo haya ya kimapokeo. Alikuwa ni mwanafalsafa na alikuwa amesoma falsafa kwa undani sana. Kazi yake ina sifa ya uwazi wa kifalsafa ambao ulimfanya awe na sifa ya kushughulikia tatizo la msingi la fikra ya kidini ambalo ndio kiini cha kitabu hiki.

Ayatullah Mutahhari alipata elimu yake ya msingi ya theolojia kutoka kwa baba yake, Sheikh Muhammad Husain, huko kwao, katika mji wa Fariman, Ayatulah alipofikisha umri wa miaka kumi na mbili alijunga na kituo cha elimu cha Mashhad, na hapo alisoma kwa miaka mitano. Kisha alienda Qum kituo kikuu cha elimu ya Kiislamu. Alikaa na kusoma hapo kwa miaka kumi na tano. Alihitimu masomo yake katika Imani za Kiislamu na Maarifa ya Sheria chini ya usimamizi wa mwanafalsafa mashuhuri Allamah Muhammad Husain Tabatabai, Imam Khomeini na wanazuoni wengine wakubwa. Kisha akahamia Tehran.

Katika kipindi cha elimu yake Ayatulah alihisi kuwa wakomunisti walitaka kuibadilisha dini takatifu ya Uislamu na kuharibu roho yake kwa kuchanganya mitazamo yao ya kumkana Mwenyezi Mungu na Falsafa ya Uislamu na kwa njia ya kuzitafsiri Aya za Qur'ani kiyakinifu. Kwa kusema kweli, sio ukomunisti tu uliomshughulisha Ayatullah. Pia aliandika tafsiri ya Qur'ani, na falsafa, maadili, sosholojia,

historia na masomo mengine mengi. Katika kazi zake zote, lengo lake lilikuwa ni kujibu hoja potofu zilizotolewa na watu mbali mbali dhidi ya Uislamu, kuonyesha udhaifu wa itikadi nyingine na kuonyesha utukufu wa Uislamu. Aliamini kuwa ili kuonyesha uongo wa Ukomunisti na itikadi nyinginezo ilikuwa muhimu sana kutoa maana juu ya ukomunisti na kuielezea taswira halisi ya Uislamu.

Ayatullah Mutahhari aliandika kwa uangalifu na bila kuacha wala kuchoka toka enzi za uwanafunzi hadi mwaka 1979, mwaka aliouawa shahidi. Kazi zake nyingi zimechapishwa ndani na nje ya Iran. Ameandika vitabu vingi na si juu ya mada anazozipendelea bali juu ya mada zinazohitajika. Kila ilipotokea kuwa kitabu fulani juu ya mada muhimu za Kiislamu kinahitajika na hakipo basi alikiandika.

Kazi za Mutahhari hazikuvumiliwa na wale wanaomkana Mwenyezi Mungu na hivyo waliamua kumuondoa mnamo tarehe 1 Mei mwaka 1979. Kifo chake cha kishahidi kilikuwa ni msiba mzito. Habari za msiba huu zilipomfikia Imam Khomeini hakuweza kuyazuia machozi yake. Katika salamu zake za rambirambi alisema; “Nimenyang’anywa mwanangu kipenzi. Ninaomboleza kifo cha yule ambaye alikuwa ni matunda ya uhai wangu”.

Maelfu wa Waislamu walihudhuira mazishi yake. Alizikwa Qum jirani na kaburi la Bibi Fatima Ma’sumah.

Ayatullah Mutahhari alikuwa ni mtu mashuhuri katika nyanja za kidini na kielimu nchini Iran. Alifanya kazi katika Chuo Kikuu cha Tehran kama Mkuu wa Idara ya Theolojia na Mafunzo ya Kiislamu.

Wakati alipouawa shahidi alikuwa ni Rais wa Baraza la Kikatiba la Jamhuri ya Kiislamu ya Iran na alikuwa akitekeleza majukumu yake kwa namna inayofaa kabisa.

Kazi zake zimetafsiriwa na kuchapishwa katika lugha za Kifaransa, Kiarabu, Kituruki, Kikurdi na Kiingereza.

‘The Islamic Seminary’ ilipata heshima ya kuchapisha baadhi ya vitabu hivi.

Neno La Awali

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيمِ

Kwa jina la Mwenyezi Mungu Mwingi wa Rehema Mwenye Kurehemu
Mahitaji ya zama zetu hizi yanalazimisha kutathmini maswali mengi yenye umuhimu na sio kuridhika na tathmini zake za awali. Mfumo wa haki za ndoa na majukumu ya kifamilia ni miongoni mwa masuala haya.

Kwa sababu mbali mbali, ambazo tutazieleza baadaye, imedhaniwa kuwa katika zama hizi, suala la msingi ni uhuru wa mwanamke na haki zake ziwe sawa na za mwanamume, na kwamba maswala mengine yote yapo chini ya suala hili kuu.

Hata hivyo kwa mtazamo wetu, suala la msingi kabisa, au angalau tuseme moja ya masuala ya msingi kabisa, juu ya haki za kifamilia, ni iwapo mfumo wa ndoa unajitegemea na hautangamani na mifumo mingine yote ya kijamii na una vigezo na mantiki yake maalum, au ni moja tu ya mifumo mingi ya kijamii na kuwa vigezo na falsafa zile zile ndizo zinazotumika kulishughulikia suala hili kama ilivyo kwa mifumo mingine ya kijamii.

Kiini cha shaka yetu ni kuwa, kwa upande mmoja, katika mfumo huu makundi makuu yanayohusika yapo katika jinsia mbili tofauti, na kwa upande wa pili, inahusisha ongezeko na muendelezo wa vizazi. Maumbile yamefanya tabia za kimaumbile na viungo vya uzazi vya makundi haya mawili kuwa tofauti. Jamii ya wanandoa ni nusu asili na nusu mkataba. Ni njia ya kati na kati baina ya jamii ya silika kama ile ya nyuki na siafu ambayo haki na majukumu yake yameshaamuliwa na maumbile na hakuna uwezekano wa kuvunja sheria, na pia baina ya jamii ya kimkataba kama jamii ya wanaadamu, ambayo ina umbile la asili au silika.

Kama tunavyojua, wanafalsafa wa kale walilichukulia suala la maisha ya familia kama tawi linalojitegemea la busara za kivitendo, na waliamini kuwa sehemu hii (maisha ya familia) ya maisha ya mwanadamu ina vigezo vyake tofauti. Plato katika kitabu chake '*The Republic'*, Aristole katika kitabu chake, *'The Politics,'* na Abu Ali bin Sina (Avicenna), katika kitabu cha A*l–Shifaa*, wamelizungumzia suala hili katika mtazamo huu pia.

Ni suala lenye utata iwapo haki za asili za mwanaume na mwanamke zinafanana au hazifanani; kwa maneno mengine, iwapo haki kwa mujibu wa maumbile ya mwanadamu, ni ya jinsia moja au jinsia mbili, na iwapo kuwa na jinsia ya kike au ya kiume kunaathiri haki na majukumu ya mwanadamu.

Katika ulimwengu wa Magharibi, harakati za haki za binadamu zilianza katika karne ya 17, kipindi cha mwamko wa harakati za kisayansi na kifalsafa. Waandishi wanafalsafa wa karne ya 17 na 18 walifanya jitihada zinazostahili sifa kwa kueneza mawazo yao juu ya haki za msingi za asili na zisizoondosheka za binadamu. Jeans Jacques Rousseau, Voltaire na Montesquieu, ambao ni miongoni mwa wanakundi hili la waandishi na wanafalsafa, ni wafadhili wakubwa wa jamii ya mwanadamu, na inafaa kusema kuwa mchango wao kwa maisha ya wanaadamu haukuwa mdogo kuliko wa wagunduzi na wavumbuzi wakubwa, vilikuwa na thamani sawa.

Wazo lao kuu lilikuwa kwamba wanaadamu wana mfululizo wa haki za asili walizozaliwa nazo pamoja na uhuru, vyote ambavyo haviwezi kuondosheka wala kuhamishwa na yeyote kwa visingizio vyovyote. Watu wote, ikiwa ni pamoja na watawala na watawaliwa, weupe na weusi, matajiri na maskini, wote ni sawa.

Matokeo ya harakati hizi za kijamii na kisomi zilionekana kwanza Uingereza na kisha Marekani na

baadaye Ufaransa. Yakaja yakatokea mapinduzi hapa na pale, mifumo ikabadilishwa na mikataba ikasainiwa. Polepole, harakati zilienea katika nchi nyingine.

Katika karne ya 19, mawazo mapya ya kiuchumi, kijamii na kisiasa juu ya haki za binadamu yaliibuka. Maendeleo mapya yalipelekea kutokea kwa ujamaa, ushiriki wa wafanyakazi katika faida za viwanda, na kuhamishwa kwa serikali kutoka kwa jamii ya mabepari kwenda kwa watetezi wa wafanyakazi (wavuja jasho).

Mpaka kufikia mwishoni mwa karne ya 19, mazungumzo yote na hatua zozote za kivitendo zilizochukuliwa katika anga ya haki za binadamu, zilikuwa zimejikita tu katika haki za mataifa juu ya serikali na haki za waajiriwa dhidi ya waajiri. Katika karne ya 20, suala la haki za wanawake liliibuka kwa mara ya kwanza mwaka wa 1948, Umoja wa mataifa ulitangaza Azimio la Dunia la Haki za Binadamu ambapo ulitoa mbiu ya usawa wa haki kati ya mwanamke na mwanaume kwa wazi kabisa.

Harakati zote za kijamii huko Magharibi toka karne ya 17 zimekuwa zikizunguka kwenye uhuru na usawa, kwa vile harakati za haki za wanawake zilikuja mwisho kabisa, na historia ya masaibu ya wanawake Ulaya, kutokana na mtazamo huu, ilikuwa mbaya sana, Azimio la Umoja wa Mataifa la Haki za Binadamu halikuzungumzia chochote zaidi ya uhuru na usawa.

Wanaounga mkono harakati hizi wanashikilia kuwa harakati hizi zinakwenda pamoja na harakati za haki za binadamu. Wanasema kuwa bila kuhakikisha uhuru na haki za wanawake hakuna maana yoyote kuzungumzia uhuru na haki za mwanadamu. Pia walidai kuwa sababu kubwa ya migogoro ya kifamilia ilitokana na mwanamke kunyimwa uhuru na usawa wake dhidi ya mwanaume, na kwamba matatizo yote haya ya kifamilia yatatatuliwa mara tu tatizo hili litakapoondolewa

Kilichosahauliwa katika hili kilikuwa ni kile tulichokieleza kama suala la msingi kuhusiana na mfumo wa haki za familia, hii ni kuwa, iwapo mfumo huu unajitegemea au unategemea mifumo mingine ya kijamii, na ikiwa una vigezo na mantiki tofauti au la. Msisitizo uliwekwa tu kwenye kanuni za jumla za uhuru na usawa na nukta pekee iliyozingatiwa ilikuwa ni ile ya haki za asili na zisizoondosheka za binadamu. Ilidaiwa kuwa mwanamke, kama binadamu, alikuwa na stahili ya kupata haki zote anazozifurahia na anazozipata mwanaume.

Katika sura fulani za kitabu hiki, tumejadili vya kutosha juu ya suala la vyanzo ambavyo kutokana navyo haki za asili zimechukuliwa au zimetengenezwa. Huko, tumeonyesha kuwa misingi ya haki zote ni maumbile yenyewe. Ikiwa mwanadamu ana haki maalum, ambazo farasi, kondoo, ndege na samaki hawana, hii inatokana na maumbile yake na jinsi alivyoumbwa. Ikiwa wanaadamu wote ni sawa katika haki za asili na wote lazima waishi maisha huru, hii ni kwa sababu mfumo huo ndio walioumbwa nao. Wasomi wanaounga mkono wazo kuwa uhuru na usawa ni haki aliyozaliwa nayo mwanadamu, hawana hoja nyingine zaidi ya hii. Hivyo katika suala la haki za familia pia, tunapaswa pia kuongozwa na maumbile.

Sasa hebu tuangalie kwa nini mazingatio ya kutosha hayakuwekwa kwenye suala tulilolielezea kama la

msingi. Je imeshathibitika kisayansi kwamba tofauti kati ya mwanaume na mwanamke ni ya kimaumbile tu na haiwaathiri kiumbo na kiroho au haki na majukumu yao, na ndio maana imepuuzwa katika falsafa ya kisasa ya jamii?

Kusema kweli, ilivyo ni kinyume kabisa na swali hili. Kwa mujibu wa utafiti wa kisayansi na ugunduzi wa kibaiolojia na kisaikolojia imethibitika kuwa kuna tofauti muhimu kati ya hizi jinsia mbili. Katika kitabu hiki, tumejadili suala hili na tumenukuu maoni ya wanabaiolojia na wanasaikolojia juu ya hili. Inashangaza kwamba licha ya yote haya, suala hili la msingi lilipuuzwa.

Labda kutolijali suala hili la msingi kumetokana na maendeleo ya haraka mno ya harakati za ukombozi wa mwanamke. Ndio maana, wakati harakati zikirekebisha hali ya mambo kuondoa taabu za wanawake, katika baadhi ya maeneo zimewasababishia maafa wao na jamii nzima kwa ujumla.

Tutaangalia baadaye katika kitabu hiki, kwamba mwanamke wa Kimagharibi, hadi mwishoni mwa karne ya 19, alinyimwa haki zake za msingi za binadamu. Ilikuwa ni juzi tu hapa katika karne ya 20 ambapo watu wa Magharibi walifikiria kurekebisha hali ya mambo. Hii harakati ilipoanza, katika kipindi cha mwamko wa harakati nyingine, kudai usawa na uhuru, walitegemea miujiza kwa maneno haya mawili tu. Walisahau kuwa usawa na uhuru ulihusiana na uhusiano baina ya watu, kama wanadamu tu.

Hakuna shaka yoyote kuwa mwanamke ni mwanadamu na amezaliwa huru kama mwanadamu mwingine yeyote na kwa sababu hiyo anastahili haki sawa. Lakini mwanamke ni mwanadamu mwenye sifa fulani za kipekee. Mwenendo wa tabia zao ni tofauti (na wanaume) na mfumo wa akili zao ni wa kipekee. Tofauti hii sio matokeo ya sababu za kijiografia, kihistoria au kijamii, bali ni ndio maumbile yao. Maumbile kwa makusudi kabisa yamewafanya wawe tofauti (na wanaume) na jitihada zozote zitakazochukuliwa dhidi ya malengo ya maumbile zitakuwa na matokeo mabaya.

Kama tulivyochukuwa hamasa zetu kutoka kwenye maumbile juu ya usawa na uhuru wa mwanadamu, basi vivyo hivyo ndivyo tunavyopaswa kupata mwongozo kutoka kwenye maumbile ili tuweze kuamua iwapo haki za mwanamke zinafanana na za mwanaume au hazifanani na iwapo jamii ya kifamilia ni angalau nusuasili (seminatural society). Ni jambo linalofaa kutafakari iwapo kuwepo kwa jinsia mbili katika wanyama, ikiwa ni pamoja na binadamu kumetokea kama ajali au ndio muundo wa maumbile uliokusudiwa; yaani iwapo tofauti za jinsia ni za juu juu tu, au ni kama Alexis Carell alivyoonyesha kuwa kila seli ya mwili ya mwanadamu ina jinsia, iwapo mwanaume na mwanamke wanayo, au hawana, kazi tofauti za kufanya, na kama haki ni za jinsia moja au za jinsia mbili. Swali kama hilo pia linaweza kuulizwa juu ya maadili, elimu adhabu, majukumu na ujumbe.

Wakati wa harakati za ukombozi wa mwanamke, haikuzingatiwa iwapo, mbali na usawa na uhuru, kuna maswali mengine pia. Hapana shaka kuwa uhuru na usawa ni mambo muhimu. Lakini mambo sio haya tu. Usawa wa haki ni jambo moja, lakini kufanana kwa haki ni jambo jingine tofauti kabisa. Usawa wa haki za mwanaume na mwanamke kwa mtazamo wa thamani ya kimaada na maadili ni tofauti na kufanana kwa haki zao.

Wakati wa harakati hizi, kwa makusudi au kwa bahati mbaya, usawa umetumika kumaanisha kufanana, na hivyo ubora umefunika uwingi. Ilisisitizwa kuwa mwanamke ni binadamu, lakini ilisahauliwa kuwa ni mwanamke pia.

Kwa kusema kweli, kutokujali huku hakukutokana na haraka peke yake, kulikuwa na sababu nyingine pia, ambazo zilimfanya mwanamke anyonywe kwa jina la uhuru.

Moja ya sababu hizo ni tamaa iliyopindukia ya wamiliki wa viwanda waliotaka kumuondoa kutoka nyumbani kwenda kiwandani ili kuvuna uwezo wake kwa maslahi yao ya kiuchumi. Wakiwa na malengo haya, walitetea haki za mwanamke, uhuru wake wa kiuchumi na uhuru wa usawa wa haki kama zile za mwanaume. Ni wao waliokazia utambulukaji rasmi wa madai haya.

Will Durant katika sura ya tisa ya kitabu chake *'The Pleasure Of Philosophy*,' baada ya kutaja baadhi ya nadharia zenye kumdhalilisha mwanamke zilizokuwa zimebuniwa na Aristole, Neitzsche, Schopenhauere na baadhi ya maandiko (matakatifu) ya kiyahudi na kuonyesha ukweli kuwa wakati wa mapinduzi ya Ufaransa japo kulikuwa mazungumzo ya uhuru wa mwanamke, kivitendo hakukuwa na mabadiliko yoyote.

Anasema kuwa hadi mwishoni mwa karne ya 19 mwanamke hakuwa na haki yoyote iliyopaswa kuheshimiwa, na ambayo mwanaume angepaswa kuizingatia au ingemfanya abanwe na sheria. Kisha anajadili mambo yaliyoleta mabadiliko katika karne ya 20. Anasema kuwa uhuru wa mwanamke ni matokeo ya ziada ya mapinduzi ya viwanda. Anaongeza kuwa wafanyakazi wa kike walikuwa ni wa gharama nafuu na waajiri walipenda kuwatumia hawa zaidi kuliko wanaume waliuokuwa jeuri (wabishi) na walikuwa ghali zaidi.

Katika karne moja iliyopita ilikuwa vigumu sana kwa wanaume kupata kazi, lakini kulikuwa matangazo yaliyokuwa yanawaomba wanaume wawapeleke wanawake wao na watoto viwandani. Hatua ya kwanza ya kumkomboa mwanamke ilichukuliwa mwaka wa 1882, ambapo sheria ilipitishwa, ambapo kwa mujibu wa sheria hiyo, wanawake wa Uingereza walipata fursa na haki ambayo haikuwahi kutokea kabla, haki ya kujiwekea fedha zozote walizopata.1

Sheria hii iliyoelezewa huafikiana na maadili matukufu ya kikristo, ilipitishwa na wamiliki wa viwanda na Bunge, ili kuwashawishi wanawake wa Uingereza kwenda kufanya kazi viwandani. Tokea mwaka huo, hamu isiyozuilika ya kujichumia fedha imewalazimisha kuhenyeka katika maduka na viwanda, na imewaondolea mzigo wa kufanya kazi za nyumbani (*The Pleasure Of Philosophy*, uk. 155159).

Kutokana na maendeleo ya mitambo na ongezeko la uzalishaji ilionekana ni muhimu kwa mabepari, ili kulazimisha bidhaa zao za ziada juu ya walaji wanapaswa kutumia mbinu zote za kusikia na kuona (TV), kiakili, kihisia, kisanii na hata ngono. Katika kuwabadilisha walaji (wanunuzi) kuwa vipengele vya utumiaji na kuwafanya wawe kama zana zisizo na nguvu katika soko la walaji, waliamua kuwatumia wanawake, lakini hawakuwatumia kama wafanyakazi tu katika mchakato wa uzalishaji pamoja na wanaume.

Wao, kwa upande mwingine walitumia urembo wao, uchangamfu na mvuto wa kingono na kuwashawishi kujitolea muhanga heshima na kujistahi kwao ili kuweza kuwapotosha hao wateja na kuwalazimisha hiari zao wenyewe juu yao. Ni dhahiri kwamba yote haya yalifanyika katika jina la uhuru kwa ajili ya wanawake na usawa wao na wanaume.

Kisiasa vile vile haikurudi nyuma katika kutekeleza kipengele hiki, mara kwa mara utakuwa unasoma taarifa kama hizo katika magazeti na majarida.

Mwanamke ananyonywa na huduma zake hutumiwa kutekeleza malengo ya wanaume chini ya joho la uhuru na usawa.

Kwa dhahiri kijana (wa kiume) wa karne ya 20 hawezi kukosa fursa hii ya thamani. Ili kumzuzua (mwanamke), bila kumbebesha dhamana za kawaida, na kucheza na akili yake kwa uhuru yeye (mwanaume) zaidi kuliko mtu yeyote yule, hutoa machozi ya mamba kwa ajili ya kutojiweza kwa wanawake na uonevu usio na maana dhidi yake (huyo mwanamke). Ili kuwa na uwezo wa kutoa mchango mkubwa kwenye 'mwenendo huu mtakatifu' huenda mpaka kiasi cha kuchelewesha ndoa yake mwenyewe mpaka kufikia umri wa miaka 40 au hata kubakia kapera maisha yake.

Hapana shaka, karne ya sasa imerekebisha malalamiko mengi ya mwanamke, lakini imeleta shida nyingi kwake. Kwa nini? Je, ameangamia daima milele na hana njia ya kufanya katika mzunguko huu? Je, haiwezikani yeye kuondokana na shida zake zote hizi za zamani na za sasa kwa mara moja na wakati huo huo? Je, wanawake wamewekwa (kutaabika) kwenye shida hizi mbili na kwamba lazima alazimike kuchagua moja ya njia hizi mbili?

Kwa kweli sio muhimu kiasi hicho kwamba apaswe kuendelea kuteseka. Alitaabika huko nyuma, zaidi hasa kwa sababu ilisasahauliwa kuwa yeye ni binadamu. Anataabika sasa hivi kwa sababu ya uwanamke wake, mahitaji yake aliyozaliwa nayo, haki zake na madai ya kawaida na vipawa vyake maalum vimepuuzwa kwa makusudi au vinginevyo.

Kinachoshangaza zaidi ni kuwa kila zinapozungumziwa tofauti za mwanamke na mwanaume, baadhi ya makundi yana tabia ya kuzichukulia tofati hizo kama kutokuwa mkamilifu kwa mwanamke na ukamilifu wa mwanaume. Fikra kama hizi zimewafanya waamini kuwa wana upendeleo fulani wa kipekee, ambao wanawake wamenyimwa. Hawaelekei kuelewa kuwa hakuna suala la ukamilifu na kutokuwa kamilifu. Haikuwa nia ya Muumba kumfanya mmoja mkamilifu na aliyependelewa, na mwingine kuwa mbovu na aliyenyimwa.

Watu wa aina hii wakiegemeza hoja zao hizi juu ya dhana zao za kushangaza za kimantiki na za busara, wanadai kwamba kwa vile maumbile yamekuwa katili kwa mwanamke, tusiongeze tusi kwenye jeraha na kwa hiyo itakuwa ni wema zaidi kuupuuza uwanauke wake! Lakini, kwa kweli ni kupuuzia nafasi ya asili ya mwanamke ambayo inasababisha yeye kunyimwa haki zake.

Ikiwa wanaume wataungana dhidi ya wanawake na kusema, "Kwa vile sisi wote ni sawa, kazi zetu,

majukumu yetu malipo na adhabu ziwe sawa. Lazima mshiriki pamoja nasi katika kazi ngumu na nzito, mlipwe kutokana na kiasi cha kazi mliyofanya na msitarajie kuhurumiwa, kuheshimiwa wala kulindwa. Bebeni gharama zenu wenyewe na tutachangia gharama za matunzo ya watoto sawa kwa sawa na muweke utaratibu wa kujilinda dhidi ya hatari zote. Mnapaswa mtugharamie kama tunavyowagharamia."

Hali kama hii ikitokea, wanawake ndio watakaoumia, kwa sababu kimaumbile hawana nguvu za kuzalisha kama wanaume, wakati wao wanatumia fedha zaidi kuliko wanaume. Hedhi zao, taabu za mimba, uchungu wa kuzaa na malezi ya watoto vinawaweka katika nafasi ya kuhitaji ulinzi wa wanaume. Wanahitaji haki zaidi na hawawezi kumudu gharama kidogo. Hali hii sio kwa binadamu tu. Hata kwa wanyama wote, madume kwa silika huyalinda majike yao.

Mazingatio sahihi ya nafasi ya asili ya mwanamke na mwanaume na usawa wao na haki zao zinazofanana kama wanaadamu yanamuweka mwanamke katika nafasi hii ya raha ambapo utu wake haudharauliwi wala haiba yake haiathiriki.

Ili kupata picha ya matokeo ya kupuuza nafasi asili ya mwanaume na mwanamke, hebu tuangalie wanachosema na kuandika wale ambao wamepitia njia hii kwa ukamilifu.

Siku za nyuma kuna makala moja iliandikwa katika gazeti la Marekani liitwalo '*Coronet'.* Linafaa kusoma. Linaelezea kisa cha mwanamke ambaye, kwa ajili ya haki sawa kati ya mwanaume na mwanamke alipoteza tahafifu aliyokuwa anapewa hapo awali. Mwanzo wanawake hawakutakiwa kunyanyua zaidi ya ratili 25, wakati kikomo hiki hakikuwepo kwa ajili ya wanaume.

Anasema sasa mazingira ya kazi katika kiwanda cha General Motors, katika jimbo la Ohio, ambapo takriban wanawake 2500 wanamenyeka, yamebadilika. Sasa anajikuta akihudumia injini yenye nguvu sana au kusafisha oven yenye uzito wa ratili 250, iliyowekwa hapo na mwanaume wa miraba minne. Anahisi kuchoka kabisa na anaona amepigika. Anasema pia kuwa kila dakika analazimika kutumia kulabu yenye kishikio cha inchi 25 mpaka 50 chenye uzito wa ratili 35. Mikono yake mara zote imevimba na inauma.

Makala baadaye inasimulia mashaka na masaibu ya mwanamke mwingine ambaye mume wake ni baharia katika jeshi la wanamaji. Hivi karibuni, Afisa wa jeshi (Admiral) aliamua kuwaingiza wanawake 40 na wanaume 480 na akawatuma kazini. Meli iliporudi baada ya safari ya kwanza, wasiwasi wa wake wa wanamaji ulithibitika. Muda si mrefu ikajulikana kwamba sio tu kwamba walifanya mapenzi ndani ya meli, lakini wanawake walio wengi walifanya mapenzi na wanaume zaidi ya mmoja.

Makala inasema kuwa katika jimbo la Florida, wajane wana wasiwasi sana tangu ukombozi wa mwanamke ulipoanza kwa vile Jaji wa jimbo hili ameitangaza sheria inayoruhusu ruzuku ya dola 500 kwa wajane kuwa inakwenda kinyume na katiba kwa vile inawabagua wanaume.

Makala inaongeza kuwa wanawake ni wa kwanza kuumia. Wengine pia, wakati wa zamu yao, wataonja ladha ya ukombozi. Kwa walio wengi swali ni iwapo wanawake wamepoteza zaidi kuliko walivyopata.

Haina maana kulilia maziwa yaliyomwagika. Onyesho limeanza na watazamaji wameshachukua viti vyao.

Mwaka huu marekebisho ya 27 ya katiba yanakusudiwa kupitishwa na kwa mujibu ya marekebisho hayo, marupurupu yote yanayohusiana na ngono yatafutwa. Hivyo, hofu iliyoelezwa na Profesa Ruscobound, wa chuo cha sheria cha Harvad, kwamba ukombozi wa mwanamke ni chanzo cha machungu yasiyoelezeka katika medani ya sheria ya mwanamke wa Marekani yatadhihirika.

G. Irvin, Seneta wa North Carolina, baada ya kuisoma jamii ya Marekani, ambapo wanawake na wanaume wana haki sawa, anapendekeza zirekebishwe na wanaume wasiwajibike tena kutunza familia.

Kwa mujibu wa makala hii, Mrs. Macdaniel anasema kuwa, kutokana na kunyanyua vitu vizito baadhi ya wafanyakazi wa kike katika kiwanda chake walipatwa na tatizo la kuvuja damu ndani kwa ndani (hemoreji). Wanawake hawa wanataka kurudi katika nafasi zao za awali. Wanataka watendewe kama wanawake na sio kama wafanyakazi tu.

Kwa wapiga kampeni wa usawa linaweza kuwa jambo rahisi. Wanakaa katika nyumba zao za fahari na kuzungumzia usawa, lakini hawajawahi kufanya kazi viwandani, ambako wanawake wengi walioajiriwa katika viwanda katika nchi hii wanafanya kazi. Mrs. Macdeniel anasema hataki usawa huu, kwa sababu hawezi kufanya kazi za kiume.

Wanaume wana nguvu zaidi kuliko wanawake. Ni bora aache kazi kuliko kushindana na wanaume. Faida ambazo wanawake wa Ohio wamezipoteza ni nyingi sana kuliko faida wanazopata chini ya sheria ya wafanyakazi. Wanawake wamepoteza haiba yao. Haifahamiki ni nini wamekipata baada ya kukombolewa. Hali ya wanawake wachache inaweza kuwa imeboreka, lakini si wanawake wote.

Hiki ndio kilikuwa kiini cha makala. Ni dhahiri kutokana na yaliyomo ndani yake kuwa wanawake hawa wamechoshwa mno na matatizo waliyosukumiwa kwa jina la uhuru na usawa kiasi kwamba wamepatwa na mzio (allergy) wa maneno haya mawili. Wanasahau kuwa maneno haya hayapaswi kulaumiwa.

Mwanaume na mwanamke ni nyota mbili kila moja ikiwa na obiti yake. **“Jua halipiti njia ya mwezi wala usiku hauuzidi mchana... Kila kimoja kinaelea katika Obiti (njia) yake.” (36:40).** Furaha yao, na pia furaha ya jamii nzima ya wanaadamu inategemea sharti kuwa kila mmoja anatembea katika obiti yake. Uhuru na usawa unaweza kuwa na maana tu ikiwa jinsia zote mbili zitafuata njia zake za asili.

Tunaposema kwamba suala la haki za wanawake nyumbani na katika jamii litathminiwe upya na lisibakie katika uzito wa tathmini ya awali, tunamaanisha kuwa tuongozwe na maumbile na tuzingatie uzoefu uchungu na utamu tulioupata huko nyuma, hasa wa karne hii. Hapo tu ndipo harakati za wanawake zitakapokuwa na maana.

Inakubaliwa na kila rafiki na adui kuwa Qur’ani Tukufu ilifufua haki za wanawake. Hata maadui wanakiri angalau kwamba Qur’ani wakati wa kuteremshwa kwake ilichukuwa hatua kubwa katika kuboresha hali

ya wanamke na kurejesha haki zao za binadamu. Qur'ani ilifufua haki za mwanamke kama mwanadamu na kama mwenzi wa mwanaume katika utu na haki za binadamu lakini haikupuuza uwanauke wake wala uwanaume wa mwanaume.

Kwa maneno mengine Qur'ani haikupuuza maumbile ya mwanamke. Ndio maana kuna kuwafikiana kikamili kati ya kanuni za maumbile na kanuni za Qur'ani. Mwanamke katika Qur'ani ni sawa na mwanamke katika maumbile. Vitabu hivi viwili vitakatifu, kimoja kikiwa kimeumbwa na kingine kikiwa kimekusanywa, vinakubaliana na kuafikiana kabisa. Nia ya kitabu chetu ni kuangazia na kuelezea kuafikiana huku.

---

1. Dr. Ali Shayagan, katika kusherehesha sheria ya Iran ya kiraia, anaandika kuwa uhuru wa kumiliki mali, ambayo mwanamke anayo sasa na ambayo imetambuliwa na sheria ya Shia'h toka awali kabisa, haikupata kuwepo siku za kale huko Ugiriki, Urumi, Ujerumani na mpaka hivi karibuni hali imekuwa hivyo katika nchi nyingine nyingi. Alionekana kama mtu mdogo tu na kama kichaa, hivyo alizuiwa kumiliki mali. Huko Uingereza, ambapo mwanamke alihesabiwa kuwa sehemu ya mume wake hivyo si mtu anayejitegemea, sheria mbili zilipitishwa, moja mwaka 1870 na nyingine mwaka 1882, ambazo ziliondoa kizuizi cha mwanamke aliyeolewa kumiliki mali.

Dibaji

Kwa jina la Mwenyezi Mungu Mwingi wa Rehema Mwenye Kurehemu.

Matatizo Ya Mahusiano Ya Kifamilia.

Tatizo la mahusiano ya kifamilia katika zama zetu sio rahisi sana kiasi kwamba mtu anaweza kulitatua kwa kuandaaa kura za maoni ya vijana wa kike na wa kiume, au kwa kuendesha semina. Sio tatizo la nchi wala hakuna nchi iliyodai kulitatua kabisa.

Will Durant, mwanafalsafa anayejulikana vyema, na mwandishi wa kitabu kiitwacho *'History of Civilization'* anasema, "Tukijaalia kuwa tunaishi katika mwaka wa 2000 A.D na tunataka kujua tukio lililokuwa muhimu kabisa katika robo ya kwanza ya karne ya 20, tutaona kuwa haikuwa vita ya kwanza ya Dunia wala Mapinduzi ya Urusi. Lilikuwa ni badiliko la nafasi ya mwanamke. Historia haikuwahi kushuhudia badiliko la kusisimua kiasi hicho ndani ya muda mfupi kiasi hicho. Nyumbani, ambapo ndio ulikuwa msingi wa kiuendeshaji wetu wa kijamii, mfumo wa unyumba (ndoa), ambao ulizuia ufisadi na zinaa na kuleta utengamano wa maisha ya familia, na sheria madhubuti ya maadili iliyotusaidia kuondoka katika ushenzi kwenda katika utamaduni na tabia inayokubalika ya kijamii, yote haya yalisukumiziwa mbali na badiliko hili la kimapinduzi."

Hata sasa tunapoishi katika karne ya 21, tunasikia malalamiko mengi kuliko kipindi kingine chochote kuwa mfumo wa familia unaporomka, msingi wa ndoa unadhoofika, wavulana wanakwepa kuoa, wasichana wanachukia kuzaa (kuwa mama), mahusiano baina ya wazazi hasa akina mama na watoto yanazidi kuwa mabaya, mwanamke wa dunia ya leo hana adabu, ngono ya bei nafuu inachukua nafasi ya mapenzi ya dhati, talaka zimeongezeka, idadi ya watoto waliozaliwa nje ya ndoa inaongezeka, mapenzi ya dhati, heshima na uchangamfu kati ya mume na mke vinazidi kupungua.

Je Tuige Wazungu Au Tujitegemee?

Inasikitisha kuona kuwa baadhi ya watu wasioelewa mambo wanafikiria kuwa suala la mahusiano ya kifamilia ni sawa na matatizo ya kuongoza watalii, kuendesha taksi, kuendesha basi na kuunganisha mtandao wa mabomba ya maji na umeme, mambo yaliyotatuliwa na wazungu miaka mingi iliyopita na hivyo tukipatwa na tatizo lolote tuwaige wao mara moja.

Hizi ni njozi tu. Wazungu wana matatizo makubwa sana ya kifamilia kuliko sisi. Wanataabika sana na wasomi wao ni waropokaji. Ukiacha elimu kwa wasichana, wana matatizo makubwa katika masuala mengine. Familia zao zina huzuni kubwa kuliko zetu.

Kulazimishwa Na Historia

Baadhi ya watu wanafikiri kuwa kuporomoka na kuchafuka kwa mfumo wa familia kunatokana na ukombozi wa wanawake, ambao kwa upande mwingine ulikuwa ni matokeo yasiyoepukika ya mapinduzi ya viwanda na maendeleo ya sayansi na ustaarabu. Ni suala la kulazimishwa na historia. Hatuna njia ya kufanya isipokuwa kukubaliana na ufisadi na vurugu hizi, na kusahau furaha ya maisha ya familia tuliyokuwa tukiyafurahia huko nyuma.

Kufikiri kwa staili hii ni kwa juu juu na kwa kitoto. Tunakubali kwamba maisha ya viwanda yameathiri mahusiano ya kifamilia na bado yanaathiri, lakini mambo makuu yaliyoathiri mfumo wa maisha ya familia huko Ulaya, ni mawili:

La kwanza ni mila katili na za kipumbavu, mazoea na sheria zilizokuwepo Ulaya hadi karne iliyopita. Ilikuwa ni mwishoni tu mwa karne ya 19 na mwanzoni mwa karne ya 20 ambapo wanawake wa Ulaya walipata haki ya kumiliki mali. Jambo jingine lililochangia ni kuwa, wale waliojitolea kurekebisha hali za wanawake walichagua njia potofu. Walikusudia kuziremba nyusi zake za macho lakini walimnyima uwezo wa kuona.

Mbali na maisha ya viwanda, sheria za zamani za Ulaya na mageuzi ya watu wa kisasa (modernists) yamechangia katika vurugu na mkanganyiko uliopo. Hivyo hakuna sababu inayotulazimisha sisi Waislamu kupita njia waliyopita na kuangukia katika utata na ugumu huu ambao wenzetu wameangukia. Tunapaswa kuwa waangalifu na kuchukua tahadhari na maisha ya kimagharibi.

Tunapaswa kuyatazama maisha ya Magharibi kwa tahadhari. Huku tukitumia na kupata maarifa yao, viwanda vyao, mbinu zao na baadhi ya kanuni za kijamii zinazofaa kuigwa. Tunapaswa kujiepusha kuiga mila zao, mazoea (desturi) na sheria ambazo zimewaletea masaibu makubwa. Kwa mfano kurekebisha sheria za kiraia na mahusianao ya kifamilia ili ziafikiane na sheria za kimagharibi.

Uhuru Wa Kijamii Wa Mwanamke

Uhuru Wa Kujichagulia Majaliwa Yake.

Siku moja msichana aliyeonekana kuwa na wasi wasi na kutatizika alikuja kwa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) na kusema: “Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu! Baba yangu amenifanyia dhulma kubwa.”

“Amekufanyia nini?”
“Ana mpwa wake na amenioza kwake bila idhini yangu.”
“Kama ni hivyo, kubaliana na alichofanya na kuwa mke wa binamu yako.”
“Simpendi binamu yangu. Vipi naweza kuwa mke wa mtu nisiyempenda?”
“Basi hakuna kilichoharibika. Kama humpendi chagua mtu mwingine unayempenda.”

“Lakini pia, ninampenda sana. Sipendi mtu mwingine. Sitakuwa mke wa mtu mwingine. Lakini kwa sababu baba yangu aliniozesha bila idhini yangu, nilikuja kwa makusudi kuzungumza na wewe. Nilitaka useme hayo uliyoyasema. Nilitaka wanawake wote wajue kuwa akina baba hawana haki tena ya kuamua watakavyo na kuwaozesha binti zao kwa yeyote ambaye wao akina baba wanayempenda.”

Kisa hiki kimesimuliwa na fakihi mashuhuri katika vitabu: *Masalik* (cha Shahid Thani), na *Jawahirul Kalam*. Katika kipindi cha kabla ya Uislamu, Waarabu, kama watu wengine wote wa zama hizo, walifikiri kuwa walikuwa na mamlaka kamili juu ya binti zao, dada zao na wakati fulani hata mama zao.

Hawakuitambua haki ya wanawake ya kujichagulia waume zao, mtu pekee aliyekuwa na haki ya kuchagua mume wa muolewaji alikuwa ni baba au kaka, na kama hawa hawapo basi baba wadogo na baba wakubwa. Ilikuwa inafikia hatua kuwa akina baba walichagua mume wa binti yao ambaye bado hata hajazaliwa. Mwanaume aliingia mkataba na mwanaume mwingine kuwa akizaa mtoto wa kike, basi akikua atakuwa mke wa huyu mwanaume wa pili.

Ndoa Kabla Ya Kuzaliwa.

Siku moja Mtume alipokuwa katika Hija yake ya mwisho, akiwa juu ya farasi na akiwa na bakora mkononi mwake alifuatwa na mtu mmoja, mtu huyo akasema:

“Nina malalamiko”
“Ndiyo, sema kuna nini?”
“Miaka kadhaa huko nyuma, katika kipindi cha kabla ya Uislamu Tariq bin Murqa’a na mimi tulishiriki katika vita. Wakati wa mapigano alikuja kutaka mkuki na akapiga kelele; “Je, kuna yeyote ambaye atanipa mkuki na achukue zawadi?” Nilimwendea na kumuuliza ni zawadi gani angetoa.

Akasema angenipa binti yake wa kwanza atakayemzaa. Toka kipindi hicho miaka mingi imepita. Hivi karibuni, baada ya kuulizia, niligundua kuwa ana binti aliyekua katika nyumba yake. Nilimwendea na kumkumbusha juu ya ahadi. Lakini alirudi nyuma na kutaka mahari mapya. Sasa nimekuja kuulizia ili kuona kama mimi ni mwenye haki au yeye ndiye mwenye haki.?”

“Huyo msichana ana umri gani?”
“Msichana ameshakua. Mvi zinaonekana kichwani mwake.”
“Kama ukiniuliza mimi, nyinyi wote hamko na haki. Endeleeni na shughuli zenu na mwacheni huyu msichana kivyake.”

Mwanaume huyu alishangazwa na jibu hili na alimtazama Mtume mara kadhaa. Alishangaa hii ni aina gani ya fatwa. Hata kama angelipa mahari mpya na baba wa binti angemuozesha kwake kwa hiari, bado ndoa hiyo isingekuwa halali.

Mtume alitazama kushangaa kwa mwanaume huyo na akasema: “Usiwe na wasi wasi. Ukifanya mambo kama nilivyokwambia, basi wewe na rafiki yako Tariq, hamtakuwa mnafanya makosa.”

Kubadilishana Mabinti.

Katika kipindi cha kabla ya Uislamu, Uarabuni kulikuwa na aina ya ndoa iliyokuwa ikipendwa ikijulikana kama ndoa ya *Shighar* (kubadilishana mabinti) ambayo ilikuwa ni dhihirisho la mamlaka yasiyo na kikomo ya akina baba juu ya binti zao. Mwanaume alikuwa akimuoza binti yake kwa mwanaume mwingine kwa matarajio ya yeye pia kupewa binti wa huyo mwanaume kama mke. Katika ndoa za aina hii, hakuna mke yeyote katika hawa wawili aliyepata mahari. Uislamu ulipiga marufuku ndoa za aina hii. Inafaa kuzingatiwa kuwa Mtume (s.a.w.w.) alimpa uhuru kamili binti yake Fatimah Zahra (a.s) katika kuchagua mume.

Aliwaoza pia binti zake wengine wengi, lakini hakuwanyima uhuru wao. Imam Ali bin Abi Talib (a.s) alimwendea Mtume (s.a.w.w) na kueleza nia yake ya kumposa Fatima (a.s), Mtume alisema wanaume wengi walimwendea Mtume, na yeye akafikisha ujumbe kwa Fatimah, lakini aligeuza uso wake pembeni, kama ishara ya kukataa. Mtume alimhakikishia Ali kuwa angefikisha ujumbe wake pia.

Mtume alikwenda kwa Fatimah na kumweleza binti yake mpendwa alichotaka Ali. Safari hii hakugeuza uso wake, lakini alinyamaza kimya na hivyo alielezea ridhaa yake. Mtume alipotoka nje, alikuwa na furaha, akasema, “Mungu ni Mkubwa!”

Harakati Za Kiislamu Juu Ya Haki Za Wanawake.

Uislamu umewafanyia wanawake mambo makubwa. Sio tu kwamba ulikomesha udhibiti usio na mipaka wa akina baba, lakini pia uliwapa wanawake uhuru, haiba na uhuru wa kufikiri na kutoa maoni.

Uislamu kirasmi kabisa ulizitambua haki zake za asili. Hata hivyo, kuna tofauti mbili za msingi kati ya hatua zilizochukuliwa na Uislamu na kile kinachotokea katika nchi za Magharibi na zinazofuatwa na wengine.

Tofauti ya kwanza inahusiana na saikolojia ya mwanaume na mwanamke. Uislamu umefanya na kufunua maajabu katika hili. Tutalijadili hili baadaye katika sura zinazofuatia.

Tofauti ya pili ni kuwa, japo Uislamu uliwafanya wanawake wazijue haki zao na ukawapa utambulisho, haiba na uhuru, haukuwachochea kuasi na kuwafanyia uovu wanaume zao.

Harakati za Kiislamu, za ukombozi wa wanawake zilikuwa nyeupe. Hazikuwa nyeusi wala nyekundu, hazikuwa bluu wala urujuani. Hazikukomesha heshima ya mabinti waliyokuwa nayo kwa baba zao wala ya wake kwa waume zao. Hazikuvuruga msingi wa maisha ya familia na hazikuwafanya wanawake wayatilie mashaka majukumu yao kwa baba zao na waume zao. Hazikutoa mwanga kwa wanaume ambao hawajaoa ambao mara zote huwa wanatafuta mwanya wa kuwalaghai wanawake.

Haukuwapokonya wanawake kutoka kwa waume zao na mabinti kutoka kwa wazazi wao na kuwakabidhi fisi wa ngono na wenye mivuto ya kilaghai ya pesa. Harakati za Kiislamu hazikufanya yale yaliyosababisha makelele na vilio katika mabahari kiasi cha mfumo wa familia kuvunjika vipande vipande. Huko ulinzi wa akina baba umetoweka.

Hakuna anayejua cha kufanya juu ya ufisadi na uchafu wa maadili uliokomaa na kuenea, juu ya uuaji wa watoto wachanga na utoaji wa mimba, juu ya asilimia 40 ya watoto waliozaliwa nje ya ndoa na juu ya wale watoto wachanga ambao baba zao hawajulikani na ambao mama zao hawataki kuhusishwa na lolote juu ya watoto hao, kwa sababu hawakuzaliwa ndani ya ndoa.

Akina mama wa watoto hao wanachokifanya ni kuwakabidhi watoto hao katika taasisi au mashirika ya kijamii na kamwe hawarudi tena kuwaulizia watoto wao.

Hapana shaka kwamba katika nchi yetu tunahitaji harakati za ukombozi wa wanawake, lakini tunazozihitaji ni harakati safi za Kiislamu na sio harakati za muundo wa Ulaya wenye madoa meusi. Tunataka harakati ambazo wavulana wenye ashiki watakuwa na nafasi ndogo na ambazo zinatakiwa zitokane na mafundisho bora ya Uislamu na yawe yamejengwa juu ya uelewa wa ndani na wa kimantiki wa jamii ya Kiislamu.

Ruhusa Ya Baba

Suala linalotakiwa kuchunguzwa kutokana na mamlaka waliyonayo akina baba juu ya binti zao, ni iwapo idhini ya baba ni ya lazima kwa ndoa ya kwanza ya binti yake.

Kwa mtazamo wa Uislamu baadhi ya mambo hayana ubishi.

Mvulana na msichana wote wana uhuru wa kiuchumi. Kila mtu mzima mwenye akili timamu anapaswa kuwa na mamlaka ya mali zake ikiwa anao uwezo wa kuzidhibiti. Baba, mama, mume au kaka hawana mamlaka ya usimamizi au uingiliaji kati katika hili.

Nukta nyingine ambayo haina ubishi ni juu ya ndoa. Watu wazima na wavulana waliokwishakua wana uhuru kamili juu ya jambo hili na hakuna mtu mwingine mwenye haki ya kuingilia. Hali hiyo iko hivi hivi pia kwa mwanamke ambaye amewahi kuolewa lakini sasa hana mume. Lakini kuna tofauti kidogo juu ya mwali ambaye anataka kuolewa kwa mara ya kwanza.

Hapana shaka kuwa baba hawezi kumlazimisha binti yake kuolewa na mtu ambaye yeye binti hajamridhia. Tayari tunajua Mtume alichomwambia yule binti ambaye baba yake alikuwa amemwozehsa bila idhini ya huyo binti. Mtume alisema ikiwa hakuridhika, anaweza kuolewa na mtu mwingine. Lakini kuna tofauti ya maoni ya wanazuoni juu ya iwapo binti anaweza kufunga ndoa bila idhini ya baba yake au iwapo idhini ya baba ni ya lazima.

Kuna nukta moja ambayo haina ubishi kabisa. Ikiwa baba atakataa kutoa idhini bila sababu ya maana, anapoteza haki yake. Mafakihi wamekubaliana kuwa katika hali hiyo binti ana uhuru wa kuolewa na yeyote anayempenda.

Lakini vinginevyo, ni kama tulivyosema, kuwa mafakihi wanatofautiana juu ya nukta hii, iwapo uthabiti wa ndoa ya binti inategemea idhini ya baba au la. Wanavyuoni wengi, hasa wa siku hizi wana maoni kuwa idhini sio lazima. Lakini kuna baadhi ambao wana maoni kuwa idhini ni ya lazima.

Kwa sababu nukta hii inabishaniwa haiwezi kujadiliwa kwa mtazamo wa Kiislamu lakini inaweza kujadiliwa kwa mtazamo wa kijamii.

Mwanaume Anahitaji Ngono, Mwanamke Anahitaji Upendo.

Msingi wa kanuni kwamba mabinti wadogo wanalazimika kutoolewa au angalau hawapaswi kuolewa bila idhini ya baba zao hautokani na kuonekana kuwa hawajakomaa ikilinganishwa na wavulana. Ingekuwa hivyo kusingekuwa na tofauti kati ya msichana wa miaka 17 ambaye hajawahi kuolewa ambaye anahitaji idhini ya wazazi wake kwa mujibu wa baadhi ya mafakihi. Na zaidi ya hayo, kama Uislamu ungekuwa unawachukulia wasichana kuwa hawajakomaa, usingetambua uhalali wa malipo wanayoyafanya (baina yao na hao wachumba kama mahari). Mbali na hoja za kisheria, nukta hii ina falsafa maalum ambayo haiwezi kupuuzwa.

Sio suala la kutokomaa au mwanamke kutokuwa na akili za kutosha. Hili linahusiana na sura maalum ya saikolojia za jinsia hizi mbili; yaani silika za mwanaume za kushawishi na silika za mwanamke za kuamini kiwepesi uaminifu na ukweli wa mwanaume.

Mwanaume anahitaji ngono na mwanamke anahitaji upendo (wa dhati). Mwanaume huelemewa na hamu na uchu wa kufanya mapenzi, wakati mwanamke kwa mujibu wa wanasaikolojia, ana uwezo mkubwa zaidi wa kudhibiti na kuficha matamanio yake. Ni sauti tamu ya mapenzi, udhati na uaminifu ambao humzidi nguvu mwanamke na kumfanya apige magoti. Hiki ndicho tunachomaanisha tunaposema tabia ya mwanamke ya kumwamini mwanaume kiwepesi.

Hivyo pindi mwanamke anapokuwa kigoli na hana uzoefu na wanaume, anaweza kushawishika kirahisi na nyimbo (za mwanaume) za kimapenzi kirahisi.

Profesa Reek, mwanasaikolojia wa kimarekani, anasema kwamba sentensi tamu na nzuri kabisa ambayo mwanaume anaweza kumwambia mwanamke ni 'Mpenzi ninakupenda' Anasema bahati kwa mwanamke ina maana kuwa na uwezo wa kuuteka moyo wa mwanaume kwa maisha yake yote.

Mtukufu Mtume, mwanasaikolojia aliyefundishwa na Mwenyezi Mungu, alieleza wazi wazi ukweli huu miaka 1425 iliyopita. Amesema kwamba mwanaume akielezea upendo wake kwa mwanamke, mwanamke huwa hasahau sentenzi hiyo.

Wanaume wenye nia ya kuwarubuni wanawake, hutumia hisia ya wanawake (ya kupenda kuambiwa wanapendwa) kwa maslahi yao. "Nitakufa kwa ajili yako' ndio maneno yao ya kuwashawishi wasichana ambao hawana uzoefu na wanaume.

Hii ni sababu muhimu kwamba msichana ambaye hana uzoefu na wanaume apate idhini ya baba yake kabla ya kuoelwa. Akina baba wanazijua akili za wanaume vizuri zaidi na mara nyingi huwatakia binti zao mema.

Katika hali hii, sheria haijamdharau mwanamke, lakini imechukua hatua kuyalinda maslahi yake (mwanamke). Kuibua pingamizi dhidi ya ulazima wa kupata idhini ya baba ni kwa ovyo zaidi kuliko kuuliza kwanini idhini ya baba au mama haijafanywa lazima kwa upande wa wavulana.

Ninashangaa kwanini watu ambao kila siku wanashuhudia uovu wa mapenzi holela kati ya wavulana na wasichana, bado wanashauri wasichana wawaasi na wasiujali ushauri wa walezi wao.

Kwa mtazamo wetu hii inatokana na hila na njama zinazofanywa kati ya wale wanaodai kumhurumia mwanamke na wale wanaowarubuni. Wa kwanza anamtengenezea mazingira mazuri huyu wa pili na kazi yao inakuwa nyepesi.

Wasichana wana mamlaka kamili juu ya ndoa zao. Ila uthabiti wake tu ndio unaegemea idhini ya baba, maadamu baba mwenyewe hatazuia idhini kwa nia mbaya au kwa sababu hana uwezo wa kutoa hukumu sahihi bila sababu yoyote ya maana. Je kuna tatizo lolote juu ya kanuni hii, au inaweza

kuonekana kwenda kinyume cha dhana ya uhuru wa binadamu? Ni tahadhari tu kwa ajili ya kulinda maslahi ya wasichana wasio na uzoefu na imejengwa juu ya dhana ya asili ya kutoaminika sana ya wanaume.

Kwa mtazamo huu hakuna pingamizi linaloweza kutolewa dhidi ya sheria ya Kiislamu. Kinachoweza kupingwa ni mila iliyoenea miongoni mwa Waislamu. Akina baba walio wengi bado wanafikiri kuwa wana mamlaka kamili na wanaona kuwa ni kinyume na stahili yake, ikiwa msichana atatoa maoni yake juu ya uchaguzi wa mwenzi wake katika maisha, ambaye atakuwa baba wa watoto wake atakaowazaa baadaye.

Hawazingatii ukomavu wa kiakili wa msichana, ambao kwa mujibu wa sheria ya Kiislamu, ni wa umuhimu mkubwa na usioweza kuepukwa. Ndoa nyinyi zinazofungwa kabla wasichana hawajakomaa, kisheria ni batili. Mara nyingi hawazingatii ukomavu wa msichana, kuvunja ungo tu kunaonekana kutosheleza. Lakini tunajua walichoandika mafakihi wakubwa juu ya kupima ukomavu wa kiakili wa wasichana.

Baadhi ya mafakihi wanazingatia kuwa ukomavu wa kidini ni sharti muhimu la ndoa. Wanashikilia kuwa ni wale wasichana tu wanaojua kanuni za dini kwa mantiki na ushahidi ndio wanaofaa kuolewa. Kwa bahati mbaya, wengi wa walezi na wale wanaosimamia sherehe za ndoa, hawazingatii masharti haya.

Tunaweza kuona kuwa katika hati za zamani za ndoa maneno ‘mtu mzima, mwenye akili timamu na aliyekomaa yalikuwepo pamoja na majina ya bwana harusi na bibi harusi.

Hata hivyo, kwa mujibu wa sheria ya Shia, mwanamke mtu mzima na aliyekomaa na ambaye amewahi kuolewa huko nyuma, hahitaji idhini ya baba.

Uislamu Na Maisha Ya Kisasa

Uislamu Na Maisha Ya Kisasa I

Suala la dini na maisha ya kisasa ni moja ya mambo ambayo hayawagusi Waislamu peke yao. Dini nyingine pia zilikumbana na tatizo hili. Watu wengi wenye kupendelea mabadiliko duniani, wameikana dini kwa sababu wanaamini kuwa dini na maisha ya sasa haviendi pamoja. Wanafikiri kuwa kudumaa, kutuama na kutobadilika ni sifa za lazima za mtu mshika dini. Kwa maneno mengine, wanafikiri kuwa kudumaa na ukinaifu unatokana na kutokuwepo kwa mabadiliko na kwamba kudumisha hali ya kizamani

ndio tabia za dini.

Marehemu Bwana Nehru aliyekuwa waziri Mkuu wa India alikuwa na mawazo ya kisekula na hakuwa akiamini dini yoyote. Inaoinekana kutokana na kauli zake kuwa kilichomfanya asipende dini ni kutobadilika kwake na ukinaifu unaotokana na kutokuwepo kwa mabadiliko.

Kuelekea kipindi cha mwisho cha maisha yake Nehru alihisi kuwa na uwazi moyoni mwake na aliamini kuwa uwazi ule ungezibwa na nguvu ya kiroho tu. Lakini hakuelekea kuiamini dini yoyote kwa sababu aliamini kuwa hali ya ukinaifu na kutokuwepo kwa mabadiliko ilikuwepo katika dini zote.

Mwandishi wa habari wa Kihindi, aitwaye Karanjia, alimhoji Nehru katika kipindi chake cha mwisho mwisho cha uhai wake (Nehru) na alivyoonekana haya yalikuwa ni mahojiano ya mwisho ambapo Nehru alitoa maoni yake juu ya matatizo ya jumla ya ulimwengu. Alipokuwa akimzungumzia Gandhi, Karanjia alisema, “Baadhi ya wanaopendelea mabadiliko (liberals) na maendeleo wanaamini kuwa Gandhiji, kwa kupitia na kwa kutokana na utatuzi wake wa matatizo kwa hisia kali, unyofu na njia za kiroho, zimedhoofisha na kuitia ubaridi imani yako ya asili ya ujamaa wa kisayansi.”

Katika kulijibu hili, Nehru alisema; “Ni muhimu na vizuri kutumia fursa ya njia za kimaadili na kiroho. Mara zote nimekubaliana na Gandhiji juu ya hili. Ninaamini kuwa ni muhimu zaidi kutumia fursa ya njia hizi, kwani sasa, kwa kiasi kikubwa kuliko ilivyokuwa huko nyuma, tunahitaji majibu ya kiroho na kimaadili juu ya maswali yanayotokana na pengo la kimaadili linalosababishwa na tamaduni za kisasa, ambazo zinazidi kuwa maarufu.”

Kisha Kiranjia aliuliza swali juu ya Ukomunisti. Nehru alikiri mapungufu yake na katika majibu yake alionyesha baadhi ya mapungufu na ubovu wake (wa ukomunisti). Kwa mara nyingine tena alipendekeza suluhisho la kiroho juu ya matatizo ya dunia. Alipofika hapa Karanjia akasema; “Bwana Nehru, je dhana yako ya utatuzi wa matatizo ya kimaadili na kiroho haikufanyi uwe tofauti na Jawahanal wa jana? (Nehru mwenyewe enzi za ujana wake). Ulichokisema kinaonyesha kuwa Bwana Nehru, katika kuelekea mwisho wa uhai wake, ameanza kumtafuta Mungu.”

Nehru alisema; “Ndiyo, nimebadilika. Msisitizo wangu juu ya unyofu na maadili ya kiroho na utatuzi wa matatizo sio wa bahati mbaya.” Akaongeza kuwa; “Swali sasa ni jinsi ya kukuza maadili na imani ya kiroho katika daraja la juu zaidi. Hapana shaka kwamba kwa ajili ya hili, dini zipo, lakini kwa bahati mbaya zimechukua mtazamo finyu na matendo yasiyobadilika na zimebaki kuwa taratibu rasmi lakini duni. Ni umbo lake la nje tu lililobaki, lakini ari na dhana yake ya kweli imetoweka.”

Uislamu Na Mahitaji Ya Wakati.

Katika dini zote ni Uislamu tu unaojihusisha zaidi na vipengele vyote vya maisha ya mwanadamu. Mafundisho yake hayajajikita katika matendo ya ibada na sala na mfumo wa ushauri wa maadili peke yake. Uislamu, kama ulivyoshughulikia uhusiano wa watu na Mwenyezi Mungu, ndivyo hivyo

hivyo ulivyoshughulikia mahusiano baina ya watu. Katika sura mbali mbali Uislamu umeshughulikia haki za watu binafsi na majukumu yao pia. Hii ndio sababu swali kwamba mafundisho yake yanafaa kutumika au la katika mazingira yanayozidi kubadilika ni thabiti zaidi katika suala la Uislamu kuliko dini nyingine yoyote.

Kwa bahati imetokea kwamba, wasomi wengi na waandishi wasiokuwa Waislamu wamezisoma sheria za kijamii na kiraia (za madai na za jinai) na wamezisifu kuwa ni chombo cha kisheria cha kimaendeleo na endelevu. Wameusifu Uislamu kwa mapana na marefu, kuwa ni dini hai na itakayodumu milele, na wameuelezea uwezo na sifa za sheria hizi za Kiislamu wa kuweza kutumika nyakati zote na katika hali zote.

Mwandishi maarufu sana wa Kiingereza aliyekuwa akipendelea msimamo wa wastani (liberal), Bernard Shaw amesema; “Mara zote nimekuwa nikiipa dini ya Muhammad heshima kubwa (daraja kubwa), kutokana na uhai wake wa ajabu. Ni dini pekee inayoonekana kwangu kuwa na uwezo wa kunyumbulika na hivyo kuweza kutumika katika dunia inayobadilika na katika zama zote. Nimetabiri kuwa imani ya Muhammad itakubaliwa na Ulaya ya kesho, na dalili za hili zinajionyesha hata sasa.

“Makasisi wa zama za kati aidha kwa sababu ya ujinga au kwa sababu ya kung’ang’ania bila hoja imani zao waliupaka Uislamu rangi mbaya kabisa. Kwa kusema kweli walifundishwa kumchukia mtu huyu, Muhammad na dini yake. Kwao Muhammad alikuwa mpinga Kristo. Mimi nimemsoma, mtu huyu wa ajabu, na kwa maoni yangu hakuwa mpinga Kristo kabisa na lazima aitwe mkombozi wa wanaadamu. Ninaamini kuwa kama mtu kama yeye angetwaa madaraka /uongozi wa dunia ya sasa angefanikiwa kutatua matatizo katika namna ambayo ingeleta amani na furaha, vitu ambavyo vinahitajika sana kwa sasa.

Dr. Shibli Shama’il ni myakinifu wa Kiarabu wa Lebanoni. Kwa mara ya kwanza alitafsiri kitabu cha ‘Darwin Kiitwacho *‘Origin of Species’* kwenda katika lugha ya Kiarabu, pamoja na sharhe ya mwanasayansi wa kijerumani aitwaye Boucher katika kitabu hicho akakipa jina la *‘A Weapon Against Religious Belief.’* (‘Silaha Dhidi Ya Imani Za Kidini.’)

Ingawa hamwamini Mwenyezi Mungu, haoni aibu kuusifu Uislamu na muasisi wake mtukuka. Ameusifu Uislamu kwa kusema kuwa ni dini hai inayoweza kutumika katika zama zote.

Mtu huyu, katika juzuu ya pili ya kitabu chake kiitwacho, *‘Philosophy of Evolution’* ambacho amekichapisha kwa Kiarabu, ameandika makala yenye kichwa cha cha habari ‘Uislamu na Ustaarabu’. Ameandika makala hii kukanusha madai ya wasio Waislamu kwa kutoa madai kuwa Uislamu ndio uliosababisha kuporomoka kwa hali ya Waislamu.

Shibli Shama’il amejaribu kuthibitisha kuwa jambo hasa lililosababisha kuporomoka kwa hali za Waislamu ni wao Waislamu kuyaacha (kuacha kutekeleza) mafundisho ya kijamii ya Uislamu. Wale wazungu wanaoushambulia Uislamu aidha hawajui au wanafanya hivyo kwa nia mbaya ya kuwafanya watu wa Mashariki (Asia) wazitilie shaka sheria zao na mfumo wao ili kuwafanya wafuate mfumo wa

Kimagharibi.

Wakati wa zama zetu, suala la iwapo Uislamu unaafikiana na hali halisi ya maisha ya sasa au la limekuwa likiulizwa sana. Tunapata picha ya ndani ya watu hasa wale wanaotoka katika tabaka la wasomi na tunakuta kuwa swali hili linaulizwa zaidi kuliko maswali mengine.

Pingamizi

Wakati fulani watu hawa wanatoa hoja za kifalsafa juu ya suala hili kuwa vitu vyote hapa duniani lazima vibadilike. Hakuna kinachobaki vile vile bila kubadilika, na halikadhalika binadamu wanabadilika. Sasa inawezekanaje sheria za Kiislamu zibaki hivyo bila kubadilika kwa zama nenda rudi?

Kama tukilitazama swala hili kwa mtazamo wa kifalsafa kabisa, jibu ni rahisi. Ni vitu (maada) vinavyobadilika kila mara, ambavyo hukua na kuporomoka na ambavyo hupasika katika kugeuka na kuoza. Lakini sheria za ulimwengu hazibadiliki. Kwa mfano, viumbe vyote hai vimegeuka na vimeendelea kugeuka kwa mujibu wa utaratibu na kanuni fulani zilizoelezwa na wanasayansi. Hapana shaka kwamba viumbe hivi vinageuka na kubadilika lakini kanuni zinazotawala mabadiliko haya hazibadiliki.

Na sasa tunazungumzia kanuni (sheria) hizi. Katika hili, hakuna tofauti yoyote iwapo sheria hizi ni za asili au zimetungwa na kukusanywa, kwani inawezekana kwamba sheria ambazo zimetungwa zinaweza kuwa na asili kama chanzo chao na kuafikiana na mchakato wa mabadiliko ya mtu mmoja mmoja na halikadhalika jamii ya wanadamu kwa ujumla.

Hata hivyo, swali kuhusiana na kuafikina au kutoafikiana kwa Uislamu na mahitaji ya muda halina sura ya kiujumla na kifalsafa peke yake.

Swali ambalo huulizwa zaidi ni kuwa kwa vile sheria huundwa kukidhi mahitaji ya wanaadamu na mahitaji yenyewe yanabadilika kila mara inawezekanaje sheria hizo za kijamii zibaki hivyo hivyo bila kubadilika?

Ni swali zuri. Na imetokea kuwa tabia za kimiujiza za Uislamu zimewezesha sheria zisizohitaji kubadilishwa kukidhi mahitaji yasiyobadilika ya mtu mmoja na jamii na sheria zinazobadilika badilika kwa mahitaji ya muda mfupi na yanayobadilika. Hii ni sifa ya kipekee ambayo Waislamu wote wajuzi wa mambo ya sheria za kiislamu na waliozisoma sheria zake wanajivunia. Tutalielezea hili vizuri zaidi baadaye.

Je Mabadiliko Ya Kijamii Yanakwenda Na Wakati?

Kabla ya kuliendea swali hili tungependa kuibua nukta mbili.

Nukta ya kwanza ni kuwa watu wengi wanaoongelea maendeleo na mabadiliko ya hali wanadhani kuwa

mabadiliko yoyote ya kijamii, hasa kama yametokea nchi za Kimagharibi, basi ni matokeo ya maendeleo. Hili ni moja ya mawazo potofu liliyoendekezwa na kizazi hiki.

Watu wanadhani kuwa kwa vile njia za maisha hubadilika siku hadi siku, zilizo duni hubadilishwa kwa zilizo bora zaidi na sayansi na viwanda vinaboreka kila siku, mabadiliko yote katika maisha ya binadamu ni aina ya maendeleo na kwa hiyo yanafaa kukaribishwa na kupokelewa kwa mikono miwili. Wanafikiri pia kuwa mabadiliko haya hayaepukiki na huja baada ya muda fulani.

Kwa kusema kweli sio kwamba mabadiliko yote ni matokeo ya maendeleo ya sayansi na viwanda wala sio kwamba hayaepukiki. Huku sayansi ikien delea kukua, asili ya ubinafsi na unyama wa mwanadamu nayo hubaki bila kubadilika. Ujuzi (elimu) na busara humpeleka mtu katika ukamilifu na asili ya unyama wa mwanadamu humsukumia kwenye ufisadi na upotofu.

Asili ya unyama wa mwanadamu mara zote hujaribu kutumia ujuzi kama njia ya kupatia matamanio yake. Kwa kadiri muda unavyokwenda, kwa kadiri maendeleo na mabadiliko yanavyotokea, ufisadi na upotofu ndivyo unavyozidi kukua na kukomaa. Tunapaswa kwenda na wakati lakini wakati huo huo lazima tupige vita ufisadi pia.

Mleta mabadiliko (mema) na mpinga mabadiliko (mema) wote wanapigana dhidi ya muda, tofauti yake ni kuwa mleta mabadiliko mema hupigana dhidi ya upotofu unaoletwa na mabadiliko ya muda na mpinga maendeleo (mabadiliko) hupigana dhidi ya mabadiliko (maendeleo halisi) yanayoletwa na mabadiliko ya muda. Kama tunauchukulia muda na mabadiliiko yake kama kigezo cha mema yoyote na maovu yote, sasa ni kigezo gani cha kuupimia muda wenyewe?

Kama kila kitu kitakwenda na wakati sasa je wakati wenyewe unapaswa kwenda na nini? Kama mwanadamu ataufuata muda na mabadiliko yake kwa utii mkubwa, sasa nini kitafanyika juu ya majukumu na nafasi ya utashi wa mwanadamu? Mwanadamu anaendesha gari la wakati, ambalo liko kwenye mwendo. Lazima awe mwangalifu na aliongoze vyema gari lake. Vinginevyo atakuwa kama mtu aliyepanda farasi na akamwachia farasi wake aende popote atakapo.

Marekebisho Au Kuondoa Kabisa?

Nukta ya pili inayofaa kutajwa hapa ni kwamba baadhi ya watu wamelitatua tatizo gumu la Uislamu na mahitaji ya wakati kwa namna rahisi sana. Wanasema kuwa Uislamu ni dini ya milele, na inaweza kurekebishwa ili kuafikiana na mahitaji ya kila zama na wakati.

Lakini wanapoulizwa marekebisho haya yanafanyikaje na kanuni yake ni nini, mara moja wanasema kuwa hali ya maisha inapobadilika, sheria zilizopo hubatilishwa na kuwekwa nyingine. Wanatoa hoja kuwa sheria za msimu (muda mfupi) za kidini lazima ziwe na uwezo wa kurekebishwa na ziafikiane na maendeleo ya elimu na sayansi pamoja na kupanuka kwa utamaduni na ustaarabu. Kwa mujibu wao, uwezo huo wa sheria wa kuweza kurekebishwa ili kuafikiana na mahitaji ya wakati haupingani na

Uislamu na sio kinyume na mafundisho yake.

Wanadai kuwa, kwa vile mahitaji ya wakati yanabadilika kila mara, basi kila zama huhitaji sheria mpya. Wanaendelea kudai kuwa sheria za kiraia na kijamii za Uislamu zinaafikiana na maisha rahisi ya Waarabu waliokuwa wakiishi kabla ya Uislamu, na ambazo kwa kiasi kikubwa zilikuwa ni kwa mujibu wa mila na desturi zao. Sasa kwa kuwa haziafikiani na maisha ya zama hizi zinatakiwa ziondolewe na ziwekwe nyingine mpya za kisasa.

Watu hawa wanapaswa kuulizwa: Kama uwezo wa sheria kuweza kurekebishwa maana yake ni uwezo wa kubatilishwa na kufutwa, basi ni sheria gani ambayo haina sifa hii? Kuna sheria basi yeyote ambayo haiendi na wakati kwa mtazamo huu?

Tafsiri hii ya uwezo wa sheria kurekebishwa na kuweza kutumika katika zama zote ni sawa na kusema kuwa vitabu vyote na maktaba ndio njia bora kabisa za kufurahia maisha kwa sababu muda wowote mtu atakapotaka starehe, anaweza kuviuza na kutumia fedha zitakazopatikana kwa ajili ya kukidhi matamanio yake.

Mwandishi wa Kiirani anasema kuwa mafundisho ya Uislamu yamegawanyika katika sehemu tatu. Sehemu ya kwanza ina imani za msingi kama vile tauhidi (imani kuwa Mungu ni mmoja tu), Utume, Ufufuo n.k.

Sehemu ya pili inahusiana na matendo ya ibada kama vile sala, saumu, udhu, tohara, hija n.k sehemu ya tatu ina sheria zinazohusiana na maisha ya watu.

Kwa mujibu wake yeye ni sehemu mbili tu za mwanzo ambazo ni za lazima katika dini na ambazo zinafaa kuhifadhiwa milele. Lakini sehemu ya tatu sio sehemu ya lazima ya dini kwa kuwa dini haihusiani na maisha ya kila siku ya watu. Mtukufu Mtume mwenyewe hakuamuru kuwa sheria hizi ziwe sehemu ya dini kwa vile hazikuhusiana na ujumbe wake yeye kama Mtume. Ilitokea tu kwamba akawa ni mkuu wa Dola, kwa hiyo akalazimika kuweka sheria pia. Vinginevyo dini haina lolote la kulazimisha katika maisha ya kidunia ya watu.

Ni vigumu kuamini kuwa mtu anayeishi katika nchi ya Kiislamu anaweza kuwa mjinga wa mafundisho ya Uislamu kiasi hiki.

Je, Qur'ani haijaelezea lengo la kuleta Mitume na Manabii? Je, Qur'ani haisemi wazi wazi kuwa

لَقَدْ أَرْسَلْنَا رُسُلَنَا بِالْبَيِّنَاتِ وَأَنْزَلْنَا مَعَهُمُ الْكِتَابَ وَالْمِيزَانَ لِيَقُومَ النَّاسُ بِالْقِسْطِ

'Tumewaletea Mitume wetu na dalili za wazi na tumewaleta pamoja nao kitabu na vipimo, ili watu wahukumiane kwa haki (*Suratul Hadidi*; 57:25).

Qur’ani imeuelezea uadilifu katika jamii kama lengo kuu la Mitume wote.

Kama unataka unaweza usiyafuate mafundisho ya Qur’ani, lakini kwa nini unatenda dhambi kubwa zaidi kwa kuusingizia na kuuzushia Uislamu na Qur’ani? Bahati yetu mbaya zaidi inatokana na ukweli kwamba maadili yetu na sheria vimepoteza chanzo pekee cha nguvu yake, yaani dini.

Ni katika nusu karne tu tulipoanza kusikia watu wakipiga kelele kuwa Uislamu ni mzuri, ili muradi tu ubakie ndani ya majumba ya ibada, na usishughulike na jamii. Kelele hii imepigwa kutoka ndani ya mipaka ya nchi za Waislamu na imeenezwa katika ulimwengu wote wa Kiislamu. Ili kuliweka lengo la kelele hizi wazi tunaweza kusema kuwa nia ni kuufanya Uislamu ubaki kuwa ni kikwazo cha kuzuia kuenea kwa ukomunisti lakini kama huu huu Uislamu utagongana na maslahi ya Magharibi basi upingwe vikali.

Kwa mtazamo wa watu wa Magharibi, matendo ya Uislamu lazima yaendelee, ili pindi ikitokea haja, Waislamu wahamasishwe kuupinga mfumo wa kikomunisti ambao hauamini mambo ya dini na Mungu, lakini sheria za kijamii za Uislamu ambazo zinatoa falsafa ya maisha ya Uislamu lazima ziondoshwe, kwa vile sheria hizi huwapa Waislamu uhuru fulani na kuwafanya wawe watu tofauti wanaojitegemea katika mfumo wao, jambo ambalo litawazuia kumezwa na nchi za Magharibi zenye tamaa kali.

Kwa bahati mbaya, watetezi wa hoja kuwa Uislamu haujihusishi na maisha ya kila siku ya watu, wamesahau baadhi ya ukweli wa msingi.

Awali miaka 1400 iliyopita, Uislamu ulipinga kanuni kuwa tunaamini baadhi ya mambo (baadhi ya mafundisho ya Uislamu) na tunayakataa mengine, na ukatamka kuwa kanuni na sheria za Uislamu hazibadiliki.

Pili, tunaamini kuwa muda umefika ambapo Waislamu hawapaswi kupotoshwa na mbiu za uongo. Watu sasa pole pole wameanza kuamka na wameanza kutofautisha kati ya maendeleo ambayo ni matokeo ya kuchanua kwa vipaji vya kisayansi na kiakili, na kudhihiri kwa ufisadi na upotofu, kutoka nchi za Magharibi.

Watu wa ulimwengu wa Kiislamu hivi sasa, kuliko kipindi kingine chochote, wameanza kufahamu thamani ya mafundisho ya Uislamu na wametambua kuwa wanaweza tu kuishi maisha huru kwa kuyafuata. Hawatayaacha, kwa gharama yoyote.

Waislamu makini wanafahamu kuwa propaganda dhidi ya sheria za kiislamu si chochote bali udanganyifu wa mabepari.

Tatu, watetezi wa hoja hii wanapaswa kujua kuwa Uislamu unapokuwa na nguvu, hushinda mifumo mingine yote, iwe ya kikafiri au vinginevyo. Uislamu unataka kutawala maisha ya jamii kama falsafa ya maisha, na hautaki kubakia misikitini tu na sehemu nyingine za ibada. Uislamu ambao utabakia kwenye nyumba za ibada, utaacha nafasi kwa ajili ya mawazo ya Kimagharibi na halikadhalika mawazo

yanayopingana na umagharibi na itikadi zake.

Adhabu ambazo nchi za magharini zinatumikia, katika baadhi ya nchi za Waislamu ni matokeo ya kutoujua ukweli huu.

Uislamu Na Maisha Ya Kisasa II

Mwanadamu sio kiumbe pekee anayeishi maisha ya kijamii. Wanyama wengi, na hususan wadudu hupenda kuishi pamoja na kushirikiana. Wanafuata kanuni za mgawanyo wa kazi, uzalishaji na ugavi na kutoa na kupokea amri.

Nyuki, na baadhi ya wadudu jamii ya mchwa wana mfumo huu bora wa maisha, mfumo ambao utamchukua mwanadamu, anayejiona kuwa ni mfalme wa viumbe vyote, miaka au hata karne ili kufikia kiwango hicho cha ufanisi.

Ustaarabu wao (wadudu hawa) haujapitia vipindi kama vile zama za mwituni, zama za mawe na zama za nyuklia. Toka mwanzo wamekuwa na ustaarabu na mfumo wa namna moja kama tu walivyo leo. Ni mwanadamu aliyeanzia sifuri. Tazama :

وَخُلِقَ الْإِنْسَانُ ضَعِيفًا

"Mwanadamu aliumbwa dhaifu ."*Suratul Nisaa* 4:28

Kwa upande wa wanyama, mahitaji yao ya maisha hayabadiliki. Kwao usasa na fasheni mpya havina maana. Ulimwengu wa kale na ulimwengu wa sasa kwao hauna tofauti yoyote. Kwao sayansi haifanyi ugunduzi wowote ule. Bidhaa mpya kabisa nyepesi na nzito za viwanda hazikuingia katika soko lao; kwa nini? Kwa sababu wanaishi kwa silika na sio kwa akili (mantiki).

Maisha ya kijamii ya mwanadamu mara zote yanabadilika. Kila karne ulimwengu unabadilika. Hapo ndio kuna siri ya mwanadamu kuwa mfalme wa viumbe vyote. Mwanadamu ni mtoto wa maumbile aliyekomaa na kustahili heshima. Amefikia hatua ambayo hahitaji muongozo wa moja kwa moja wa ile nguvu ya ajabu iitwayo silika.

Maumbile yanafahamu kuwa mwanadamu ni kiumbe aliyekomaa, na ndio maana yamemuacha huru. Yale ambayo wanyama wanayatekeleza kwa silika na kwa kufuata kanuni za maumbile ambazo hawawezi kuzivunja/kukiuka, wanaadamu wanatakiwa kuyatekeleza kwa kutumia akili na elimu na kwa kufuata sheria zilizopitishwa na zinazoonekana.

Mwanadamu akiwa ni mwamuzi wa mwisho wa majaaliwa yake mara zote anaweza kupotoka na kuiacha njia ya maendeleo, na hapa ndio kuna siri ya kuteleza kwake, vipingamizi vyake (anavyokumbana navyo) kupotoka na kushindwa kwake.

Kama tu ilivyo kuwa maendeleo yapo wazi kwake, halikadhalika njia ya kuelekea upotofu, ufisadi na kushindwa haijafungwa.

Wanaadamu wamefikia hatua ambayo kwa mujibu wa maneno ya Qur'ani wanaweza kubeba dhamana ambayo mbingu, ardhi na milima haviwezi kubeba; kwa maneno mengine, wanaweza kuishi maisha huru na wanaweza kuchukua majukumu ya kisheria, kitaalamu na mengineyo. Hii ndio sababu hawana kinga ya makosa, ubinafsi, ujinga na dhulma.

Pale Qur'ani inapouelezea uwezo huu wa ajabu wa binadamu, mara moja unamtaja kuwa ni 'dhalimu na mjinga'.

Uwezo na sifa hizi mbili za mwanadamu, uwezo wa kuboreka (kuwa bora zaidi) na uwezo wa kupotoka havitenganishiki. Mwanadamu sio kama mnyama ambaye katika maisha yake ya kijamii, huwa haendi mbele wala nyuma, hageukii kulia wala kushoto. Lakini mwanadamu kwa upande wake, katika maisha yake wakati fulani huenda mbele na wakati fulani nyuma. Katika maisha ya wanadamu kama kuna mwendo na kasi, basi kuna kusimama na kupumzika pia. Kama kuna maendeleo na kubadilika kwenda katika hali bora zaidi basi kuna ufisadi na upotofu pia. Kama kuna haki na wema, basi kuna udhalimu na ushari pia. Kama elimu na busara vimedhihiri basi ujinga na matamanio duni yamedhihiri pia.

Inawezekana kwamba mabadiliko yanayotokea na hali mpya zinazoonekana vikawa ni vya kundi la pili (la mabaya).

Wasiotaka Kubadilishwa Na Waliopotoshwa.

Ni moja ya tabia za mwanadamu kwamba wakati fulani hufanya jambo kupita kiasi na wakati fulani hufanya jambo kwa kiasi kidogo zaidi kuliko inavyohitajika. Kama akichagua kundi la kati na kati hufanya jitihada kutofautisha kati ya mabadiliko ya aina sahihi na mabadiliko ya aina potofu. Hujaribu na hufanya jitihada kuusukuma muda mbele kwa msaada wa elimu na ubunifu wake na kujinasibisha na maendeleo huku akijaribu kuudhibiti upotofu na kuepuka kutangamana nao.

Lakini kwa bahati mbaya, si mara zote mwanadamu huchagua njia hii. Anaandamwa na magonjwa mawili ya hatari, ugonjwa wa kutotaka kubadilika na ugonjwa wa ujinga. Ugonjwa wa kwanza matokeo yake ni kubaki bila mabadiliko na kujiepusha na maendeleo na matokeo ya ugonjwa wa pili ni upotofu wa kuangamia.

Asiyetaka kubadilika huchukia kila jambo jipya na hawezi kuafikiana na kitu chochote isipokuwa cha zamani. Kwa upande wa pili, limbukeni huona kila kitu kipya kuwa ni cha kisasa na maendeleo na hukiaona kuwa ndio hitajio la wakati. Kwa yule asiyetaka mabadiliko (rigid) kila maendeleo mapya kwake

anaona ni ufisadi na upotofu wakati limbukeni anaona mambo yote mapya bila kubagua yote yana maana kupanuka kwa utamaduni na elimu.

Asiyetaka mabadiliko hatofautishi kati ya pumba na kiini safi na kati ya njia na malengo. Kwa maoni yake kazi ya dini ni kuhifadhi yale yote ya kale na kuukuu hata kama hayatumiki. Anafikiri kuwa Qur'ani iliteremshwa ili kudhibiti mwendo wa wakati na kuibakiza hali ya dunia iwe vile vile siku zote.

Kwa mujibu wa mtazamo huu, mila za zamani na zilizopitwa na wakati, kama vile kuanza kusoma Qur'ani kuanzia mwisho, kuandikia kalamu za matete na wino wa kuchovya kunawia kwenye beseni la kituruki; kula kwa mikono, kutumia taa ya mafuta ya taa na kubakia bila ya kujua kusoma na kuandika ni mambo ya kidini ambayo lazima yahifadhiwe na kudumishwa.

Kwa upande mwingine limbukeni huelekeza macho yake yote nchi za Magharibi ili aweze kuiga mtindo wowote mpya utakaotokea na kila mila mpya. Huiita hali hii kuwa ni kisasa na jambo la lazima kufuatwa lililoletwa na wakati. Wote wawili, wasiotaka mabadiliko na waliopotoka (wajinga) wanaamini kuwa mila na desturi zote za zamani ni kanuni/matendo ya kidini, tofauti ni kuwa asiyetaka mabadiliko anataka kuzihifadhi wakati mjinga anaona kuwa dini ni sawa na kudorora (bila mabadiliko yoyote).

Katika karne chache zilizopita suala la migongano kati ya dini na sayansi limekuwa likibishaniwa sana miongini mwa watu wa nchi za Magharibi.

Wazo la migongano liliibuka kutokana na mambo mawili. Kwanza kanisa lilikuwa limezikubali baadhi ya dhana za kisayansi na kifalfasa kuwa ni imani za kidini, lakini maendeleo ya sayansi yakathibitisha uongo wa dhana hizo. Pili, sayansi imebadilisha muundo na hali za maisha.

Wale wasiotaka mabadiliko, ambao wana muonekano wa kushika dini, wanataka kuufanya muonekano wa nje wa maisha ya kimaada kuwa sehemu ya dini, kama tu, bila ulazima wowote walivyoyapa sura ya kidini baadhi ya masuala ya kifalsafa.

Limbukeni nao wanaamini kuwa dini imeamuru muundo fulani wa maisha ya kimaada, na kwa vile sayansi imeamuru kuwepo kwa mabadiliko katika muundo huu, dini inapaswa kutupiliwa mbali.

Kupinga mabadiliko kwa kundi moja, na ujinga wa kundi jingine, kumezua wazo la kubuni la mgogoro kati ya sayansi na dini.

Hadith Ya Mafumbo Katika Qur'ani

Uislamu ni dini ya kimaendeleo na inataka wafuasi wake waendelee. Qur'ani imetumia hadith ya mafumbo (yenye mafundisho) kuwashawishi Waislamu wasonge mbele, chini ya nuru ya Qur'ani. Inasema kuwa wafuasi wa Mtume Muhammad (s.a.w.w) ni kama mbegu iliyopandwa katika ardhi. Kwanza matawi yake hutokeza kama majani laini ya mbegu. Kisha hukua na kuimarika sana kiasi cha kuweza kusimama katika kikonyo chake. Hakua haraka mno kiasi cha kuwashangaza sana wakulima.

Huu ni mfano wa jamii ambayo Qur'ani inaukusudia. Qur'ani inachokikusudia ni kukua. Qur'ani inataka kuweka msingi wa jamii ambayo mara zote itakuwa ikikua, ikiendelea na kupanuka.

Will Durant anasema hakuna dini iliyowataka wafuasi wake kuwa na nguvu kama Uislamu ulivyofanya. Historia ya Uislamu wa awali inaonyesha ni kiasi gani Uislamu ulivyo na nguvu ya kuijenga upya jamii na kuisukuma mbele kimaendeleo.

Uislamu unapingana na vyote viwili kutaka mabadiliko na ulimbukeni (ujinga) na unaviona vyote hivi viwili kuwa ni hatari. Uchakavu wa kiakili wa wasiotaka mabadiliko na kung'ang'ania kwao mila za zamani ambazo hazina uhusiano wowote na Uislamu, kumetoa kisingizio kwa limbukeni kuuona Uislamu kuwa unapingana na maisha ya kisasa (usasa).

Kwa upande mwingine kufuatana na kuiga mitindo mipya zaidi na namna za maisha za Magharibi kunakofanywa na limbukeni, imani yao kwamba kufuata utaratibu wa Kimagharibi kimwili na kiroho, kukubali kwao tabia, adabu na desturi za Magharibi, na kuiga kibubusa sheria za kiraia na kijamii kutoka katika nchi za Magharibi, kumetoa kisingizio kwa wasiotaka mabadiliko kukitazama kila kitu kipya kwa mashaka na kukiona kama tishio kwa dini yao, uhuru wao na kwa haiba ya kijamii ya jumuiya yao.

Kwa sasa, Uislamu unagharamikia makosa ya makundi yote mawili. Ung'ang'anizi wa wasiotaka mabadiliko umeacha uwanja wazi kwa limbukeni kufanya uharibifu na ujinga wa limbukeni umewafanya wasiotaka mabadiliko kuwa ving'ang'anizi zaidi katika imani zao.

Inashangaza kuona kuwa hawa wanaojiita wameelimika na kustaarabika ingawa kiuhalisia ni watu wajinga, wanafikiri kuwa muda ni maasumu (haubebi dhambi). Ukweli ni kuwa mabadiliko yote yanaletwa na watu, na mwanadamu sio maasumu hata kidogo (hajaepukana na madhambi). Sasa vipi inaweza kufikirika kuwa mabadiliko ya muda mara zote huwa hayana makosa na matatizo.

Kama ilivyo tu kuwa mwanadamu ana matakwa ya kupenda sayansi, maadili, sanaa na dini, na mara zote huchukua hatua mpya kwa maslahi ya wanadamu, pia ana baadhi ya tabia mbaya. Ni mbinafsi, mwenye uchu wa madaraka na mwenye kupenda raha. Anapenda fedha na unyonyaji kama tu alivyo na uwezo wa kugundua mambo mapya na kutafuta njia bora zaidi za kufanya mambo pia ana dhamana ya kutenda makosa. Lakini limbukeni na waliopotoka hawajui mambo hayo. Wanarudia mahadhi yale yale kuwa ulimwengu wa kisasa upo hivi na vile.

Kinachoshangaza zaidi ni kuwa wanalinganisha kanuni za maisha na vitu; kama vile viatu, kofia na gauni. Kwa vile vitu hivi hutafutwa na kuhitajika vinapokuwa vipya na kutupwa vinapochakaa, halikadhalika kwa mujibu wao, hali iwe hivyo hivyo kwa ukweli usiobadilika. Kwao, kizuri na kibaya havina maana zaidi ya kipya na cha zamani. Ukabaila ni mbaya kwa sababu tu ni mfumo wa zamani na umepitwa na wakati. Vinginevyo ulikuwa mzuri kabisa wakati unaanzishwa duniani kwa mara ya kwanza.

Halikadhalika unyonyaji wa wanawake ni mbaya tu kwa vile haupendwi na ulimwengu wa kisasa;

vinginevyo hadi hivi majuzi, watu hawa hawa walikuwa hawampi mgao wa urithi. Walikuwa hawajaitambua haki yake ya kumiliki mali na walikuwa hawaheshimu ridhaa na maoni yake.

Kwa mujibu wa watu hawa, katika zama hizi, zikiwa ni zama za anga (kuruka na ndege n.k), kama ilivyokuwa tu haiwezekani kusafiri kwa punda na kuacha ndege, kuwasha kibatari na kuacha umeme, kushona nguo kwa mkono na kuandika kwa mkono huku ukiacha mashine kubwa za kisasa za kuchapishia, halikadhalika haiwezekani kuacha kwenda kwenye sherehe za muziki, sherehe ambazo watu wanavaa mavazi ya kuogelea, mialiko ya chakula cha usiku chenye nyama za kubanikwa, kutoshiriki katika vicheko vya ovyo, kutocheza karata, kutovaa visketi vifupu kwani vitu vyote hivi ni mitindo ya karne hii. Wanahofu kuwa wasiposhiriki katika mambo haya watarudi nyuma katika zama za kuendesha farasi.

Wanadai kuwa hizi ni zama za nyukilia, zama za sayansi, zama za miezi ya kubuni na zama za makombora ya masafa marefu. Hili ni jambo zuri! Sisi pia tunamshukuru Mungu kuwa tunaishi katika zama hizi na tunaomba kwamba tufurahie na kufaidika na sayansi na viwanda kwa kiwango cha juu kabisa. Lakini je, mambo yote haya yanasababishwa na sayansi tu? Je, hali zote za karne hii ni matokeo ya maendeleo ya kisasa ya sayansi? Je, sayansi inadai kuwa imedhibiti mambo yote hapa duniani?

Sayansi haijawahi kudai hivyo hata siku moja. Balaa la karne yetu ni kuwa kundi la wanasayansi kwa nia njema kabisa, huitumia sayansi kufanya ugunduzi mpya, lakini kundi jingine la wabinafsi na wenye uchu wa madaraka na wanaoabudu fedha huyatumia vibaya matunda ya jasho la wanasayansi ili kuyafikia malengo yao ya kiovu. Sayansi inalalamika kuwa inatumiwa vibaya na wanaadamu wakorofi na hii ndio bahati mbaya ya kizazi chetu.

Sayansi inasonga mbele katika fani za fizikia na inagundua sheria za mwanga na kuakisi na kundi la wakorofi na wabinafsi wanaitumia kutengenezea filamu za bluu (ngono) za uharibifu na uovu. Kemia inaendelea na kugundua tabia za vitu mbali mbali na michanganyiko yake.

Baadhi ya watu wanaamua kutumia ugunduzi huu kutengeneza madawa ya kulevya, heroin ambayo ni laana kwa wanaadamu. Sayansi iligundua chanzo kizuri cha nishati ndani ya atom, lakini kabla ya ugunduzi haujatumika kwa manufaa ya wanaadamu, wenye tamaa ya madaraka walifanya haraka kutengeneza bomu la atomiki, na kuwadondoshea watu wasio na hatia.

Mapokezi yalipoandaliwa, kwa ajili ya heshima ya Einstein, mwanasayansi mkubwa wa karne ya 20, yeye mwenyewe alipanda juu ya jukwaa na kusema, “Mnampa heshima mtu ambaye amechangia kwa namna fulani kutengenezwa kwa bomu la atomiki?”

Einsten mwenyewe hakutumia elimu yake kutengeneza bomu. Ni wengine waliotumia ugunduzi wake kwa lengo hili.

Matumizi ya heroin, mabomu ya atomiki na filamu za matusi (bluu) haviwezi kuhalalishwa eti kwa madai kuwa ni mambo ya karne hii.

Ikiwa ndege za kisasa kabisa za mabomu zinatumika kurushia mambomu bora kabisa kwa watu wa nchi nyingine, na watu walioelimika sana wanaajiriwa kufanya kazi hii, je, usasa huu unaweza kupuguza ushenzi wa kurithi wa tendo hili?

Uislamu Na Usasa – lll

Hoja kuu ya wale ambao wanasema kuwa katika masuala ya haki za kifamilia tunapaswa kufuata mfumo wa Kimagharibi, ni kuwa muda umebadilika na mahitaji ya karne hii yanatutaka tufanye hivyo. Tunaonelea kuwa ni vizuri tuyaweke maoni yetu wazi juu ya nukta hii, kwa sababu bila kufanya hivyo, mjadala juu ya nukta yoyote hautakuwa kamili, ingawa kwa sababu ya uchache wa nafasi haiwezekani kulijadili suala hili kwa mitazamo yake yote, kifalsafa, kisheria, kijamii na kimaadili. Itatosheleza hapa kujadili nukta mbili tu.

Nukta ya kwanza ni kwamba kuafikiana kwayo na kukubaliana na mabadiliko ya wakati sio suala rahisi sana kama baadhi ya watu wasiojua wanavyofikiri. Mabadiliko yanayoletwa na wakati, wakati fulani huwa ni ya kurudisha maendeleo nyuma. Tunapaswa kwenda na mabadiliko ya wakati ya kimaendeleo na tunapaswa kuyapiga vita mabadiliko yanayoletwa na wakati ambayo ni ya kiharibifu. Ili kutofautisha aina hizi mbili za mabadiliko na kujua asili yake, tunapaswa kujua chanzo cha maendeleo (ugunduzi au mabadiliko) haya mapya na yameelekezwa katika mwelekeo gani. Tunapaswa kuangalia ni tabia gani za kibinadamu zimeyaleta (njema au mbaya) na ni matabaka gani ya watu yanatetea mambo haya mapya?

Tunapaswa kuangalia je yameletwa na tabia tukufu za mwanadamu au matamanio duni yanayofanana na wanyama, na kama yamekuja kama matokeo ya uchunguzi usio wa kibinafsi wa wanazuoni na wasomi, au yameletwa na matamanio duni ya wanaotumikia nafsi zao na tabia za kifisadi za jamii.

Mnyambuliko Wa Sheria Za Kiislamu

Nukta ya pili inayofaa kuwekwa wazi ni kuwa baadhi ya wasomi wa kiislamu wanaamini kuwa Uislamu una uwezo na sifa ambazo zinaupa uwezo wa kutumika zama zote. Kwa mujibu wa wasomi hawa, mafundisho ya Uislamu yanaafikiana na maendeleo ya wakati, kupanuka kwa utamaduni na matokeo ya mabadiliko haya.

Hebu tuangalie asili, sifa na uwezo huu ambao Uislamu unao. Kwa maneno mengine hebu tuangalie ni vifaa gani vimewekwa katika jengo hili la dini, na ikiwa vimeipa sifa ya kuafikiana na hali zote zinazobadilika, bila kuwa na haja ya kuacha baadhi ya mafundisho yake na bila mgogoro wowote kati ya mafundisho yake na hali yoyote inayojitokeza ya kupanuka kwa elimu na ustaarabu.

Ingawa suala hili lina sura ya kiufundi, ili kuondoa shaka shaka ya wale wanaotilia shaka ukweli huu

kuwa Uislamu una sifa hii, tunalielezea kwa kifupi hapa.

Kwa undani zaidi juu ya suala hili, wasomaji wanaweza kusoma kitabu kiitwacho '*Tanbihul Ummah'* cha hayati Ayatullah Naini au kitabu kingine kiitacho '*Marjaiyyat Wal Imama't* cha mwanazuoni mkubwa wa zama hizi Allamah Tabatabai. Lakini vitabu vyote hivi vipo katika lugha ya kifursi.

Kuna nukta nyingi, ambazo zinaunda siri ya Uislamu kuwa na uwezo wa kuafikiana na kupanuka kwa elimu na ustaarabu, na uwezo wa kutumika kwa sheria zake thabiti na imara katika hali mbali mbali za maisha. Hapa tutataja baadhi yake.

Msisitizo Katika Roho Na Kutojali Sana Kiwiliwili.

Uislamu haujashughulikia maisha ya nje (kimwili) tu ambayo hutegemea kiwango cha maendeleo ya elimu ya mwanadamu. Mafundisho ya Uislamu hushughulikia roho pia na malengo ya maisha na hutoa njia bora kabisa ya kuyafikia malengo haya. Sayansi haijabadilisha roho na malengo ya maisha wala haijapendekeza njia yoyote nzuri zaidi, fupi zaidi na salama zaidi ya kuyafikia malengo haya. Imetoa tu njia bora zaidi na vifaa vya kukwamisha njia ya kuyafikia malengo haya.

Uislamu, kwa kuhifadhi malengo tu katika himaya yake na kuacha muundo na mbinu kwenye himaya ya sayansi na teknolojia, umeepuka migongano dhidi ya utamaduni na ustaarabu. Sio hivyo tu lakini pia kwa kuhimiza mambo yanayosaidia kupanuka kwa ustaarabu, yaani elimu, kazi, uchamungu, ridhaa, ujasiri na uvumilivu bila kukata tamaa, umejitolea kuwa kigezo kikuu cha kupanua ustaarabu.

Uislamu umeweka alama za barabarani katika njia yote ya maendeleo ya mwanadamu. Alama hizi kwa upande mmoja zinaonyesha njia na kituo cha mwisho na kwa upande wa pili zinaonyesha makorongo na sehemu za hatari. Sheria zote za Kiislamu ni alama za barabara, aidha za aina ya kwanza au ya pili.

Njia za maisha katika zama hutegemea juu ya kiwango cha elimu ya wanaadamu. Kwa kadri elimu ya watu inavyopanuka, ndivyo njia bora zaidi za kujipatia kipato zinavyotokea na moja kwa moja zinachukua nafasi ya zile njia duni (za zamani).

Mifumo ya nje na ya kimaada ya njia hizi (za kupatia riziki) haina utakatifu katika Uislamu, na Waislamu hawalazimiki kuzidumisha.

Uislamu haujasema kifaa hiki na kile kitumike kwa ushonaji, ususi, kilimo, usafiri, vita au kazi nyingine. Hivyo hapawezi kuwa mgogoro wowote kati ya sayansi na Uislamu, pindi kifaa kinapopitiwa na wakati, cha kisasa zaidi kinaweza kutumika badala yake. Uislamu haujaagiza kutumika kwa mtindo maalum ya viatu au nguo, wala haujapendekeza aina fulani ya ujenzi wa majengo. Halikadhalika hauhimizi juu ya mbinu fulani fulani za uzalishaji na ugavi.

Hii ni moja ya sifa hizo za Uislamu, ambazo zimeuwezesha kuweza kutumika katika maendeleo yote ya wakati.

Sheria Madhubuti Kwa Mahitaji Madhubuti

Na Sheria Zinazobadilika Kwa Mahitaji Yanayobadilika.

Sifa nyingine ya Uislamu, ambayo ina umuhimu mkubwa ni kuwa umeweka sheria madhubuti (zisizobadilika) kwa ajili ya mahitaji madhubuti (yasiyobadilika) na sheria zinazobadilika kwa mahitaji yanayobadilika. Mbali na mahitaji ya wanaadamu, mahitaji ya mtu mmoja mmoja na vikundi, yote yana asili ya kudumu. Hayabadiliki kwa mujibu wa wakati. Kanuni za mifumo inayotawala silika za binadamu na mahusiano ya kijamii hazibadiliki.

Tunazijua nadharia za 'Maadili husianishi' na 'Uadilifu husianishi' ambazo zina wafuasi wake, na tutatoa maoni yetu kuhusiana nao baadaye.

Sehemu nyingine ya mahitaji ya mwanadamu ni ile ya mahitaji yanayobadilika, na hii huhitaji sheria zinazobadilika. Uislamu ulishayaona mahitaji hayo na umeyaunganisha na kanuni fulani ambazo zina sheria ndogo zinazobadilika kila hali inapobadilika.

Kufafanua nukta hii hebu tuangalie mifano hii;

وَأَعِدُّوا لَهُمْ مَا اسْتَطَعْتُمْ

'**Andaeni majeshi kwa ajili yao** (**maadui**)' (***Suratul Anfal 8:60***.)

Wakati huo huo tunasoma hadith kadhaa za Mtume katika vitabu vya sheria za Kiislamu chini ya kichwa cha habari 'Kuendesha farasi na kurusha mishale.' Mtume aliwaelekeza Waislamu wajifunze kuendesha farasi na kurusha mishale na wawafundishe watoto wao pia. Haya yalikuwa ni sehemu ya mafunzo ya Kiislamu katika zama hizo.

Ni dhahiri kabisa hapa kuwa amri ya msingi ni 'Kuandaa majeshi.' Upinde na mshale, jambia na mkuki na farasi sio vya muhimu. Kilicho cha muhimu ni kuwa imara kijeshi dhidi ya maadui. Kuandaa majeshi ni amri ya kudumu ambayo imetokana na hitajio la kudumu.

Hata hivyo ulazima wa kupata ujuzi katika kuendesha farasi na kurusha mishale sio wa kudumu, na hubadilika kutokana na wakati. Kutokana na kubadilika kwa hali, ujuzi wa kufyatua risasi umechukua nafasi ya kurusha mishale.

Mfano mwingine ni sheria ya kijamii inayohusu kubadilishana mali, iliyotajwa katika Qur'ani. Uislamu umetambua kanuni ya umiliki wa mali wa mtu binafsi. Hata hivyo umiliki huu unaotambuliwa na Uislamu ni tofauti na ule uliopo katika nchi za kibepari. Tabia ya umiliki wa mali wa watu binafsi katika Uislamu ni kanuni ya kubadilishana.

Kwa utaratibu huu Uislamu umeweka sheria fulani. Mojawapo imeelezwa na Qur'ani Tukufu katika maneno haya

وَلَا تَأْكُلُوا أَمْوَالَكُمْ بَيْنَكُمْ بِالْبَاطِلِ

'Na msile mali zenu (kila mmoja kula za mwenzake) kwa batili' (*Suratul Baqarah, 2:188*).

Kwa maneno mengine katika mauzo ya biashara, fedha isitoke mkono mmoja kwenda mwingine isipokuwa kwa kubadilishana na kitu kingine cha halali chenye kuwa na mamlaka ya mwisho juu ya mali hiyo.

Imelezwa na kufafanuliwa katika sheria ya Kiislamu mauzo na manunuzi ya vitu fulani yamekatazwa. Vitu hivyo ni pamoja na damu na kinyesi cha binadamu. Sababu ni kuwa vitu hivi havina thamani inayoviwezesha kuhesabika kuwa sehemu ya mali ya mwanadamu. Kanuni hii ni sawa ya mali ya mwanadamu. Kanuni hii ni sawa na ile iliyo katika Aya iliyonukuliwa hapo juu. Ubatili wa mauzo na manunuzi ya damu na kinyesi cha binaadamu ni sehemu au mfano tu wa matumizi ya kanuni hiyo. Hata kama hakuna ubadilishaji uliofanyika, (wa bidhaa au bidhaa kwa fedha) fedha au mali inayomilikiwa na mtu fulani haiwezi kufujwa au kuliwa bure.

Sheria inayokataza kula mali ya mtu mwingine bure (bila kufanya kazi) au kiwizi ni kanuni madhubuti na inatumika zama zote, na imetokana na hitajio la kudumu la jamii. Lakini kanuni kuwa damu na kinyesi cha binadamu havihesabiki kama mali na haviruhusiwi kuuzwa, inahuisiana na wakati na kiwango cha ustaarabu. Kanuni hii inaweza kubadilishwa kutokana na mabadiliko ya hali, maendeleo ya sayansi na viwanda na uwezekano wa kuzitumia bidhaa hizi katika namna sahihi na yenye manufaa.

Mfano mwingine; "Imam Ali (a.s) hakuwahi kuweka dawa kwenye nywele zake hata siku moja, ingawa zilikuwa zimekuwa za mvi katika miaka ya mwisho ya uhai wake. Siku moja mtu mmoja alimwambia, 'Je Mtume hakuamrisha nywele za mvi ziwekwe dawa?"

Ali alijibu 'Ndiyo aliamrisha' Sasa kwa nini huweki dawa kwenye nywele zako? Yule mtu aliuliza. Ali akasema; "Katika wakati ule ambao Mtume alitoa maelekezo haya, idadi ya Waislamu ilikuwa ndogo na kulikuwa wazee wengi waliokuwa wakishiriki vitani. Mtume aliwaamrisha wazipake dawa ili kuficha umri wao halisi, kwani kama adui angeona kuwa anapambana na kundi la wazee tu, hamasa yake ingeongezeka. Kwa kuwa Uislamu umeenea dunia yote, hali imebadilika. Kila mtu yupo huru kupaka dawa nywele zake au kuacha."

Kwa maoni ya Imamu Ali, maelekezo ya Mtume hayakuwa ya kudumu wala haikuwa sheria ya kudumu. Uislamu unajali muonekano wa nje na roho ya ndani pia. Lakini unataka pumba kwa ajili ya punje yenyewe na unataka nguo kwa ajili ya mwili.

Suala La Kubadilisha Herufi

Katika siku za hivi karibuni hapa Iran kumekuwa na ubishani juu ya kubadlisha herufi. Suala hili linaweza kuangaliwa katika pande mbili kwa mtazamo wa kanuni za Kiislamu, na kwa sura mbili. Kwanza ni iwapo Uislamu unapendelea herufi fulani na kuzibagua nyingine. Je Uislamu unaziona herufi za sasa, ambazo ni za Kiarabu, kama zake, na herufi nyinginezo kama zile za kilatini zinazoonekana ni za kigeni? Uislamu ambao ni dini ya ulimwengu mzima unaziona herufi zote duniani kuwa ni sawa.

Sura ya pili ni kuwa kiasi gani kubadilika kwa herufi kutachanganya utamaduni wa Taifa la Kiislamu na watu wengine na kutakuwa na madhara gani kwa utamaduni wa taifa hili. Na zaidi ya hayo, katika karne 14 zilizopita, vitabu vya Kiislamu na kisayansi vilivyozalishwa na Irani vimeandikwa katika herufi za sasa (za kiarabu), je kubadilisha herufi si kutazifuta (haribu) kazi zote hizi? Swali jingine ni, 'Ni akina nani wanaopendekeza mabadiliko haya, na ni akina nani watakaoyatekeleza? Maswali yote haya ni thabiti.'

Kuwategemea Wengine Ndio Kumekatazwa, Sio Kofia Ya Kizungu

Watu kama mimi mara nyingi wanakumbana na maswali, yanayoulizwa kwa dharau au kejeli. "Sheria ya Kiislamu inasemaje kuhusu kula ukiwa umesimama?' Ni vipi kuhusu kula kwa kijiko au uma?' Je kuvaa kofia ya kizungu kumekatazwa?' Je kutumia lugha za kigeni kumekatazwa?'"

Katika kujibu maswali haya, tunasema kuwa Uislamu haujatoa maelekezo yoyote mahsusi juu ya hili. Uislamu haujawaelekeza wafuasi wake kula kwa mkono au kijiko. Ulichowaelekeza ni kuzingatia usafi. Uislamu haujaelekeza matumizi ya mitindo ya aina fulani ya viatu, kofia au nguo. Kwa mtazamo wa Uislamu lugha zote Kiingereza, Kijapani, Kifursi, zina hadhi sawa.

Hata hivyo, Uislamu unasema kitu fulani zaidi. Umesema kuwa imekatazwa mtu kupoteza utambulisho wake. Kuwaogopa wengine bila ulazima kumekatazwa, Kuwaiga wengine kumekatazwa, kuchekeshwa na kuvutiwa na wengine kama sungura anavyovutiwa na nyoka, kumekatazwa. Kumchukulia punda mgeni aliyekufa kuwa ni farasi kumekatazwa. Kuingiza nchini upotofu na ukosefu wa maadili kutoka nje, kwa madai ni mambo ya kisasa ya karne hii, kumekatazwa. Kuamini kuwa Waislamu wanapaswa kufuata mila na utamaduni wa Kimagharibi ndani na nje, kimwili na kiroho, kumekatazwa. Kwenda nchi ya Kimagharibi kwa siku chache na baada ya kurudi, unaanza kutamka maneno yetu kama wao (wazungu) kumekatazwa.

Muhimu Na Muhimu Zaidi.

Sura nyingine ya Uislamu inayoufanya uende na mahitaji ya wakati ni kukubaliana kwa mafundisho yake na akili/mantiki. Uislamu umetangaza kuwa sheria zake zimezingatia maslahi makubwa zaidi. Na wakati huo huo, Uislamu wenyewe umetoa madaraja mbali mbali ya umuhimu wa maslahi haya. Hii

inarahisisha kazi ya wataalamu wa sheria za Kiislamu katika fani hizo ambapo maslahi tofauti yanaonekana kugongana.

Katika hali hizo, Uislamu umewaruhusu wataalamu wa sheria za Kiislamu kupima uzito wa maslahi tofauti, na kuzingatia mwongozo ambao Uislamu wenyewe umetoa, katika kuangalia ni maslahi gani hilo ni muhimu zaidi. Katika fani ya sheria za Kiislamu, hii huitwa suala la “muhimu na muhimu zaidi.” Kuna mifano mingi ambapo kanuni hii ya maslahi ya juu na ya juu zaidi imepata kutumika. Hata hivyo kwa sababu ya uchache wa nafasi, tunairuka sehemu hii

Sheria Yenye Haki Ya Turufu.

Sifa nyingine ya Uislamu ambayo imeipa dini hii uwezo wa kuhamishika na kutumika katika hali mbali mbali na imeifanya kuwa dini inayoishi na ya kudumu milele ni kuwa ndani yake kuna chombo cha sheria ambacho kazi yake ni kudhibiti na kurekebisha sheria nyingine. Mafakihi wanaziita kanuni hizi kuwa ni “ kanuni za kuongozea.”

Kanuni ya ‘Hakuna madhara’ na ‘Hakuna hasara’ kwamba sheria haitatumika pale ambapo inaweza kusababisha ugumu au madhara kwa maslahi ya mtu asiye na hatia, imeuenea (imeutawala) mfumo mzima wa kisheria. Lengo la kanuni hizi ni kudhibiti na kurekebisha sheria nyingine. Kwa kusema kweli Uislamu umezipa nguvu ya turufu kanuni hizi ambazo hubadilisha kanuni nyingine.

Madaraka Ya Mtawala

Kwa nyongeza kuna mfululizo mwingine wa kanuni za kuweka mambo katika mizania ambazo Mwenyezi Mungu ameipa dini hii ya mwisho. Ayatullah Na’ini na Allamah Tabatabai, juu ya hili, wametegemea madaraka ambayo Uislamu umeipa serikali ongofu ya Kiislamu.

Kanuni Ya Ijtihadi

Mshairi na mwanafalsafa wa Kipakistani anasema kuwa Ijtihadi (kuzalisha sheria kutoka vyanzo vyake vya asili) ni nguvu ya hamasa ya Uislamu. Yuko sawa kusema hivyo. Lakini kilicho muhimu zaidi ni kuwa Uislamu una sifa maalum ya kuruhusu Ijtihadi. Hakuna dini nyingine yenye sifa hii katika namna hii hii. Jengo la ndani la Uislamu limejengwa katika namna ambayo kwa msaada wa Ijtihadi, unaweza mara zote kwenda na mahitaji yanayobadilika katika maisha.

Abu Ali Ibn Sina (Avicenna) katika kitabu chake *AlShifa*, ameelezea haja ya Ijtihadi kuwa inatokana na kubadilika kila mara kwa mahitaji. Anasema kuwa hali za maisha mara zote zinabadilika. Matatizo mapya yanaibuka kila mara, lakini misingi ya Uislamu haibadiliki. Hivyo katika hali hii, lazima wawepo watu wanaojua sheria za kiislamu vizuri na mafundisho ya Kiislamu vizuri ili waweze kujibu maswali yote yanayoibuka katika kila zama na hivyo kukidhi mahitaji ya wakati.

Katiba ya Iran inaamuru kuwa pawepo chombo cha mujtahidi wasiopungua watano (wanazuoni wakubwa wa Theolojia wanaoweza kufanya ijtihadi) kitakachokuwa kikichunguza sheria zinazopitishwa na serikali kila wakati.

Lengo hapa ni kuwa watu hawa (mujtahidi) kwa vile sio wapinga mabadiliko wala hawapingi maendeleo ya kisasa, wala sio limbukeni wala hawawafuati wengine kibubusa, waangalie na kudhibiti mfumo wa sheria wa nchi.

Inapaswa kueleza kuwa ijtihad kwa namna halisi ina maana kubobea na inahitaji uelewa wa ndani sana wa misingi ya Uislamu na nguzo zake na elimu kubwa kabisa ya kanuni za fikihi ya Kiislamu, ambayo si kila mtu aliyesoma Uislamu kwa muda fulani anaweza kudai kuwa mujtahid.

Hapana shaka kuwa hii ni kazi ya umri mzima wa mtu ili kubobea katika kanuni na mafundisho ya Uislamu, na mbali na kipaji, nia na akili, inahitaji pia msaada wa Mungu.

Mbali na kubobea (kwenye mchepuo maalum) na Ijtihad, baadhi ya watu wanaweza kupata elimu na kufikia kiasi kwamba maoni yao yanaweza kuchukuliwa kuwa ni *fatwa*. Historia ya Uislamu inawataja watu hao ambao licha ya elimu yao kubwa na maadili yao ya hali ya juu walikuwa na hadhari kubwa, walipokuwa wakitoa maoni yao, juu ya masuala ya kisheria.

Mwanamke Katika Qur'ani

Sasa tunataka kujibu swali iwapo Uislamu unamtazama mwanamke kuwa ni sawa na mwanaume kama binadamu au unamuona ni wa hadhi ya chini kuliko mwanaume.

Falsafa Maalum Ya Uislamu Juu Ya Haki Za Kifamilia.

Kuhusiana na haki za mwanaume na mwanamke, Uislamu, una falsafa yake maalum ambayo ni tofauti, yale yaliyotokea miaka 1400 iliyopita na yanayotokea hivi sasa. Uislamu hauamini kuwa katika mambo yote mwanaume na mwanamke wana haki na majukumu yanayofanana. Katika mambo fulani haki na majukumu yao ni tofauti na matokeo yake ni kuwa katika baadhi ya mambo nafasi yao inafanana na ya wanaume na katika baadhi ya mambo haifanani na ya wanaume.

Hii sio kwa sababu Uislamu, kama falsafa nyingine, unamtazama mwanamke kwa dharau au jinsia yake sio bora kama ya mwanaume. Uislamu unazitofautisha jinsia hizi mbili kwa sababu nyinginezo za msingi.

Unaweza kuwasikia wafuasi wa mifumo ya Kimagharibi wakitaja kanuni za Kiislamu kama vile mahari, matunzo, talaka, ndoa za mitala na mengineyo, kuwa haya yote ni kama matusi kwa mwanamke na

yanashusha hadhi yake. Wanawapotosha watu kuwa sheria na kanuni hizi hazina maana na ulazima na zinamfanya mwanaume aonekane ni bwana mkubwa.

Wanasema kwamba katika kipindi chote cha historia, kabla ya karne ya 20, sheria na kanuni zote duniani ziliwekwa kwa kuzingatia kuwa mwanaume ni mwenye jinsia bora zaidi na kwamba mwanamke aliumbwa kwa maslahi na starehe ya mwanaume. Sheria zilizopitishwa na Uislamu pia ziko hivyo hivyo, zinampendelea mwanaume.

Wanadai kuwa Uislamu ni dini ya jinsia ya kiume. Hawamtambui mwanamke kuwa ni binadamu kamili. Hii ndio sababu haujampa haki sawa na mwanaume. Ungekuwa unamtambua kuwa ni binadamu kamili usingeruhusu ndoa za mitala (mke zaidi ya mmoja), usingehesabu ushahidi wa wanawake wawili kuwa ni sawa na wa mwanaume mmoja, usingeamuru gawio la mwanamke liwe nusu ya gawio la mwanaume, usingeamrisha papangwe bei ya mwanamke chini ya kivuli cha mahari na usingemfanya mwanamke awe tegemezi kwa mwanaume kwa upande wa matunzo, badala ya kufanya ajitegemee kiuchumi na kijamii.

Kwa kuzingatia yote haya ni dhahiri kuwa mafundisho ya Uislamu yanamtazama mwanamke kwa jicho la dharau. Uislamu unadai kuwa dini ya usawa lakini, katika mahusiano ya kifamilia hakuna usawa wowote uliozingatiwa.

Wanashikilia kuwa katika suala la haki, Uislamu wazi wazi unampendelea mwanaume na ndio maana umempa miliki zote hizi.

Tukipenda tunaweza kuweka hoja yao katika muundo wa kimantiki kuwa: Kama Uislamu unamhesabu mwanamke kuwa ni binadamu kamili ungekuwa umempa haki sawa na zinazofanana na zile za mwanaume, maadamu haujafanya hivyo basi haumhesabu kuwa ni binadamu kamili.

Usawa Au Kufanana?

Hoja hii imejengwa juu ya msingi kwamba kwa vile heshima ya binaadamu ni sawa kwa mwanaume na mwanamke, hivyo lazima wote wapate haki zinazofanana bila kujali majukumu yao katika maisha. Hapana shaka, utu na heshima yao ni sawa kwao wao wote; wote wanapaswa kuwa na haki sawa. Lakini vipi kuhusu kufanana kwa haki zao?

Ikiwa badala ya kufuata kibubusa mawazo ya Kimagharibi tutaamua kufikiri sisi wenyewe, swali la kwanza linalokuja akilini ni iwapo kweli haki sawa zinamaanisha haki zinazofanana. Kwa kweli hayo ni mambo mawili tofauti. Usawa ni haki ya kuwa na daraja sawa kithamani na hadhi ambapo kufanana maana yake ni kulandana. Inawezekana baba akagawa mali zake kwa watoto wake watatu kwa usawa lakini sio kwa kulingana.

Jaalia mali yake inajumuisha vitu mbali mbali kama vile maduka, mashamba na badhi ya mali zilizokodishwa. Baba kwa kuzingatia vipaji vyao na mambo ambayo kila mmoja anapenda, anaamua

kumpa mmoja duka, mwingine shamba na wa tatu mali zilizokodishwa. Anazingatia kuwa thamani ya mali aliyopewa kila mmoja wao ni sawa na wengine na kila mmoja amepewa kutokana na kipaji chake. Hivyo aligawa mali yake kwa usawa lakini sio kwa kulingana.

Uwingi ni tofauti na ubora, na usawa ni tofauti na kufanana. Uislamu hauamini juu ya kulingana (*uniformity*) kwa mwanaume na mwanamke. Lakini wakati huo huo hauwapendelei wanaume katika maswala ya haki. Umezingatia kanuni ya usawa kati ya mwanamke na mwanaume lakini haukubaliani na kufanana kwa haki zao.

Usawa ni neno linalifurahisha, kwa sababu linaashiria hali ya kutobagua. Lina utukufu maalum. Linaamsha na kuleta heshima, hasa linapohusiana na haki.

Ni neno zuri lilioje 'Usawa na Haki.' Mtu yeyote mwema atafurahishwa na uzuri wake.

Lakini hatuwezi tukaelewa ni kwa jinsi gani mambo yalifika hatua hii kiasi cha kuwa wengine ambao walikuwa vinara wa sayansi na falsafa nao wanataka kuingiza mawazo yao juu ya kufanana kwa haki kati ya wanawake na wanaume huku kwetu.

Hii ni sawa na mtu kuuza viazi vitamu kwa jina la mapeasi.

Hapana shaka kuwa Uislamu haujatoa haki zinazofanana kati ya mwanaume na mwanamke katika mambo yote. Lakini pia haujaamuru majukumu na adhabu zinazofanana kwa jinsia hizi mbili. Yote kwa yote ni kuwa thamani ya jumla ya haki za mwanamke sio ndogo kuliko ile ya mwanaume. Tunataka kuthibitisha nukta hii.

Hapa linazuka swali, kwa nini haki za mwanaume na mwanamke hazijafanana katika mambo yote. Je isingekuwa vizuri zaidi kama haki zao zingekuwa zinafanana katika mambo yote? Ili kulijadili hili swali kikamilifu, tutajadili chini ya vichwa vya habari vitatu.

Mtazamo wa Uislamu juu ya nafasi ya mwanamke kutokana na maumbile yake.

Athari za tofauti za kimwili kati ya mwanaume na mwanamke. Je, hili linasababisha tofauti ya haki zao pia?

Ni nini falsafa ya sheria za Kiislamu, ambazo wakati fulani zinatofautisha kati ya mwanaume na mwanamke? Je falsafa hii bado ni thabiti?

Nafasi Ya Mwanamke Katika Utaratibu Wa Kiislamu.

Qur'ani sio mkusanyiko tu wa sheria. Sio chombo cha sheria na kanuni kavu bila maelezo ya madhumuni yake. Ina sheria na pia ina historia, mawaidha ya kidini, maelezo ya malengo ya maisha, na maelfu ya mambo mengine katika sehemu mbalimbali, Qur'ani huelezea mambo yenye sura ya kisheria na katika sehemu nyingine hueleza lengo la maisha. Hufunua siri za dunia, mbingu, mimea, wanyama

na wanaadamu. Huelezea siri za maisha na kifo, heshima na aibu, kupanda na kushuka, mali na umaskini.

Qur'ani sio kitabu cha falsafa, lakini kimeelezea kwa ufasaha sana maoni yake (Qur'ani) juu ya falsafa ya masomo matatu ya msingi; Ulimwengu, mwanadamu na jamii. Haiwafundishi wafuasi wake sheria peke yake, na haijishughulishi na mawaidha na nasaha (maonyo) peke yake, bali kwa kupitia tafsiri yake ya maisha (maumbile), huwapa wafuasi wake mtazamo maalum na namna pekee ya kufikiri. Msingi wa kanuni za Kiislamu juu ya masuala ya kijamii kama vile umiliki, serikali, haki za kifamilia n.k ni tafsiri ya maisha na mambo mengine tofauti tofauti.

Moja ya mambo yaliyoelezwa katika Qur'ani ni kuumbwa kwa mwanaume na mwanamke. Qur'ani haijakaa kimya juu ya jambo hili. Haijaacha mwanya kwa wadukuzi wa kifalsafa kuibua falsafa yao juu ya kanuni za mwanaume na mwanamke. Uislamu umetoa maoni yake juu ya mwanamke.

Ili kujua maoni ya Uislamu juu ya mwanamke, tutazame Qur'ani inachosema juu ya tabia yake ya ndani. Dini nyingine pia zimelizungumzia suala hili, lakini ni Qur'ani peke yake ambayo katika Aya kadhaa inaelezea wazi wazi kuwa mwanamke ameumbwa kutokana na *spishi* za mwanaume, na wote mwanamke na mwanaume wana tabia za ndani zinazofanana. Akimzungumzia Adam, Mwenyezi Mungu anasema;

الَّذِي خَلَقَكُمْ مِنْ نَفْسٍ وَاحِدَةٍ وَخَلَقَ مِنْهَا زَوْجَهَا

"Yeye (Allah) aliwaumba nyinyi wote kutokana na nafsi moja, na kutokana nayo (hiyo nafsi moja) akamuumbia mwenza wake (*SuratunNisaa 4:1*).

Na juu ya mwanadamu kwa ujumla, Qur'ani inasema; **"Amewaumbieni wake zenu kutokana na nyinyi.' (*Suratul Nisaa, Suratul Aali Imran na Suratul Ruum*).**

Tofauti na vitabu vingine vya kidini hakuna sehemu yoyote katika Qur'ani ambapo imetajwa kuwa mwanamke ameumbwa kwa kutumia vitu duni au kuwa ana asili ya ukupe au ni wa asili ya upande wa kushoto. Uislamu hauungi mkono dhana ya kibiblia kuwa mwanamke ameumbwa kutokana na ubavu wa kushoto wa Adam. Uislamu hauna mtazamo wa dharau juu ya asili ya mwanamke na tabia zake za ndani.

Kuna nadharia nyingine ya dharau kwa wanawake iliyokuwa imeenea sana siku za nyuma, na imeacha alama mbaya katika siku za nyuma, na imeacha alama mbaya katika fasihi ya dunia. Kwa mujibu wa nadharia hiyo mwanamke ndio chanzo cha madhambi yote. Kuwepo kwake tu kunahamasisha uovu. Mwanamke ni shetani mdogo. Inasemekana kuwa katika kila dhambi na uhalifu uliotendwa na mwanaume kuna mkono wa mwanamke. Wanaume wenyewe hawatendi madhambi, ni wanawake wanaowasukumia kwenye madhambi.

Pia inasemekana kuwa shetani hawezi kumwendea mwanaume moja kwa moja. Ni kupitia mwanamke ndio huwapotosha wanaume. Shetani humchochea mwanamke na mwanamke humchochea mwanaume. Adam aliondolewa peponi kwa sababu ya mwanamke. Shetani alimshawishi Hawa, na ni Hawa aliyemshawishi Adam.

Qur'ani imesimulia kisa hiki cha peponi lakini hakuna iliposema kuwa shetani au nyoka alipompotosha Hawa na Hawa akampotosha Adam. Haimlaumu Hawa wala haimuondoi katika hatia.

Qur'ani inasema;

وَقُلْنَا يَا آدَمُ اسْكُنْ أَنْتَ وَزَوْجُكَ الْجَنَّةَ وَكُلَا مِنْهَا رَغَدًا حَيْثُ شِئْتُمَا وَلَا تَقْرَبَا هَٰذِهِ الشَّجَرَةَ فَتَكُونَا مِنَ الظَّالِمِينَ

"Tulimwambia Adam, 'Kaa Peponi; wewe na mke wako, na kuleni humo matunda popote mpendapo lakini msiusogelee mti ule msije kuwa miongoni mwa madhalimu." (***Suratul Baqara, 2:35***).

Inaweka kiwakilishi cha watu wawili. Pia Qur'ani inasema;

فَوَسْوَسَ لَهُمَا الشَّيْطَانُ قَاسَمَهُمَا إِنِّي لَكُمَا لَمِنَ النَّاصِحِينَ

"Kisha Shetani aliwatia wasiwasi." "Naye akawaapia (kuwaambia) kwa hakika mimi ni mmoja wa watoao shauri njema kwenu. (***Suratul Aaraf 7:20–21***).

Hivyo Qur'ani inapinga vikali dhana ya uongo iliyokuwa imeenea sana wakati wa kuteremshwa Qur'ani na miwangwi ambayo bado inasikika katika sehemu mbali mbali za dunia hii leo. Ilimuondoa mwanamke katika mashitaka kwamba yeye ni mchochezi wa dhambi na kwamba yeye ni shetani mdogo.

Nadharia nyingine ya dharau kwa mwanamke ambayo imekuwepo ni juu ya nafasi ya kiroho ya mwanamke. Ilidaiwa kuwa mwanamke hawezi kuingia peponi. Hana uwezo wa kiroho na msaada wa Mungu kumuwezesha kufanya hivyo. Hana uwezo wa kufikia ukaribu wa Mwenyezi Mungu kama mwanaume anavyoweza kufanya.

Lakini Qur'ani katika Aya mbali mbali imesema wazi wazi kuwa malipo ya pepo na ukaribu na Mwenyezi Mungu havitegemei jinsia ya mtu. Inategemea na imani na amali (vitendo), na hakuna tofauti kati ya mwanamke na mwanaume juu ya hili katika Qur'ani, wametajwa watakatifu wa kiume na watakatifu wa kike. Qur'ani imewatukuza wake wa Adam na Ibrahim na mama yake Nabii Isa na Musa.

Imewataja wake wa Nuhu na Lut kuwa hawakuwa stahili ya waume zao na haijamshahau mke wa Firauni ambaye ametajwa kuwa ni mwanamke mtukufu aliyekuwa mikononi mwa mwanaume muovu. Katika visa vyake Qur'ani imeweka mizania. Mashujaa wake ni wa kiume na wa kike.

Wakati, ikimzungumzia mama yake Nabii Musa, Qur'ani inasema, "Tulimjulisha mama yake Musa kwa kumwambia:

أَنِ اقْذِفِيهِ فِي التَّابُوتِ فَاقْذِفِيهِ فِي الْيَمِّ فَلْيُلْقِهِ الْيَمُّ بِالسَّاحِلِ يَأْخُذْهُ

'**Muweke katika sanduku na mtupe katika mto. Mawimbi yatamfikisha ufukweni.** (***Suratul Taha 20:39***).

Juu ya mama yake Issa, Qur'ani inasema kuwa alifikia daraja tukufu ya kiroho kiasi kwamba malaika walikuwa wakiongea naye wakati anasali. Alikuwa akipokea chakula kutoka peponoi. Daraja la kiroho lilimshangaza hata Zakaria, Mtume wa wakati huo.

Kumekuwa na mifano mingi ya wanawake mashuhuri na watakatifu katika historia ya Uislamu. Ni wanaume wachache tu wanaweza kufikia daraja la Khadija, mke kipenzi wa Mtume (s.a.w.w) na hakuna mwanaume anayefikia daraja la bibi Fatima Zahra, binti kipenzi wa Mtume isipokuwa Mtume mwenyewe na Imam Ali (a.s). Ana daraja kubwa kuliko hata la watoto wake ambao ni Maimamu, na hata la Mitume wote isipokuwa Mtume wa mwisho.

Uislamu hauwabagui wanawake dhidi ya wanaume katika 'safari ya kumuendea Allah' isipokuwa humuona mwanaume kuwa mwenye kufaa zaidi kuchukua jukumu la utume, ambalo yaweza kuelezewa kama safari ya kurudi kutoka kwa Mwenyezi Mungu kwenda kwa watu.

Nadharia nyingine ya dharau kwa wanawake inahusiana na kujihini na kutooa/kutoolewa. Baadhi ya dini zinaona kuwa tendo la ndoa ni kitu kichafu, kwa mujibu wa imani ya wafuasi wake, wanaoweza kufikia kilele cha juu cha daraja la kiroho ni wale tu ambao watamaliza maisha yao yote bila kuoa/kuolewa.

Kiongozi mmoja wa dunia wa kidini anasema, "Kateni mti wa ndoa kwa shoka ya ubikira.' Viongozi hawa wa kidini wanavumilia ndoa tu kama uovu wenye nafuu. Kwa maneno mengine wanashikilia kuwa kwa kuwa watu wengi hawawezi maisha ya bila kuoa/kuolewa na inaeleweka kwamba hawataweza kujidhibiti na hivyo kujiingiza katika zinaa za wanawake/wanaume wengi, basi ni bora waoe ili wasije kukutana na mwanamke zaidi ya mmoja. Watu hawa wanatetea kukaa bila kuoa au kuolewa na kujihini kwa sababu wanaona tendo la ndoa si kitu kizuri. Wanaona upendo kwa mwanamke kuwa ni uovu mkubwa wa kimaadili.

Uislamu unapinga vikali upuuzi huu. Unaiona ndoa kuwa ni taasisi tukufu na kukaa bila kuoa/kuolewa kuwa ni uchafu. Kumpenda mwanamke ni sehemu ya tabia ya Mtume. Mtukutu Mtume amesema;

“Napenda vitu vitatu, manukato, mwanamke na swala.”

Bertrand Russel anasema, “Dini zote, isipokuwa Uislamu, zinalitazama tendo la ndoa kwa jicho baya. Uislamu unalitazama kwa maslahi ya kijamii, umeliwekea utaratibu maalum na kulidhibiti, lakini haulitazami kama uchafu.”

Nadharia nyingine ya dharau kwa mwanamke ni kuwa mwanamke ameumbwa kwa maslahi ya mwanaume.

Uislamu hausemi hivyo. Umeeleza malengo ya maisha kwa uwazi kabisa. Imeeleza kuwa dunia, mbingu, hewa, mawingu, mimea na wanyama vyote vimeumbwa kwa ajili ya mwanadamu. Haijasema mwanamke ameumbwa kwa ajili ya mwanaume. Kwa mujibu wa Qur’ani mwanaume ameumbwa kwa ajili ya mwanamke na mwanamke ameumbwa kwa ajili ya mwanaume.

هُنَّ لِبَاسٌ لَكُمْ وَأَنْتُمْ لِبَاسٌ لَهُنَّ ؟

‘Wao (wanawake) ni nguo zenu na nyinyi (wanaume) ni nguo zao (2:187).

Ingekuwa Qur’ani imeeleza kuwa mwanamke ni nyongeza (kiambatanisho) ya mwanaume na aliumbwa kwa ajili ya starehe yake (mwanaume) mtazamo huu ungekuwa umetazamwa katika sheria za Kiislamu, lakini Qur’ani haijasema hivyo. Hauyaelezei malengo ya maisha hivi. Haumuoni mwanamke kuwa ni kiambatanisho tu cha mwanaume. Ndio maana mtazamo huu haujazingatiwa katika sheria za Kiislamu.

Nadharia nyingine ya dharau kwa mwanamke ni kuwa mwanamke ni uovu usioepukika. Katika siku za nyuma, watu walimtazama mwanamke kwa dharau sana na walimuona kuwa ni chanzo cha mikosi na aina zote za matatizo. Kinyume chake Qur’ani imesisitiza kuwa mwanamke ni baraka kwa mwanaume na ni chanzo cha raha na faraja kwake.

Kwa mujibu wa nadharia nyingine ya dharau kwa mwanamke ni kuwa hawakuthamini mchango wa mwanamke katika uzazi. Waarabu wa kabla ya Uislamu na baadhi ya jamii nyingine waliomuona mwanamke kama mfuko tu wa kukuzia mbegu ya mwanaume. Sehemu mbali mbali ya Qur’ani imesema **‘Tumewaumba kutokanana na mwanaume na mwanamke.’** Wazo hili limeelezwa katika Aya nyingine za Qur’ani. Hivyo Uislamu ulikomesha fikra hiyo kuwa mwanamke ni mfuko tu wa kukuzia mbegu ya mwanaume.

Ni dhahiri sasa kuwa Uislamu hauna kabisa mitazamo yoyote ya kumdharau mwanamke.

Sasa muda umefika wa kueleza kwa nini haki za mwanaume na mwanamke hazifanani.

Ni Kufanana, Hapana, Ni Kulingana, Sawa.

Tayari tumeshasema kuwa katika suala la mahusiano ya kifamilia na haki za mwanamke na mwanaume, Uislamu una falsafa yake ambayo ni tofauti kabisa na ile iliyokuwa ada (kawaida), miaka 1400 iliyopita na ilivyo sasa.

Pia tumesema kuwa hakuna ubishi wowote kuwa mwanaume na mwanamke ni sawa kama binadamu na haki zao za kifamilia zinapaswa kuwa sawa kithamani. Kwa mtazamo wa Uislamu wao wote ni binadamu na hivyo wana haki sawa.

Nukta inayopaswa kuangaliwa hapa ni kuwa mwanaume na mwanamke, kwa sababu ya tofauti zao za kijinsia, wanatofautiana katika mambo mengi. Asili yao haitaki wafanane. Nafasi hii inataka wasifanane katika haki nyingi, majukumu, wajibu na adhabu. Katika nchi za Magharibi jitihada inafanyika sasa kuzifanya haki na majukumu yao kufanana, na kupuuza tofauti zao za asili na za ndani. Hapa ndio kuna tofauti kati ya mtazamo wa Kiislamu na mfumo wa Kimagharibi katika nchi yetu, nukta inayobishaniwa ni suala la kufanana kwa haki sio usawa wa haki kati ya mwanamke na mwanaume. Usawa wa haki ni nembo tu ambayo imewekwa kwa makosa katika zawadi hii ya Kimagharibi.

Mwandishi wa kitabu hiki katika vitabu na hotuba zake mara zote amejiepusha kutumia nembo hii ya uongo na kamwe hajakubali kulipa jina la usawa jambo ambalo kiuhalisia ni kufanana kwa haki. Ulaya ya kabla ya karne ya 20 ni mfano dhahiri wa dhulma kwa mwanamke. Mpaka mwanzoni mwa karne ya 20 mwanamke wa Ulaya alinyimwa haki za kibinadamu katika maisha ya kila siku na kisheria. Hakuwa na haki sawa wala zinazofanana na mwanaume.

Ni katika muongo uliopita ambapo kutokana na harakati za pupa, wameanza kumpa haki zake za msingi, lakini bado hajaweza kupata haki zinazochukuana na maumbile yake na mahitaji yake kimwili na kiroho. Kama mwanamke anataka haki na usawa na furaha katika familia lazima alitupilie mbali wazo la kufanana kwa haki. Hiyo ndio njia pekee ya kuimarisha uchangamfu kati ya mwanaume na mwanamke. Katika hali hiyo, sio tu kwamba mwanaume atazikubali haki za mwanamke, lakini pia atakuwa tayari kumpatia, na katika baadhi ya mambo atatoa haki nyingi zaidi tena bila kumdanganya.

Halikadhalika hatudai kuwa katika jamii ya Kiislamu mwanamke anapata haki sawa na mwanaume. Mara nyingi tumesema kuwa ni muhimu kwamba nafasi ya mwanamke iangaliwe upya na apewe haki lukuki ambazo Uislamu umempatia, na ambazo amekuwa akinyimwa katika kipindi chote cha historia. Hata hivyo, haifai kuiga staili na mifumo ya Kimagharibi kibubusa, mifumo ambayo imesababisha madhara makubwa huko Magharibi kwenyewe. Tunachodai ni kuwa kutofanana kwa haki kati ya mwanaume na mwanamke, kwa mujibu wa mipaka ya maumbile na tofauti zao ndio kutenda haki zaidi. Hukidhi mahitaji ya haki za asili vizuri zaidi, hutoa hakikisho kwa furaha ya familia na huisukuma jamii mbele katika njia ya maendeleo bora zaidi.

Inaweza kukumbukwa kuwa tunadai kuwa haki ya asili inataka kwamba, katika baadhi ya mambo, kuwe

na kutokufanana kwa haki ya mwanaume na mwanamke. Kwa vile linahusiana na falfsafa ya haki, suala hili lina sura ya kifalsafa asilimia mia moja. Linahusiana pia na kanuni ya haki na usawa, kanuni kuu za sheria ya Kiislamu na falsafa ya uanazuoni wa Kiislamu. Ni kanuni ya usawa iliyoleta mafundisho ya kukubaliana kati ya akili na sheria ya Mwenyezi Mungu.

Kwa mujibu wa elimu ya sheria ya Kiislamu au tuseme ya Kishia, kama ikithibitika kuwa usawa unataka kuwa katika hali fulani, basi sura hiyo ndiyo itachukua sura ya kisheria bila kujali hoja zozote nyingine dhidi yake, kwani kwa mujibu wa mafundisho ya msingi ya Uislamu, sheria lazima katika hali yoyote isivunje au kuhalifu uadilifu wa asili na haki na za msingi. Wanazuoni wa Kiislamu kwa kufafanua kanuni za usawa waliweka msingi wa falsafa ya haki, ingawa kufuatia matukio fulani ya kihistoria yasiyofurahisha, hawakuweza kuiendeleza kazi nzuri waliyoianza. Walikuwa ni Waislamu ambao, kwa mara ya kwanza walilitupia macho suala la haki za kibinadamu na kanuni za usawa, na walizitoa katika haki yake ya asili na kama kanuni zinazojitegemea bila kuathiriwa na sheria za kimikataba. Waislamu walikuwa vinara katika fani ya haki za asili za binadamu.

Lakini hawakujaaliwa kuiendeleza kazi yao na hatimaye, baada ya karne nane, iliendelezwa na wasomi na wanafalsafa wa kizungu na wakajichukulia sifa hiyo. Wazungu walileta falsafa za kijamii, kisiasa na kiuchumi na walijulisha watu, jamii na mataifa juu ya thamani ya maisha na haki za binadamu.

Kwa maoni yetu mbali na sababu za kihistoria kulikuwa na sababu za kisaikolojia na kimkoa pia, ambazo ziliwazuia Waislamu wa Mashariki (Asia) kuendeleza suala la haki za msingi za binadamu.

Ni moja ya tofauti kati ya hulka ya nchi za Mashariki (Asia) na zile za Magharibi. Nchi za Mashariki zinazingatia maadili na za Magharibi zinazingatia haki. Mtu wa Mashariki ana upendo zaidi na anaamini kuwa lazima asamehe awe na moyo wa ubinadamu. Lakini mtu wa Magharibi anaamini kuwa kama binadamu lazima azijue na kuzilinda haki zake na lazima asiruhusu wengine wazipore.

Utu unahitaji maadili na haki pia. Utu unahusiana na haki na maadili. Moja tu katika hizi haitoshi kuwa kigezo cha sifa bora za binadamu.

Uislamu ulikuwa na hadi sasa unazingatia yote mawili haki na maadili. Katika Uislamu, dhati, kusamehe, na matendo mema ni sifa takatifu na za kibinadamu. Lakini wakati huo huo mtu kujua haki zake na kuwa tayari kuzitetea, ni jambo takatifu na la kibinadamu. Hata hivyo, nchi za Mashariki kwa kiasi kikubwa zimekaliwa na Waislamu, na kwa hiyo, japokuwa awali yote yalikuwa yakizingatiwa maadili na haki lakini pole pole walijikuta wanabaki kushikilia maadili peke yake.

Hivi sasa tunashughulikia suala la haki ambalo pia linaweza kuwa suala la kifalsafa na linafaa kujadiliwa kwa kirefu. Inahusiana sana na maana halisi ya haki na ukweli halisi wa haki uadilifu na sheria uliokuwepo hata kabla ya kuwepo kwa sheria duniani, na ambao maana zake haziwezi kubadilishwa na sheria yoyote.

Montesquieu anasema, “Kabla ya sheria kutungwa na watu, kulikuwepo mahusiano yenye uadilifu baina

ya watu kwa msingi wa sheria ambazo zilitawala mahusiano baina ya vitu vyote vilivyokuwepo. Ni kuwepo kwa mahusiano haya kulikosababisha kuundwa kwa sheria hizi. Kusema kwamba kabla ya watu kutunga sheria hapakuwa na uadilifu au dhuluma katika kuyaongoza na kuyadhibiti mahusiano ya watu ni sawa na kusema kuwa kabla ya mduara kuchorwa, nusu vipenyo vyake havilingani."

Herbert Spencer anasema; "uadilifu unachaganganyika na kitu fulani mbali na hisia; yaani haki za msingi za binadamu. Lazima tuheshimu haki za binadamu ili uadilifu uwepo kiuhalisia."

Wengi wa wasomi wa Ulaya wana mtazamo kuwa maazimio yote ya haki za binadamu yamechukuliwa kutoka katika haki za msingi za binadamu. Kwa maneno mengine, haki za msingi za binadamu zimechukuwa sura ya maazimio ya haki.

Kama tunavyojua, Montesquieu, Spencer n.k. wamesema kitu kimoja, juu ya uadilifu kama walichosema wanafalsafa wasomi wa Kiislamu juu ya msingi wa razini wa wema na uovu na kanuni ya usawa. Miongoni mwa Waislamu wamekuwepo wasomi ambao wamekana kuwepo kwa haki za asili na wanashikilia kuwa uadilifu ni jambo la kimkataba. Halikadhalika, imani hii imekuwepo miongoni mwa wazungu. Mwanafalsafa wa Kiingereza, Thomas Hobbes alikana kabisa na akadai kuwa uadilifu sio kitu halisi.

Azimio La Haki Za Binadamu Ni Falsafa Sio Sheria.

Ni kejeli kusema kuwa Azimio la Dunia la haki za binadamu ambalo linatoa hakikisho la usawa wa haki kati ya mwanaume na mwanamke, imeidhinishwa na Bunge la nchi fulani, wanaume na wanawake wa nchi hiyo wanapaswa kuwa na haki sawa.

Hata hivyo, si jambo lililo katika mamlaka ya kisheria kwa Bunge la nchi yoyote kuidhinisha au kukataa Azimio kwa vile yaliyomo humo kwenye Azimio, hayana sura ya kimkataba, hivyo hayaangukii kwenye mamlaka yake ya kisheria.

Azimio la Dunia hushughulikia haki za asili, zisizoondosheka na zisizobatilishika za binadamu na kama inavyodaiwa na Azimio lenyewe, haki hizi ni sehemu muhimu na ya lazima ya heshima ya mwanadamu na zimebuniwa na mamlaka yenye nguvu ya maumbile yenyewe. Kwa maneno mengine, haki hizi zimetolewa na kupewa wanaadamu na chanzo kile kile kilichowapa akili, utashi na heshima.

Kama ni hivyo, hali ya mambo yaliyomo katika Azimio hili inalazimisha kuwa hakuna mamlaka yoyote ya binadamu inayoweza kuyabuni au kuyafuta. Sasa hapa linakujaje suala la kuidhinisha Azimio hilo katika chombo cha kutunga sheria?

Kwa kusema kweli, Azimio la Haki za Binadamu ni falsafa sio sheria. Na kama ni hivyo inafaa kuidhinishwa na wanafalsafa na sio na watunga sheria (wabunge). Hakuna Bunge ambalo linaweza kutunga falsafa kwa kulumbana na kupiga kura. Vinginevyo kwa nini, muswada unaoelezea nadharia ya Einstein juu ya 'relativity' (kwamba vipimo vya mwendo nafasi na wakati vinawiana) au nadharia

nyingine inayosema kuwa kuna maisha katika karne nyingine haijapelekwa Bungeni ili ikaidhinishwe na chombo kitukufu?

Kiuhalisia, sheria ya asili haiwezi kupitishwa au kukataliwa kama sheria ya kimkataba. Kupitisha sheria ya asili (maumbile) ni sawa na kupitisha sheria kuwa kupandikiza chipukizi la mpeasi kwenye muepo (tufaa) kutafanikiwa lakini kupandikiza mpeasi kwenye mforosadi (mulberry) hakutafanikiwa.

Kila azimio lolote linapotolewa na kikundi cha wanafalsafa, kila taifa hupeleka kwa wanafalsafa wake, na kama watalipitisha basi ndio wananchi wote wa nchi hiyo wanapaswa kuzingatia maelekezo yake kama ukweli wa ziada wa kisheria. Mamlaka ya kisheria itapaswa kutopitisha sheria inayopingana na maelekezo hayo.

Lakini mataifa mengine hayatalazimika kuyazingatia maazimio haya maadamu hayajathibitishwa, kwa mujibu wa maoni yao, kuwa haki hizo zipo duniani. Na zaidi ya haya, kwa vile suala hili haliwezi kupimwa au kujaribiwa, halihitaji vifaa au maabara n.k Ni suala la kifalsafa ambalo vifaa vyake ni ubongo, akili na nguvu ya hoja.

Hata kama mataifa mengine yatalazimika kuwafuata walio wengi katika suala la mantiki na falsafa na wanahisi kuwa hawana uwezo wa kutosha wa kufikiri kifalsafa wao wenyewe, sisi Waislamu hatuwezi kufuata mfano wao. Tumeonyesha huko nyuma kuwa tuna uwezo mkubwa wa kushughulikia masuala ya mantiki na kifalsafa. Kwanini tuwafuate wengine leo? Inashangaza kwamba wakati wasomi wa Kiislamu walitilia uzito sana kanuni ya uadilifu na haki za msingi za binadamu na wanazikubali kama sheria ya dini, bila kusita wala ubishi wowote, yote haya yakakubaliwa na akili (kuwa ni haki), leo mambo yameharibika kiasi cha kuwa tunataka wabunge waidhinishe kutambuliwa kwa haki za binadamu.

Falsafa Haiwezi Kuthibitishwa Kwa Kujaza Kuponi.

Ni kejeli na dhihaka kubwa kuliko hata hiyo iliyotangulia, kujaribu kuamua suala la haki za binadamu kwa kuandaa kura za maoni kwa wavulana wadogo na wasichana wadogo. Je ni akili kweli kuchapisha kuponi na kuwaambia wavulana na wasichana wadogo waijaze ili kujua asili ya haki za binadamu na kama ni za aina moja au mbili.

Hata hivyo, hapa tunataka kulijadili suala la haki za mwanamke kwa utaratibu mzuri na kifalsafa, na kwa kuzingatia haki za msingi za binadamu. Tungependa kujua kama kanuni zinazotaka wanadamu wote wapate na kufaidi haki zao za msingi walizopewa na Mwenyezi Mungu, zinalazimisha au hazilazimishi kuwa mwanaume na mwanamke wawe na nafasi moja sawa katika haki zao.

Tunawaomba wasomi, wanafalsafa na wanasheria wa nchi yetu, ambao wanaweza kuwa ni watu pekee wenye mamlaka ya kutoa maoni juu ya suala hilo na kuziangalia hoja zetu kwa jicho la umakinifu. Tutawashukuru sana kama watatoa maoni yao ya kimamlaka kukubaliana na hoja zetu au kuzipinga.

Katika kulijadili suala hili, ni muhimu kwanza kujadili msingi wa haki za binadamu. Haki za mwanaume

na mwanamke zitajadiliwa baadaye. Katika muktadha huu, haitakuwa makosa kuzungumzia kidogo harakati za kutaka mabadiliko katika karne chache zilizopita, ambazo zimeleta wazo la usawa wa haki kati ya mwanaume na mwanamke.

Tazamo Fupi La Historia Ya Haki Za Wanawake Ulaya.

Mazungumzo ya haki za binadamu yalianza karne ya 17. Waandishi na wanafalsafa wa karne ya 17 na 18, kwa uvumilivu mkubwa, waliyatangaza na kuyaeneza mawazo yao juu ya suala la haki za msingi na zisizobatilishika za binadamu. Jeans Jacques Rouseau, Voltaire na Montesquieu ni miongoni mwa waandishi na wanafalsafa hawa. Matokeo ya kwanza ya kivitendo ya kuenea kwa mawazo yao yalikuwa ni mapambano ya muda mrefu kati ya watawala na raia wa Uingereza. Mwaka 1688 Waingereza walifanikiwa kumshawishi mfalme akubali kuwapa baadhi ya haki za kisiasa na jamii walizokuwa wameziandika katika hati iliyojulikana kama 'The Bill of Rights.'

Matokeo mengine muhimu ya kuenea kwa mawazo haya yalikuwa ni Vita vya Uhuru vya Wamarekani dhidi ya Uingereza. Makoloni kumi na tatu ya Uingereza huko Amerika ya kaskazini yaliasi, kufuatia kuwekewa kodi kubwa sana, na hatimaye walipata uhuru wao.

Mwaka 1776 mkutano ulifanyika Philadelphia, mkutano ambao ulitoa Azimio la Uhuru. Dibaji yake inasema; "Tunauchukulia ukweli huu kuwa dhahiri kwamba watu wote wameumbwa wakiwa sawa na kwamba wamepewa na muumba wao haki fulani zisizoondosheka, na kwamba miongoni mwa hizo ni haki ya kuishi, uhuru na kupata furaha au kufurahia. Ili kuhakikisha kupatikana kwa haki hizi, serikali zinawekwa na watu, zinapata madaraka yao kutokana na idhini ya watawaliwa; na kwamba wakati wowote serikali ya muundo wowote inapokiuka malengo haya, ni haki ya watu kuibadilisha au kuiondoa, na kuweka serikali mpya, ikijengwa chini ya msingi wa kanuni hizi na kupata madaraka yake kwa utaratibu huu, itawahakikishia wananchi usalama na furaha yao.

Na lile linaloitwa Azimio la Haki za Binadamu lilitolewa baada ya Mapinduzi ya Ufaransa, lina kanuni fulani za jumla zinazoonekana kuwa sehemu muhimu na ya lazima ya katiba ya Ufaransa. Azimio lina dibaji na ibara 17. Ibara ya kwanza inasema kuwa watu wote huzaliwa wakiwa huru na hubaki huru katika maisha yao yote. Haki zao zinafanana.

Katika karne ya 19 mawazo mapya yalitokeza katika uwanja wa haki za binadamu kiuchumi, kijamii na kisiasa. Haya yalisababisha kuibuka kwa ujamaa, ushiriki wa wafanyakazi katika faida na kuiondoa serikali kutoka mikononi mwa mabepari kwenda mikoni mwa wavuja jasho (wafanyakazi).

Hadi mwanzoni mwa karne ya 20, majadiliano yote yalikuwa yamejikita juu ya haki ya watu dhidi ya serikali au haki za tabaka la wavuja jasho dhidi ya waajiri na makabaila.

Katika karne ya 20, suala la haki za mwanamke dhidi ya haki za manaume liliibuka. Ni juzi tu katika karne ya 20 ambapo Uingereza iliyokuwa ikijulikana kama demokrasia kongwe, ilipotambua usawa wa

haki kati ya mwanaume na mwanamke. Ingawa Marekani kiujumla ilikuwa imezitambua haki za binadamu katika karne ya 18 katika Hati ya Azimio la uhuru, lakini bado haki ya kupiga kura kwa wote ilitolewa mwaka 1920. Ufaransa pia ilitoa haki ya wanawake kupiga kura katika karne ya 20.

Kwa kiasi fulani, katika karne ya 20 sehemu kubwa ya watu duniani walijitokeza kuunga mkono mabadiliko makubwa katika mahusiano kati ya mwanaume na mwanamke, katika nyanja za haki na majukumu. Kwa mujibu wao lengo la uadilifu wa kijamii halingeweza kufikiwa kwa

kufanya mabadiliko baina ya mataifa na kati ya wafanyakazi na waajiri na mabepari bila pia kuleta mabadiliko katika mahusiano kati ya mwanaume na mwanamke.

Hii ndio maana dibaji ya Azimio la Haki za Binadamu kwa wote, lililotolewa mwaka 1948 linasema kwamba “Ambapo heshima ya utu wa mtu mmoja mmoja na usawa wa haki kati ya mwanaume na mwanamke…”

Machafuko yaliyosababishwa na maendeleo ya kuboreka kwa mashine (mitambo) katika karne ya 19 na 20, na hali mbaya ya wafanyakazi iliyofuatia, hasa kwa wafanyakazi wa kike, yalisababisha macho yaelekezwe kwenye masaibu ya mwanamke na ndio maana suala la haki zao lilizingatiwa sana. Mwanahistoria anasema, “Kwa vile serikali ilikuwa haijali, masaibu ya wafanyakazi na tabia ya waajiri wao, mabepari walifanya walivyopenda”. Wamiliki wa viwanda walikuwa wakiwaajiri wanawake na watoto kwa ujira mdogo sana, na kwa vile masaa ya kufanya kazi yalikuwa mengi mno, wengi wao waliugua magonjwa mbali mbali na wengine walikufa katika umri mdogo.”

Hii ilikuwa ni historia fupi ya harakati za Haki za Binadamu Ulaya. Kama tunavyojua, ibara zote za Azimio la Haki za Binadamu ambazo ni mpya kwa wazungu, zilishawekwa na Uislamu katika karne 14 zilizopita, na baadhi ya wasomi wa Kiarabu na Kiirani katika vitabu vyao wamefanya ulinganisho kati ya mafundisho ya Uislamu na maelekezo (masharti) ya ibara hizi. Bado kuna tofauti katika baadhi ya vipengele vya maazimio haya na mafundisho ya Uislamu. Hili ni somo la kuvutia. Kwa mfano Uislamu unakubali usawa kati ya haki ya mwanaume na mwanamke, lakini haukiubali kufanana kwa haki hizi.

Heshima Ya Mwanadamu Na Haki Za Binadamu.

“Ambapo kuitambua heshima na utu wa mwanadamu na haki zisizoondosheka za wanaadamu wote ni msingi wa uhuru, haki na amani duniani.”
“Ambapo kutozingatia na kudharau haki za kibinadamu kumesababisha vitendo vya kishenzi na kuikasirisha dhamira njema ya mwanadamu na kuja kwa ulimwengu ambao ndani yake watu watafurahia uhuru wa kujieleza na imani, na uhuru wa kuondokana na hofu na shida imetamkwa kuwa ni hamu kubwa ya watu wa kawaida.”

“Ambapo italazimu, ikiwa mwanadamu hana kimbilio, kama njia ya mwisho, ana haki ya kuasi utawala wa kidhalimu, na kwamba haki za binadamu zitapaswa kulindwa na utawala wa kisheria.”

“Itakapobidi, kukuza maendeleo ya uhusiano wa kirafiki kati ya mataifa.”

“Ambapo watu wa Umoja wa Mataifa, katika heshima ya utu wa mwanadamu na katika usawa wa haki za mwanaume na wanawake, na wamedhamiria kukuza maendeleo ya kijamii na kiwango cha ubora wa maisha, katika hali ya uhuru zaidi.”

“Ambapo Baraza kuu la Umoja wa Mataifa linatamka Azimio hili la Haki za Binadamu kwa wote kama kigezo cha wote cha kupimia mafanikio ya watu wote na mataifa yote ili hadi kufika mwisho kila mtu na chombo cha jamii, kwa kulizingatia Azimio akilini mwao walijitahidi kwa kufundisha na kutoa elimu, kukuza tabia ya kuheshimu haki hizi na uhuru na kwa hatua za kimaendeleo za kitaifa na kimataifa, ili kulinda utambulisho na zingatio miongoni mwa nchi wanachama wenyewe na miongoni mwa watu wa nchi zilizo chini ya mamlaka yao ya kisheria …”

Kama tulivyoona mwanzo, kila neno na kila sentensi katika azimio hili limepigiwa hesabu kali, limechukuliwa kwa uangalifu mkubwa. Hili ni dhihirisho la mawazo ya wanafalsafa na wanasheria wataka mabadiliko wa karne nyingi.

Nukta Muhimu Za Dibaji Ya Azimio La Haki Za Binadamu.

Azimio hili lina ibara 30, japo baadhi ya ibara zimezidi kiasi na baadhi ya nukta zimerudiwa katika ibara nyingi.

Nuktra muhimu za ibara ni kama ifuatavyo:
Binadamu wote wana haki za msingi zisizobatilishika na haki ya kutambuliwa utu wao.

Utu wa binadamu na haki za binadmau ni kwa ajili ya wote na hivi havigawiki. Vinawahusu watu wote bila kujali rangi, utaifa au jinsia. Binadamu wote ni wanafamilia, hivyo hakuna aliyebora kuliko mwingine.

Kuzitambua kikamilifu haki za binadamu na utu wa binadamu ni msingi wa uhuru, haki na amani.

Yaliyomo katika Azimio yanaashiria kuwa chanzo cha matatizo yote, vita, vitendo vya kishenzi vinavyofanywa na mtu mmoja mmoja na watu dhidi ya wengine ni kutozitambua haki za binadamu na utu wa binadamu. Kutozitambua huku huwalazimisha baadhi kuasi dhidi ya wengine na hivyo kuhatarisha amani na usalama.

Hitajio na kinachotamaniwa kikubwa zaidi katika kufanikisha azma hii ni kuzaliwa kwa dunia ambayo ndani yake kutakuwa hakikisho la uhuru wa imani, usalama na hali nzuri kimaisha pamoja na hakikisho la kuondokana na ukandamizaji, hofu na umasikini. Azimio lenye ibara 30 limeundwa ili kufikia lengo hili.

Imani juu ya heshima kwa utu wa mwanadamu na haki za msingi za kibinadamu lazima ikaziwe na kuingizwa pole pole akilini mwa watu wote, kupitia ufundishaji na elimu.

Heshima Kwa Utu Wa Mwanadamu.

Kwa vile Azimio la Haki za Binadamu limeundwa kwa msingi wa heshima kwa utu, uhuru na usawa kwa nia ya kufufua haki za binadamu, lazima liheshimiwe na kila mtu makini. Sisi watu wa Mashariki (Asia) tumekuwa tukiamini juu ya kuuheshimu utu wa binadamu kwa muda mrefu. Uislamu umetilia sana mkazo katika kuuheshimu utu pamoja na haki za binadamu, uhuru na usawa. Hao waliyoyahamasisha haya, wanastahiki shukrani zetu. Hata hivyo, haya ni maandishi ya kifalsafa yaliyoandikwa na mikono ya kibinadamu, sio malaika. Hivyo kila mwanafalsafa anayo haki ya kuyachambua na kuonyesha nukta zake dhaifu.

Hapana shaka kwamba Azimio la haki za Binadamu lina udhaifu wake, lakini hivi sasa hatuna nia ya kuonyesha udhaifu huo. Badala yake; tunaonyesha nukta zake nzuri.

Msingi wa Azimio hili ni heshima ya utu wa mwanadamu kwa sababu, kwa kuwa nazo hizo, mwanadamu anapata haki fulani ambazo viumbe wengine hawapati, kwa vile hawana utu huo. Hii ndio nukta nzuri ya Azimio hili.

Falsafa Ya Kimagharibi Inamshusha Hadhi Mwanadamu.

Hapa tena tulikutana na swali kongwe la kifalsafa; Ni nini asili ya utu wa wanadamu ambao humtofautisha yeye na farasi, ng'ombe na njiwa?

Hapa ndipo inapodhirika migongano kati ya msingi wa Azimio la Haki za Binadamu na tathhmini ya Kimagharibi juu ya mwanadamu.

Falsafa ya Kimagharibi toka zamani imekuwa ikimshushia hadhi mwanadamu. Chanzo cha yote ambayo yalikuwa yakisemwa zamani kuhusu mwanadamu na cheo chake kitukufu ilikuwa ni katika Mashariki (Asia). Sasa mifumo mingi ya falsafa ya Ulaya inayakejeli yote hayo.

Mwanadamu kwa mtazamo wa Kimagharibi, amekuja (duniani) akiwa na cheo cha mashine. Kuwepo kwa roho na asili ya ukarimu kumekataliwa.

Wazo kwamba ulimwengu una lengo la msingi linaonekana kuwa ni wazo la kupinga maendeleo.

Sasa hakuna mtu katika nchi za Magharibi anayeweza kusema kuwa mwanadamu ni mfalme wa viumbe. Kwa mujibu wa nadharia ya sasa ya kizungu, imani hiyo ilikuwa ni chipukizi (tawi) la unajimu wa Ptolem, ambayo ilikuwa inaaminika kuwa dunia ndio kitovu cha ulimwengu na nyota ziliaminika kuwa zinaizunguka dunia. Sasa kwa kuwa nadharia hii imeshakufa na kwa kutoweka kwake, hakuna nafasi tena ya mwanadamu kudai kuwa ni mfalme wa ulimwengu. Kwa mujibu wa Wazungu, hata zamani ilikuwa ni kwa sababu ya ubinafsi wake ndio maana akajifanya kuwa bora kuliko viumbe wengine. Maisha yake ni ya kiumbo tu. Mtu akishakufa, mwili wake huoza na hapo ndio mwisho wa habari!

Mzungu haamini kuwa roho inaweza kuishi peke yake. Kwa mtazamo huu, hajioni kuwa na tofauti yoyote kati yake na mimea na wanyama. Kwa hiyo anaona kuwa hakuna tofauti yoyote ile ya msingi kati ya asili ya vipawa vya kiakili na kiroho vya mwanadamu na sifa nyingine za maada kama vile joto, linalotoka kwenye makaa ya mawe.

Maisha kwa viumbe vyote, ikiwa ni pamoja na mwanadamu, yanamaanisha mapambano yasiyokwisha ya kuweza kuishi. Hii ndio kanuni ya msingi ya maisha. Mwanadamu mara zote amekuwa akipambana ili awe mshindi katika mapambano haya, na ili kuilinda nafasi (hadhi) yake amebuni kanuni za kimaadili kama vile uadilifu, wema, ushirikiano, uaminifu n.k.

Kwa mujibu wa baadhi ya matapo yenye nguvu ya kifalsafa ya Kimagharibi mwanadamu ni mashine tu inayosukumwa na maslahi ya kiuchumi. Dini, maadili, falsafa, sayansi, fasihi na sanaa nyingine, vyote ni vikorombwezo tu. Miundo mbinu yake ni mfumo wa uzalishaji mali na ugawaji wa mali, na mambo haya ndiyo yanayotawala nyanja zote za maisha ya mwanadamu.

Sio hivyo tu, baadhi ya wanafalsafa wa Kimagharibi wana mtazamo kwamba vipengele vya kijinsia ndivyo vyenye ushawashi halisi wenye nguvu katika shughuli zote za mwanadamu. Maadili, falsafa, sayansi, dini na sanaa vyote hivyo ni miundo ilyobadilishwa na kurekebishwa ya jinsia. Hatuelewi ni jinsi gani tunaweza kuzungumzia utu wa mwanadamu na haki za msingi na ni jinsi gani tunaweza kuzifanya kuwa msingi wa matendo yetu yote, ikiwa tunakana kwamba maisha hayana lengo lolote la msingi.

Ikiwa tunafikiri kuwa mapambano ya kuweza kuishi na mapambano yatakayombakisha mwenye nguvu zaidi ndio sheria pekee zinazotawala maisha, ikiwa tunaamini kuwa mwanadamu ni mashine tu kama mashine nyingine (lakini) iliyopewa mikono ya binadamu, ikiwa tunashikilia kuwa hakuna roho na kwamba yote yanayozungumzwa juu ya roho ni kuzidisha chumvi kwa kiroho, ikiwa tunashikilia kuwa maslahi ya kiuchumi na ngono ndiyo yanayosukuma shughuli zote za mwanadamu, ikiwa tunajali kuwa wema na uovu ni dhana linganifu tu, ikiwa tuna maoni kuwa muongozo wa kimungu wa asili na wa kimaono ni upuuzi na ikiwa tutasema kuwa mwanadamu ni mtumwa wa matamanio yake na anaweza kunyenyekea kwa nguvu tu.

Maoni ya Kimagharibi juu ya mwanadamu yanapingana na utu wake na yameiporomosha hadhi yake katika kila pembe katika pembe ya sababu ya kuumbwa kwake, umbile lake, nia yake na dhamira yake.

Baada ya kufanya yote haya, nchi za Magharibi zimetangaza Azimio la hali ya juu lenye busara kuhusu utu wa mwanadamu na cheo na haki za msingi zisizoondosheka na takatifu, na wametoa wito kwa kila mtu kulitekeleza hilo.

Kabla ya kutoa Azimio hili la hali ya juu zuri na lenye busara, nchi za Magharibi kuhusu utakatifu na haki za asili za mwanadamu, wangeipitia upya tafsiri yao juu ya mwanadamu.

Tunakiri kuwa sio wanafalsafa wote wa Kimagharibi wana mtazamo huu. Wengi wao wanamtazama mwanadamu kama tunavyofanya sisi watu wa Mashariki (Asia). Tuna mtazamo ambao watu wengi wa

Magharibi wanaung'ang'ania na ambao unawashawishi watu duniani kote.

Azimio la Haki za Binadamu lilipaswa litolewe na wale ambao wanamuona mwanadamu kuwa ni zaidi ya roboti ambao wanafikiri kuwa malengo yake hayaishii kwenye silika za kibinadamu na kinyama na ambao wanaamini juu ya dhamira ya kibinadamu. Azimio la Haki za Binadamu lilipaswa litolewe na watu wa Mashariki ambao wanaamini kuwa mwanadamu ni khalifa wa Mwenyezi Mungu katika dunia. Qur'ani Tukufu inasema:

إِنِّي جَاعِلٌ فِي الْأَرْضِ خَلِيفَةً ؟

"Kwa hakika nitamuweka khalifa katika ardhi." (2:30)

Ni wale tu wanaoamini kuwa mwanadamu ana lengo na makusudio ndio wanaoweza kuzungumzia juu ya haki za binadamu.

يَا أَيُّهَا الْإِنْسَانُ إِنَّكَ كَادِحٌ إِلَىٰ رَبِّكَ كَدْحًا فَمُلَاقِيهِ

"Enyi watu, bila shaka lazima mjitahidi sana kwa ajili ya Mola wenu, kujitahidi kukubwa kabisa hadi mtakapokutana Naye." (84:6).

Azimio la haki za binadamu linaifaa mifumo ile ambayo inaamini kuwa mwanadamu ana muelekeo wa asili wa kutenda mema;

وَنَفْسٍ وَمَا سَوَّاهَا {7}

فَأَلْهَمَهَا فُجُورَهَا وَتَقْوَاهَا {8}

"Naapa kwa roho na kwa yule aliyeifanya kuwa timilifu na aliyeipa ujuzi (elimu) juu ya uovu na uchamungu." (91:7–8).

Azimio la haki za Binadamu haliafikiani na njia za fikra za Kimagharibi.

Kufikiri kwao kunazifaa tu tabia za watu wa kimagharibi ambao huua hisia za kibinadamu, hucheza na tabia za wanaadamu, hujali fedha zaidi kuliko mtu, huabudu mashine (mitambo), huona mali kama

Mungu na huwanyonya wanaadamu wengine. Ubepari umepata nguvu na mamlaka yasiyo na kikomo kiasi cha kuwa ikitokea kuwa milionea mmoja atamrithisha mbwa wake kipenzi mali zake, mbwa huyo ataheshimika kuliko watu, watu wengi tu watamtumikia mbwa huyo kama makatibu muhtasi na makarani na wataonyesha heshima ya hali ya juu kwa mbwa huyo.

Leo hii swali kubwa la kijamii kwa mujibu wa Qur'ani, ni je, mwanadamu amejisahau mwenyewe? Sio tu kwamba amejisahau yeye tu bali amemsahau hata Mungu wake pia. Akili zake zote amezielekeza kwenye maisha ya kidunia na mali na amepuuza kabisa kujifikiria na kujipima. Anafikiri kuwa amepoteza roho yake. Mawazo kama haya ni ya hatari sana na yanaweza kuondoa kabisa thamani ya utu na ubinadamu. Ustaarabu wa sasa unaweza kuzalisha kila kitu chenye ubora wa juu kabisa, lakini hauwezi kumtengeneza mtu halisi.

Gandhi anasema kuwa mzungu anastahili kuitwa bwana wa dunia. Anamiliki raslimali zote za kidunia na anafanya vitu ambavyo mataifa mengine wanaamini kuwa ni Mungu tu anayeweza kuyafanya. Lakini ni kitu kimoja tu ambacho mzungu hawezi kukifanya nacho ni kujifikiria na kujipima. Hilo peke yake linatosha kuthibitisha kutokuwa na maana kwa kumeremeta kwa ustaarabu wa kisasa.

Kama ustaarabu wa Kimagharibi umemtaabisha mzungu kwa ulevi na ngono basi ni kwa sababu ya kujisahau na kujipoteza badala ya kujitafuta. Uwezo wake wa kivitendo wa kuvumbua, kugundua na kuzalisha zana za kivita unatokana na kujikwepa nafsi yake na sio kwa sababu ya uwezo wake wa kipekee wa kujidhibiti.

Kuogopa kwake upweke, ukimya wake na tamaa yake ya fedha kumemfanya asiweze kusikia sauti yake ya ndani. Kushindwa kwake kujitawala ndio kichocheo chake cha kuuteka ulimwengu. Hii ndio sababu kila anakokwenda mzungu hueneza mitafaruku na ghasia. Kama mtu akipoteza nafsi yake mwenyewe, hakuna faida yoyote kuushinda ulimwengu.

Wale ambao wamefundishwa na Injili kuwa wamisionari wa ukweli, upendo na amani, wanazunguka kutafuta dhahabu na watumwa. Badala ya kutafuta msamaha wa Mwenyezi Mungu na uadilifu katika ufalme wa Mungu, kama Injili inavyofundisha wanatumia dini yao kama kifutio cha madhambi zao (kwa kumfanya Yesu, Mtume mtukufu wa Mungu kuwa kafara ya dhambi kwa kila amuaminiye). Badala ya kufundisha na kuhubiri ujumbe wa Mungu, wanawadondoshea mabomu watu wasio na hatia.

Hii ndio sababu, Azimio la Haki za Binadamu linakiukwa na nchi za Magharibi. Falsafa inayofuatwa na watu wa Magharibi katika maisha yao kivitendo inafanya kushindwa kwa Azimio hili kusiepukike.

Dhana Za Asili Za Haki Ya Familia.

Tumesema kwamba mwanadamu hufaidi aina fulani ya heshima ya asili. Asili ya maumbile yake imempa haki kadhaa za msingi zisizoondosheka. Huu ndio msingi wa Azimio la haki za Binadamu kwa wote.

Uislamu na falsafa za Mashariki (Asia) zinaunga mkono dhamira hii. Kisichofaa katika Azimio hili na kinachokwenda kinyume ni jinsi mifumo mbali mbali ya falsafa za Kimagharibi inavyoitafsiri asili na maumbile ya mwanadamu.

Ni dhahiri kuwa chanzo pekee chenye mamlaka na kisicho na makosa juu ya elimu ya haki za binadamu ni kitabu adhimu na kitukufu cha maumbile. Ni kwa kuzirejea tu kurasa za kitabu hiki ndio tunaweza kuziona haki ambazo zinawahusu watu wote, na kupata hakikisho la nafasi linganishi za haki za mwanaume na mwanamke.

Inastaajabisha kwamba baadhi ya watu wenye mawazo finyu hawakijui chanzo hiki kitukufu. Kwa mujibu wao, chanzo pekee cha kuaminika ni chombo cha wale watu wachache wanaoitawala dunia waliopata nafasi ya kuliandika Azimio hili. Ingawa wao wenyewe wanaweza, kivitendo wasiyazingatie hayo waliyoyaandika lakini wengine hawana haki ya kupinga. Lakini sisi, kwa kutumia hizi hizi haki za binadamu, tunaamini kuwa tuna haki ya kutofautiana. Kwa maoni yetu, chanzo pekee ambacho hakiwezi kupingwa ni maumbile yenyewe ambayo yanaweza kuchukuliwa kuwa ni kitabu cha Mwenyezi Mungu.

Tunawaomba radhi wasomaji wetu, kwa sababu inatupasa tuibue baadhi ya masuala ambayo kwa kiasi fulani ni ya kifalsafa na hivyo yanaonekana makavu. Yanaweza pia kuwa yanakinaisha kwa baadhi ya wasomaji. Tungeweza kuwa tuliyaepuka masuala haya, lakini somo la haki za mwanamke linahusiana sana na masuala hayo hivyo haiwezekani kuyaachilia mbali moja kwa moja.

Uhusiano Kati Ya Haki Za Asili/Msingi Na Malengo Ya Maumbile.

Kwa mtazamo wetu, haki za asili na za msingi zimeibuka kutokana na mpango wa Mungu, ambapo kwa mujibu wa mpango huu, utaratibu wa kibunifu, kwa kuzingatia malengo yake, huvisukuma mbele vitu vyote kuelekea katika hali ya ukamilikifu, uwezo ambao tayari umefichwa ndani ya maumbile yao.

Kila uwezo wa kiasili ni msingi wa moja ya haki za asili na, wakati huo huo, ni mamlaka ya asili ya kuitekeleza haki hiyo. Kwa mfano kila mtoto wa mwanadamu ana haki ya kujifunza na kwenda shule, lakini mtoto wa kondoo hana haki hizo. Kwa nini iko hivyo?

Ni kwa sababu mtoto wa binadamu ana uwezo wa kujifunza na kupata busara zaidi wakati mtoto wa kondoo hana uwezo huu. Utaratibu wa kibunifu umeweka mamlaka kwa ajili ya haki hii ndani ya umbile la mwanadamu, lakini mamlaka haya hayakuwekwa ndani ya kondoo. Mambo yako hivi hivi katika haki

za kufikiri, kupiga kura na utashi.

Baadhi ya watu wanafikiri kuwa nadharia ya haki za asili na wazo kwamba maumbile yamempatia mwanadamu haki maalum ni madai ya kibinafsi na ya kipuuzi. Kwa kusema kweli hakuna tofauti kati ya haki za wanaadamu na viumbe wasiokuwa wanaadamu.

Lakini huu sio uhalisia, vipawa vya kiakili ni tofauti. Maumbile yameiweka kila spishi (kiumbe) iliyopo ulimwenguni katika obiti yake maalum, na inaweza kuwa na mafanikio tu kama itasonga ndani ya mipaka yake. Muumba amefanya hivyo kwa malengo, na mpangilio huu sio wa bahati nasibu.

Msingi wa haki za kifamilia, ambalo ndilo jambo linalojadiliwa hapa, lazima litazamwe kiasili (kimaumbile) kama ilivyo kwa haki nyingine za asili. Kama tukitazama vipaji vya asili vya mwanaume na mwanamke, tunaweza kuona kwa urahisi, iwapo wanaweza kuwa na haki na wajibu unaofanana au la. Lazima ikumbukwe kuwa, kama tulivyoonyesha huko nyuma kuwa nukta inayohisabiwa ni kufanana kwa haki zao sio usawa wa haki zao.

Haki Za Kijamii.

Nafasi ya mwanadamu, kuhusiana na haki za kijamii zisizo za kifamilia, siku zote hazinafanani. Katika hali fulani huwa na haki zinazofanana lakini katika hali fulani nyingine haki zao huwa hazifanani lakini huwa na haki sawa. Katika jamii haki zote za msingi huwa sawa kwa watu wote. Kila mtu, kwa mfano, ana haki ya kutumia vipaji vyake kufanya kazi na kushiriki katika mashindano ya maisha, huwa mgombea katika nafasi fulani ya kijamii na kuipata katika njia za halali, kuonyesha uwezo wake kiakili na kivitendo.

Lakini usawa huu huu wa wote juu ya haki za msingi huwaweka katika nafasi zisizo sawa. Kwa mfano, kila mtu ana haki ya kufanya kazi na kushiriki katika ushindani wa maisha, lakini inapokuja katika utendaji wenyewe kivitendo, haiwezekani wote wakafanya kazi vizuri kwa ubora unaolingana. Wengine wanaweza sana na wengine kidogo. Halikadhalika wengine wana ufanisi mkubwa zaidi kuliko wengine. Tena wengine wana elimu zaidi wanamudu zaidi majukumu, wana ufanisi mkubwa zaidi na wanafaa zaidi kuliko wengine. Ni dhahiri kuwa haki zao walizojipatia haziwezi kufanana. Kujaribu kuzifanya haki zao walizojipatia kwa jitihada na vipaji vyao, zifanane haitakuwa kitu kingine isipokuwa dhulma iliyo wazi.

Sababu ambayo ni kwa nini wanaadamu wana haki sawa na zinazofanana ni kuwa uchunguzi wa masuala ya binadamu unathibitisha kuwa hakuna aliyeumbwa akiwa bwana mkubwa, au bwana mdogo. Hakuna aliyezaliwa akiwa mfanyakazi, fundi, mwalimu, ofisa, askari au waziri. Nafasi hizi na madaraja mbali mbali ni sehemu ya haki anazojipatia mtu kwa kipaji na jitihada zake binafsi. Watu wanapaswa kujitafutia haki hizi kwa mujibu wa uwezo, vipaji na jitihada zao.

Hapa ndipo ilipo tofauti kati ya maisha ya kijamii ya wanaadamu na yale ya wanyama wanaopenda kushirikiana kama vile nyuki. Muundo wa maisha ya nyuki ni wa asili/silika kwa asilimia mia moja.

Majukumu na kazi mbali mbali zimegawiwa kwa kila mmoja wao na maumbile yenyewe. Baadhi yao wamezaliwa wakiwa machifu na wengine wamezaliwa wakiwa na vyeo vya chini. Baadhi yao huzaliwa wakiwa wahandisi, wengine wakiwa maafisa utawala na wengine wakiwa wafanya kazi wa kawaida. Lakini maisha ya mwanadamu yako tofauti kabisa.

Hii ndio sababu baadhi ya wasomi wameikana kabisa ile nadharia ya kale ya kifalsafa inayosema kwamba mwanadamu ni kiumbe wa kijamii kimaumbile na wameonelea kuwa jamii ya wanaadamu ni ya kimkataba (kimaafikiano) kwa asilimia mia moja.

Haki Za Kifamilia

Haya yote yalikuwa yanahusu jamii isiyo ya kifamilia. Sasa vipi kuhusu jamii ya kifamilia? Je, watu wote katika jamii ya familia pia wana nafasi inayofanana na ile ya haki zao wanazojipatia, au je, suala la jamii ya kifamilia, ambayo ina mke na mume, wazazi na watoto na kaka na dada ni tofauti, na je, kuna sheria maalum ya asili inayohusiana na haki za kifamilia?

Katika suala hili kuna kuwepo na uwezekano wa mambo mawili. Mojawapo ni kuwa uhusiano kati ya mke na mume au kati ya wazazi na watoto ni kama mahusiano mengine yoyote ya kijamii. Ushirikiano wao ni sawa na ule wa chombo cha watu serikalini na kwenye makampuni. Mahusiano haya hayamaanishi kuwa baadhi ya watu kiasili wana nafasi maalumu.

Ni kutokana tu na sifa binafsi za mtu ndio inatokea kuwa mwingine ni bosi na mwingine ni wa cheo cha chini, mmoja hutoa amri na wengine hutii, mwingine kwa mwezi anapata mshahara mkubwa na mwingine mdogo. Kuwa mume au mke au kuwa baba, mama au mtoto pia haimaanishi kuwa kila mmoja katika hawa ana nafasi maalum. Ni sifa zao wanazojipatia ambazo huamua nafasi zao katika mahusiano yao.

Nadharia ya kufanana kwa haki za kifamilia kati ya mwanaume na mwanamke (ambayo kwa makosa inaitwa usawa wa haki) imeegemea katika uwezekano huu. Kwa mujibu wa nadharia hii, mwanaume na mwanamke hushiriki katika maisha ya kifamilia kwa uwezo sawa, mahitaji sawa na haki sawa za asili. Hivyo, haki zao za kifamilia lazima ziwekwe katika msingi wa kufanana.

Kwa mujibu wa uwezekano mwingine, hata haki zao za msingi zinatofautiana. Mume ana haki na majukumu fulani na mke ana haki na majukumu yake fulani. Halikadhalika kwa baba, mama na mtoto. Katika hali yoyote ile jamii ya kifamilia ni tofauti kabisa na taasisi nyingine za kijamii. Ni uwezekano huu, ambao kwawo dhana ya kutofanana kwa haki kati ya mwanamke na mwanaume imejengwa, na ambayo imekubaliwa na Uislamu.

Sasa hebu tuangalie ni uwezekano upi kati ya aina hizi mbili hapo juu ni sahihi, na ni jinsi gani tunaweza kujua usahihi wake.

Madai Ya Asili Ya Haki Za Kifamilia.

Ili kufikia katika hitimisho sahihi wasomaji wanashauriwa kuzingatia nukta zifuatazo ambazo tayari tumeshazijadili katika suala hili:

Haki za asili zimeibuka kutokana na ukweli kuwa maumbile yana lengo lililo wazi, na kuzingatia lengo hilo katika mtazamo, maumbile yamejaalia viumbe vyote hai uwezo fulani na kuweka juu yao haki fulani.

Mwanadamu kama alivyo anafaidi haki fulani zijulikanazo kama haki za binadamu, haki ambazo wanyama hawazifaidi.

Ili kuzijua haki za asili na sifa zake, tunapaswa kuyatazama maumbile yenyewe. Kila uwezo wa asili ni mamlaka kwa ajili ya haki ya asili.

Wanaadamu wote, kama wanajamii, wana haki za asili sawa na zinazofanana, lakini wanatofautiana katika haki walizojipatia wenyewe ambazo zinategemeana na kazi zao, sifa zao na ushiriki wao katika ushindani wa maisha.

Sababu ambayo kwa nini wanaadamu wote katika jamii wana haki sawa na zinazofanana ni kwamba uchunguzi wa masuala ya wanaadamu umeweka wazi kuwa hakuna aliyezaliwa akiwa bwana mkubwa au akiwa na cheo cha chini, akiwa mwajiri au mwajiriwa, akiwa mtawala au mtawaliwa, au akiwa kamanda au askari wa kawaida. Maisha ya mwanadamu ni tofauti na yale ya wanyama wanaopenda kushirikiana kama vile nyuki. Muundo wa maisha ya mwanadamu haukuamuliwa na maumbile wala maumbile hayakuwapangia watu kazi na vyeo mbali mbali.

Nadharia ya kufanana kwa haki za kifamilia za mwanaume na mwanamke imejengwa juu ya dhana kuwa jamii ya kifamilia (wanafamilia) ni kama jamii nyingine ya watu. Wanafamilia wote wanaishi kwa uwezo sawa na mahitaji sawa. Maumbile yamewapa haki zinazofanana. Sheria ya maumbile haijawapangia muundo fulani maalumu, wala haijawapangia kazi na majukumu mbali mbali.

Ama nadharia ya kutofanana kwa haki za familia imejengwa juu ya dhana kuwa jamii ya kifamilia ni tofauti na jamii nyinginezo za kiraia. Mwanaume na mwanamke hawana uwezo na mahitaji sawa. Sheria ya uumbaji imewaweka katika nafasi zinazotofautiana na imepanga majukumu tofauti kwa kila mmoja.

Sasa hebu tunagalie ni nadharia gani ni sahihi na kwa nini.

Suala hili linaweza kuamuliwa kirahisi tukitumia kigezo ambacho tayari tumeshakitaja na kama tukitazama uwezo na mahitaji ya jinsia zote mbili, ambazo zinajenga mamlaka ya asili ya kudai haki za asili.

Je, Maisha Ya Kifamilia Ni Ya Asili Au Ya Kimkataba?

Tumeshataja hapo awali kuwa kuna mitazamo miwili juu ya maisha ya kijamii ya mwanadamu. Baadhi wanaamini kwamba kwa asili mwanadamu ni jamii kwa maumbile, ambapo wengine wanashikilia kuwa maisha ya kijamii ni suala la kimkataba na maisha haya yamechaguliwa na mwanadamu kwa hiari yake chini ya ushawishi wa vipengele vinavyolazimisha. Lakini vipengele hivi ni vya nje sio vya ndani.

Hata hivyo, kama ambavyo maisha ya kifamilia yahusikavyo, hakuna mtazamo zaidi ya mmoja. Wote wanakubali kuwa maisha ya kifamilia ni ya asili kwa asilimia mia moja. Mwanadamu amezaliwa akiwa mwanafamilia kwa asili. Hakuwezi kuwa na rai mbili juu ya hili.

Hata baadhi ya wanyama, kama vile njiwa na baadhi ya wadudu ambao wanaishi kwa jozi, japo hawaishi maisha ya kijamii kabisa lakini wana aina fulani ya ndoa.

Hivyo, suala la maisha ya kifamilia ni tofauti na maisha ya kijamii. Maumbile yamechukua hatua fulani kuhakikisha kuwa mwanadamu na baadhi ya wanyama kwa silika wanakuwa na mwelekeo wa kupenda kuishi maisha ya kifamilia, kuunda familia na kuwa na watoto.

Maisha ya mwanadamu wa kale, yawe ni ya kurithi mfumo jike au mfumo dume, lakini wakati wote aliishi maisha ya kifamilia.

Nadharia Ya Vipindi Vinne.

Kuhusiana na suala la umiliki wa mali jambo hili linakubaliwa na wote kuwa awali mali ilimilikiwa na jamii nzima (kwa pamoja) na kwamba kumiliki mali mtu mmoja mmoja kulikuja baadaye. Lakini hilo halijawahi kuwa suala la jinsia. Sababu ya umiliki mali binafsi mwanzoni kuwa na kipengele cha kijamii ni kwamba maisha wakati ule yalikuwa ni ya kikabila na kabila zima liliunda familia moja. Wanakabila ambao walikuwa wakiishi pamoja walikuwa na mawazo ya kuishi katika familia moja. Ndio maana mali ilikuwa ikimilikiwa na kabila zima.

Katika jamii duni za kale hapakuwa na sheria wala mila ambayo ingeamua jukumu la mwanaume na mwanamke. Yalikuwa ni maumbile tu na hisia za asili ambazo ziliwafanya watekeleze majukumu fulani na waheshimu haki fulani. Hata katika hali hii hawakujiingiza katika ngono holela.

Vile vile wanyama wale waliokuwa wakiishi katika jozi, japo hawakuwa na sheria ya kimkataba au kijamii walizingatia sheria ya asili ya haki na majukumu, na hivyo maisha yao ya ngono sio ya holela.

Mrs. Mehr Angiz Manuchehriyan katika dibaji ya kitabu chake, '*Maoni Juu Ya Katiba Na Sheria Ya Kiraia Ya Iran*' anasema: Kwa mtazamo wa kisosholojia maisha ya mwanaume na mwanamke katika sehemu mbali mbali za dunia yanapitia katika moja ya hatua hizi nne.

1. Hatua ya asili

2. Hatua ya mwanaume kumtawala mwanamke

3. hatua ya mwanamke kupinga kutawaliwa na mwanaume

4. Hatua ya usawa wa haki kati ya mwanaume na mwanamke.

Anaendelea kusema kuwa katika hatua ya mwanzo mwanamke na mwanaume walikuwa wanachanganyika bila kizuizi chochote.

Sosholojia haikubaliani na mtazamo huu kabisa. Kama kuna kikubwa zaidi sosholojia inachokikubali ni kuwa ilikuwa ni mila katika baadhi ya makabila duni (ya kijima) kwamba makaka kadhaa kwa pamoja walioa madada kadhaa. Na hao makaka wote walikuwa wakiwaingilia madada wote mchanganyiko na watoto walikuwa ni wa wote. Mila nyingine ni kuwa wavulana na wasichana kabla ya ndoa hawana kizuizi. Ni ndoa tu inayowawekea kizuizi. Hizi ni mila mbili tu zinazojulikana. Hata hivyo, kama kuna kabila la kijima linalokwenda zaidi ya mipaka hii na linaruhusu ngono holela basi suala lake ni la kipekee na sio la kawaida.

Will Durant katika kitabu chake, *'History of Civilization'* Jalada la kwanza, anasema 'Ndoa ni ugunduzi wa wahenga (mababu) wetu waliokuwa wanyama. Katika baadhi ya ndege inaonekana kuwa ni ukweli kuwa kila ndege hubaki kushikamana na mke/mume wake maalum. Miongoni mwa sokwe na jamii ya nyani wakubwa kujamiiana kati ya dume na jike huendelea hadi mtoto aliyezaliwa anapokuwa mkubwa. Katika mambo mengine uhusiano huu unafanana na uhusiano kati ya mwanaume na mwanamke (watu). Jike linapojaribu kujisogeza kwa dume jingine, hufokewa vikali na lile dume –mume. Jamii ya nyani wanaishi katika familia yenye dume, jike na mtoto. Ni kawaida kwa sokwe, baba na mama (sokwe) kukaa chini ya mti kula matunda wakati mtoto anakwea miti jirani yao.

Historia ya mahusiano ya unyumba ni kongwe kuliko mwanadamu mwenyewe. Kuna jamii chache ambazo hazina mahusiano ya unyumba. Hata hivyo, mtu akijaribu kuzitafuta anaweza kupata chache sana.

Tunachosisitiza hapa ni kuwa hisia za kifamilia ni za asili na za silika kwa wanaadamu, na sio zao la ustaarabu na tabia. Kuna wanyama wengi pia wenye hisia kama hizi kisilika.

Hii ndio sababu, hakuna wakati wowote katika historia ambapo wanaume na wanawake waliishi pamoja bila kuwekeana mipaka ya ngono. Hata wale wanaodai kuwepo kwa ukomunisti wa kifedha katika zama za ujima hawadai kuwepo kwa ukomunisti wa ngono.

Nadharia ya vipindi vinne vya mahusiano ya mwanaume na mwanamke ni muigizo wa kitoto wa vipindi vinne vya umiliki wa mali, ambavyo wajamaa wanaamini. Wanashikilia kuwa katika suala la kumiliki mali, mwanadamu amepitia vipindi vinne, kipindi cha ujima, ukabaila, ubepari na ujamaa wa kisayansi, ambao ni kurudia kwa ujima lakini katika kiwango cha juu.

Inachekesha kuona kuwa Mrs. Manushehriyan anakiita kipindi cha nne uhusiano kati ya mwanaume na

mwanamke kuwa ni kipindi cha usawa wa haki na hakiiti kuwa ni kurudi kwa ujima. Katika hili hakufuata mfano wa wajamaa, ingawa anadai kuwa kuna mambo mengi yanayofanana kati ya kipindi cha nne na kipindi cha kwanza. Anasema kuwa kipindi cha nne kinafanana na kipindi cha kwanza kwa sababu katika zama zote hizi mbili mwanaume na mwanamke waliishi bila yeyote kati yao kuwa na madaraka juu ya mwenzake.

Bado hatuelewi anachokimaanisha hasa pale anaposema vipindi hivi (cha kwanza na cha nne) vinafanana kwa kiasi kikubwa. Kama anamaanisha kuwa katika kipindi cha nne vipingamizi vya kuchanganyika kiholela pole pole vitaondoka na familia haitakuwepo tena basi anachomaanisha juu ya usawa wa haki ambao yeye ni mtetezi wake mkubwa, ni tofauti kabisa na kile watetezi wengine wa haki za binadamu wanachokidai na wazo lake hili linaweza hata kuwakera wengine.

Sasa hebu tugeuzie macho yetu kwenye asili ya hali za kifamilia za mwanaume na mwanamke. Katika hili lazima tuzingatie mambo mawili kichwani. Moja ni iwapo asili (maumbile) ya mwanamke ni tofauti na mwanaume au la kwa maneno mengine, kuangalia kama tofauti kati ya mwanaume na mwanamke ipo katika mfumo wa uzazi tu, au ina kwenda ndani zaidi.

Nukta ya pili ni kuwa iwapo kuna tofauti nyingine pia, je tofauti hizi zinaathiri haki na majukumu yao au la, au ni kama tofauti ya rangi na utaifa, mambo ambayo hayana uhusiano wowote na asili ya haki za binadamu?

Mwanamke Katika Maumbile

Kuhusiana na nukta ya kwanza, hatudhani kwamba ina ubishi. Kila mtu aliyesomasoma juu ya suala hili anajua kuwa tofauti kati ya mwanamke na mwanaume haibakii katika mfumo wa uzazi tu. Suala hapa ni iwapo tofauti hizi zinasababisha katika haki na majukumu yao au la.

Wanasayansi na wachunguzi wa kizungu wameifanyia utafiti mkubwa nukta hii, na matokeo ya utafiti wao wa kibailojia, kisaikolojia na kisosholojia hayajaacha chembe yoyote ya shaka juu ya ukweli huu. Lakini ambacho wasomi hawa hawajakitupia macho vya kutosha ni kuwa tofauti hizi kati ya mwanamke na mwanaume zinasababisha kutofanana kwa haki zao na majukumu ya kifamilia, na kuwa tofauti hizi zinawaweka katika nafasi zinazofanana.

Msomi mashuhuri duniani wa kifaransa ambaye ni mwanasaikolojia, daktari wa upasuaji na mwanabaiolojia, Alexis Carrel, katika kitabu chake bora kabisa, *'Man, the Unkown Being'* (mwanadamu kiumbe asiyefahamika), anakiri kuwa, kwa mujibu wa sheria ya maumbile, mwanaume na mwanamke wameumbwa tofauti na kwamba tofauti zao zinafanya haki na majukumu yao kuwa tofauti.

Katika kitabu chake ameweka sura moja yenye jina "Kazi za Kijinsia na Jenetiksi" katika sura hiyo anasema; korodani na ovari zina kazi nyingi sana. Viungo hivi havizalishi mayai na mbegu za uzazi na hivyo muungano wake kusababisha kuzaliwa kwa binadamu mpya peke yake, lakini pia huzalisha

uowevu (fluid) ambao humwagwa katika damu na hivyo husababisha tabia za kike na kiume katika hisia zetu na katika tishu na viungo vyetu vya mwili. Ni uoevu unaozalishwa na korodani ambao husababisha ukakamavu, ushujaa, moyo (thabiti) na kutoogopa. Ni sifa hizi zinazomtofautisha ng'ombe maksai na fahali. Ovari pia humuathiri mwanamke hivyo hivyo.

Tofauti zilizopo kati ya mwanaume na mwanamke hazihusiani pekee na sura ya viungo vyao vya uzazi au mwanamke kuwa na tumbo la uzazi na kujifungua watoto na mfumo wao maalum wa elimu, bali ni matokeo ya sababu kubwa zaidi. Inatokana na kemikali zinazozalishwa na tezi za uzazi na kumwagwa katika damu.

Ni kutokana na kuipuuza nukta hii muhimu ndio baadhi ya watetezi wa harakati za wanawake wanafikiri kuwa jinsia zote mbili zinaweza kupata aina moja ya elimu na mafunzo na wanaweza kuchukua elimu na mafunzo ya aina moja na wanaweza kusomea aina moja ya fani/kazi na majukumu yanayofanana. Kwa kusema kweli mwanamke anatofautiana na mwanaume katika mambo mengi.

Kila seli ya mwili wa mwanadamu na mifumo yote ya maungo, hasa mfumo wa misuli, ina alama ya jinsia. Sheria za fiziolojia pia, kama za unajimu ni thabiti na hazibadiliki. Tabia za watu haziwezi kuzibadilisha. Tunapaswa kujaribu kuendeleza vipaji vyao katika mwelekeo unaoafikiana na haiba yao ya ndani, bila kuwaiga wanaume kibubusa. Ni jukumu lao kutoa mchango mkubwa zadi kuliko mwanaume katika maendeleo ya mwanadamu. Wasiyachukulie majukumu yao kiwepesi.

Carrel, baada ya kuelezea kukua kwa manii na mayai na jinsi muungano wao unavyotokea anaonyesha kuwa kuwepo kwa mwanamke ni muhimu kwa uzazi lakini sio kuwepo kwa mwanaume. Anaongeza kuwa mimba huukamilisha mwili na roho ya mwanamke. Mwisho wa sura anasema tusiwatazame/tusiwachukulie wasichana wadogo kwa mtazamo wa kufikiri aina moja ya maisha na namna moja ya ndoto na namna moja ya ukamilifu wao kama wavulana wadogo. Wataalamu wa masuala ya elimu na mafunzo wazingatie tofauti zao za maungo na kifiziolojia na majukumu ya asili ya mwanaume na mwanamke. Zingatio la nukta hii ya msingi ni muhimu sana kwa mustakabali wa ustaarabu wetu.

Kama ulivyoona, mwanasayansi huyu mkubwa anaweka msisitizo katika tofauti nyingi zilizopo kati ya mwanamke na mwanaume na anaamini kuwa tofauti hizi zinawaweka katika nafasi tofauti.

Katika sura inayofuata pia, tutanukuu maoni ya wanasayansi juu ya nukta hii, na kisha tutafikia hitimisho kuwa ni maeneo gani ambayo mwanaume na mwanamke wana uwezo na mahitaji sawa na hivyo wanastahili haki na majukumu yanayofanana na ni katika maeneo gani wana nafasi tofauti na hivyo haki na majukumu yasiyofanana.

Sehemu hiyo ya kitabu itakuwa muhimu sana kuliko nyingine zote juu ya somo na upangaji wa haki na majukumu ya kifamilia kati ya mwanaume na mwanamke.

Tofauti Kati Ya Mwanamke Na Mwanaume.

Hii inaonekana kuwa sentensi isiyofaa. Inaonekana kuwa japo tupo katika karne hii, bado kuna baadhi ya watu, hapa na pale, ambao wana mawazo ya kizamani, na bado wanang'ang'ania wazo lililopitwa na wakati la tofauti kati ya mwanaume na mwanamke. Kama watu wa zama za kati (1500 A.D), watu hawa bado wanamuona mwanamke kuwa wa jinsia ya cheo cha chini na kwamba sio mwanadamu kamili na kamilifu. Yupo katikati si binaadamu wala si mnyama. Hafai kuishi maisha ya kujitegemea na lazima aishi chini ya uangalizi na udhibiti wa wanaume.

Lakini sasa tunajua kuwa mawazo yote haya yamepitwa na wakati na hayafai. Leo hii tunajua fika kuwa dai potofu la kudaiwa kuwa mwanamke sio mkamilifu lilizushwa na mwanaume katika enzi zile ambazo alikuwa anamtawala mwanamke. Sasa, habari iliyothibitishwa ni kwamba mwanamke anatokana na jinsia bora zaidi na mwanaume anatokana na jinsia duni.

Haya ni maoni ya baadhi ya Wamagharibi wa kisasa. Kwa ukweli kabisa, maendeleo ya sayansi ya karne ya 20 yamethibitisha wazi wazi kuwepo kwa tofauti kati ya mwanaume na mwanamke. Kuwepo kwao sio uwasilishaji mbaya wa kijicho, bali ni ukweli wa kisayansi, uliotokana na uchunguzi na majaribio. Hata hivyo tofauti hizi hazipo ili kuthibitisha ni jinsia gani ni bora kuliko nyingine. Sheria ya maumbile imeziweka tofauti hizi ili mahusiano ya ndoa yawe imara zaidi na kuufanya msingi wa muungano kati ya mume na mke uwe mkubwa, imara na bora zaidi.

Maumbile yalitaka kugawa haki za kifamilia na majukumu yake baina yao kwa mikono yake (maumbile) yenyewe. Sheria ya maumbile umezifanya tofauti kati ya mwanaume na mwanamke sawa na tofauti ya viungo mbali mbali vya mwili. Imetoa nafasi mbali mbali kwa macho, masikio, mikono, nyayo na uti wa mgongo. Lakini haimaanishi kuwa imefanya dhulma na ubaguzi dhidi ya kiungo chochote.

Je Ni Uwiano Au Ukamilifu Na Kutokamilika?

Inashangaza kwamba baadhi ya watu wanasisitiza kuwa tofauti katika nguvu za kimwili na kisaikolojia za mwanaume na mwanamke hutokana na ukamilifu wa mwanaume na kutokamilika kwa mwanamke. Wanashikilia kuwa, kwa sababu fulani nzuri, kwa makusudi kabisa mwanamke ameumbwa akiwa sio mkamilifu.

Dhana ya kutokuwa mkamilifu kwa mwanamke imekuwa maarufu zaidi katika nchi za Magharibi kuliko Asia. Watu wa Magharibi wamemuonea. Wakati fulani wamekuwa wakitoa tafsiri mbaya ya maandiko ya kidini juu ya mwanamke, wanasema kwamba mwanamke ajione haya. Wakati fulani wanasema, 'Mwanamke ni kiumbe mwenye nywele ndefu na ubongo usiofaa,' 'mwanamke ni nusu ya mnyama na nusu ya mtu'n.k.

Bado inashangaza zaidi kuona kwamba baadhi ya watu wa Magharibi wamebadilisha mwelekeo wao

kwa nyuzi 180, hivi karibuni wameanza kuleta hoja elfu na moja kuthibitisha kwamba kwa mujibu wa maumbile, mwanaume ni duni na sio mkamilifu na kwamba jinsia ya mwanamke ni bora na mkamilifu.

Kama umeshakisoma kitabu, "*Woman, the Superior Sex,'* cha Ashley Montague, unaweza kuona ni jinsi gani mwandishi huyu, kwa kupotosha ukweli na kuleta hoja zisikubaliana na ukweli alivyojaribu kuthibitisha kuwa mwanamke ni mkamilifu zaidi kuliko mwanaume. Katika fani za utabibu, saikolojia na takwimu za jamii kitabu hiki kinafaa sana, lakini pale mwandishi anapojaribu kutoa hitimisho lake kuthibitisha dai lake, ambalo ndio jina la kitabu anakwenda kwenye upuuzi mkubwa kabisa.

Haifahamiki kwa nini ni lazima kwa watu wa Magharibi kwamba siku moja wamuumbue mwanamke na kumuadhiri ili siku ya pili warekebishe yale ya nyuma, wanalazimika kumuondolea mapungufu na udhaifu waliokuwa wamembandikia na badala yake wanambandikia hayo mwanaume. Kuna umuhimu gani wa kuangalia tofauti kati ya mwanaume na mwanamke kwa matokeo ya ukamilifu wa jinsia mmoja na upungufu wa jinsia nyingine, ili kwamba wakati mwingine tulazimike kumuweka mwanaume upande na wakati mwingine mwanamke?

Mwandishi wa kitabu hiki anasisitiza kuwa mwanamke ni bora kuliko mwanaume na anaona kuwa utukufu alionao (mwanaume) ni matokeo ya sababu za kihistoria na kijamii na sio matokeo ya sababu za asili.

Kwa kusema kweli, tofauti kati ya mwanaume na mwanamke ni suala la uwiano sio ukamilifu na kutokamilika. Sheria ya maumbile imeamua kuwa kwa kuwa mwanaume na mwanamke wameumbwa ili waishi pamoja, lazima wawe na uwiano mahususi wa vipaji vyao licha ya tofauti hizi. Nukta hii itafafanuliwa baadaye.

Nadharia Ya Plato.

Suala la tofauti kati ya mwanamke na mwanaume sio jipya ambalo tunaweza kusema kuwa limeibuka katika zama zetu. Lina umri wa miaka zaidi ya 2400. Lilijadiliwa katika sura yake ya sasa, na Plato katika kitabu chake *'The Republic'.*

Kwa uwazi anaelezea kwamba wanaume na wanawake wana vipaji sawa, na wanawake wanaweza kufanya kazi za kiume na kupata haki kama zile za wanaume.

Chanzo cha mawazo yote kuhusu mwanamke, ambayo yameibuka katika karne ya 20, na hata sehemu ya mawazo haya yanayoonekana kuwa ya ovyo na yasiyobadilika kwa watu wa karne ya 20, yamo katika mitazamo ya Plato. Hii ndio sababu watu wanavutiwa naye sana na kumuita 'Baba wa Falsafa'.

Plato katika sura ya tano ya kitabu chake, *'The Republic'* alizungumzia masuala kama vile ukomunisti wa wanawake na watoto, kuboresha kizazi (breed), kuwa hasi baadhi ya wanaume na wanawake, kuwaruhusu kuzaa wale tu wenye sifa zilizotukuka za kijenetiki, kulea watoto nje ya mazingira ya kifamilia na kuruhusu kuzaa katika miaka fulani tu ya uhai, katika kipindi ambacho nguvu (za uzazi) zipo

kilelelenі. Plato anaamini kuwa kama ilivyo kwa mwanaume, mwanamke anapaswa kupewa mafunzo ya kijeshi na kama mwanaume anavyoshiriki katika riadha, mwanamke ashiriki pia.

Hata hivyo, kuna mambo mawili ambayo Plato ameyasema. Moja ni kuwa anakiri kuwa kimwili na kiakili wanawake ni dhaifu kuliko wanaume. Kwa maneno mengine anaiona tofauti kati ya mwanaume na mwanamke kuwa ni ya kiasi (ukubwa), sio sifa (ubora) wa vipaji vyao. Anaamini kuwa wote mwanaume na mwanamke wana vipaji. Kitu pekee ni kuwa katika baadhi ya mambo mwanamke ni dhaifu kuliko mwanaume, lakini haoni sababu kwa nini awe na mfumo wa kipekee wa kuendesha mambo.

Kwa vile Plato anamuona mwanamke kuwa dhaifu kuliko mwanaume, anamshukuru Mungu kuwa alizaliwa mwanaume. Anasema; “Namshukuru Mungu kwa kuzaliwa kwangu Mgiriki (myunani) na sio vinginevyo, kwa kuzaliwa kwangu nikiwa huru na sio mtumwa na kuzaliwa kwangu mwanume na sio mwanamke.”

Nukta ya pili ni kuwa yote aliyoyasema Plato ya kuhusu kuboresha ukoo (uzazi), vipaji vya jinsia zote mbili na ukomunisti wa mwanamke na watoto yanahusiana na tabaka tawala, yaani wanafalsafa watawala, kwa sababu kwa mujibu wake, ni tabaka hili tu ndio linafaa kuwa watawala. Kama tunavyojua kisiasa, Plato alikuwa ni mpinga demokrasia na alikuwa akitetea utawala wa matabaka. Hivyo, alichokisema katika nukta hizo, kinahusiana na tabaka tawala. Kuhusiana na matabaka mengine, ana maoni tofauti.

Aristole Dhidi Ya Plato.

Mwanafunzi wa Plato, Aristole ni mwanafikra mwingine wa ulimwengu wa kale, ambaye maoni na mawazo yake tunayo. Ametoa maoni juu ya tofauti kati ya mwanamke na mwanaume na ameyapinga vikali maoni ya mwalimu wake. Anaamini kuwa mwanaume na mwanamke wanatofautiana sio kwa kiasi tu bali hata kwa sifa. Anasema kwamba jinsia hizi mbili zina vipaji vya aina tofauti na majukumu waliyopewa na sheria ya maumbile na haki walizopewa, vyote vinatofautiana sana.

Kwa mujibu wa Aristole, kanuni zao za maadili pia zinatofautiana katika mambo mengi. Inawezekana kuwa sifa ya maadili ikawa bora kwa mwanaume lakini isiwe hivyo kwa mwanamke na kinyume chake. Katika ulimwengu wa kale maoni ya Plato yaliondolewa, yakachukuliwa ya Aristole. Wasomi waliofuatia walipendelea maoni ya Aristole kuliko ya Plato.

Mtazamo Wa Ulimwengu Wa Sasa.

Hayo yalikuwa ya ulimwengu wa kale. Sasa hebu tuangalie ulimwengu wa sasa unavyosema. Ulimwengu wa sasa haubahatishi wala kukadiria. Unatumia njia za kisayansi. Hitimisho zake zimejengwa juu ya ukweli, takwimu na utafiti katika ulimwengu wa sasa. Kama matokeo ya elimu kubwa na sahihi zaidi katika medani za utabibu, saikolojia na maarifa ya jamii, tofauti nyingi na kubwa, zaidi kati ya mwanamke na mwanaume, zilizokuwa hazijulikani katika ulimwengu wa kale, sasa zimegunduliwa.

Watu wa kale walitathimini mwanaume na mwanamke kwa msingi wa kuwa mmoja ni mwenye kukwaruza sana, mrefu ana nywele nyingi zaidi mwilini, ana maungo makubwa zaidi na ana sauti nene zaidi wakati mwingine ana mwili nyororo zaidi, mfupi zaidi, na msafi zaidi, ana sauti nyembamba zaidi na ana maungo madogo zaidi. Waliozama zaidi walizingatia tofauti ya umri wao wa kukua (kubalehe na kuvunja ungo) na tofauti ya akili na hisa zao. Walimchukulia mwanaume kama alama ya busara, na mwanamke kama alama ya upendo na mihemko.

Lakini leo tofauti nyingi zaidi zinajulikana sasa kwamba ulimwengu wa mwanamke ni tofauti na ulimwengu wa mwanaume katika mambo mengi. Kwanza tutasimulia tofauti kati ya mwanaume na mwanamke, kwa mujibu wa tulivyozikusanya kutoka kwa wataalamu mabingwa wa fani hii. Kisha tutaeleza falsafa yake na tutaonyesha tofauti zipi ni za asili na zipi ni matokeo ya kihistoria, kiutamaduni na vipengele vya kijamii. Baadhi ya tofauti hizi ziko wazi mno kiasi cha kuwa huwezi kuzikana. Elimu ya wengine (juu ya hili) inaweza kupatikana kwa kusoma kidogo na uzoefu.

Uwili

Kimwili, mwanaume kwa wastani ana maungo makubwa na mwanamke ana maungo madogo. Mwanaume ni mrefu zaidi na mwanamke ni mfupi zaidi. Mwanaume ana ngozi inayo kwaruza na mwanamke ana ngozi laini zaidi. Sauti ya mwanaume inaparuza na ni nzito, na sauti ya mwanamke ni nyororo na inavutia.

Mwili wa mwanamke unakuwa haraka zaidi na wa mwanaume unakuwa pole pole zaidi. Inasemekana hata mimba ya mtoto wa kike inakua haraka ziadi kuliko mimba ya mtoto wa kiume. Mwanaume ana nguvu zaidi kuliko mwanamke, na ana misuli imara zaidi, lakini mwanamke ana uwezo mkubwa zaidi wa kustahimili kuliko mwanaume. Mwanamke huvunja ungo mapema na hufikia umri wa kuacha kuzaa mapema zaidi. Msichana huwahi kuanza kuzungumza kuliko mvulana.

Ubongo wa mwanaume ni mkubwa kuliko ubongo wa mwanamke lakini ukiwianishwa na mwili mzima (ukubwa wake ukigawanywa na ukubwa wa mwili mzima), mwanamke ana ubongo mkubwa zaidi. Mapafu ya mwanaume yanaweza kuvuta hewa nyingi zaidi kuliko mapafu ya mwanamke. Moyo wa mwanamke hupiga haraka zaidi kuliko moyo wa mwanaume.

Kisaikolojia, mwanaume anapenda zaidi mazoezi, kuwinda na maisha ya heka heka nyingi. Hisia za mwanaume ni changamoto na ugomvi ambapo mwanamke ni mwenye kupenda amani. Mwanamume ni mchokozi na mtu wa hima, mwanamke ni mtulivu na mkimya. Mwanamke huepuka mapigano na mambo ya nguvu nguvu na ndio maana kesi za wanawake kujinyonga ni chache zaidi.

Hata wakati wa kujinyonga wanaume hutumia njia za hatari kama vile kujipiga risasi, kujinyonga kwa kamba au kujirusha kwenye majengo marefu wakati wanawake hutumia, vidonge vya usingizi, madawa ya kulenya n.k. kwa ajili ya lengo hili. Mwanamke ana mihemko (jazba, hasira, furaha) ya haraka zaidi kuliko mwanaume na wanasisimka haraka zaidi. Mwanaume ni mtulivu wa akili zaidi.

Kwa asili mwanamke anapenda mapambo, manukato, vipodozi na vitu vya mitindo mipya mipya vya nguo, viatu n.k wakati mwanaume hayuko hivyo. Hisia za mwanamke sio thabiti (hazidumu), akili yake huwa inabadilika. Ni mwangalifu na huchukua tahadhari zaidi, ni mshika dini zaidi, mzungumzaji zaidi, muoga zaidi na anafuata taratibu zaidi kuliko mwanaume. Hisia zake ni za mfumo jike mama toka utoto wake. Hawezi kushindana na mwanaume katika maarifa ya kufasiri mambo yalivyo na masomo mengine makavu. Lakini katika fasihi na sanaa kama kupaka rangi, hayuko nyuma ya mwanaume.

Mwanaume ana uwezo mkubwa zaidi wa kuficha siri zake. Anaweza kuficha tukio baya lililomfika likabaki moyoni mwake tu na ndio sababu anakumbwa sana na magonjwa yanayosababishwa na undani (kuficha mambo moyoni). Mwanamke ni mwepesi kuhisi na mwenye moyo laini kuliko mwanaume, anaweza kuamua kulia kirahisi na wakati mwingine anaweza kupoteza fahamu.

Mtazamo Linganishi Wa Kila Mmoja

● Mwanaume ni mtumwa wa matamanio yake; mwanamke ni mtumwa wa mapenzi.

● Mwanaume humpenda mwanamke aliyempenda, mwanamke humpenda mwanaume aliyeitambua thamani yake (ya mwanamke huyo) na kutamka upendo wake kwake.

● Mwanaume hutaka kummiliki mwanamke, mwanamke hutaka kuutawala moyo wa mwanaume.

● Mwanaume hutaka kumzidi nguvu madaraka mwanamke, mwanamke hutaka kupenya katika moyo wa mwanaume.

● Mwanaume hutaka kumteka mwanamke; mwanamke hutaka kutekwa.

● Mwanamke hutaka mwanaume awe jasiri na shujaa na anayemjali, mwanaume hutaka mwanamke mwenye sura nzuri na mcheshi.

● Mwanamke hutaka ulinzi wa mwanaume, na huchukulia ulinzi huo kuwa ni kitu cha thamani zaidi anachoweza kukimiliki. Anaweza kuyadhibiti matamanio yake. Hisia za ngono za mwanaume ni kali na zenye nguvu za mwanamke ni baridi na zenye kusisimka.

Tofauti Kati Ya Mwanaume Na Mwanamke.

Mwana saikolojia wa kimarekani, Profesa Reek amechapisha matokeo ya utafiti wake juu ya mwanaume na mwanamke katika kitabu kikubwa. Anasema: Ulimwengu wa mwanaume ni tofauti kabisa na ule wa mwanamke. Ikiwa mwanamke hawezi kufikiri au kufanya mambo kama mwanaume, ni kwa sababu wanaishi katika dunia mbili tofauti.

Ameendelea kusema kuwa; “Kwa mujibu wa Agano la Kale, mwanaume na mwanamke wametokana na mwili mmoja. Hivyo ni kweli lakini ingawa wametokana na mwili mmoja, wana miili miwili tofauti, ambayo

haifanani kabisa katika maumbile yake. Hawana hisia za aina moja na hawaonyeshi mwitikio wa aina moja katika matukio na ajali mbali mbali. Wako kama sayari mbili zinazozunguka katika njia mbili tofauti. Wanaweza kuelewana na wanaweza kukamilishana, lakini sio kitu kimoja (sawa). Hii ndio sababu wanaweza kukaa pamoja, kupendana na wanaweza wasichokane.

Profesa Reek analinganisha roho ya mwanaume na mwanamke na anagundua tofauti nyingi. Anasema; “Inakinaisha (chosha) kwa mwanaume kukaa na mwanamke anayempenda muda wote. Lakini hakuna kitu kizuri kwa mwanamke kuwa karibu na mwanaume anayempenda.

Mwanaume mara zote anataka kubaki vile vile. Lakini mwanamke anataka kuamka akiwa tofauti na mpya kila siku.

Sentensi bora kabisa ambayo mwanaume anaweza kumwambia mwanamke ni kuwa ‘Mpenzi wangu, nakupenda.’ Sentensi nzuri kabisa ambayo mwanamke hupenda kumwambia mwanaume ni, ‘Naona fahari kuwa na wewe.’

Mwanaume aliyepata kuwa na wanawake wengi katika maisha yake huwavutia sana wanawake wengine. Lakini wanaume hawapendi wanawake waliopata kuwa na wanaume wengine huko nyuma. Wanaume wanapokuwa wazee hukosa furaha kwa sababu wanapoteza kazi walizokuwa wanazitegemea. Wanawake wazee huwa na furaha kwa sababu, kwa mtazamo wao huwa wameweza kumiliki vitu bora kabisa ambavyo mtu anaweza kutamani, nyumba na wajukuu wachache.

Bahati nzuri kwa mwanaume ni kujipatia nafasi inayoheshimika katika jamii. Lakini kwa mwanamke bahati ni kuuteka moyo wa mwanaume na kubaki nao katika maisha yake yote.

Mwanaume mara zote hutaka kumbadilisha mwanamke wa chaguo lake ili afuate dini na utaifa wake.

Kwa mwanamke ni rahisi kubadilisha dini yake na uraia kwa ajili ya mwanaume aliyempenda ikiwa ni pamoja na kubadilisha ubini wake baada ya kuolewa.

Kazi Bora Ya Uumbaji

Bila kujali swali iwapo kutofanana kati ya mwanaume na mwanamke kunasababisha tofauti ya haki na majukumu yao au la, kutofanana kwenyewe ni moja ya kazi bora kabisa na ya ajabu mno ya uumbaji. Ni suala amabalo humuelekeza mtu katika kumtambua Allah na Umoja wake. Kunathibitisha kuwa mfumo wa dunia hii umepangiliwa kwa busara kubwa sana na ubora usio na mfano. Kunaonyesha kuwa uumbaji sio suala la bahati nasibu. Maumbile sio kazi ya upofu. Haiwezekani kutafsiri mambo ya ulimwengu bila kumtambua ‘**Msababishaji Mkuu**.’ Kwa nia ya kuhifadhi jamii ya viumbe, utaratibu mkubwa wa uumbaji umefanya mfumo wa uzazi kuwepo.

Wanaume na wanawake wanazaliwa kila siku. Kwa vile kuendelea kwa jamii ya wanaadamu kunategemea ushirikianao wao, maumbile yakaona mwanaume na mwanamke wanahitaji kuishi pamoja.

Kwa ajili ya kusudio hili maslahi binafsi ambayo ni ya lazima kwa kila kiumbe yamebadilishwa na kuwa hisia za upendo, huduma, ushirikianao na uvumilivu. Ili kuufanya mpango huu uwezekane, na kuhakikisha kuwa miili yao na roho zao zinakubaliana vizuri na kwa raha, tofauti fulani za kiroho na kimwili zimewekwa kwa kila mmoja wao.

Tofauti hizi kati ya mwanamke na mwanaume zinawavuta wote kila mmoja kwa mwenzake. Kama mwanamke angekuwa na maumbile sawa kimwili, mihemko sawa na tabia sawa na mwanaume, isingewezekana kwake kumvutia mwanaume, kama ilivyo sasa. Kama mwanaume naye angekuwa na umbile la kimwili na kifiziolojia kama mwanamke, mwanamke asingemuona kuwa ndio sawa yake, asingefanya chochote kuuteka moyo wake. Mwanaume ameumbwa kuutawala ulimwengu, na mwanamke ameumbwa kumtawala mwanaume.

Sheria ya maumbile imepanga kwamba wote mwanamke na mwanaume wahitajiane na watafutane lakini uhusiano wao sio wa asili sawa na ile waliyo nayo kwa vitu vingine wanavyomiliki, uhusiano huo unatokana na ubinafsi. Wanataka kumiliki vitu kwa ajili ya matumizi yao, na wanavitafuta ili viwe chanzo cha raha na starehe yao. Lakini uhusiano kati ya mwanamke na mwanaume una maana kila mmoja miongoni mwao anataka furaha na raha ya mwenzake, na hufurahi kujitolea kwa ajili ya mwenzake.

Muungano Mkubwa Zaidi Kuliko Uchu Wa Ngono.

Inashangaza kwamba baadhi ya watu hawawezi kutofautisha kati ya uchu wa ngono na mapenzi. Wanafikiri kuwa uhusiano kati ya mume na mke umejengwa juu ya tamaa, matamanio na hisia ya unyonyaji. Wanashikilia kuwa uhusiano huu ni wa aina moja na ule alionao mtu kwa vitu anavyokula, kunywa, kuvaa au kuendesha. Watu hawa hawajui kuwa katika maumbile, mbali na mahusiano hayo yaliyojengwa juu ya maslahi binafsi, kuna mahusiano mengine pia. Haya ndio mahusiano ambayo yanayoonyesha ubinadamu. Mahusiano haya, kwa kiasi fulani yapo kwa wanyama pia hususani linapokuja suala la majike/madume yao na watoto.

Watu hawa wanafikiri kuwa mwanaume mara zote humtazama mwanamke, kama vile mwanaume asiye na mke anavyomtazama mwanamke malaya. Wanaamini kuwa ni uchu na matamanio ya ngono tu yanayoweza kuwaunganisha mwanamke na mwanaume. Kwa kusema kweli muungano wa ndoa ni kitu kikubwa zaidi kuliko uchu wa ngono, na msingi wake ni ule uliotajwa katika Qur'ani.

وَمِنْ آيَاتِهِ أَنْ خَلَقَ لَكُمْ مِنْ أَنْفُسِكُمْ أَزْوَاجًا لِتَسْكُنُوا إِلَيْهَا وَجَعَلَ بَيْنَكُمْ مَوَدَّةً وَرَحْمَةً ؟

"Na miongoni mwa dalili zake ni kuwa amewaumbia wenza wenu kutokana na nyinyi ili mpate utulivu kwao na baina yenu ameweka mapenzi na huruma." (***Suratul Ruum; 30:21***).

Ni kosa kubwa lilioje kuitafsiri historia ya uhusiano wa mwanaume na mwanamke kwa mtazamo wa ajira na unyonyaji au kwa msingi wa kupambana ili uishi. Lakini bado kuna watu wanaofanya hivyo na wanatoa hoja zisizo na msingi kutetea mawazo yao. Kwa kweli tunashangazwa sana kwa msingi wa migogoro na ukinzani, kana kwamba mwanaume na mwanamke ni matabaka mawili tofauti ya kijamii ambayo mara zote yapo katika migogoro. Kama inawezekana kuielezea historia ya uhusiano wa akina baba na watoto wao kwa msingi wa ajira na unyonyaji, basi hapo itawezekana pia kuielezea historia ya uhusiano wa waume na wake zao kwa msingi huo.

Ni kweli kwamba mwanaume amekuwa na nguvu zaidi kuliko mwanamke, lakini sheria ya maumbile imemuamrisha katika namna ambayo kwa silika hajaweza kumtendea vibaya au kwa ukatili mke wake kama ambavyo amekuwa akifanya kwa watumwa wake, walio chini ya cheo chake au miliki yake na wakati fulani hata kwa majirani zake.

Hatukatai kwamba mwanaume hajapata kufanya ukatili kwa mwanamke. Tunachopinga ni jinsi ukatili wake unavyoelezewa katika kipindi chote cha historia, wanaume wamewakandamiza wanawake, lakini pia waliwatendea vibaya watoto wao, licha ya upendo wote waliokuwa nao kwao. Sababu za ukatili huu zilikuwa ujinga, mila na kujipendelea wenyewe lakini sio kwa ajili ya kumnyonya mwanamke. Sababu hizi ndio hizo hizo zinazomfanya hata yeye mwenywe mwanaume ajikandamize na kujidhulumu, sababu hizi ni ujinga, desturi na tabia zilizozoeleka, na upendeleo (chuki) na sio tamaa binafsi zaidi.

Uwili Na Hisia Za Mwanamke Na Mwanaume Kwa Kumhusu Kila Mmoja

Sio tu kwamba mahusiano ya kifamilia ya mwanaume na mwanamke kwa mwenzake ni tofauti lakini pia hisia na mielekeo ya kila moja kwa mwenzake ni tofauti. Kwa maneno mengine, asili ya uhusiano wa mwanaume kwa mwanamke ni tofauti na uhusiano wa mwanamke kwa mwanaume, ingawa kila mmoja anavutiwa na mwenzake, lakini tofauti na ilivyo kwa viumbe visivyo hai, hapa kitu kidogo hukivutia kitu kikubwa kwake. Mwanaume ameumbwa kama udhihirisho wa kusubiri kwa hamu, mapenzi na mshughulikaji, na mwanamke kama udhihirisho wa mvuto na kutamanika. Hisia za hawa wawili ni tofauti lakini zinazokamilishana. Mmoja humtafuta mwenzake na mwingine huhitaji kutafutwa.

Wakati fulani uliopita, gazeti lilichapisha picha ya msichana mdogo wa Kirusi aliyekuwa amejinyonga. Msichana huyu aliacha ujumbe kuwa hakuna mwanaume aliyepata kumbusu hivyo maisha yake yamekuwa hayavumiliki tena.

Kwa msichana ni jambo la kukatisha tamaa sana kwamba hakuna mwanaume aliyepata kumbusu. Lakini mvulana mdogo haimsumbui kama msichana hajawahi kumbusu.

Will Durant katika mjadala wake mrefu, anasema msichana ambaye sifa yake kubwa ni elimu na uwezo mkubwa wa kufikiri tu, lakini hana ucheshi wa asili na ujanja wenye akili kidogo, haelekei kufanikiwa kupata mume. Asilimia sitini ya wanawake wenye elimu ya chuo Kikuu hubaki bila waume.

Amesema kwamba mwanamke mmoja mashuhuri na msomi alilalamika kuwa hakuna mtu aliyekuwa tayari kumuoa. Alikuwa akisema; “Kwa nini hakuna anayenipenda? Ninaweza kuwa mke bora kuliko wanawake wengine wengi. Lakini bado wanawake wasio na elimu na umuhimu wowote kijamii wanatafutwa na kuolewa lakini mimi sitafutwi.”

Inaweza kuonekana hapa kuwa hali ya kuvunjika moyo kwa mwanamke huyu ni tofauti na kwa mwanaume yeyote. Analalamika kwamba kwanini hakuna anayempenda.

Mwanaume huvunjika moyo tu pale ambapo anapokuwa hawezi kumpata mwanamke wa chaguo lake au anamtaka lakini anashindwa kumpata.

Hisia za mwanaume na mwanamke zimepangwa hivi, kwa makusudio maalumu ya kuufanya muungano wa mke na mume uwe mzuri zaidi, imara zaidi na wenye furaha zaidi. Katika maisha yao kwa kusema kweli, msingi wa jamii ya watu na malezi ya kizazi kijacho yamejengwa juu ya muungano huu.

Mwanasaikolojia wa kike anaandika; “Kama mwanasaikolojia shauku yangu kubwa imekuwa kujifunza juu ya roho (akili) za wanaume. Siku za nyuma huko nilipewa kazi ya kuchunguza sababu za kisaikolojia za mwanaume na mwanamke. Mwisho nilihitimisha kuwa; Wanawake wote wanapenda kufanya kazi chini ya uangalizi wa mtu mwingine. Wanapenda kufanya kazi katika vyeo vya kawaida sio kama bosi.

Wanawake wote wanapenda kuhisi kuwa kuwepo kwao kunatambulika na kunahitajika.

Mwanasaikolojia huyu anaeleza maoni yake kuwa; “Ninaamini kuwa mahitaji haya mawili ya kiroho yanatokana na ukweli kwamba wanawake wanaongozwa na mihemko (emotions) wakati wanaume huongozwa na akili. Mara nyingi inaonekana kwamba wanawake sio tu kwamba wana akili sawa na wanaume, bali wakati fulani hata huwazidi (wanaume).

Udhaifu wao pekee ni kuwa wana jazba sana (mno). Kufikiri kwa wanaume kunatekelezeka zaidi, wanahukumu vizuri zaidi, wanapanga mambo vizuri zaidi na wanawaelekeza wengine (ni wakurugenzi) vizuri zaidi. Ubora wa roho (akili) ya wanaume (kuizidi ya wanawake) ni kitu kilichopangwa na maumbile yenyewe. Jitihada yeyote mwanamke atakayofanya kubadilisha ukweli huu, itakuwa ni kujisumbua bure.

Wanawake lazima waukubali uhalisia kuwa kwa vile wao wana mhemuko sana wanahitaji usimamizi wa wanaume katika maisha yao. Lengo kubwa la maisha ya mwanamke ni ‘Kujihakikishia’ hatima yake ya baadaye. Akishalipata, huziambia kwa heri shughuli zake nyingine. Ni mwoga kufanya mambo ya hatari (ambayo haijulikani kama matokeo yake yatakuwa mazuri au mabaya). Uoga ni hisia za moyoni, na ili kuzishinda mwanamke anahitaji msaada wa mwanaume. Kazi zote zinazohitaji kufikiri muda wote zinamchosha.

Harakati Za Papara (Pupa).

Harakati za wazungu za kurejesha haki za wanamke zilikuwa ni suala la papara lililofanywa kwa uharaka

usio wa lazima. Mpango wenyewe wa mageuzi ulikuwa mzuri, lakini ukweli wa kisayansi haukuzingatiwa katika utekelezaji wa mageuzi haya, na matokeo yake yakawa ni mchanganyiko wa nukta za maana na za ovyo.

Hakuna shaka kwamba mlolongo wa masaibu na taabu za wanawake uliondolewa, walikubaliwa na kupewa haki nyingi na milango sasa kwa ajili yao ikafunguliwa na harakati za haki za wanawake. Lakini wakati huo huo mageuzi haya yalileta mikosi na balaa kubwa. Sio kwa mwanamke tu, bali kwa wanaadamu wote. Kama papara na pupa visingepewa nafasi, haki za wanawake zingekuwa zilirejeshwa kwa namna bora zaidi na kusingekuwa na mayowe na vilio vya wasomi dhidi ya matokeo yake maovu.

Hata hivyo, tunatarajia kuwa ushauri mzuri utashinda na kuenea na katika mageuzi yatakayofuatia, badala ya kuwa na jazba, watayatumia na kutanguliza maarifa (elimu) na uelewa. Maoni ya wasomi yanaashiria wema na heri siku za usoni. Inaonekana kwamba watu wa Magharibi bado wanataabishwa na madhara ya mageuzi haya ambayo yanaonekana kuwasisimua na kuwafurahisha waigaji wao wa nchi za Mashariki (Asia).

Mtazamo Wa Will Durant.

Will Durant, katika kitabu chake, *'Pleasures of Philosophy'* anaeleza vizuri kabisa masuala ya kijisia na familia. Hapa tutachagua baadhi ya mawazo yake ili wasomaji wetu waelewe uelekeo wa mkondo wa fikra miongoni mwa wasomi wa Kimagharibi na kuepuka hitimisho la papara.

Chini ya sura ya *Love* (mapenzi) anasema, 'Utaratibu wa kwanza wa wazi huanza wakati wa kubalehe. Kubalehe kwa kiingereza ni '*Puberty'* neno ambalo ni la kilatini lenye maana ya zama za nywele, yaani ni kipindi cha kuota nywele katika miili ya wavulana, hasa kifuani, jambo ambalo huwa ni la fahari kwao, na ndevu huota usoni, ndevu ambazo huzinyoa kila baada ya muda fulani. Ubora na uwingi wa nywele na vitu vingine unahusiana na nguvu ya uzazi na asili (chimbuko). Nywele huwa katika ubora wa juu kabisa katika zama za kilele cha urijali (nguvu za kiume). Kukua huku kwa nywele, pamoja na sauti kuanza kuparuza, ni sehemu ya tabia za awamu ya pili ya jinsia zinazotokea kwa wavulana wakati wa kubalehe.

Kwa upande wa wasichana wakati wa kuvunja ungo, maumbile huifanya tabia mienendo yao kuwa mizuri mno kiasi cha kuwavutia wanaowatazama. Matako yao huanza kuwa bapa ili kurahisisha kubeba mimba. Matiti yao hukua na kuchomoza kwa ajili ya kumnyoyesha mtoto. Hakuna anayejua kwa yakini kinachosababisha kuonekana kwa tabia za awamu ya pili za jinsia (*secondary sex characteristics*).

Hata hivyo nadharia ya Profesa Starling, katika siku za hivi karibuni imepata wafuasi wengi. Kwa mujibu wa nadharia hiyo seli za via vya uzazi, wakati wa hatua hii ya ukuzi, hazizalishi manii na mayai ya kike peke yake, bali pia huzalisha homoni ambazo huingizwa katika damu na kusababisha mabadiliko ya kimwili, kiroho na mengineyo. Katika umri huu, sio tu kwamba mwili hupata nguvu mpya, bali pia roho, tabia na mwenendo huathirika kwa namna nyingi.

Romain Rolland anasema kuwa katika miaka ya mtu, huja wakati ambapo mabadiliko mengi ya polepole ya kimwili husababisha maendeleo zaidi ya mwanaume au mwanamke. Mabadiliko muhimu kabisa huwa ni ukakamavu na nguvu kwa wanaume na uzuri unaovutia pamoja na ulaini wa ngozi na mwili kwa mwanamke.

Damoseh anasema kuwa kwa asili 'wanaume wote ni waongo, walaghai, wanafiki, wana hila, na ni wagomvi; na wanawake wote ni wabinafsi, wanajishaua na sio waaminifu. Lakini kuna kitu kimoja duniani ambacho ni kitukufu na kitakatifu, na kitu hicho ni muungano wa watu hawa wawili ambao sio wakamilifu... kuelekea kwenye ukamilifu.

Taratibu za kutafuta mwenza kwa wakubwa zinakuwa na uanzishaji kwa mwanaume kupata mkono wa kheri, lakini kujiondoa kwa mwanamke kwa ajili ya ushawishi na udanganyifu (kama mambo yalivyo, kuna hali za kipekee). Kwa vile mwanaume, kwa asili ni kama mpiganaji na mnyama anayewinda, matendo yake ni ya hakika na halisi na pia yeye ndiye muanzaji (mchokozi). Mwanamke kwake (kwa mwanaume) ni zawadi ambayo lazima ichukuliwe na imilikiwe. Kutafuta mke/mwenzi ni juhudi na mapambano na ndoa ni umiliki na utawala, kuwepo kwa usafi thabiti (kutozini) kwa mwanamke husaidia maslahi ya uzazi, kwa vile kujizuia (kuzini) kwa mwanamke kutokana na aibu kunamsaidia mwanamke katika kuchagua mwenzi wake.

Usafi (kutozini) huwazuia wanawake kutokuwa waangalifu katika kuchagua wenzi (wanaume) wao, ambao ni baba wa wana wao watakaowazaa. Mwanamke huzungumza kwa maslahi ya wote lakini mwanaume hujizungumzia maslahi yake peke yake. Mwanamke anaujuzi zaidi wa kufanya uchunguzi kwa vile matamanio yake sio makubwa kiasi cha kufanya ashindwe kutumia akili yake vizuri.

Darwin amegundua kwamba katika jamii za viumbe wengi, majike hayapendi sana kufanya mapenzi. Wanaviumbe wengine wanaochunguza mimea na wanyama, kama Lemberzo, Cash na Kraft Ebing nao pia wana maoni kuwa wanawake wanapendelea zaidi kuonekana wanavutia, pamoja na kupokea sifa za juu juu (wakati fulani za uongo) na za jumla za wanaume, na wanapendelea pia kuona wanaume wanajali mahitaji yao halisi ya ndani kuliko kutaka kufanya ngono.

Lemberzo, na wengine wanasema kwamba 'Msingi wa asili wa mapenzi ya mwanamke ni kuwa mama (na kuwajali watoto) ndio tabia na sifa ya kwanza ya mwanamke, kisha mapenzi ndio yanafuatia. Hisia zote na michomo ya moyoni inayomuunganisha mwanaume na mwanamke haitokani na mahitaji yake ya kimwili lakini inatokana na silika yake ya unyenyekevu (kujiweka chini ya uangalizi wa mwanaume). Silika hii ina kazi ya kutimiza na kutekeleza majukumu ya nafasi yake halisi.

Will Durant katika sura aliyoiita *'Man and Woman'* (mwanaume na mwanamke), anasema; 'Kazi kubwa ya mwanamke ni kuhakikisha kwamba jamii ya watu inaendelea kuishi na kudumu, na kazi kubwa ya mwanaume ni kuwatumikia mke na watoto wake. Wanaweza kuwa na kazi nyingine pia, lakini kwa misingi ya busara na kuangalia manufaa, hizo kazi nyingine ziko chini ya majukumu haya mawili. Haya ni majukumu mawili ya msingi ya binadamu anayoyafanya bila kujijua, ambayo utekelezaji wake ndio

utakaoleta furaha kwa wanaadamu. Mwanamke kwa asili hutaka amani, sio vita. Inaonekana kwamba katika jamii nyingi za viumbe, mwanamke hana silika ya ugomvi na ukorofi kabisa. Akiamua kupigana, basi ni kwa ajili ya watoto wake.

Mwanamke ana subira zaidi kuliko mwanaume ingawa mwanaume ni jasiri zaidi katika kukabiliana na kazi za hatari na matatizo katika maisha. Ana uvumilivu mkubwa zaidi, na anaweza kukabiliana na ugumu na kero ndogo ndogo nyingi tu vizuri zaidi. Roho yake ya kupenda vita au ujasiri inaishia katika kupenda kuiona sifa hii kwa wengine. Anawapenda askari na wanaume wenye nguvu na majabari, kwa sababu hii anaweza kushawishiwa na fikra ya kufurahia au kupata ashiki kutokana na kuumia (masochism) na anaweza kuwa mhanga wa nguvu za kiume.

Moyo wa kupenda nguvu na ushujaa wakati fulani huyafunika hata maslahi yake ya kiuchumi, na wakati mwingine huchagua kuolewa na mtu shujaa (na kumuacha tajiri). Humkubali kwa furaha mwanaume ambaye hutoa amri kwa wengine kwa njia ya haki na uadilifu. Kama wanawake sio watii kiasi hicho siku hizi, tofauti na walivyokuwa zamani, ni kwa sababu wanaume siku hizi ni dhaifu, hawana nguvu kama zamani na mazingira yanayowazunguka. Silika yake humfanya apende desturi za zamani. Kimwili na kiakili hapendi kujaribujaribu vitu kama vile kuzini kabla ya ndoa n.k ingawa baadhi ya wanawake wanaoishi katika miji mikubwa wanaweza kuwa tofauti. Akiamua kufanya mapenzi (ngono) nje ya ndoa, si kwa sababu anataka uhuru katika hilo (ngono), bali ni kwa sababu bado hajapata mume mwaminifu na muwajibikaji.

Ikiwa katika ujana wake alipata kuvutiwa na shughuli za siasa na akawa anatamani kufanya kazi katika fani mbali mbali na tofauti za kazi, kwa kawaida huachana na kazi hizo baada ya kupata mume mwaminifu na mara moja hujiondoa yeye na mume wake katika mambo ya umma. Humkumbusha mume wake kuwa uaminifu na uwajibikaji wake aurudishe nyumbani kwake kwa kuwa mwanamke hahitaji kufikiri sana kujua kwamba mageuzi yote huanzia nyumbani. Anapofanikiwa kumrudisha mwanaume mbunifu na mzururaji nyumbani na kumfanya aiangalie nyumba na watoto wake, basi kusalimika na kuendelea kuishi kwa mwanadamu kunamtegemea yeye. Kwa asili hahusiki na mambo ya sheria na serikali. Nyumba na watoto ndio vitu anavyovipenda. Akishafanikiwa kuvitazama na kuvitunza vizuri, hajali ni serikali gani inaingia madarakani na ni serikali gani inaondoka madarakani.

Maumbile hayajali juu ya sheria za serikali. Vitu vya maana kabisa kwa maumbile (nature) ni nyumba (familia) na mtoto. Yakifanikiwa kuvihifadhi hivi vitu viwili, hayashughulishwi tena na mambo ya serikali, na huwacheka wale wanaojaribu kubadili sheria za msingi. Kama leo maumbile yanayoonekana kushindwa kuihifadhi familia (nyumba) na mtoto, hii ni kwa sababu mwanamke tangu siku nyingi ameyasahau maumbile. Lakini kushindwa kwa maumbile sio kwa kudumu. Yanaweza kuwapatia mamia ya manufaa yalionayo, yakiruhusiwa na kupewa nafsi ya kufanya hivyo. Kuna mataifa na watu wa rangi nyingi sana kuliko tulivyo na maumbile yanayohakikishia kuendelea kuishi na kudumu kutokana na faida ambazo maumbile yanazo.

Mahari Na Matunzo

Mahari na Matunzo I

Ni moja ya desturi za zamani za mahusiano ya kifamilia ya mwanadamu kwamba wakati wa kuoa mwanaume hulipa mahari kwa mwanamke (anayemuoa) au kwa baba yake (huyo mwanamke). Na mbali na hili, hujitolea kugharamia gharama zote za mke wake na watoto katika kipindi chote cha uhai wake.

Ni nini msingi wa desturi hii? Ni kwa nini na ni kwa namna gani? Ni nini mantiki ya mahari? Je mahari na matunzo bado ni mambo yanayofaa kuendelezwa hadi sasa, hata kama mwanaume na mwanamke wana haki sawa za kibinadamu na za asili na mahusiano baina yao yamejengwa kwa msingi wa uadilifu na usawa? Au ni mabaki (masalia) yaliyobakia ya enzi zile ambapo mwanaume alimmiliki mwanamke? Je uadilifu na usawa wa haki, hasa katika karne hii unaamrisha kuwa desturi hizi zilizopitwa na wakati zipigwe marufuku? Na kwamba ndoa ifungwe bila mahari? Na mwanamke ajitunze mwenywe? Na kwamba jukumu la kulea watoto (gharama zake) liwe jukumu la kuchangia wote wawili, mke na mume?

Tunataka kujibu maswali haya, na tutaanza na swali la mahari. Hebu tuangalie jinsi hii desturi ilivyoanza, falsafa yake ni nini na jinsi wanasosholojia wanavyoeleza chanzo /asili yake:

Historia Fupi Ya Mahari.

Inasemekana kwamba zamani kabla ya historia kuanza kuandikwa, mwanadamu aliishi maisha ya kishenzi, yaliyokuwa na muundo wa kikabila. Kwa sababu zisizojulikana ndoa kati ya ndugu wa damu moja ilikatazwa. Hivyo vijana wa kiume wa kabila waliotaka kuoa, walilazimika kuchagua wake zao kutoka katika kabila jingine. Mara nyingi waliyatembelea makabila mengine kwa madhumuni haya. Enzi hizo mwanaume hakuwa anajua jukumu lake katika kusababisha mimba (yaani hakujua kama tendo lake la ndoa ndilo linalosababisha mimba). Alifikiri kuwa mtoto alikuwa ni mali ya mama kwa asilimia mia moja. Ingawa aliona watoto wakifanana naye sana. hakujua sababu ya kufanana huko. Kwa hali hii watoto nao walifikiri kuwa walikuwa ni mali ya mama yao na sio baba yao. Wakati huo ukoo ulitambulishwa kwa kupitia mfumo jike.

Wanaume walionekana kuwa ni wagumba na tasa. Baada ya ndoa, waliishi na watu wa kabila la mke wake kama kiambatanishi tu, kwa sababu mwanamke alihitaji uswahiba wa mume wake. Kipindi hiki kinajulikana kama kipindi cha mfumo jike (*matriarchy*).

Haikuchukua muda mrefu, mwanaume akagundua jukumu lake katika uzazi (utungaji mimba) na

akaamini kwamba kumbe kiuhalisia watoto walikuwa ni wake. Kuanzia wakati huo na kuendelea, alimtawala mwanamke na akajipa cheo cha ukuu wa familia. Hivyo, kipindi cha mfumo dume, kikaanza.

Katika kipindi hiki pia ndoa ya ndugu wa damu moja ilikatazwa. Mwanaume alipaswa kuchagua mke kutoka katika kabila (au ukoo) mwingine, na kumleta katika kabila lake. Kwa vile kulikuwa na hali ya kutokuelewana baina ya makabila kutokana na vita vya kikabila, njia pekee ya kupata mke ilikuwa ni kumdaka na kumbeba kwa nguvu binti wa kabila jingine.

Pole pole maelewano na amani yakachukua nafasi ya mapigano na magomvi, na makabila mbali mbali yakaweza kuishi pamoja kwa amani. Katika kipindi hiki mila ya kuwadaka na kuwabeba kwa nguvu wasichana ilipigwa marufuku. Ili kumpata mke aliyempenda, mwanaume alipaswa kwenda kufanya kazi kwa baba wa msichana huyo kwa muda fulani. Kwa kuzingatia kazi alizozifanya hapo ukweni, baba wa msichana alimuozesha kwa huyo mwanaume, naye alimchukua na kwenda naye kwenye kabila lake.

Mfumo wa malipo wa fedha ulipoenea, mwanaume aligundua kuwa badala ya kufanyakazi kwa baba wa bibi harusi kwa miaka, ilikuwa ni bora zaidi kupeleka ukweni zawadi maridhawa na kumchukua msichana mara moja. Huu ndio ukawa mwanzo wa mahari.

Kwa mujibu wa nadharia hii, katika siku za mwanzo mwanaume aliishi kama kiambatanisho cha mwanamke na alimtumikia (mwanamke). Katika kipindi hiki mwanamke alimtawala mwanaume. Katika hatua inayofuata, madaraka yalipohamia mikononi mwa mwanaume, aliteka nyara wanawake kutoka katika kabila jingine. Wakati wa hatua ya tatu, ili kumpata mwanamke, mwanaume alikwenda kwa baba wa mwanamke na kumhudumia kwa miaka kadhaa. Wakati wa hatua ya nne, mwanaume aliwasilisha kiasi cha fedha kwa baba wa mwanamke. Na hivyo ndio desturi ya mahari ilivyoanza.

Inasemekana kwamba tangu wakati mtu alipofutilia mbali mfumo jike na kuweka msingi wa mfumo dume, alimpa mwanamke hadhi ya utumwa au zaidi kama mfanyakazi au mtumishi wake. Alimchukulia kama chombo cha uchumi, ambacho kwa njia nyingine ataweza kukidhi matamanio yake vile vile. Hakumpa uhru wa kijamii au wa kiuchumi. Mapato ya kazi ya mwanamke yalikuwa ni mali ya baba au ya mumewe. Hakuwa na haki ya kujichagulia mume wake, wala kuendesha shughuli yoyote ya kiuchumi kwa ajili yake mwenyewe. Fedha ambayo mwanaume amelipa kama mahari na gharama ambazo anatoa kama matumizi (*nafaqah*) zilikuwa kabisa zinatokana na pato la uchumi ambalo amelipata kutoka kwa mwanamke katika kipindi cha wakati wa mahusiano ya ndoa.

Mahari Katika Mfumo Wa Haki Wa Kiislamu.

Kuna hatua ya tano pia ambayo wanasosholojia na wasomi wengine hawakuisema. Katika hatua hii mwanaume humpa zawadi mwanamke. Wazazi wote wawili wa mwanamke hawana haki ya kuidai zawadi hiyo. Mwanamke hupokea zawadi, lakini hubaki na uhuru wake wa kiuchumi na kijamii. Humchagua mume kwa hiari yake mwenyewe, bila kulazimishwa na baba wala kaka. Na zaidi ya hayo, si baba wala mume wake mwenye haki ya kumnyonya. Matunda ya kazi na jasho lake ni mali yake

binafsi, na hakuna mwenye haki ya kumuingilia juu ya mali hiyo. Katika masuala ya kifedha hahitaji uangalizi au usimamizi wa yeyote.

Mume ana haki moja tu. Anaweza kufurahia tendo la ndoa na mke wake. Katika muda wote wa ndoa yao, mwanaume anawajibika kumtimizia mkewe mahitaji yote ya halali kwa mujibu wa uwezo wake.

Hii ndio hatua inayotambuliwa na Uislamu na ambayo juu yake Uislamu umejenga msingi wake wa mahusiano ya ndoa. Aya nyingi za Qur'ani zinasisitiza kuwa mahari ni mali ya mwanamke. Na mbali na mahari, mwanaume anapaswa kumtunza na kubeba gharama zote za mkewe. Na wakati huo huo chochote anachokipata mwanamke ni mali yake peke yake na sio ya mtu mwingine yeyote, sio ya baba yake wala mume wake.

Hapa ndipo suala la mahari na matunzo linapotatanisha kidogo. Maadamu mahari inalipwa kwa baba wa msichana na anakwenda kwenye nyumba ya mume kama mtumwa na mume akawa na mamlaka ya kumnyonya, hapa suala lingekuwa rahisi kueleweka. Mahari ililipwa kama bei ya msichana na alipaswa kutunzwa kama mtumwa mwingine yeyote. Sasa kwa vile baba wa msichana hakulipwa chochote, mume haruhusiwi kumnyonya mke wake, mwanamke ana uhuru kamili wa kiuchumi, na kuhusiana na haki zake hahitaji usimamizi, udhibiti au uangalizi wa mtu yeyote. Sasa kwa kuwa mambo yako hivi kuna maana gani ya kulipa mahari na kugharamia matunzo?

Tuitazame Historia Kidogo.

Ili tuweze kuelewa falsafa ya mahari na matunzo katika hatua hii ya tano, tunapaswa kuitazama kiumakinifu nadharia ya vipindi vinne iliyotajwa hapo juu. Ukweli ni kwamba yote yaliyosemwa juu ya vipindi hivi si chochote zaidi ya nadharia tete iliyojengwa juu ya dhana na makisio tu. Hayana taarifa za kihistoria wala ukweli wa kisayansi. Hatuna elimu ya uhakika juu ya mwanadamu aliyeishi kabla ya kuanza kuandikwa kwa historia. Yote yaliyosemwa juu ya kipindi cha mfumo jike, akina baba kuwauza binti zao, na wanawake kunyonywa kiuchumi na waume zao, si ya kuaminika sana.

Kuna mambo mawili yaliyoisumbua akili juu ya dhana na makisio. La kwanza ni kuwa mtu duni (wa kale) amewakilishwa kama mtu mshenzi, mgomvi na asiyekuwa na hisia za kibinadamu. Jambo la pili ni kuwa mpangilio wa ajabu wa maumbile katika kufikia malengo yake umepuuzwa.

Tafsiri hii ya asili ya mwanadamu pengine inaweza kutolewa na watu wa Magharibi na sio watu wa Mashariki isipokuwa wale watu wa Mashariki ambao wanafuata mila za Kimagharibi kwa sababu fulani fulani, mzungu hazifahamu vizuri hisia na mawazo ya kibinadamu. Hawezi kukiri kuwa ana mchango wa msingi katika historia. Kutokana na uchu wake wa kiuchumi, akili yake yote iko kwenye mkate na siagi. Huitazama historia kama mashine, ambayo huwa haitembei mpaka iwekewe mafuta. Kama mwelekeo wake ni ngono huwaona wanaadamu wote na historia ya mwanadamu, pamoja na utamaduni wao, sanaa, maadili na dini kama miundo iliyorekebishwa ya mchezo wa ngono. Kama maoni yake ni ya kisiasa, basi huiona historia yote ya mwanadamu kuwa ni mfululizo wa vita, umwagaji damu na vitendo

vya ukatili.

Mzungu aliteswa mno kwa kutumia jina la dini katika zama za kati, ambapo watu mara nyingi walikuwa wakichomwa moto wakiwa hai, kiasi cha kuwa amekuwa na mzio na jina la Mungu, dini na vitu vyote vinavyowakilisha dini. Hii ndio sababu, licha ya ushahidi wote wa ukweli kwamba maumbile yana makusudio na mfumo wa ulimwengu haufanyi kazi kwa bahati nasibu hajathubutu kukiri kuwepo kwa 'Sababu Sababishi' (yaani Mwenyezi Mungu).

Hatuwaombi wafasiri wa historia wa Kimagharibi kukiri kuwepo kwa mitume, waliokuwa wakitokea katika historia yote ya mwanadamu kuja kutangaza ujumbe wa uadilifu na ubinadamu na kupiga vita ufisadi, mambo ambayo waliyafanikisha kwa ukamilifu. Tunachowataka ni angalau wasipuuzie jukumu la utambuzi waliopewa na maumbile.

Hakuna shaka kwamba katika historia ya uhusiano wa mwanaume na mwanamke, kumekuwa na matukio mengi ya ukatili uliopindukia, na mengine yakiwa ni maovu mno, ambayo yamesimuliwa katika Qur'ani pia, lakini hatuwezi kusema kwamba historia yote ya mwanadamu ilikuwa imejaa vitendo vya ukatili na mapigano.

Falsafa Ya Kweli Ya Mahari

Kwa mujibu wa imani yetu, mahari ilikuja kutokana na mipangilio makini, iliyowekwa katika usanifu wa uumbaji ili kuweka sawa uhusiano kati ya mwanaume na mwanamke. Mahari imetokea (imekuwepo), kwa sababu, kwa asili majukumu ya mwanaume na mwanamke kila mmoja kwa mwenzake yako tofauti. Kwa mujibu wa mafunzo ya dini sheria ya mapenzi na mvuto ipo kila sehemu ulimwengu. Kwa vile kila kitu kimetengenezwa ili kutekeleza kazi maalum, basi majukumu yake ni tofauti na vitu vingine vyote.

Tulipokuwa tukijadili tofauti kati ya mwanaume na mwanamke, tulishaeleza tayari kuwa hisia na shauku zao kuhusiana na kila mmoja, hazifanani. Sheria ya uumbaji imeshaamuru kuwa mwanamke awe na sifa za urembo (uzuri), fahari na kutojali ambapo mwanaume awe na sifa za kubembeleza na kushughulika. Hivi ndiyo udhaifu wa kimwili wa mwanamke ulivyofidiwa, na kwa sababu hii mara zote mwanaume ndiye amekuwa akimtaka mwanamke pamoja na kutoa pendekezo la kuoa. Kama tulivyoona huko nyuma kwa mujibu wa wanasosholojia katika vipindi vyote vya mfumo jike na mfumo dume, ni mwanaume ndiye amekuwa akimtaka mwanamke.

Wanasayansi wanasema kwamba mwanaume ana uchu (tamaa) zaidi (ya ngono) kuliko mwanamke. Baadhi ya hadithi za Kiislamu zinasema kuwa mwanaume hana tamaa (uchu) zaidi. Ilivyo, mambo ni kinyume chake lakini mwanamke ana uwezo zaidi wa kujizuia. Kivitendo, maoni yote mawili yanaleta kitu kimoja. Hata hivyo, ni jambo la hakika kwamba mwanaume ana uwezo mdogo zaidi wa kujizuia. Sifa hii imemuwezesha mwanamke asimfuate (asianze kumtaka) mwanaume, wala kujipeleka kwake kirahisi. Silika ya mwanaume humlazimisha kumwendea na kumtaka mwanamke, na huchukua hatua kadhaa ili ampate. Moja ya hatua hizi ni kumpa zawadi.

Wanaume mara zote wamekuwa wakichuana kumpata mwanamke (msichana). Wamekuwa hata wakipigana ili kufikia lengo hili. Lakini wanawake kamwe hawajapata kuonyesha umakini na shauku kama hii ya kumpata mwanaume. Mambo yako hivi kwa sababu majukumu ya mwanaume na mwanamke kila mmoja kwa mwenzake sio sawa. Mwanaume mara zote humfukuzia mwanamke wakati mwanamke humuonyesha hali fulani ya kutokumjali.

Mahari yanahusiana sana na staha na usafi wa kimaadili (hususan kutozini). Mwanamke anafahamu kwa silika kuwa heshima na staha yake vinataka asijitoe bure kwa mwanaume.

Hivi ndivyo mwanamke alivyo, licha ya udhaifu wake wa kimwili aliweza kuwapigisha magoti wanaume, kuwalazimisha kuchuana vikali na kuwafanya akina Romeo kuwakimbilia akina Juliet. Mwanamke anapokubali kuolewa na mwanaume, hupokea zawadi kutoka kwa huyo mwanaume kama ishara ya urafiki, furaha na dhamira njema.

Inasemekana kwamba miongoni mwa makabila ya kishenzi, msichana alipokuwa na waposaji zaidi ya mmoja alikuwa akiwashawishi wapigane mapigano rasmi ili kutetea hadhi yao. Aliyeshinda au kumua mwenzake (mpinzani wake) alionekana ndiye anayefaa kumuoa msichana huyo.

Kulikuwa na habari kwenye gazeti kwamba msichana mmoja katika mji wa Tehran aliwashawishi wavulana wawili kupigana ili kutetea hadhi yao mbele yake. Kwa wale wanaofikiri kuwa nguvu ni mabavu ya kikatili na wanashikilia kuwa historia ya uhusiano wa mwanaume na mwanamke haina chochote zaidi ya vitendo vya ukatili na unyonyaji, si jambo linaloaminika kwamba jinsia dhaifu na ya kike inaweza kuwashawishi watu wawili wa jinsia yenye nguvu kushambuliana/kupigana. Lakini kwa wale wenye elimu kidogo juu ya nguvu ya ajabu ambayo maumbile yamempa mwanamke, hapa hakuna kitu cha ajabu.

Mwanamke ana ushawishi mkubwa sana kwa mwanaume. Ushawishi wa mwanamke kwa mwanaume umekuwa mkubwa zaidi kuliko ule wa mwanaume kwa mwanamke. Mwanaume anamhitaji sana mwanamke, na pia anauhitaji sana ucheshi wake, usafi wake wa kimaadili na staha ili apate mafanikio katika sanaa na medali za ujasiri. Sifa ya kujenga watu wenye haiba kubwa na wenye vipaji vikubwa inamrudia yeye. Mwanamke anamjenga mwanaume na mwanaume anaijenga jamii. Mwanamke akipoteza sifa ya usafi wa kimaadili, staha na kujizuia, na akajaribu kufanya majukumu ambayo ni ya mwanaume, kwanza mwanamke huyu anaweza kujishushia hadhi, kisha mwanaume anaweza kupoteza uanaume wake, na mwisho wa safari jamii inaweza kuangamia.

Ustadi ule wa mwanamke, umemuwezesha kudumisha haiba yake katika kipindi chote cha historia, kumlazimisha mwanaume kwenda katika mlango wake, kama mchumba, kumshawishi mwanaume kuingia katika uadui na hata kupigana kwa ajili yake, kudumisha staha na usafi wa kimaadili kama nembo yake ya ubora, kuuficha mwili wake usionekana kwa wanaume, kumhamasisha mwanaume apende kufanya matendo magumu ya kishujaa, kama rasilimali takatifu, kufanya vizuri katika mambo ya kiakili na matendo ya ubunifu, kuimba nyimbo za mapenzi na kunyenyekea mbele ya jinsia dhaifu kwa

unyenyekevu mkubwa. Kwa hiyo tabia hii imemlazimisha mwanaume kutoa zawadi kwa bibi harusi wakati wa ndoa kama mahari.

Mahari ni sehemu ya sheria ya maumbile, ambayo imeanzishwa na maumbile yenyewe.

Mahari Katika Qur'ani

Muundo wa mahari ulioelezwa hapo juu kuhusiana na hatua ya tano sio ubunifu wa Qur'ani. Qur'ani ilichokifanya ni kuurejesha katika muundo wake wa asili na mzuri kabisa. Qur'ani inasema kwa ufasaha:

وَآتُوا النِّسَاءَ صَدُقَاتِهِنَّ نِحْلَةً ؟

"Wapeni wanawake mahari yao, hali yakuwa ni hadiya (zawadi)..." (*Suratul Nisa 4:4*).

Hii ina maana kwamba mahari ni haki ya wanawake (hao wanaoolewa) na ni zawadi wanayopewa wao moja kwa moja. Haiwahusu baba na kaka zao. Katika sentensi hii fupi Qur'ani imetaja nukta tatu za msingi:

Kwanza: imetumia neno *Saduqatihinna* (yaani ukweli na uaminifu) badala ya neno mahari. Hivyo mahari ni alama ya ukarimu na wema wa mwanaume anayeilipa. Nukta hii imeelezwa na wafasiri mbalimbali mashuhuri wa Qur'ani Tukufu, kama vile Zamakhshari, mwandishi wa tafsir mashuhuri ya Qur'ani iitwayo *Kashshaf*. Halikadhalika mwanasayansi wa asili na maendeleo ya lugha, Righib Isfahani amesema katika kamusi yake ya Qur'ani kuwa mahari imeitwa Saduqah kwa sababu ni alama ya uaminifu wa imani.

Pili: ni dhahiri kutokana na lAya hiyo ya Qur'ani kuwa mahari inapaswa kulipwa kwa mwanamke moja kwa moja, na wazazi wa mwanamke hawapaswi kudai chochote katika mahari hiyo. Mahari sio fidia ya jitihada walizozifanya wazazi katika kumlea binti yao.

Tatu: ni dhahiri pia kuwa mahari si chochote zaidi ya hadiya na zawadi.

Sifa Ya Hisia (Za Kimapenzi) Miongoni Mwa Wanyama.

Sheria ya mahusianao ya kimapenzi haiwahusu binadamu peke yao bali hata wanyama. Ingawa jinsia zote mbili zinahitajiana, jinsia ya kiume huhisi haja kubwa zaidi kwa ajili ya mwanamke, na huanzisha jitihada za kumpata. Hii ndio sababu mwanaume/dume huwa hatumii vibaya nguvu nyingi alizonazo (kumuonea mwanamke /jike), na huonyesha wema kwa mwanamke.

Zawadi Katika Mahusiano Haramu

Hata mwanaume na mwanamke wanapotaka kufurahia ngono katika mahusiano haramu (nje ya ndoa), ni mwanaume ambaye humpatia mwanamke zawadi. Wanapopata chai, kahawa au chakula pamoja ni mwanaume ambaye huona kuwa ni juumu lake kulipa bili. Mwanamke huona kuwa ni matusi kutakiwa kumlipia mwanaume. Baadhi ya watu hudai kuwa mvulana anahitaji uwezo wa kifedha ili kujiingiza katika zinaa ambapo kwa msichana hiyo ni njia ya kujipatia zawadi. Mila hizi ambazo tunazikuta katika mahusiano halali (ya ndoa) na haramu (ya nje ya ndoa) zinatokana na kutofautiana kwa hisia za mwanaume na mwanamke za kila mmoja kwa mwenzake.

Mzungu Ana Mahusiano Ya Asili Zaidi Katika Kufanya Mapenzi Ya Haramu Kuliko Katika Ndoa.

Katika nchi za Magharibi ambako hali za kifamilia zimeharibiwa kwa jina la usawa wa haki za binadamu, na jitihada inafanyika kugawa majukumu sawa ya kazi za ndani (kama kupika, kudeki n.k) lakini bado mwanaume anatekeleza majukumu yake ya asili katika mahusiano ya nje ya ndoa. Katika mahusiano ya nje ya ndoa, bado mwanaume hutoa zawadi kwa mwanamke na hubeba gharama za huyo mwanamke, lakini katika ndoa, sio tu kwamba hakuna mahari, lakini mwanamke pia hubeba mzigo mkubwa wa gharama za matumizi ya nje ya nyumbani. Hii ina maana kuwa kwa wazungu mapenzi nje ya ndoa ni ya asili zaidi kuliko mapenzi ndani ya ndoa ya kizungu.

Mahari ni mfano unaoonyesha kuwa mwanaume na mwanamke wameumbwa kwa vipaji tofauti na sheria ya maumbile imewapangia haki za asili zisizofanana.

Mahari Na Matunzo –II

Katika sura hii tumeelezea falsafa na asili ya mahari. Tumeonyesha kuwa sheria ya maumbile imeweka mahusiano kati ya jinsia hizi mbili na imeweka majukumu tofauti ya watu wa jinsia hizi mbili katika maisha. Ilionyeshwa pia kuwa mahari ilitokana na hisia za upendo na upole wa mwanaume, na sio kutokana na hisia zake za kutawala na ukatili. jukumu la mwanamke katika jambo hili limetokana na utambuzi wake wa pekee wa kujizuia, (yaani kujizuia kujitoa kirahisi kwa mwanaume) na sio kwa sababu ya udhaifu wowote au kutokuwa na uwezo wowote.

Malipo ya mahari ni zana iliyoamuriwa na sheria ya maumbile ili kuonyesha thamani ya mwanamke. Thamani yake ya kimaadili ni kubwa sana kuliko thamani yake ya kimwili.

Mila Za Kabla Ya Uislamu Ziliondolewa Na Uislamu.

Qur'ani iliondoa mila nyingi za Waarabu zilizokuwepo kabla ya Uislamu zilizokuwa zikihusiana na mahari, na ikairejesha mahari katika nafasi yake ya asili na inayostahili.

Katika kipindi cha kabla ya Uislamu wazazi walifkiri kuwa mahari ni mali yao wanayopewa kama hadiya ya taabu walizopata katika kumlea na kumkuza msichana. Imetajwa katika Kashshaf (Tafsiri ya Qur'ani inayosikifa sana) n.k kuwa pindi msichana alipozaliwa na mtu alipotoka kumpongeza baba wa msichana huyo basi alitoa pongezi hizo kwa kusema, "Mkoba huu unaonukia uzuri uwe na manufaa kwako", msemo wenye maana, "Mungu ajalie umuozeshe na upokee mahari yake".

Katika kipindi cha kabla ya Uislamu, akina baba au kama wao hawakuwepo makaka, kama walinzi na walezi wa asili wa msichana walimuozesha kwa mwanaume waliyemtaka wao sio ambaye msichana mwenyewe alimtaka. Na wakati huo huo waliona mahari yake kuwa ni mali yao.

Wakati mwingine walibadilishana mabinti. Mwanaume alikuwa akimtoa binti yake au dada yake na kumpa mwanaume mwingine kwa matarajio ya yeye pia kupewa binti au dada wa huyo ambaye yeye amemuozesha. Katika ndoa ya aina hii iliyokuwa ikiitwa ndoa ya *Shighar,* waolewaji wote wawili walikuwa hawapokei mahari yoyote. Uislamu ulipiga marufuku aina hii ya ndoa. Mtukufu Mtume alisema; "Hakuna *Shighar* (kubadilishana mabinti au akina dada) katika Uislamu."

Kwa mujibu wa desturi ya Kiislamu, sio tu kwamba baba hapaswi kudai chochote katika sehemu ya mahari ya binti yake, lakini pia hairuhusiwi kuingiza katika mkataba wa ndoa sharti la kwamba mbali na mahari, malipo mengine ya ziada yatalipwa kwa baba wa binti. Kwa maneno mengine, baba haruhusiwi kunufaika kifedha kwa namna yeyote kutokana na ndoa ya binti yake.

Uislamu pia ulipiga marufuku mila ambayo ilimlazimisha muoaji kufanya kazi kwa baba mkwe mtarajiwa kama mahari katika kipindi ambacho kulikuwa hakuna fedha. Mila hii haikuja tu kuwepo kwa sababu mababa walitaka kunufaika kupitia kwa mabinti zao. Kulikuwa na sababu nyingine pia, ambazo zilikuwa ndio ada ya zama hizo ambazo kiumuhimu hazikuwa za uonevu. Hata hivyo, hakuna shaka yeyote juu ya kuwepo kwa mila hii katika zama za kale.

Kisa cha Musa na Shu'aib, kilichosimuliwa katika Qur'ani kinaonyesha kuwepo kwa mila hiyo. (Nabii) Musa alipokuwa akitoroka kutoka Misri, alipofika katika kisima cha Madyan aliwahurumia binti zake Shuayb, waliokuwa wamesimama pembeni na kondoo zao na hakuna aliyekuwa akiwajali. Musa aliwachotea maji. Wasichana wale walimsimulia baba yao kisa hicho (cha kusaidiwa na Nabii Musa) na baba yao alimtuma mmoja wao kwenda kumwita Musa nyumbani kwake.

Baada ya kujitambulisha, Shuaib alimwambia Musa; "Ningependa nikuozeshe binti yangu mmoja kwa sharti kwamba utanifanyia kazi kwa miaka minane. Ukipenda unaweza kunifanyia kwa miaka miwili zaidi na hivyo jumla kuwa miaka kumi." Musa aliikubali pendekezo hilo na akawa mkwe wa Shuaib. Mila hiyo

ndio ilikuwa utamaduni wa zama hizo.

Kulikuwa na sababu mbili zilizosababisha mila hii. Kwanza, fedha hazikuwepo wakati huo na huduma pekee ambayo bwana harusi angeweza kuitoa kwa mke wake au baba mkwe wake ilikuwa ni kuwafanyia kazi. Sababu ya pili ilikuwa ni kuwepo kwa mila ya mahari. Wanasosholojia wanaamini kuwa mila ya kumpa baba (mkwe) mahari ni moja ya desturi ya zamani sana. Ili kutoa mahari, imma baba mkwe alimpa muoaji kazi za kufanya au alichukua fedha kutoka kwake. Kimsingi alichokichukua kutoka kwa mume wa binti yake ilikuwa ni kwa ajili ya manufaa ya binti yake.

Hata hivyo, tayari Uislamu umeshapiga marufuku mila hiyo, na sasa baba wa mwanamke hapaswi kudai chochote katika mahari ya binti yake, hata kama anataka aitumie kwa ajili ya binti yake. Ni mwanamke mwenyewe tu ndiye mwenye haki ya kuitumia apendavyo.

Katika zama za kabla ya Uislamu, kulikuwepo mila nyingine pia, ambazo kimsingi zilimnyima mwanamke mahari yake. Moja ya mila hizo ilikuwa ni kurithi haki za unyumba. Ilikuwa mwanaume akifa, mtoto wake wa kiume au kaka yake alirithi haki za unyumba (yaani alimrithi mke wa marehemu) pamoja na mali za marehemu. Mtoto au kaka wa marehemu alikuwa na haki ya ama kumuozesha mjane kwa mwanaume mwingine na mahari kuichukua yeye au yeye mwenyewe kujitangaza kuwa ni mume wa mjane tena kwa kutumia mahari ile ile aliyoitoa marehemu.

Qur'ani Tukufu ilipiga marufuku mila hii pia. Inasema:

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا لَا يَحِلُّ لَكُمْ أَنْ تَرِثُوا النِّسَاءَ كَرْهًا ؟

"Enyi mlioamini! Sio halali kwenu kuwarithi wanawake kwa nguvu." (Suratul Nisaa; 4:19).

Katika Aya nyingine, Qur'ani Tukufu imepiga marufuku kabisa ndoa ya kumuoa mke wa baba (mama wa kambo) hata kama ataridhia. Qur'ani inasema;

وَلَا تَنْكِحُوا مَا نَكَحَ آبَاؤُكُمْ مِنَ النِّسَاءِ

"Msiwaoe wanawake waliopata kuolewa na baba zenu." (*Suratul Nisa; 4:22*).

Qur'ani Tu kufu ilipiga marufuku mila zote zilizomnyima mwanamke mahari yake. Moja ya mila hizo ilikuwa ni kwamba mwanaume alipomchoka mke wake, alimtesa kwa matarajio kuwa mwanamke huyo atakubali kupewa talaka kwa sharti la kurudisha mahari yote au nusu aliyopewa. Qur'ani Tukufu inasema;

وَلَا تَعْضُلُوهُنَّ لِتَذْهَبُوا بِبَعْضِ مَا آتَيْتُمُوهُنَّ

“Wala msiwazuie wanawake kuolewa ili mpate kuchukua sehemu ya yale mliyowapatia.” (***Suratul Nisaa, 4:19***)

Mila nyingine mbaya ilikuwa mwanaume alimuoa mwanamke na hata kulipa mahari kubwa, lakini baada ya kumchoka alikuwa akimchafulia jina lake, kwa kumshutumu kwa uzinifu na kudai arudishiwe mahari yake. Mila hii pia ilipigwa marufuku na Uislamu.

Uislamu Una Mfumo Wake Wa Mahari.

Ni kanuni ya Uislamu isiyo na ubishi wowote kuwa mwanaume hana haki yoyote juu ya mali au fedha ya mke wake, wala hana haki ya kumlazimisha kumfanyia chochote. Mapato ya mke anayefanya kazi hayawezi kutumiwa na mume wake bila ruhusa yake (ya mke). Katika hili hakuna tofauti kati ya mwanaume na mwanamke.

Kinyume na mila ya kikristo iliyoenea huko Ulaya hadi mwanzoni mwa karne ya 20, mwanamke kwa mtazamo wa Uislamu, hayuko chini ya udhibiti wa mume wake katika masuala ya kifedha. Ana uhuru kamili na fedha zake. Ingawa Uislamu umempa mwanamke uhuru kamili wa kiuchumi na umezuia mume wake asimuingilie mke wake katika mali zake bado umebakisha mfumo wa mahari. Hii inaonyesha kuwa kwa mtazamo wa Uislamu mahari hailipwi kwa mwanamke ili mwanaume aje kunufaika na nishati yake ya mwili au kumnyonya kiuchumi. Uislamu una mfumo wake wa mahari, ambao hautakiwi kuchanganywa na mfumo mwingine wowote. Vipingamizi vinavyotolewa dhidi ya mifumo mingine, havina mwanya wowote katika mfumo wa Kiislamu.

Kama ilivyoelezwa katika sura hii, Qur’ani Tukufu imelezea mahari kama, **‘hadiya.’** Kwa mujibu wa Qur’ani, mahari ni wajibu (lazima).

Qur’ani imezingatia kwa uangalifu tabia zote za maumbile ya mwanadamu, na ili kuhakikisha kuwa si mwanaume wala mwanamke anayepewa nafasi ya kusahau majukumu na mchango wao wa asili, imehimiza umuhimu wa kupanga mahari. Mchango au jukumu la mwanamke ni kuitikia penzi la mwanaume. Ni vizuri ikiwa atampenda mwanaume lakini upendo wake unatakiwa kuwa ni mwitikio wa hatua za mwanzo zilizochkuliwa na mwanaume. Ikiwa atampenda mwanaume ambaye tangiapo hampendi, basi atakumbana na matatizo mengi ikiwa ni pamoja na kushindwa kulimiliki pendo hilo na hili litakuwa ni pigo kubwa sana kwa haiba yake. Lakini ikiwa upendo wake ni mwitikio wa upendo wa mwanaume, hapa kunakuwa hakuna suala la kushindwa au pigo kwa haiba yake.

Je, ni kweli kwamba mwanamke sio mwaminifu, kwamba hana msimamo katika penzi lake, na kwamba hawezi kutumainiwa? Ni kweli na pia sio kweli. Ni kweli kama atakayelianzisha penzi ni mwanamke. Kama yeye ndio wa kwanza kuanguka katika penzi, basi hilo sio la kuaminika. Muda si mrefu atapoteza

penzi lake. Lakini sio kweli ikiwa penzi la mwanamke ni mwitikio wa penzi la dhati la mwanaume, katika hali hii, penzi halielekei kudumaa, isipokuwa kama mwanaume mwenywe atapoteza penzi lake kwa mwanamke huyo. Hapo ndio penzi litadumaa. Hili ndio penzi la asili la mwanamke.

Ni kutokana na penzi la aina ya kwanza ambapo mwanamke anabobea katika kutokuwa mwaminifu, na ni kutokana na aina ya pili ya penzi ambalo amepewa katika uaminifu. Ikiwa jamii inataka uimara wa familia, basi haina budi kuifuata Qur'ani ambayo imeweka kanuni tofauti kwa mwanaume na mwanamke. Sheria ya mahari inaafikiana na maumbile, kwa sababu ni ishara kwamba penzi lilianzishwa na mwanaume, na mwanamke aliitikia tu. Mwanaume hutoa zawadi kama ishara ya upendo na heshima kwa mwanamke. Hivyo sio jambo la maana kuifuta sheria hii ambayo huunda sehemu muhimu ya sheria iliyoundwa na maumbile yenyewe.

Kama tulivyoona, Qur'ani Tukufu ilipiga marufuku mila nyingi zilizokuwepo kabla ya Uislamu pamoja na desturi zilizokuwa zinahusiana na mahari, ingawa watu wa zama hizo walikuwa wamezizoea sana. Qur'ani ilichokiamrisha ni tofauti na mila zilizokuwepo katika siku hizo. Hivyo haiwezi ikadaiwa kuwa Qur'ani haijasisitiza kuwepo au kutokuwepo kwa mahari. Ingeweza kuwa ilipiga marufuku kabisa suala la mahari lakini haikuona kuwa ni jambo la busara kufanya hivyo.

Ukosoaji Wa Wanaopinga Kuwepo Kwa Mahari

Sasa baada ya kuona maoni ya Uislamu juu ya mahari, hebu tuangalie ukosoaji unaotolewa na wale wanaopinga sheria hii ya Uislamu.

Mkosoaji mmoja anasema; "Kama ilivyo kwa mtu anavyotumia fedha kupata bustani, nyumba, au farasi, halikadhalika fedha lazima itumike katika kumnunua mwanamke. Na kama ilivyo kuwa bei ya nyumba, bustani au farasi hutegemea ukubwa, uzuri na ubora wa matumizi yake halikadhalika bei ya mwanamke hutegemea uzuri au ubaya wake na mali au umasikini wake. Hio ndio falsafa ya mahari. Hakuna unyumba bila kutoa pesa na kutoa kulipa bei ya manunuzi."

Kama ingekuwa ni mila ya Kimagharibi, je, watu wangezusha fitna za chuki dhidi yake? Ikiwa mtu mmoja atampa pesa mtu mwingine, je, hii ina maana kuwa amemnunua? Je mila ya kupeana zawadi ipigwe marufuku? Qur'ani inaeleza wazi wazi kuwa mahari si chochote zaidi ya zawadi. Na zaidi ya hili Qur'ani imeweka sheria za uchumi ambazo haziruhusu mwanaume kumnyonya mwanamke kiuchumi.

Unaweza kusema kuwa wanaume wengi wa Asia wanawanyonya wake zao kiuchumi. Hilo tunakubali. Lakini hakutokani na mahari. Wanaume hawa hawasemi kuwa wanafanya hivyo kwa kuwa waliwalipia wake zao mahari. Kuna sababu nyingine zilizosababisha kuwa mara nyingi wanaume wanawatawala wanawake. Kwanini sheria ya maumbile ichafuliwe badala ya kuwabadilisha wanaume wanaohusika? Lengo kuu la hoja zote hizi ni kuwafanya watu wa Mashariki wasahau falsafa yao ya maisha na kanuni za kibinadamu, ili waweze kumezwa kirahisi na wageni.

Mkosoaji huyu anaendelea kusema kuwa; “Ikiwa kuna usawa kamili wa kiuchumi kati ya mwanaume na mwanamke, hakuna sababu kwanini mwanaume ashikwe shati kumtunza mke wake na kumpatia chakula, mavazi na mahari. Hapa mwanamke analipwa mara mbili, jambo ambalo mwanaume hajawahi kufikiriwa kufanyiwa.”

Tukiichambua hoja hii kwa uangalifu, tutaona inamaanisha kuwa katika kipindi ambapo mwanamke hakuwa na haki ya kumiliki mali na hakuwa na uhuru wa kiuchumi, mahari na matunzo vilihalalishwa kwa kiasi fulani. Lakini katika hali ambazo mwanamke amepewa uhuru wa kiuchumi, kama Uislamu ulivyompa, hakuna uhalali wa kumtunza na kumpa mahari.

Mkosoaji huyu anaonekana kuwa na imani potofu kuwa mahari ilikuwa ikilipwa ili kufidia dhulma ya kiuchumi aliyokuwa akifanyiwa mwanamke. Ukweli ni kinyume chake. Tukiitazama Qur’ani falsafa halisi ya mahari inaweza kuthibitika.

Mkosoaji mwingine ameandika; “Kwa vile mwanaume na mwanamke wameumbwa sawa, mmoja kumlipia gharama au kumpa marupurupu mwingine hakuna sababu ya kiakili. Kama ilivyo mwanaume anavyomhitaji mwanamke, halikadhalika ndivyo mwanamke anavyomhitaji mwanaume. Hivyo katika hili wote wawili wanahitajiana. Hivyo itakuwa sio haki kumuamrisha mmoja wao kulipa gharama za mwenzake. Lakini kwa vile mwanaume alikuwa na haki ya kutoa talaka na mwanamke hakuwa na uhakika wa kuishi na mwanaume huyo kama mume wake katika uhai wake wote, hivyo alipewa haki ya kudai aina fulani ya usalama (kinga) kutoka kwa mwanaume.”

Anaongeza kuwa; “Katika mazingira ambapo mwanaume hana haki kabisa kutoa talaka, basi hakuna uhalali kabisa wa kuendelea kwa desturi hii.”

Ni dhahiri kuwa kutokana na tulivyoyasema hoja hizi hazina msingi wowote. Mahari sio bei wala mshahara. Hapana shaka kwamba mwanaume na mwanamke wanahitajiana, lakini nafasi zao hazifanani. Maumbile yamewaweka katika nafasi tofauti.

Pia ni upuuzi kuielezea mahari kuwa ni kinga ya kifedha dhidi ya haki ya talaka, na juu ya hilo, kudai kuwa hii ndio sababu iliyoufanya Uislamu uiamrishe, ni kilele cha upuuzi. Tungependa kuwauliza watu hao kuwa kwanini awali Uislamu ulimpa mwanaume haki ya kutoa talaka? Kama haki hii ya talaka isingekuwepo je kusingekuwa na haja ya usalama (kinga)? Na zaidi ya haya sentensi hii ina maana kuwa Mtukufu Mtume (s.a.w.w) alipopanga mahari kwa ajili ya wake zake wenyewe, alikuwa na nia ya kuwapa kinga dhidi yake mwenyewe. Halikadhalika alipopanga mahari ya Bibi Fatima wakati wa ndoa yake kwa Imam Ali alifanya hivyo kwa sababu alitaka kuweka kinga kwa bibi Fatima dhidi ya Imam Ali.

Ikiwa, kwa ajili ya kujenga hoja tu, tutakubali kuwa mahari ni aina ya kinga, sasa swali linaloibuka ni kuwa, kwa nini Mtume (s.a.w.w.) aliwashauri wanawake kusamehe mahari yao kwa waume zao kama ishara ya wema. Kwa nini alikielezea kitendo hicho kuwa ni cha heri na kina thawabu nyingi? Kwa nini alihimiza kuwa mahari iwe ndogo kwa kadiri inavyowezekana? Je hii haionyeshi kuwa Mtume aliichukulia mahari kuwa ni zawadi na alichukulia kuwa kuisamehe ilikuwa ni njia ya kuimarisha mapenzi

baina ya mume na mke?

Kama Uislamu uliitazama mahari kuwa ni kinga, kwa nini basi Qur'ani inasema, **"Wapeni wanawake mahari yao kama hadiya;** kwa nini haikusema wapeni wanawake mahari yao kama kinga."

Aidha, inaonekana kuwa mkosoaji huyu ana imani potofu kuwa, katika siku za awali za Uislamu, mahari ilikuwa na muundo sawa na wa sasa. Hivi sasa utaratibu uliozoeleka ni kuwa hulipa kiasi fulani cha mahari, lakini mke huwa hapati mahari yote, isipokuwa kunapokuwa na ubishani. Aina hii ya mahari huchukua sura ya kinga. Lakini katika kipindi cha awali cha Uislamu, utaratibu ulikuwa ni kulipa fedha ya mahari yote iliyokubaliwa. Katika mazingira haya haiwezi kudaiwa kuwa mahari ni mfumo fulani wa kinga.

Historia inaonyesha kuwa Mtume Mtukufu hakuwa akikubali kufungisha ndoa yoyote bila mahari kupangwa. Kisa kifuatacho kilichotajwa katika vitabu vya Shia na Sunni ni mfano wa desturi ya Mtume: Mwanamke alikuja kwa Mtume akasema; "Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu! Nikubali niwe mke wako." Mtume Mtukufu alinyamaza kimya na hakusema kitu. Mwanamke alikaa chini.

Mmoja wa masahaba wa Mtume aliinuka na kusema; "Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu! Kama hauko tayari, mimi niko tayari kumuoa." Mtume akauliza ni mahari gani utakayotoa?" "Sina kitu." Mtume akasema: "hiyo haitafaa. Nenda nyumbani kwako. Labda unaweza kupata kitu cha kumpa mwanamke huyu kama mahari yake. Mwanamume yule alienda kwenye nyumba yake. Mara akarudi na kusema; "Sikupata chochote." Mtume akasema nenda tena ukatafute, hata pete ya chuma itafaa."

Mwanaume yule alienda tena. Alirudi na kusema kuwa hakuweza kupata pete ya chuma. Alisema kuwa alikuwa tayari kutoa nguo alizovaa kama mahari kwa mwanamke yule.

Mmoja wa masahaba wa Mtume, aliyekuwa akimjua mtu huyo vizuri, alisema kuwa anafahamu kuwa mtu huyo alikuwa hana nguo nyingine. Hivyo alimuomba Mtume ampangie zile zile nguo alizovaa ndio ziwe mahari ya mwanamke huyo.

Mtume alisema; "Ikiwa nusu ya nguo zake zitapangwa kuwa mahari nani atakayezivaa? Yeyote kati ya hawa wawili atakayevaa nguo hizi atamuacha mwenzake bila nguo. Hilo haliwezekani."

Mchumbiaji alikuwa amekaa kwenye sehemu yake. Mwanamke pia alikuwa akisubiri uamuzi wa mwisho. Wakati huo, Mtume na masahaba wake wengine walikuwa wamejishughulisha katika kuzungumza juu ya jambo jingine. Muda mrefu ulipopita, mwanaume yule aliinuka ili aondoke. Mtukufu Mtume alimwita kwa kumwambia, "'Njoo hapa' Akaja.

Mtume akamuliza "Unaikumbuka Qur'ani? "Ndiyo ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu!" Ninaikumbuka sura hii na ile." "Je unaweza kuzisoma kutoka kichwani (bila kitabu)?" "Ndiyo, ninaweza" Mtume akasema; "Vizuri sana. Sasa ni sawa. Ninakuozesha mwanamke huyu na mahari yake ni kuwa umfundishe Qur'ani."

Mwanaume yule aliushika mkono wa mwanamke yule na wote wawili wakaondoka!

Kuna nukta nyingine, pia zinazohusiana na suala la mahari kwa sasa tunaziacha.

Mahari Na Matunzo –III

Tumeelezea mtazamo wa Uislamu juu ya mahari na falsafa yake. Sasa hebu tuliangalie suala la matunzo.

Lazima ieleweke kuwa kama ilivyo kwa mahari, matunzo pia yana muundo wake katika sheria ya Kiislamu na isichanganywe au kufananishwa na utaratibu wa wasiokuwa Waislamu.

Kama Uislamu ungemruhusu mwanaume amtumikishe mwanamke na yeye mwanaume achukue mapato ya jasho la mke wake, sababu ya kwa nini mume anapaswa kutoa matunzo kwa mke wake ingekuwa dhahiri, kwani ni wazi kuwa ikiwa mtu anamyonya mtu (au mnyama) mwingine kiuchumi ni lazima amgharamie gharama zote za maisha yake (maisha ya huyo anayenyonywa). Ikiwa mfugaji hatamlisha farasi wake, basi farasi huyo hatambebea mizigo.

Lakini Uislamu haujamruhusu mwanaume kumnyonya mwanamke. Kwa upande mwingine mwanamke ana haki ya kumiliki mali na kujipatia fedha, na mume hana haki ya kutenga mikono kwa kile alichojichumia mwanamke. Na wakati huo huo ni wajibu wa mume kubeba gharama zote za matunzo ya familia. Anapaswa kumtunza mkewe, watoto wake pamoja na wafanyakazi wa ndani na kununua vyombo vya ndani n.k. kwa sababu gani?

Kwa bahati mbaya, watu wenye akili za Kimagharibi hawako tayari kufikiri hata kidogo juu ya vitu hivi. Wanarudia maoni yale yale ya chuki dhidi ya muktadha wa sheria ya Kiislamu, ambayo wazungu wanayatumia kuhalalishia mfumo wao wa kisheria.

Ni sawa kusema kuwa matunzo kwa mke katika nchi za Magharibi, hadi kufika karne ya 19, ilikuwa ni ishara ya utumwa wa mwanamke, kwa sababu huko mwanamke alipaswa kuendesha kazi zote za ndani za nyumba ya mumewe bure tena bila kuwa na haki ya kumiliki chochote. Ni dhahiri kuwa chakula, mavazi, n.k alivyokuwa akipewa mwanamke havikuwa na tofauti na mgao wa kila siku wa mfungwa au mgao wa chakula anachopewa mnyama mbeba mizigo.

Lakini suala la Uislamu ni tofauti kabisa. Ni mfumo wa kipekee duniani ambao humuondoa mwanamke katika majukumu ya kuendesha maisha ya familia ya mwanaume, humpa uhuru kamili wa kiuchumi na wakati huo huo humuondoa katika kuchangia chochote katika bajeti ya familia. Hapa tuna falsafa tofauti ambayo inahitaji maelezo yetu maalumu.

Kumuweka Mwanamke Wa Kizungu Katika Kizuizi Hadi Katika Nusu Ya Karne Ya 19.

Dr. Shayagan anasema; “Uhuru wa kiuchumi wa mwanamke ambao umetambuliwa na sheria ya Shia toka awali kabisa, haukuwepo Ugiriki (Uyunani), Urumi na Japan hadi hivi karibuni katika nchi zilizo nyingi. Mwanamke kama mtu mdogo tu na kichaa alizuiwa kuingia katika malipo yoyote ambayo yangesababisha yeye kumiliki mali. Huko Uingereza ambako mwanamke alionekana kuwa si mtu kamili bali ni sehemu ya mume wake, sheria mbili zilipitishwa, moja mwaka 1870, na nyingine mwaka 1882, ambazo ziliondoa kizuizi hicho cha mwanamke kumiliki mali. Huko Italia, sheria ilipitishwa mwaka 1919 ili kuondoa kizuizi dhidi ya mwanamke. Sheria ya kiraia ya mwaka wa 1900 nchini Ujerumani na ile ya Uswisi ya mwaka 1907 zilimpa mwanamke haki sawa na zile alizokuwanazo mwanaume.

Hata hivyo, Wareno na Wafaransa waliendelea kuweka kizuizi kwa wanawake walioolewa kumiliki mali katika sheria zao hadi mwaka 1938 ambapo Ufaransa ilibadilisha sheria yake kwa kiasi fulani.

Kama ulivyoona ni karne moja tu imepita tangu sheria ya kwanza ya uhuru wa kiuchumi wa mwanamke ilipopitishwa huko Uingereza mwaka wa 1882 na hicho kilichoitwa kizuizi kwa mwanamke aliyeolewa kiliondolewa.

Kwa Nini Ulaya Ilimpa Mwanamke Uhuru Wa Kiuchumi Ghafla?

Sasa hebu tuangalie nini kilitokea katika karne iliyopita kiasi cha tukio hili muhimu kutokea? Je, utambuzi wa wazungu uliamka ghafla na hivyo kuwafanya watambue udhalimu wa nyendo zao?

Will Durant katika kitabu chake, ‘*Pleasure of Philosophy*” anajibu swali hili. Humo tunakutana na ukweli wa kushtusha. Tunagundua kuwa mwanamke wa kizungu kwa kusema kweli anapaswa kuzishukuru mashine na siyo mtu yeyote kwa ukombozi alioupata pamoja na haki ya kumiliki mali.

Anapaswa kulishukuru Bunge la Uingereza kwa kupitisha sheria ya uhuru wa kiuchumi wa mwanamke na sio wamiliki wa viwanda waliotaka kupata faida zaidi kwa kulipa mishahara midogo.

Will Durant anasema; “Mabadiliko ya haraka katika tabia na mila, kongwe zaidi kuliko historia ya Ukristo, yanaelezewa na uwingi na aina tofauti tofauti za mashine. Ukombozi wa mwanamke ni matokeo ya mapinduzi ya viwanda.”

Katika karne moja iliyopita ilikuwa ni vigumu sana kwa wanaume wa Uingereza kupata kazi. Lakini matangazo ya biashara yaliwataka wao wawapeleke wake zao na watoto viwandani. Waajiri walikuwa na shida ya faida viwandani na mgao, na hawakushughulishwa na maadili. Walikuwa ni mabepari wamiliki wa viwanda wa karne ya 19 ambao bila kujua walikula njama ya kuvuruga maisha ya familia ya watu.

Hatua ya kwanza ya kuwakomboa bibi zetu ilikuwa ni sheria ya mwaka 1882. Kwa mujibu wa sheria hiyo, wanawake wa Uingereza waliweza kufurahia fursa ambayo haikupata kutokea kabla. Walipewa haki ya kukaa na fedha zao wenyewe. Sheria hii iliyokuwa inawakilisha maadili yaliyotukuka ya Kikristo ilipitishwa na wamiliki wa viwanda katika Bunge la Uingereza. Tokea mwaka huo wanawake wamekombolewa kutokana na kazi ngumu za ndani na badala yake wanamenyeka kutokana na sulubu za madukani na viwandani.

Kama unavyoona walikuwa ni wamiliki wa viwanda wa Uingereza ambao kwa ajili ya kutaka faida kubwa zaidi, walichukua hatua hii kwa manufaa ya mwanamke.

Qur'ani na Uhuru wa kiuchumi wa mwanamke.

Uislamu miaka **1425** iliyopita uliweka sheria hii;

لِلرِّجَالِ نَصِيبٌ مِمَّا اكْتَسَبُوا ۚ وَلِلنِّسَاءِ نَصِيبٌ مِمَّا اكْتَسَبْنَ ۚ

"Wanaume wana sehemu ya walichochuma na wanawake wana sehemu ya walichochuma," (***Suratul Nisa; 4:32***).

Katika Aya hii Qur'ani imetambua nyadhifa za wote wawili mwanaume na wanamke juu ya matunda ya jasho lao. Katika sehemu nyingine Qur'ani nasema

لِلرِّجَالِ نَصِيبٌ مِمَّا تَرَكَ الْوَالِدَانِ وَالْأَقْرَبُونَ وَلِلنِّسَاءِ نَصِيبٌ

"Wanaume wana sehemu ya waliyoyaacha wazazi (wao) na wanawake wana sehemu ya waliyoaacha wazazi (wao)." (*Suratul Nisa; 4:7*).

Aya hii inathibitisha kustahiki kwa mwanamke kupata urithi, jambo ambalo lilikuwa halitambuliwi na Waarabu wa kabla ya Uislamu.

Ulinganishaji

Qur'ani Tukufu ilitoa uhuru wa kiuchumi karne 13 kabla ya Ulaya, na kukiwa na tofauti hizi:
Sababu zilizoufanya Uislamu utoe uhuru huo wa kiuchumi zilikuwa ni ubinadamu, maadili na maamrisho ya Mwenyezi Mungu. Hapakuwepo sababu kama vile tamaa ya wenye viwanda wa Uingereza ambao kwa kutaka kujaza matumbo yao, walipitisha sheria na kisha wakapiga kelele kubwa dunia nzima kuwa wamezitambua rasmi haki za wanawake, na kwamba walikuwa wameweka usawa kati ya mwanaume na mwanamke.

Uislamu ulitoa haki sawa kwa mwanamke, lakini haukuvuruga msingi wa familia yake, wala haukuwahamasisha wanawake na mabinti kuwaasi waume zao na baba zao. Uislamu ulileta mapinduzi makubwa, lakini ulifanya hivyo kwa utulivu na usalama.

Kwa mujibu wa Will Durant, nchi za Magharibi zilichokifanya ilikuwa ni kumnusuru mwanamke na sulubu za kazi za ndani na badala yake kumtwisha sulubu za madukani na viwandani. Kwa maneno mengine, Ulaya ilimfungua mwanamke pingu moja na kwa kutumia pingu nyingine ikamfunga mikono na miguu. Uislamu ulimuokoa mwanamke kutoka katika utumwa (kwa mwanaume), ndani ya nyumba na shambani, na ulimuondolea mzigo wa kugharamia gharama za familia.

Kwa mujibu wa mtazamo wa Uislamu, mwanamke ana haki ya kuchuma mali (fedha), kuzitunza na kuziendeleza mali zake, lakini wakati huo huo haifai alazimishwe kufanya kazi ngumu ambazo zinaweza kuharibu uzuri na fahari yake.

Lakini wapi! cha ajabu ni kuwa macho na masikio ya baadhi ya waandishi wetu yameziba kiasi cha kuwa hawawezi kuzitambua taarifa za kihistoria na ukweli wa kifalsafa.

Shutuma Za Wakosoaji Na Majibu Yetu.

Mwanamke mmoja anaikosoa sheria ya matunzo kwa kusema kuwa sheria hii inamtaka mume atoe chakula, mavazi na malazi kwa mke wake sawa tu na mfugaji anavyopaswa kumpa chakula na malazi mnyama wake.

Tungependa kumuuliza mkosoaji huyu ni kwa namna gani amefikia hitimisho kuwa mume anammiliki mke wake au ni namna gani umiliki huu umekuwa sababu ya mwanaume kumtunza mke wake.

Ni umiliki gani huo ambao mmiliki hana haki hata ya kuomba huyo anayemmiliki kumpa glasi ya maji. Ni umiliki gani huo ambao unampa haki mmilikiwa anachokichuma kuwa ni chake mwenyewe na sio cha mmiliki wake? Ni umiliki gani huo ambao anayemilikiwa akipenda anaweza kuomba malipo kutoka kwa mmiliki hata kwa kazi ndogo aliyoifanya? Ni aina gani hii ya umiliki ambapo mmiliki hana haki ya kumzalimisha huyo anayemmiliki hata kumnyonyesha mtoto wake ambaye pia ni mwanaye pia?

Pili, je, ni kweli kwamba mtu ambaye gharama zake zinalipiwa na mtu mwingine huwa mtumwa wa huyo mmiliki? Kwa mujibu wa sheria ya kila nchi ni wajibu wa baba au baba na mama kubeba gharama za watoto wao. Je, inaweza kudaiwa kuwa watoto wanamilikiwa na wazazi? Uislamu umefanya kuwa ni wajibu kwa watoto kuwasaidia wazazi wao pindi wanapohitaji msaada huo. Je hii ina maana kuwa kwa mujibu wa Uislamu, wazazi wanamilikiwa na watoto wao?

Aina Tatu Za Matunzo.

Uislamu unazitambua aina tatu za matunzo:
1. Mtu anayemiliki wanyama lazima awatunze. Msingi wa matunzo haya ni umiliki.

2. Mwanaume anapaswa kubeba gharama za watoto wake kama ni wadogo au kama ni maskini. Halikadhalika anapaswa kuwatunza wazazi wake ikiwa wao ni maskini. Msingi wa matunzo haya sio umiliki. Ni haki za asili. Watoto wana haki kwa wazazi wao waliowaleta duniani. Halikadhalika wazazi wana haki kwa watoto wao waliowazaa. Aina hii ya matunzo inakuwepo tu pindi kunapokuwepo na haja (yaani inapokuwa wazazi au watoto ni maskini).

3. Mume anapaswa kumtunza mke wake. Msingi wa aina hii ya matunzo sio umiliki wala haki za asili kama ilivyo hapo juu. Wala hautegemei uhitaji (wa mke), hali ya uzee au vinginevyo. Hata ikitokea kuwa mke ni milionea mwenye kipato kikubwa na mume wake ana kipato kidogo, bado ni jukumu la mume kubeba gharama za matunzo kwa mke wake. Na sifa ya pekee ya aina hii ya matunzo, tofauti na zile mbili za mwanzo, ni kuwa ina ulazima wa kisheria, yaani mwanaume anaweza kulazimishwa na mahakama kutekeleza jukumu hili. Ni nini msingi wa aina hii ya matunzo? Tutajadili hili katika sura inayofuatia.

Je Mwanamke Wa Kisasa Hataki Mahari Na Matunzo?

Tumeshaeleza kuwa kwa mtazamo wa Uislamu, ni jukumu la mwanaume kubeba gharama za familia yote ikiwa ni pamoja na za mke wake, mke ambaye yeye hana jukumu kama hili. Hata kama utajiri wa mwanamke ni mkubwa mara nyingi kuliko wa mwanaume, mwanamke halazimiki kuchangia chochote katika bajeti ya familia. Akiamua kuchangia basi ni kwa hiari yake.

Kwa upande mwingine, mwanaume analazimika kubeba gharama za mke wake, lakini Uislamu haumruhusu yeye kumnyonya mke wake kiuchumi. Katika hili matunzo ya mke yanafanana na wazazi, ambayo katika baadhi ya hali, huwa ni wajibu. Lakini mtoto hana haki ya kuwatumikisha wazazi ili apate kuwatunza, jukumu ambalo ni lake.

Kulinda Maslahi Ya Kiuchumi Ya Mwanamke.

Uislamu, kwa namna bora isiyo na mfano umeyalinda maslahi ya kiuchumi na kifedha ya mwanamke. Kwa upande mwingine umempa uhuru wa kiuchumi na umemzuia mwanaume kuingilia fedha zake au kuidhibiti mali yake na wakati huo huo umemuondolea jukumu la kusimamia gharama za familia. Hivyo hana haja ya kukimbizana na fedha.

Watu wa Magharibi, ambao wanataka kuikosoa sheria ya matunzo walikosa cha kusema hivyo wakaamua kuzusha uongo mkubwa. Wanasema kuwa falsafa ya matunzo ni kwamba mwanaume hujiona kuwa ni mtawala wa mwanamke na humfanya amtumikie. Kama ilivyo kwa mfugaji anavyopasa kubeba gharama za mnyama wake ili mnyama huyo aendelee kumtumikia ndiyo kwa msingi na lengo hilo hilo kwamba sheria ya matunzo imefanya kuwa ni wajibu kwa mwanaume kutoa japo mkate na siagi kwa mke wake.

Kwa kusema kweli, ikiwa mtu anataka kuishambulia sheria ya Kiislamu, anaweza kufanya hivyo kirahisi

kwa kulaumu kuwa kwa nini mwanamke amependelewa kiasi hicho na kumtwisha mwanaume mzigo wa majukumu makubwa kiasi hicho, badala ya kuikosoa kwa kutumia jina la kumtetea mwanamke.

Ukweli ni kuwa Uislamu haujakusudia kumpendela mwanaume wala mwanamke. Uislamu haukukusudia mafanikio ya mwanaume na mwanamke peke yao bali hata kwa watoto watakaozaliwa na wanaadamu wote. Uislamu unaamini kuwa njia pekee ya kutoa hakikisho la mafanikio ya mwanaume, mwanamke, watoto wao na wanaadamu wote ni kutopuuza sheria za maumbile na amri za Muumba Mwenye Nguvu Zote.

Kama tulivyoonyesha tena na tena, Uislamu umelizingatia hili mara zote kuwa mwanaume ni alama ya kuhitaji, matamanio na kushughulika na mwanamke ni alama ya kutojali. Uislamu umemuonesha mwanaume kama mteja na mwanamke kama mmiliki wa mali. Kwa mtazamo wa Uislamu, mwanaume anapaswa ajione kama mfadhiliwa na anapaswa awe tayari kubeba gharama zake za msingi. Mwanaume na mwanamke wanapaswa wasisahau kuwa wamepangiwa nafasi tofauti na maumbile katika suala la mapenzi. Ndoa inaweza kuwa imara na ya furaha ikiwa kila mmoja atatekeleza kikamilifu jukumu alilopangiwa na maumbile.

Sababu ya pili inayofanya mume awajibike kumtunza mke wake ni kuwa, ni mwanamke anayetaabika na maumivu yote ya uzazi wa mtoto. Mchango wa mwanaume katika hili ni kwa muda mfupi tu na ni yenye kuleta starehe. Ni mwanamke anayestahamili taabu za mimba, kujifungua, kunyonyesha na kulea mtoto.

Kazi zote hizi zinatumia nishati (nguvu) yake na kupunguza uwezo wake wa kufanya kazi. Kama itaamuliwa kwamba sheria haitatoa kinga kwa mwanamke na ikaamuru kuwa wote mume na mke wachangie bajeti sawa katika kuendesha familia basi bila shaka mzigo wa mwanamke utakuwa mzito mno.

Kama tunavyojua, wale wanyama wanaoishi kwa jozi, mara zote dume hutoa ulizi kwa jike na husaidia jike wakati wa kuzaa kwa kuleta chakula.

Aidha, kutokana na mtazamo wa kiwango cha kufanya kazi na uwezo wa kufanya kazi ngumu na zinazohitaji nguvu nyingi, zenye kuzalisha zaidi na za kiuchumi zaidi, haulingani kati ya mume na mke (sio sawa). Ikiwa mahusiano baina yao yatabadilika na mwanaume akakataa kutoa hata senti kwa ajili ya mkewe, mwanamke hataweza kushindana naye.

Isitoshe, mwanamke huhitaji fedha zaidi kuliko mwanaume. Kujipamba na kujirembesha ni sehemu ya maisha ya mwanamke, na moja ya mambo ya lazima kabisa. Fedha anazotumia kujipamba katika maisha yake ya kawaida ni nyingi mno zikilinganishwa na anazotumia mwanaume. Tabia yake ya kujirembesha imemfanya apende aina mbali mbali za manukato. Kwa mwanaume, suti inaweza kuvaliwa kwa muda wote hadi hapo itakapokwisha, lakini mwanamke huivaa nguo tu pale inapoonyesha upya. Mara nyingi nguo au pambo hupoteza thamani yake baada ya kuvaliwa mara moja tu. Uwezo wa mwanamke wa kuzalisha ni mdogo kuliko wa mwanaume lakini yeye ndiye mwenye matumizi makubwa zaidi.

Uwanamke wa mwanamke, yaani uzuri wake, urembo wake, fahari yake na uchangamfu huhitaji raha zaidi na jitihada kidogo. Ikiwa mazingira yatamlazimisha kufanya kazi kwa bidii na kufanya jitihada mara zote katika kujipatia fedha, fahari yake huondoka/huharibika. Mashaka ya kifedha yatamsabashia makunyazi katika uso wake kama yanavyosababisha katika uso wa mwanaume. Inasikika mara nyingi kwamba wale wanawake maskini wa kimagharibi, wanaolazimika kufanya kazi viwandani au katika karakana ili kujipatia riziki wanatamani kuwa wangeishi maisha ya mwanamke wa Mashariki (Asia). Ni dhahiri kuwa mwanamke ambaye akili yake haijatulia (haijaridhika) hawezi akajitunza vizuri wala hawezi akawa chanzo cha furaha kwa mume wake.

Hivyo sio kwa maslahi ya mwanamke bali kwa maslahi ya mwanaume na familia pia kuwa mwanamke asilazimishwe kubeba mzigo mzito wa kujitafutia riziki yake. Mwanaume pia anataka mazingira ya nyumbani yawe katika hali ambayo yeye atajisikia kupumzika na kusahahu mashaka yake yote. Mazingira kama haya yanaweza kuandaliwa na mwanamke tu, ikiwa yeye mwenyewe hajachoka wala hana mashaka. Ni huzuni iliyoje kwa mwanaume anayekuja nyumbani akiwa amechoka na kumkuta mke wake akiwa amechoka kuliko yeye!

Hivyo utulivu wa mwanamke, uzuri na kuridhika kwake ni mambo ya muhimu hata kwa mwanaume pia.

Sababu inayowafanya wanaume wawe tayari kuwakabidhi wake zao fedha walizozipata kwa jasho na taabu nyingi na kuwaruhusu wazitumie kwa uhuru na kwa raha zao ni kuwa wanajua kuwa wanawahitaji wake zao kwa ajili ya utulivu wao wa kiakili. Wanafahamu kuwa Mwenyezi Mungu amemfanya mwanamke kuwa chanzo cha furaha na utulivu kwa mwanaume. Qur'ani inasema:

هُوَ الَّذِي خَلَقَكُمْ مِنْ نَفْسٍ وَاحِدَةٍ وَجَعَلَ مِنْهَا زَوْجَهَا لِيَسْكُنَ إِلَيْهَا ؟

"Yeye ndiye aliyekuumbeni katika nafsi moja na katika (nafsi) hiyo alimuumba mwenzi ili apate utulivu kutoka kwake." (***Suratul A'raf, 7:189***).

Mwanaume anafahamu kuwa chochote anachotoa ili kumridhisha mke wake, hutoa kwa kupitia mlango wa pili kujihakikishia furaha yake mwenyewe na kung'arisha maisha ya familia yake. Anajua kuwa ili waridhishane na kupeana utulivu na raha inatakiwa angalau mmoja wao asielemewe na uchovu, na katika mgawanyo huu wa majukumu, ni mwanaume anayefaa zaidi kushiriki katika mapambano ya maisha na mwanamke anafaa zaidi kuchukua nafasi ya mliwazaji.

Mwanaume na mwanamke wameumbwa katika namna ambayo mwanamke humtegemea mwanaume kifedha na mwanaume humtegemea mwanamke ili kupata msaada wa kiroho na kimaadili. Mwanamke hawezi kujitosheleza kifedha na kimali bila msaada wa mwanaume na ndio maana Uislamu umemuamrisha mume wake wa halali (mume wa halali tu) kumsaidia mke wake.

Ikiwa mwanamke anataka kuishi kifahari kama anavyotaka basi lazima apate msaada wa mume wake

wa ndoa. Vinginevyo itambidi awategemee wanaume wengine, hali ambayo imekuwa ya kawaida kabisa na kwa bahati mbaya inazidi kuongezeka.

Propaganda Dhidi Ya Matunzo.

Wapotoshaji wa kijinsia wamegundua kuwa ikiwa mahitaji ya kifedha ya mwanamke hayatakidhiwa na mume wake, basi wao wanaweza kumnasa kirahisi. Hiyo ni moja ya sababu zinazosababisha kuwapo propaganda nyingi dhidi ya mume kumtunza mkewe. Ukichunguza falsafa ya wanawake kulipwa mishahara minono na makampuni ya kibiashara, unaweza kuelewa kirahisi tunachomaanisha.

Hakuna shaka yeyote kuwa kufuta mfumo wa mume kumtunza mkewe kutamfanya mwanamke kuwa malaya. Inawezekanaje kwa mwanamke anayejitegemea mwenyewe bila msaada wa mume akakidhi mahitaji yake ya asili yeye mwenyewe?

Wazo hili la kupiga marufuku matunzo ya mume kwa mkewe linaungwa mkono na wanaume waliochoshwa na israfu (ufujaji) wa wake zao. Wanataka kulipiza kisasi kwa wanawake wafujaji na wapenda mitindo kwa ujumla kupitia wanawake wenyewe na kulipa jina (wazo hili) la uhuru na usawa.

Will Durant, baada ya kufafanua maana ya *'neomarriage'* (ndoa mambolea) kama aina ya ndoa ya kisheria yenye uzuiaji mimba wa kisheria, talaka kuhitaji ridhaa ya pande zote mbili, na kutokuwepo na watoto (kutozaa watoto) na kutokuwepo matunzo anasema kuwa, "Wanawake wapenda mitindo wa tabaka la kati punde watasababisha kisasi cha wanaume wachapa kazi kuishia juu ya jinsia yote ya kike. Ndoa itapata mabadiliko makubwa kiasi cha kuwa wanawake wasiokuwa na kazi, ambao ni wapenda mapambo na manukato ghali watatoweka.

"Wanaume watawaomba wanawake wabebe gharama zao wenyewe. Ndoa za kirafiki au ndoa mamboleo humtaka mwanamke afanye kazi hadi mimba inapokuwa kubwa kabisa. Kuanzia sasa na kuendelea atapaswa kubeba gharama zake zote yeye mwenyewe na hivyo ukombozi wake utakuwa umekamilika. Mapinduzi ya viwanda yanadhihirisha madhara yake ya kikatili. Mwanamke analazimika kufanya kazi pamoja na mumewe viwandani. Mwanamke, badala ya kukaa chumbani na kumlazimisha mumewe kufanya kazi mara mbili kufidia kutozalisha kwake, atapaswa kuwa sawa na mumewe katika kazi, adhabu, haki na majukumu.

Kisha kwa kejeli, Will Durant anasema; "Hii ndio maana ya ukombozi wa mwanamke."

Dola Badala Ya Mume.

Ni ukweli usiopingika kuwa kuzaa ni jukumu la asili la mwanamke na kwa sababu hiyo analazimika kumtegemea mwanaume kwa ajili ya msaada wake wa kiuchumi na kifedha.

Baadhi ya watu katika Ulaya ya sasa, katika kutetea kwao ukombozi wa mwanamke, wamekwenda mbali zaidi mpaka kufikia kuunga mkono kurejeshwa kwa mfumo jike (*matriachal System*). Wanaamini

kuwa baada ya mwanamke kupata uhuru kamili na kupata usawa wake na mwanaume katika mambo yote, huko baadaye baba ataonekana kama nyongeza/kiambata kisicho cha lazima na hatimaye ataondolewa katika orodha ya wanafamilia.

Wakati huo huo, watu wanatoa wito kwa serikali kuchukua nafasi ya baba na kutoa ruzuku kwa wanawake ambao hawako tayari kubeba mzigo wa kuanzishsa familia peke yao, ili wasiache kuzaa watoto na ili wanaadamu wasitoweke duniani. Kwa maneno mengine, mwanamke ambaye huko nyuma alikuwa tegemezi na kwa mujibu wa wakosoaji wengine, alikuwa mtumwa wa mwanaume, huko baadaye atakuwa tegemezi na mtumwa wa serikali. Majukumu na haki za baba yatahamishiwa serikalini.

Mtu anaweza kutamani kuwa watu hawa ambao wamedhamiria kwa upofu wao kuudondosha muundo huu mtukufu wa familia uliojengwa kwa sheria za Mwenyezi Mungu, laiti wangekaa na kutafakari madhara ya kitendo chao.

Bertrand Russel katika kitabu chake kiitwacho, *'Marriage and Morals'* (Ndoa na Maadili) anajadili suala la uingiliaji wa serikali kiutamaduni na kiafya katika suala la watoto, anasema: "Inavyoonekana baba anapoteza umuhimu wake kama sababu ya kibaiolojia. Sababu nyingine yenye nguvu inayomuondoa katika nafasi yake ni mwelekeo wa wanawake katika uhuru wa kiuchumi. Wanawake wanaoshiriki kupiga kura, wengi wao hawajaolewa. Wanawake walioolewa wana matatizo zaidi kuliko wale ambao bado hawajaolewa licha ya kinga ya kisheria bado wako nyuma katika kufanikiwa kupata kazi.

Ikiwa wanawake walioolewa wanataka kudumisha uhuru wao wa kiuchumi, wanapaswa kuchagua moja kati ya haya mawili, ama washikilie kazi zao na kuacha jukumu la malezi ya watoto kwa mayaya wanaolipwa, au kupokea ruzuku wanayolipwa na serikali ili kuwawezesha kuwatunza watoto wao na wao wenyewe. Katika chaguo la kwanza, idadi ya vituo vya kulelea watoto wachanga na chekechea itaongezeka sana, na kwa mtazamo wa kisaikoloji, madhara ya asili ya hali hii yatakuwa kwamba watoto hawa hawatatambua kuwepo kwa baba wala mama.

Chaguo la pili peke yake halitoshi. Lazima liongezewe nguvu ya kisheria ya kuwaajiri tena kwa lazima akina mama, umri wa watoto wao unapofika umri fulani. Njia hii ina faida moja. Mwanamke anaweza kumlea mtoto wake mwenyewe bila kumtegemea mwanaume. Ikiwa sheria hii itapitihswa, itatupasa tusubiri kuona matokeo yake katika maadili ya familia.

Inawezekana sheria ikaamua kuwa mtoto aliyezaliwa nje ya ndoa hana haki ya kupata ruzuku au ikiwa kuna dalili kuwa mama alizini, ruzuku hiyo atapewa baba wa mtoto. Katika hali hii polisi wa kila eneo watapaswa kuwachunguza wanawake ambao hawajaolewa. Matokeo ya sheria hii hayatakuwa mazuri sana na yanaweza kuwafadhaisha wazazi (waliozini na kuzaa). Kwa sababu licha ya kinga ya kisheria, bado wazo la polisi kuwachunguza wanawake ambao hawajaolewa litaachwa na ruzuku itatolewa hata kwa akina mama waliozaa watoto nje ya ndoa. Katika hali hii, jukumu la kiuchumi la baba litatoweka kabisa miongoni mwa wafanya kazi na umuhimu wake kwa watoto wake hautakuwa zaidi ya ule wa mbwa au paka... Ustaarabu kwa jumla au huu ustaarabu ambao kwa sasa hivi umezuka unaelekea

kuzidhoofisha hisia za kimama.

Ili kuulinda ustaarabu huu, ambao tayari umeshaendelea sana, inaweza kuonekana kuwa ni muhimu kuwapa wanawake fedha nyingi ili waone kuwa mimba zina faida. Katika hali hii, haitakuwa muhimu au lazima kwa wanawake wote kuzaa. Itakuwa ni kazi ya kitaalamu kama kazi nyingine na itachaguliwa na wanawake kwa sifa zao. Lakini zote hizi ni dhana. Tunachomaanisha ni kuwa harakati za ukombozi wa wanawake zinasababisha kuporomoka kwa mfumo dume (*patriarchy system*), ambao toka zama za kabla ya kuandikwa kwa historia, ulikuwa ni alama ya ushindi wa mwanaume dhidi ya mwanamke. Katika nchi za Magharibi inaaminika kuwa ni alama ya ustaarabu kuwa serikali inachukua nafasi ya baba..."

Kama ilivyo dhahiri kutokana na maelezo hayo hapo juu (ya Bertrand Russel), kufuta matunzo ya mwanamke, au kama mabwana hawa wanavyopenda kuuita uhuru wa mwanamke wa kiuchumi, kutakuwa na madhara yafuatayo:

Baba ataondolewa katika orodha ya wanafamilia au kwa uchache atapoteza umuhimu wake. Mfumo jike utafufuliwa. Serikali itachukua nafasi ya baba. Akina mama watasaidiwa na serikali. Hisia za kimama zitadhoofika. Kuzaa/kubeba mimba kutapoteza hisia za asili na sasa kutakuwa ni kazi ya kuajiriwa kama kazi nyingine.

Ni wazi kuwa, matokeo ya maendeleo yote haya yatakuwa ni kubomoka kwa familia ambako kutamaanisha kuanguka kwa ubinadamu. Katika hali hiyo kila kitu kitakwenda vizuri isipokuwa kitu kimoja tu ndio kitakosekana nacho ni furaha na utulivu wa kiakili, vitu vinavyopatikana katika familia tu.

Hata hivyo, tunachomaanisha ni kuwa hata wanaounga mkono uhuru kamili wa mwanamke na kumuondoa baba katika orodha ya wanafamilia wanashikilia kuwa jukumu la asili la mwanamke la kuzaa watoto linampa haki ya kupata ruzuku na katika baadhi ya mazingira mshahara, au marupurupu na kwa mujibu wao, malipo haya yalipwe na serikali. Kwa upande mwingine mchango wa mwanaume katika uzazi (kutunga mimba) haumpi haki hiyo (ya kulipwa ruzuku n.k).

Sheria za kazi duniani, zinapopanga mshahara wa chini wa mfanyakazi wa kiume, huzingatia mahitaji ya mke wake na watoto pia, jambo linalomaanisha kuwa sheria za kazi duniani zinatambua rasmi kuwa mwanaume anawajibu kumtunza mke wake na watoto.

Je Azimio La Haki Za Binadamu Kwa Wote Limemdhalilisha Mwanamke?

Azimio la Haki za Binadamu kwa wote (kifungu cha 23, ibara iii) linasema; "Kila mtu ambaye anafanya kazi ana haki ya kupata malipo ya haki na yanayofaa, ili kumhakikishia yeye mwenyewe mwanaume na familia yake maisha yenye heshima na kukiwa na haja apewe kinga nyingine ya ziada."

Ibara ya (i) kifungu cha 25 kinasema; “Kila mmoja ana haki ya kuishi maisha mazuri, yanayofaa kwa afya na siha yake yeye mwenywe (mwanaume) na familia yake, ikiwa ni pamoja na chakula, mavazi nyumba, matibabu na mahitaji mengine yote ya lazima ya kijamii na kinga sahihi wakati mtu anapopoteza ajira, ugonjwa, kupata ulemavu, kufa na kuacha mjane, uzee au hali nyinginezo ambazo ziko nje ya udhibiti wake.

Vifungu hivi viwili vinamaanisha kuwa kila mwanaume, anayeanzisha familia anapaswa kubeba gharama za mke wake na watoto na kwamba gharama zao zinahesabika kuwa sehemu ya gharama zake mwenyewe.

Ingawa Azimio la haki za Binadamu limeeleza wazi wazi kuwa mwanaume na mwanamke wana haki sawa halijaona kuwa mwanaume kumtunza mwanamke kuwa ni matusi kwa mwanamke au kuwa ni doa kwa usawa wake. Hivyo wale wanaolinukuu azimio hili kama rejea yao muhimu wanapaswa kuliangalia suala la matunzo ya mume kwa mkewe kuwa limewekwa wazi katika azimio hili. Je, wale wenye akili za Kimagharibi wanaokiita kila kitu cha Kiislamu kuwa ni cha kupinga maendeleo watalikasirikia pia hili azimio na kuliezea kuwa linarejesha utumwa wa mwanamke?

Aidha, Azimio la Haki za Binadamu linaposema kuwa kila mmoja ana haki ya usalama au kinga pindi anapopoteza kazi anapougua, anapopata ulemavu, anapokufa na kuacha mjane, uzee au kukosa njia ya kujipatia riziki katika hali ambazo yeye hana udhibiti nazo, sio tu kwamba zinauelezea ujane kuwa ni pigo kwa riziki lakini linautaja sambamba na ukosefu wa ajira, maradhi na ulemavu. Hivyo linawaweka wanawake katika kundi la wasio na ajira, wagonjwa, walemavu na wazee. Je, hili sio tusi kubwa kwa mwanamke? Kama maelezo haya yangekutwa katika vitabu au sheria za nchi ya Mashariki (Asia), bila shaka kelele kubwa ingekuwa imeshapigwa mpaka sasa kulilaani hilo.

Lakini wale wanaotazama mambo kwa uhalisia wake kiasi cha kutorubuniwa kirahisi na propaganda za uwongo wanaelewa fika kuwa sheria ya maumbile na hata Azimio la Haki za Binadamu, zilizoweka ujane katika kundi la wasio na ajira haiwadhalilishi. Halikadhalika, sheria ya Kiislamu ambayo imefanya matunzo ya mwanamke kuwa wajibu kwa mwanaume, haijamshusha hadhi mwanamke. Ni ukweli kwamba ameumbwa hivyo kwamba anamhitaji mwanaume na anamtegemea.

Mwanaume na mwanamke wameumbwa katika hali ya kutegemeana kwa nia ya kuufanya muungano wao uwe na nguvu na imara na kuyafanya mahusiano ya kifamilia ambayo ni muhimu kwa furaha ya mwanadamu kuwa thabiti zaidi, ikiwa mwanamke atamtegemea mwanaume kifedha mwanaume naye humtegemea mwanamke kwa utulivu wa akili. Hivyo kutegemeana huwaleta karibu zaidi na huwaunganisha vizuri zaidi.

Mirathi

Zama za kale mwanamke alikuwa harithi kitu na, hata aliporithi, alitendewa kama mtoto. Alikuwa hana haiba ya kisheria inayojitegemea. Kwa mujibu wa baadhi ya mifumo ya kisheria ya kale, mtoto wa kike alipata urithi lakini watoto wake hawakupata. Kwa upande mwingine, mtoto wa kiume sio tu anapata urithi yeye mwenyewe, bali pia watoto wake walirithi mali iliyoachwa na mababu zao. Baadhi ya mifumo mingine ya sheria ilimruhusu mwanamke kurithi lakini si kwa kupata asilimia maalum au kwa lugha ya Qur'ani 'gawio lililopangwa.' Walichokifanya ilikuwa ni kumruhusu mzazi kuusia kuwa apewe, kama muusiaji anataka.

Wanahistoria na wachunguzi wameeleza kwa kina aina mbali mbali za sheria zilizokuwepo kale, lakini kwa sasa hatutaki kwenda kwa undani zaidi. Kwa sasa ufupisho tulioueleza hapo juu unatosha.

Kwa Nini Mwanamke Alinyimwa Urithi?

Sababu kuu ya kumnyima mwanamke urithi ilikuwa ni kuzuia kuhama kwa mali kutoka familia moja kwenda nyingine. Kwa mujibu ya imani za kale, mchango wa mwanamke katika uzazi haukuwa wa thamani sana. Akina mama walitumika kama mifuko tu ambamo mbegu ya baba ilikua na kuwa mtoto. Kwa sababu hii waliamini kuwa watoto wa mtoto wa kiume walikuwa sehemu ya familia lakini watoto wa mtoto wa kike hawakuwa sehemu ya familia yake, kwa vile walikuwa sehemu ya familia ya babu yao mzaa baba. Hivyo kama binti angepata urithi, hiyo ingemaanisha kuhamisha mali kwenda kwa watoto wake (binti), watoto ambao hawahusiani na familia ya marehemu.

Marehemu Dr. Musa Ameed anasema kuwa katika siku za kale dini na sio mahusiano mengine yoyote ya asili, ndio ilikuwa msingi wa uundwaji wa familia. Babu, mbali na kuwa mkuu wa kijamii wa watoto na wajukuu wake, pia alikuwa mkuu wao wa kidini. Utekelezaji wa sherehe za kidini na matendo ya ibada yalikabidhiwa kwa kizazi kinachofuatia kupitia kwa watoto wa kiume tu. Wahenga waliwaona wanaume peke yao kuwa ndiyo njia ya kuhifadhi na kuendeleza kizazi. Baba wa familia mbali na kumpa maisha mwanaye wa kiume, pia alimkabidhi imani na matendo ya kidini. Kwa mujibu wa Maveda wa Kihindi na Wagiriki na sheria za kirumi, nguvu ya kizazi ilikuwa kwa wanaume tu, na hivyo dini za familia zilikuwa ni miliki ya wanaume pekee, na wanawake hawakuwa na usemi wowote isipokuwa kupitia kwa baba zao au waume zao. Kwa vile hawakuweza kushiriki katika utekelezaji wa sherehe na shughuli za kidini, basi walikosa faida na manufaa yote ya kifamilia. Hivyo mfumo wa urithi ulipokuja wanawake walitengwa.

Kutengwa kwa wanawake katika urithi kulikuwa na sababu nyingine pia, mojawapo ikiwa ni kuwa hawakuwa wakakamavu vya kutosha kuwa askari. Katika jamii ambazo ziliweka umuhimu mkubwa katika matendo ya kishujaa na nguvu ya kupigana, na mpiganaji alionekana kuwa bora kuliko watu laki moja wasio wapiganaji, mwanamke alinyimwa urithi kwa vile hakuwa na uwezo wa kupigana.

Kwa sababu hii, Waarabu wa zama za kabla ya Uislamu, walikuwa hawakubali suala la mwanamke kurithi mali, maadamu kulikuwepo wanafamilia wa kiume hata kama kiukoo walikuwa ni ndugu wa mbali. Hii ndio sababu walishangazwa sana Qur'ani iliposema wazi wazi kuwa;

لِلرِّجَالِ نَصِيبٌ مِمَّا اكْتَسَبُوا ۚ وَلِلنِّسَاءِ نَصِيبٌ مِمَّا اكْتَسَبْنَ ۚ

"Wanaume wana sehemu katika kile kinachoachwa na wazazi na ndugu wa karibu, kiwe kikubwa au kidogo gawio lililopangwa." (***Suratul Nisa, 4:32***)***.***

Ilipata kutokea wakati fulani ndugu yake na Hasan bin Thabit, mshairi maarufu, alifariki katika siku hizo, huku akiacha mke na binti zake wengi. Binamu zao wa mfumo dume waligawiana mali zote na hawakuwapa chochote mjane na binti zake. Mjane alilalamika kwa Mtume ambaye aliwaita ndugu wa mume. Walisema kuwa mwanamke hakuwa na uwezo wa kubeba silaha na kupigana na adui. Ni wanaume waliojilinda wao na wanawake. Hivyo ni wao tu waliokuwa na haki ya kurithi mali. Walipofikia hapo Mtume akawasomea amri ya Allah, kama ilivyo katika Aya hiyo hapo juu.

Urithi Wa Mtoto Wa Kiume Wa Kupanga.

Waarabu wa kipindi cha kabla ya Uislamu wakati fulani walimfanya mtu fulani kuwa mtoto wao wa kiume wa kupanga. Mtoto huyu wa kupanga kama mtoto halisi, alichukuliwa kuwa mrithi. Mila ya kujipatia watoto wa kupanga ilikuwepo katika mataifa mengine pia kama vile Urumi na Iran. Mtoto wa kiume wa kupanga, kama ilivyo kwa mtoto halisi alikuwa na haki zote ambazo mabinti halisi wa kuzaliwa hawakuwa nazo. Haki hizi zilikuwa ni pamoja na haki ya kurithi. Halikadhalika kumuoa mke wa mtoto wa kupanga hakukuwa kunaruhusiwa. Qur'ani Tukufu ilipiga marufuku mila hizi.

Urithi Wa Mshirika

Mila nyingine, iliyokuwa ya kawaida miongoni mwa Waarabu wa kabla ya Uislamu ilikuwa ni ile ya ushirika (*alliance*)*.* Watu ambao hawakuwa na uhusiano wa damu walikula yamini ya undugu kuwa; "Damu yako ni damu yangu, uchokozi wowote dhidi yako utakuwa ni uchokozi dhidi yangu; utarithi mali yangu na mimi nitarithi mali yako." Kwa mujibu wa ushirika huu, makundi yote yalikuwa yakiwajibika kumlinda mshirika wake katika kipindi chote cha uhai wao, na mmoja wao alipokufa, mshirika aliyebaki alichukua mali za marehemu.

Mke Kama Sehemu Ya Mirathi.

Wakati fulani zama za kabala ya Uislamu, Waarabu walikuwa wakimhesabu mjane kuwa sehemu ya mali ya mume aliyefariki na hivyo, yeye pia alirithiwa. Ikiwa marehemu alikuwa na mtoto wa kiume

kutoka kwa mke mwingine, huyo alikuwa na uwezo wa kumrushia mjane kipande cha nguo kama ishara ya kumrithi. Baada ya hapo alikuwa na uhuru wa kumwamulia atakavyo au kumfanya vyovyote apendavyo kwa raha zake. Alikuwa na hiari ya ama kumuoa yeye mwenyewe au kumuozesha kwa mtu mwingine na yeye kuchukua mahari. Mila hii ambayo haikuwepo miongoni mwa Waarabu peke yao ilipigwa marufuku na Qur'ani.

Kuhusiana na suala hili la mirathi katika madaraja mbali mbali, sheria za jamii za kale za Wahindi, Wajapan, Warumi, Wagiriki (wayunani) na Wairani zilikuwa ama haziruhusu wanawake kurithi au zilikuwa zinawabagua (yaani walikuwa wanapewa kidogo sana). Kutokana na uchache wa nafasi hatuwezi kuyaandika hapa yote yaliyoandikwa na wataalamu wa fani hii.

Mila Ya Kuwarithi Wanawake Katika Kipindi Cha Sasania.

Hayati Saeed Nafisi katika kitabu chake, '*Social History of Iran from the Sasanian times to the end of the Ummayad period'* ameandika kuwa; "Tabia nyingine ya kuvutia au kushangaza ya utamaduni wa Wasasania ilikuwa ya kwamba mvulana alipobaleghe, baba yake alimuozesha mwanae huyo mmoja wa wake zake wengi (wa baba huyo). Katika zama hizo mwanamke hakuwa na haki yoyote ya kisheria. Baba na mume walikuwa na madaraka makubwa sana juu ya mali ya mwanamke.

"Lilikuwa ni jukumu la baba au mkuu wa familia kumuoza binti yake alipofikia umri wa miaka 15. Lakini umri wa kuoa kwa wavulana ulikuwa miaka 20. Baada ya kuolewa binti huyo hakuwa na haki ya kurithi mali ya baba yake au mlezi wake. Hakuwa na haki ya kuchagua mume, lakini alikuwa na hiari ya kufanya ndoa ya haramu ikiwa baba yake alishindwa kumuoza baada ya kuwa amevunja ungo. Katika hali hiyo, pia hakuruhusiwa kurithi chochote kutoka kwa baba yake.

Hapakuwa na kikomo cha idadi ya wanawake ambao mwanaume angeweza kuoa. Kumbukumbu za Wagiriki zinaonyesha kuwa mume alikuwa akimiliki mamia ya wanawake katika nyumba yake. Vitabu vya kidini vya Wazoroastria vinaonyesha kuwa kanuni za ndoa katika zama za Sasania zilikuwa tata na zilizokorogeka.

Urithi Wa Mwanamke Katika Uislamu.

Sheria ya mirathi ya Kiislamu imeepukana na mapungufu yote ya huko nyuma. Kitu kinachopingwa na wale wanaodai kutetea usawa kati ya mwanaume na mwanamke, ni kwamba gawio la mwanamke ni nusu ya gawio la mwanaume. Kwa mujibu wa sheria ya Kiislamu mtoto wa kiume hupata mara mbili ya mtoto wa kike, kaka hupata mara mbili ya dada yake na mume hupata mara mbili ya kile anachopata mke wake. Gawio la baba na mama ndio halifuati utaratibu huu.

Ikiwa marehemu ana watoto, na wazazi (wa huyo marehemu) wako hai, kila mmoja wa wazazi wawili atapata moja ya sita ya mali iliyoachwa na marehemu. Ni kutokana na nafasi maalum ya mwanamke katika mahari, matunzo, huduma za kijeshi na baadhi ya sheria za jinai ndio maana gawio lake

limefanywa kuwa nusu ya lile la mwanaume.

Kwa sababu zilizotajwa hapo awali, Uislamu unachukulia matunzo na mahari kuwa ni mambo muhimu na ya lazima katika kuiimarisha ndoa. Yanatoa hakikisho la maelewano na masikilizano. Kuyaondoa ni kulitikisa jengo zima la familia na kumsukumia mwanamke katika umalaya. Kwa vile mahari na matunzo ni wajibu wa lazima wa mume, basi ni wazi kuwa majukumu ya kifedha ya mwanamke yamepunguzwa sana na mzigo wa mwanaume umeongezwa. Ili kufidia jukumu zito alilonalo mwanaume, gawio lake la urithi limepangwa kuwa mara mbili ya lile la manamke. Ni mahari na matunzo yaliyopunguza gawio la mwanamke.

Pingamizi La Wamagharibi.

Baadhi ya watu wa Magharibi wanapokosoa udogo wa gawio la mwanamke la urithi na wanapolitumia hili kama silaha ya propaganda dhidi ya Uislamu, wanadai kuwa hakuna ulazima wowote wa kupunguza gawio la mwanamke ili kuja kulifidia kwa mahari na matunzo. Je, kuna haja yoyote ya kupita vichochoroni na kuzunguka vichaka? Kwanini gawio la mirathi la mwanamke lisilingane na gawio la mwanaume ili tusilazimike kulifidia kwa mahari na matunzo?

Hawa mabwana ambao wanaonekana kumpenda mfalme kuliko mfalme mwenywe anavyojipenda wamechanganya habari. Sababisho wamelipeka kwenye matokeo na matokeo wameyapeleka kwenye sababisho. Wanafikiri kuwa mahari na matunzo ni matokeo ya nafasi ya pekee kuhusiani na urithi, wakati ambapo ukweli ni kinyume chake.

Aidha, wanaelekea kuwa na mawazo kuwa kipengele cha fedha ndio kitu pekee kinachozingatiwa, kama hiki kingekuwa ndio kigezo pekee basi kusingekuwa na haja ya mfumo wa mahari na matunzo wala mfumo unaotoa tofauti ya gawio kati ya mwanaume na mwanamke.

Kama tulivyoeleza mwanzo, Uislamu umezingatia vipengele vingi, vingine ni vya asili na vingine ni vya kisaikolojia. Umezingatia mahitaji maalumu ya mwanamke, yanayotokana na jukumu lake la uzazi. Kimsingi mwanaume hana mahitaji hayo. Mbali na hayo, kwa upande mwingine, uwezo wa mwanamke wa kuzalisha ni mdogo kuliko wa mwanaume na kwa upande mwingine matumizi yake ni makubwa kuliko ya mwanaume.

Kwa nyongeza, kuna vipengele vingine mbali mbali vya kujirembesha kuhusiana na mfumo wa akili zao. Kwa mfano mwanaume mara zote hupenda kutumia fedha zake kwa ajili ya mwanamke anayempenda. Vipengele vingine vya kisaikolojia na kijamii, vinavyosaidia kuimarisha mahusiano ya kifamilia pia vimezingatiwa. Kwa kuzingatia nukta zote hizi, Uislamu umefanya mahari na matunzo kuwa ni wajibu wa lazima. Hivyo sio suala la pesa, ambalo inaweza kusemwa kwamba kuna haja ya kupunguzwa mgao wa mwanamke sehemu moja na kumfidia sehemu nyingine.

Pingamizi La Waasi Wa Kipindi Cha Awali Cha Uislamu.

Tumesema kuwa mahari na matunzo ni sababisho na nafasi ya pekee ya mwanamke na tofauti zilizopo katika mirathi ni matokea yake. Nukta hii haijaanzishwa leo. Ilikuwepo hata katika siku za awali za Uislamu.

Katika karne ya pili Hijria alikuwepo mtu mmoja aliyeitwa Ibn Abi alAwja, ambaye hakuwa akiamini juu ya dini. Kwa kutumia fursa ya uhuru wa kidini (imani) ya wakati ule alikuwa akielezea waziwazi mawazo yake ya kikafiri. Wakati fulani alikuwa akija katika Masjid alHaram (Makka) au Masjid Nabawi (Madina) na alikuwa akijibizana na wanavyuoni wa wakati ule juu ya kanuni za Uislamu.

Moja ya pingamizi lake dhidi ya Uislamu lilihusu mirathi. Alikuwa akisema; “Ana kosa gani huyu mwanamke maskini anayepata sehemu moja wakati mwanaume anapata sehemu mbili.” Kwa mujibu wake yeye hii ilikuwa ni dhulma kwa mwanamke. Imam Jafar asSadiq (as) katika kumjibu alisema kuwa hali iko hivyo kwa sababu mwanamke amesamehewa kazi za jeshi. Na zaidi ya hilo Uislamu umemuamrisha mwanaume kulipa mahari na kumtunza mkewe na katika baadhi ya kesi za jinai ambapo ndugu wa mhalifu walipaswa kulipa fedha za damu (kufidia mtu aliyeuliwa) mwanamke aliondolewa (alisamehewa) katika malipo hayo. Hizi ndio sababu zilizofanya gawio lake lipunguzwe.

Hivyo Imam Jafar Sadiq (as) alieleza wazi wazi nafasi ya pekee ya mwanamke juu ya mirathi, sheria ya mirathi na matunzo, kusamehewa kwake kutoa huduma ya jeshi na malipo ya fedha za damu.

Maimamu wengine pia walijibu hivyo hivyo walipoulizwa swali hilo.

Talaka

Talaka I

Hakuna zama kama hizi za kwetu ambapo uzingativu umefanywa sana kwenye hatari ya kusambaratika kwa familia na madhara yake. Na tena, hakuna zama kama hizi za kwetu ambapo mtu amekabiliana na hatari halisi ya kusambaratika huko.

Kuongezeka Kwa Talaka Katika Maisha Ya Kisasa.

Huko nyuma uzingativu sana haukuwekwa katika tatizo la talaka, sababu zake na madhara yake pamoja

na mbinu za kulizuia vilikuwa havijadiliwi sana na bado idadi ya talaka ilikuwa ndogo sana. Hakuna shaka kuwa ongezeko la talaka hivi sasa ikilinganishwa na zamani linatokana na kuongezeka kwa sababu za talaka. Maisha ya kijamii yamebadilika mno kiasi cha kuwa sasa kuna uwezekano mkubwa zaidi wa kuvurugika kwa familia, na hii ndio sababu jitihada za wasomi na watu wanaoshughulikia masuala ya kijamii zimeshindwa kuzaa matunda. Inasikitisha kuwa kizazi kijacho kinakubaliwa na hatari zaidi.

Gazeti la Kimarekani, '*Newsweek'* katika makala inayovutia yenye kichwa cha habari *'Divorce in America'* (Talaka katika Marekani) linaandika kuwa ukiwa Marekani ni rahisi zaidi kupata talaka kuliko kupata taksii.

'Newsweek' linaandika zaidi kuwa methali mbili kuhusu talaka zinajulikana zaidi miongoni mwa Wamarekani kuliko methali nyingine zozote zile. Mojawapo ni kuwa 'Usuluhishi mgumu kabisa kati ya mume na mke ni bora kuliko talaka.' Methali hii ina umri wa miaka 400 na zaidi.

Ya pili ambayo imebeba ujumbe ulio kinyume na hii methali ya kwanza imepata umaarufu katika nusu ya pili ya karne ya 20. Inasema kuwa 'penzi la pili ni tamu zaidi kuliko la kwanza."

Makala inaonyesha kuwa methali ya pili ndiyo inayofanya kazi zaidi nchini Marekani. Jinamizi la talaka linajivutia kwake, sio kwa ndoa mpya tu, bali hata za mama zao na za wanandoa waliooana zamani huko. Tangu wakati wa Vita vya pili vya Dunia na kuendelea, kwa wastani idadi ya talaka kwa mwaka si chini ya laki nne (400,000). Katika hizo ndoa zilizovunjika, 40% zilikuwa zimeweza kudumu kwa miaka kumi na zaidi na 13% ndizo zilikuwa zimeweza kudumu kwa zaidi ya miaka 20. Wastani wa umri wa talaka (umri wa wanawake wanaotalikiwa) wa wanawake milioni mbili ilikuwa ni miaka 45, 62% ya hao walikuwa na watoto wenye umri wa chini ya miaka 18 wakati ndoa ilipokuwa inavunjika. Wanawake hawa, kwa kusema kweli, wanaunda kizazi maalum.

Ingawa mwanamke wa Kimarekani hujisikia huru kabisa baada ya talaka, lakini bado hao waliotalikiwa, wawe vijana au wa umri wa kati, huwa hawana furaha. Kutokuwa kwao na furaha kunaweza kupimwa kutokana na ongezeko la idadi ya wanawake wanaowaita madaktari wa akili au ambao ni walevi wa kupindukia.

Katika kila wanawake wanne, mmoja ni mlevi. Idadi ya wanawake waliotalikiwa wanaojinyonga ni kubwa mara tatu kuliko ya wale wenye waume. Kwa kifupi ni kuwa mara tu mwanamke anapoibuka mshindi katika mahakama ya talaka hugundua kuwa maisha baada ya talaka sio kitanda cha maua ya waridi. Ni vigumu ulimwengu kuwa na maoni mazuri juu ya mwanamke anayeivunja ndoa yake, nyumba thabiti kabisa ya mahusiano ya mwanadamu. Jamii inaweza kumheshimu mwanamke huyo na pengine kumuonea wivu, lakini haiwezi kumuona kuwa ni mtu aliyeingia katika maisha ya mtu na kumletea furaha (mumewe).

Katika makala hii ya gazeti la *Newsweek* suali limeibuka kuwa ongezeko hili la talaka linalozidi kukua linatokana na mwenendo usio kubaliana kati ya mume na mke, au sababu nyingine. Mwandishi wa

makala hii amesema kuwa hata kama tofauti za tabia na kutopatana zitakubaliwa kuwa sababu ya kutengana kwa wanandoa waliooana hivi punde, nini tunaweza kusema juu ya talaka za wanandoa walioishi ndani ya ndoa kwa muda mrefu? Tukizingatia msaada wa kisheria unaotolewa na sheria ya Marekani kuhusiana na talaka, tunaweza kusema kuwa kutofautiana kwa mihemko na tabia sio sababu ya kutengana kwa wanandoa walioishi kwa miaka kumi au zaidi.

Katika zama za vidonge vya kuzuia mimba, mapinduzi ya ngono (ufuska) na kuboreka kwa hadhi yao ya kisheria, wanawake wengi wametokea kuamini kuwa furaha na raha ni bora kuliko uimara wa maisha ya ndoa. Mara nyingi unaweza kuona kuwa mume na mke wanaishi pamoja kwa miaka, wana watoto, kila mmoja anashiriki furaha na huzuni ya mwenzake lakini ghafla mke anaomba talaka bila ya kuwepo mabadiliko yoyote ya kimali au hadhi na makubaliano ya mume. Sababu ni kuwa, mpaka jana, mwanamke alikuwa tayari kuvumilia uchoshi wa maisha, lakini hayuko tayari kufanya hivyo leo.

Ongezeko la kesi za talaka haliko Marekani peke yake. Sehemu yoyote ambayo utamaduni wa Kimagharibi umejipenyeza kwa kiasi fulani, kiwango cha talaka kiko juu. Hata katika nchi za Mashariki, talaka imekuwa ni jambo la kawaida zaidi katika miji mikubwa ya kisasa kuliko katika miji midogo na vijiji.

Mazingira Yanayochangia Talaka Nchini Marekani.

Tayari tumeshalinukuu gazeti la Newsweek likisema kuwa mwanamke wa kimarekani hujali zaidi starehe na burudani kuliko uthabiti na uimara wa maisha ya familia. Sasa hebu tupige hatua moja mbele ili tuone kwanini amechukua mwelekeo huo. Hapana shaka kwamba tabia hii sio ya asili wala ya kuzaliwa nayo. Imetokana na sababu fulani za kijamii. Ni mazingira ya Marekani yaliyosababisha akili hii ya mwanamke wa Kimarekani. Baadhi ya watu wa Magharibi wanafanya jitihada kubwa kumsukumia mwanamke wa Mashariki katika mwenendo wanaoufuata wanawake wa Kimarekani. Kama wakifanikiwa majaaliwa ya mwanamke wa Mashariki na familia ya Mashariki hayatakuwa na tofauti na yale ya mwanamke wa kimarekani na familia ya Kimarekani.

Gazeti maarufu la Ufaranza litolewalo kila siku linaandika kuwa katika migahawa zaidi ya 200 na nyumba za kulala wageni katika jimbo la Califonia, wafanyakazi (wahudumu) wa kike wanavaa nguo za nusu uchi. Nguo hizo ambazo ni za kuogelea zinatambuliwa kuwa ndio sare za kazini katika miji ya SanFransisco na Los Angeles.

Katika jiji la New York kuna kumbi nyingi za sinema zinazoonyesha filamu za ngono tu, na picha za uchi za wanawake zinaweza kuonekana zikionyeshwa mbele ya milango ya kuingilia kumbini. Majina ya filamu za ngono ni ya aina hii; “Wanaume wanaobadilishana wake zao’, ‘Wasichana wasio na maadili,’ ‘Magauni ambayo hayafichi chochote.’ Maktaba kuna vitabu vichache sana vya hadithi za kubuni (*fiction books*) ambavyo katika majalada yake hakuna picha za wanawake walio uchi.

Majina ya vitabu kama vile ‘Tabia ya ngono ya wanaume wa kimarekani,’ ‘Tabia ya ngono ya wanaume wa Kimagharibi,’ Tabia ya ngono ya vijana walio chini ya miaka 20,’ ‘Mbinu mpya za ngono zilizotokana

na habari mpya kabisa," vimekuwa maarufu na vingi mno. Mwandishi wa makala katika gazeti hili la Kifaransa anauliza kwa mshangao na wasiwasi; "Marekani unakwenda wapi?'

Katika mazingira kama haya ikiwa mwanamke wa Kimarekani amepoteza mizania yake na anajali burudani na raha zaidi kuliko uaminifu kwa mume wake na familia, hawezi kulaumiwa. Ni mazingira ya kijamii ambayo yameharibu kila mzizi wa mfumo wa utakatifu wa familia.

Inashangaza kuwa viongozi wa zama zetu wanazipa nguvu na msukumo zaidi sababu zinazosababisha talaka na kusambaratika kwa maisha ya familia na kwa upande mwingine wanapiga mayowe na kelele kuwa kiwango cha talaka kimekuwa kikubwa mno. Hii ni sawa na kumwambia mtu afagie bohari na kuomba asichafue nguo zake.

Nadharia Tano.

Hebu tuangalie, iwapo kimsingi talaka ni nzuri au mbaya. Swali ni je ni jambo zuri kuuacha wazi mlango wa talaka, hata katika hatari ya kusambaratika kwa maisha ya familia? Ikiwa ni jambo zuri basi hakuna tatizo hata kama kiwango cha talaka kitakuwa kikubwa. Na ikiwa sio jambo zuri, je talaka ipigwe marufuku kabisa na ndoa ifanywe kuwa ya milele? Wazo la tatu ni kuwa talaka isipigwe marufuku kisheria, kwani katika baadhi ya hali haiepukiki, lakini wakati huo huo jamii ichukue kila hatua inayowezekana kuondosha sababu za mikwaruzano na kutengana kwa mume na mke na hivyo kuwanusuru watoto kukosa familia. Ni dhahiri kuwa sheria peke yake haiwezi kufanya chochote ikiwa jamii yenyewe inazipalilia sababu zinazosababisha talaka.

Ikiwa talaka haifai kupigwa marufuku kabisa, je iruhusiwe katika muundo gani? Je ni nani awe na mamlaka ya kutoa talaka? Mwanaume peke yake, mwanamke peke yake au wote? Na wazo la mwisho ni kuwa je mwanaume na mwanamke wote wafuate taratibu zinazofanana katiksa kutoa au kuomba talaka au kila jinsia iwe na utaratibu wake?

Yote kwa yote, hizi ni nadharia tano zinazohusiana na Talaka:

Talaka inayotolewa bila kikwazo chochote cha kisheria au kimaadili. Hawa ni wale wanaoitazama ndoa kwa mtazamo wa kupata raha tu, ambao hawaipi utakatifu wowote, na ambao hawajali thamani ya kijamii ya familia. Wanafikiri kuwa mara tu baada ya ndoa kuvunjika na ndoa mpya kuchukua nafasi ya ndoa ya zamani (iliyovunjilka) wanaume na wanawake walioachana hupata furaha zaidi. Yule anayesema kuwa penzi la pili ni tamu kuliko penzi la kwanza ndiye huiunga mkono nadharia hii. Katika nadharia hii, sio tu kwamba thamani ya kijamii ya kifamilia imesahauliwa lakini pia furaha na kuridhishana kunakosababishwa na ndoa kumepuuzwa pia. Hivyo nadharia hii ni ya kipuuzi na ya kitoto kabisa.

Ndoa ni taasisi takatifu. Ni muungano wa mioyo na roho, taasisi ambayo lazima itunzwe kwa usalama na isiharibiwe. Neno talaka linapaswa kuondolewa kutoka katika kamusi ya jamii ya wanaadamu.

Mwanaume na mwanamke wanaooana lazima wajue kuwa hakuna kitakachowatenganisha zaidi ya kifo.

Hii ndio nadharia ambayo imekuwa ikitetewa na Kanisa Katoliki kwa karne nyingi na bado inatetewa.

Wanaoiunga mkono nadharia hii wanazidi kupungua dunaini. Hivi sasa ni Italia na Hispania tu wanoifuata. Ni mara nyingi tu tunasikia kwamba, hata Italia, wanaume na wanawake wanaipinga sheria hii na jitihada zinafanyika ili sheria ya talaka itambuliwe rasmi. Watu wengi hawako tayari kuendelea kutaabika na michosho ya ndoa zao zisizo na mafanikio.

Miaka kadhaa huko nyuma, gazeti la *'The Daily Express'* lilichapisha makala yenye kichwa cha habari, 'Ndoa Italia ina maana kifungo kwa mwanamke.' Makala hii ilisema kuwa, hivi sasa kutokana na kutokuwepo kwa talaka, watu wa Italia wanajiingiza katika mahusiano ya haramu (zinaa). Zaidi ya Waitalia milioni tano walikuwa wakiamini kuwa maisha yao yamejaa madhambi.

Gazeti la Italia litolewalo kila siku liliandika kuwa kuzuia talaka kumesababisha tatizo kubwa sana kwa Waitalia. Wengi wao walilazimika kuukana uraia wa Italia kwa sababu hiyo. Taasisi fulani ya Italia ilipoitisha kura ya maoni, 97% ya wanawake wa Italia walijibu 'hapana' kwa swali lililoulizwa kuwa iwapo talaka ilikuwa ni jambo linalochukiza katika kanuni za dini.

Bado kanisa linashikilia msimamo wake na kuendelea kutoa hoja kuutetea (msimamo huo).

Hapana shaka yeyote kuwa ndoa ni taasisi takatifu na inatakiwa idumu. Lakini inaweza tu kudumu iwapo wanandoa wote wawili wanashirikiana. Kuna hali ambapo maelewano kati ya mke na mume huwa hayawezekani. Katika hali kama hizi nguvu za sheria haziwezi kuwapatanisha na kuwaunganisha kwa jina la muungano wa ndoa. Nadharia ya kanisa imeshindwa kabisa kufanya kazi. Sio ajabu muda si mrefu kanisa lenyewe likabadilisha msimamo wake. Hivyo hatuhitaji kuijadili nadharia hii zaidi.

Ndoa inaweza kuvunjwa na mwanaume sio mwanamke. Katika ulimwengu wa zamani watu wengi walikuwa na mtazamo huu, lakini sasa hatudhani kuwa una wafuasi. Hivyo hatuhitaji kuijadili pia.

Ndoa ni taasisi takatifu na mfumo wa kifamilia unaheshimika, lakini mlango wa kutoa talaka kwa masharti fulani, uwe wazi kwa wanandoa wote na taratibu za kuvunja ndoa zinapaswa zifanane kwa jinsia zote mbili. Watetezi wa kufanana kwa haki za familia ambao kwa makosa walikuita usawa wa haki kati ya mwanaume na mwanamke, wanaiunga mkono nadharia hii. Kwa mujibu wa watu hawa, masharti yanayofanana, mipaka inayofanana na vikwazo vinavyofanana vinapaswa vitumike kwa wote wawili, mwanamke na mwanaume wakati wa kuvunja ndoa. Wanapinga suluhishi jingine ambalo ni la kidhalimu na linalobagua.

Hapana shaka ndoa ni taasisi takatifu, mfumo wa familia unaheshimika, talaka ni jambo linalochukuza na ni jukumu la jamii kuondoa visababisho vyote vya talaka, lakini bado talaka haiwezi kuzuiwa moja kwa moja na kwamba mamlaka ya kutoa au kuomba talaka yapo kwa wote wawili, mwanamke na mwanaume. Hata hivyo utaratibu wa kufuatwa katika uvunjaji wa ndoa uwe tofauti kati ya jinsia hizi

mbili. Talaka ni moja ya haki zisizofanana (lakini zinazolingana) kati ya mwanaume na mwanamke.

Hii ndio nadharia inayowakilisha maoni ya Uislamu na nchi za Waislamu zinaifuata.

Talaka II

Katika zama zetu, talaka imekuwa tatizo la dunia kwani wote wanalinung'unikia na kulilalamikia. Wale ambao sheria zao zinazuia talaka kabisa wanalalamikia kutokuwepo kwa njia ya kuepuka ndoa zisizo na mafanikio. Halikadhalika wale walioruhusu talaka, wanaume na wanawake, wanalalamikia ongezeko la talaka na kuyumba kwa maisha ya familia na madhara yake. Wale waliotoa haki ya kutoa talaka kwa wanaume peke yao, wanaeleza kutoridhishwa kwao na mambo mawili.

Kwanza baadhi ya watu wa ovyo, baada ya miaka ya maisha ya ndoa, ghafla huwataliki wake zao wa zamani ambao wameishi nao katika kipindi bora kabisa cha ujana wao (hao wanawake) kwa sababu tu sasa wanatamani kuwa na mke mpya.

Pili baadhi ya watu wakorofi wanakataa kuwataliki wake zao, na ilhali hakuna uwezekano wowote wa kufikia maelewano na kuendelea na maisha ya ndoa pamoja.

Mara nyingi hutokea kuwa, kwa sababu mbali mbali tofauti kati ya mume na mke hufikia hatua ambayo hakuna uwezekano wowote wa usuluhishi, na kiuhalisia wanatengana. Katika hali hiyo, njia pekee ya maana ni kuvunja uhusiano wao kisheria, uhusiano ambao kiuhalisia tayari umeshavunjika na kumruhusu kila mmoja wao kutafuta mwenzi mpya maishani. Lakini baadhi ya wanaume ili kuwatesa wake zao na kuwanyima haki ya kufurahia unyumba, hukataa kuwataliki wake zao. Wanamuacha mwanamke, kwa mujibu wa Qur'ani, katika hali ya kuning'inia (talaka ya kuangika). Watu hawa wako mbali kabisa na mafundisho ya Uislamu, ingawa wanatumia mamlaka ya sheria ya Kiislamu kwa tabia yao isiyofaa. Mwenendo wao huwapa maoni wale wasiojua Uislamu vyema kuwa hivi ndivyo Uislamu unavyotaka talaka iwe.

Wakosoaji wanauliza kwa kejeli kuwa iwapo ni kweli kwamba Uislamu umeruhusu wanaume kuwatesa wake zao kadri wapendavyo wakati fulani wanawapa talaka na wakati fulani wanaibatilisha na bado wakati huo huo wanajiridhisha mioyoni mwao kuwa wametumia haki yao halali na ya kisheria.

Wakosoaji wanasema kuwa kitendo hiki ni mfano mzuri wa dhuluma na ukatili. Wanauliza: "Kama ni kweli, kama Waislamu wanavyodai kuwa sheria za Kiislamu zimeundwa kwa kuzingatia msingi wa haki na uongofu, je ni hatua gani ambazo Uislamu umechukua kuzuia aina hii ya dhulma?"

Juu ya ukatili na dhulma ya matendo hayo, hakuna shaka yeyote kuwa ni matendo yasiyofaa. Uislamu, kama tutakavyoonyesha hapa, umezingatia hali hii na una njia za kukabiliana na tatizo hili. Swali

muhimu ni: ipi njia bora ya kuzuia dhulma na ukatili huu? Je vitendo vya dhulma vinatokana na ubovu wa sheria ya talaka? Au sababu zake zitafutwe sehemu nyingine? Je matendo haya yanaweza kukomeshwa kwa kurekebisha sheria au hatua nyinginezo zinapaswa kuchukuliwa?

Uislamu una njia zake za kutatua matatizo ya kijamii. Baadhi wanafikiri kuwa yanaweza kutatuliwa kwa imma kuunda sheria mpya au kurekebisha zilizopo. Lakini Uislamu unaelewa kuwa sheria ina mipaka yake. Inaweza kufaa tu katika mahusiano makavu ya kimikataba. Lakini katika mahusiano ya hisia za moyo (kama mapenzi), sheria peke yake haiwezi kufanya mambo mengi, na lazima tuangalie hatua nyingine pia.

Kama tutakavyoonyesha baadaye Uislamu unaitumia vyema nguvu ya sheria pale tu ambapo kweli sheria inaweza kufanya kazi. Haujashindwa katika hili.

Talaka Za Aibu/Za Kuumbua.

Kwanza tuliangalie tatizo la talaka za kuumbua na kuaibisha katika zama hizi.

Kimsingi, Uislamu unapinga kabisa talaka. Unataka talaka isiwepo. Umeiruhusu talaka kama njia ya mwisho ambapo kutengana hakuepukiki. Wale wanaoowa wake wapya kila mara na kuwaacha wa zamani, Uislamu unawakana na umewaita kuwa ni maadui wa Mwenyezi Mungu.

Kitabu maarufu cha hadithi, *alKafi*, kinasimulia kisa kifuatacho;
Mtukufu Mtume alimuuliza mtu mmoja; “Umemfanya nini mke wako?” Akasema “Nimemtaliki,’ Mtume akamuuliza; “Je ulimuona anafanya jambo lolote baya?” “hapana sikuona.” Mwanaume yule alioa tena. Mtume akamuliza, ‘Je umeoa mke mwingine?” “Ndio”

Baada ya muda fulani Mtume akamuuliza tena, “Umemfanya nini mke wako?” Nimemtaliki” Je amefanya kosa lolote?” “Hapana” Mtu yule alioa mara ya tatu. Mtume akamuliza tena kama alikuwa ameoa mke mpya. Akajibu ndio, Baada ya muda fulani Mtume akamuuliza tena, “Umemfanya nini mke wako?”

“Nimemtaliki” “Je amefanya kosa lolote?” “Hapana”.

Mtume akasema kuwa Mwenyezi Mungu hampendi na anamchukia mtu ambaye hubadilisha wake kila mara, na wanawake wanaobadilisha waume kila mara. Watu hao ni maadui wa Mwenyezi Mungu.

Iliripotiwa kwa Mtume kuwa Abu Ayub Ansari alikuwa ameamua kumtaliki mke wake. Mtume alikuwa akimjua mwanamke huyo vizuri. Alijua pia kuwa uamuzi wa Abu Ayub haukuwa na sababu za maana.

Mtume akasema, “Kumtaliki Umme Ayub (mke wa Abu Ayub) ni dhambi kubwa.”

Mtume alisema kuwa Jibril alimuusia mno juu ya kuwatendea wema wanawake mpaka akahisi kuwa hairuhusiwi kumtaliki mwanamke isipokuwa kama amezini.

Imam Ja'far Sadiq (a.s) amesema kuwa Mtukufu Mtume (s.a.w.w) amesema; "Hakuna kitu kinachopendeza kwa Mwenyezi Mungu kama nyumba ambayo ndani yake ndoa inafungwa na hakuna jambo linalochukiza mbele ya Allah kama nyumba ambayo ndani yake talaka inatolewa."

Imam Ja'afar Sadiq (a.s) pia amesema kuwa neno 'Talaka' limetajwa tena na tena katika Qur'ani na maelezo yake ya kina yametolewa kwa sababu Allah anachukia kutengana kwa wanandoa.

AlTabarisi katika kitabu chake "*Makarim alAkhlaq*" amemnukuu Mtume akisema: "Oeni lakini msitoe talaka kwani talaka huitikisa Arshi ya Mwenyezi Mungu".

Hadithi kama hizi pia zimo katika vitabu vya Kisunni. Abu Daud katika kitabu chake, *Sunan* amesimulia kwamba Mtume amesema: "Mwenyezi Mungu hajaruhusu jambo lolote lenye kuchukiza kama talaka." Kwa maneno mengine, ingawa Allah ameruhusu talaka, bado talaka ndilo jambo analolichukia mno.

Viongozi wakubwa wa kidini (Maimamu) walikuwa wakijiepusha mno kutoa talaka kwa kadri inavyowezekana. Katika maisha yao matukio ya talaka yalikuwa na sababu za msingi sana. Kwa mfano, Imam Baqir (a.s) alimuona mwanamke. Alikuwa akimpenda sana mke huyo, lakini wakati fulani aligundua kuwa mwanamke huyu alikuwa na chuki na uadui mkubwa dhidi ya Imam Ali ibn Abi Talib. Ilimbidi amtaliki.

Alipoulizwa kwa nini alimtaliki na ilhali alikuwa akimpenda sana, Imam alisema kuwa hakutaka kuishi na kaa la moto wa Jahanamu pembeni yake.

Uvumi Usio Na Msingi.

Inafaa kuelezea hapa uvumi usio na msingi uliotungwa na makhalifa wa ukoo wa Abbas. Uvumi huu ulienea mno kiasi cha kuweza kurekodiwa na waandishi mashuhuri katika vitabu vyao. Kwa mujibu wa uvumi huo, Imam Hassan Mujtaba (a.s), mtoto wa Imam Ali ibn Abi Talib (a.s) ni mmoja wa wale waliooa wake wengi na kuwataliki. Uvumi huo ulienezwa karne moja baada ya kufariki kwa Imam. Uvumi huu ulienezwa mno kiasi cha kuwa hata wafuasi wake waliuamini bila kuzingatia ukweli kuwa kitendo hicho cha kuchukiza sio stahili ya Imam Mtukufu na kisingetarajiwa kwake, mtu aliyekuwa akienda Hija kwa miguu, na aligawa nusu ya mali yake kwa maskini zaidi ya mara ishirini.

Kama tunavyojua, tofauti na watoto wa kizazi cha Imam Husayn (a.s) ambao waliongozwa wakati ule na Imam Sadiq (a.s.) watoto wa kizazi cha Imam Hassan (a.s) walishirikiana na Bani Abbas wakati wa kuuangusha utawala wa kiukoo wa Bani Umayya. Awali Bani Abbas walielezea imani na utii wao kwa watoto wa kizazi cha Imam Hassan (a.s), lakini walipofanikiwa kupata madaraka waliwasaliti na wengi wao waliwatenga, ama kwa kuwaua au kwa kuwafunga gerezani.

Katika kuendeleza sera yao hii, Bani Abbas walianzisha kampeni za propaganda dhidi ya kizazi cha Imam Hassan (a.s). Moja ya hila walizozifanya ilikuwa ni kumshutumu babu yake na Imam Hassan ambaye pia ni ami yake na Mtukufu Mtume, Abu Talib (a.s), kuwa hakupata kusilimu na alikufa kafiri.

Walitaka kujenga hoja kuwa wao kwa vile ni kizazi cha ami mwingine wa Mtume, aliyekuwa amesilimu, wanastahili zaidi kuwa makhalifa. Ili kufikia lengo lao walitumia fedha nyingi sana na walibuni visa vingi vya uongo.

Idadi kubwa ya Masunni ambao walishawishika na propaganda hizi, bado wanaamini kuwa Abu Talib alikuwa kafiri. Ingawa utafiti wa hivi karibuni kabisa uliofanywa na wanazuoni wa Kissuni umebainisha ukweli wa jambo hili kwa kiasi kikubwa, lakini hata hivyo bado baadhi yao wanatia shaka.

Uzushi mwingine uliozushwa na Bani Abbas, ulikuwa kwamba Imam Hassan (a.s) alirithi ukhalifa baada ya baba yake, lakini kwa vile alikuwa mtu muasherati, hakuweza kutawala vizuri na akalazimika kuusalimisha ukhalifa kwa adui yake makini, Muawiya ambaye alimpatia fedha na kwa kutumia fedha hizo Imam Hassan alijishughulisha na kuoa na kutoa talaka.

Kwa bahati nzuri, utafiti wa wanazuoni wa zama zetu umekiweka wazi chanzo cha uzushi huu. Mtu wa kwanza kutamka uzushi huu alikuwa ni Kadhi (Qazi) aliyeteuliwa na khalifa Mansur aliyemwelekeza kubuni na kusambaza uzushi dhidi ya Imam. Mwanahistoria mmoja, alipokuwa akitoa maoni yake dhidi ya uongo huu, anahoji kuwa ikiwa Imam Hassan (a.s) alioa wanawake wengi kiasi hicho mbona watoto wake hatuwaoni? Kwa nini idadi ya watoto wake ni ndogo? na ilhali tunajua kuwa Imam hakuwa tasa na njia za kuzuia mimba au kutoa mimba hazikuwa mila ya zama hizo?

Tunashangaa wepesi wa kuamini wa baadhi ya wakusanyaji wa hadithi za Kishia. Wanaweza vipi kuandika kuwa Imam Hassan (a.s) alikuwa na tabia ya kutaliki wanawake, wakati wao wenyewe wanaripoti kuwa Mtukufu Mtume na Maimamu wamesema kuwa Allah anaichukua talaka na anamkana mwanaume ambaye ana tabia ya kuwataliki wake zake. Kamwe haikutokea kwa mabwana hawa kuchagua moja katika haya mambo matatu; (i) Talaka si kitu kibaya, (ii) Imam Hassan (a.s) hakuwa na ada ya kuwataliki wakeze au (iii) Imam Hassan (a.s) hakuambatana na mafundisho ya Uislamu. Lakini cha ajabu ni kuwa si tu wanaamini juu ya usahihi wa hadithi inayosema talaka inachukiza mbele ya Allah, lakini pia wakati huo huo, licha ya kuwa wafuasi waaminifu kwa Imam, wananukuu ripoti kuwa, Imam alikuwa na tabia ya kuwataliki wanawake mara kwa mara. Wanaziruka ripoti hizi bila kuzitolea maelezo.

Baadhi ya wanahadith (Muhadithina) wamekwenda mbali zaidi kiasi cha kusimulia kwamba Imam Ali (a.s) hakuwa akifurahia tabia ya mtoto wake. Katika hotuba yake ya hadhara aliwaomba watu wasimuozeshe binti zao kwa vile alikuwa na tabia ya kuwataliki. Lakini inasemekana kuwa watu walijibu kuwa lilikuwa ni jambo la fahari kwao kwamba binti zao walipata kuwa wake za mtoto (mjukuu) wa Mtume hata kwa muda mfupi.

Inaelekea kuwa baadhi ya watu walikuwa na fikra kuwa talaka si jambo baya ikiwa mwanamke mwenyewe na familia yake walikuwa radhi. Wanafikiri kuwa talaka inachukiza tu iwapo upande wa pili haikuridhia, lakini hakuna tatizo kabisa kama mwanamke ameridhia kuishi na mwanaume anayejifaharisha naye kwa siku chache.

Hata hivyo huu sio uhalisia. Ridhaa ya mwanamke au wazazi wake haibatilishi ubaya wa talaka. Talaka inachukiza kwa vile Uislamu unataka ndoa idumu na familia iwe imara. Ridhaa ya wanandoa pia haibadilishi ubaya wa talaka. Uislamu hauioni talaka kuwa inachukiza kwa baadhi tu ya tabaka la wanawake. Ni suala la kanuni.

Tumelijadili suala hili la Imam Hassan (a.s) si tu kwa nia ya kuurudia uongo wa kihistoria dhidi ya mtu mwenye umuhimu wa kihistoria, lakini pia kuwaonya wale watu waovu ambao wanaweza kujiingiza kwenye vitendo vya namna hii na kuhalalisha tabia yao hii kwa kutumia mfano wa Imam Hassan (a.s) kama kiigizo chao.

Hapana shaka yoyote kuwa talaka ni jambo lenye kuchukiza sana katika Uislamu.

Kwa Nini Uislamu Haukuharamisha Talaka?

Hapa maswali kadhaa yanaibuka. Kama talaka haipendezi na inachukiwa kiasai hicho na Allah, kwa nini haikuharamishwa moja kwa moja na Uislamu? Uislamu ungekuwa angalau umeweka masharti ya kuthibitisha usahihi wa talaka (yaani yawepo mambo ambayo hayo yakifanywa yatachukuliwa kuwa ni sababu tosha ya kutoa talaka). Katika hali hiyo mtu yeyote ambaye angetaka kumtaliki mke wake angelazimika kisheria kueleza sababu zake za msingi mbele ya mahakama ya sheria za kutaka kutoa talaka.

Swali la pili ni kuwa; “Sentensi hii ina maana gani?: Katika vitu vyote vilivyoruhusiwa, talaka ndio kitu kinachochukiwa zaidi kwa Mwenyezi Mungu.” Kama inaruhusiwa haiwezi kuchukiza na kama inachukiza haiwezi kuruhusiwa. Kuruhusiwa na kuchukiza ni maneno mawili yanayokinzana.

Mwisho, je idara ya mahakama inayoiwakilisha jamii, ina haki ya kuingilia suala la talaka kiasi cha kuweza kuibatilisha? Au kuweza kusikiliza mashauri mpaka idhihirike kuwa usuluhishi hauwezekani na hivyo hakuna namna isipokuwa kuvunja ndoa?

Talaka – III

Tumesema kwamba kwa mtazamo wa Uislamu, talaka ni jambo linalochukiza. Uislamu unataka ndoa iwe imara na idumu. Tuliibua swali kuwa ikiwa talaka inachukiza, kwa nini Uislamu haujaipiga marufuku? Je Uislamu haukupiga marufuku vitendo vyote vinavyochukiza kama vile kunywa pombe, kucheza kamari, ukatili n.k? Kama jibu ni ndiyo, sasa kwa nini Uslamu haujaiharamisha kabisa talaka kisheria? Kimsingi inapingana na mantiki kusema kuwa talaka inaruhusiwa na wakati huo huo inachukiza. Kama inaruhusiwa, vipi inaweza kuchukiza? Kama inachukiza vipi inaweza kuruhusiwa? Uislamu kwa upande mmoja unamkunjia uso mtu anayemtaliki mke wake na wakati huo huo haumuwekei kikwazo cha

kisheria (cha kutoa talaka), kwa nini?

Ni swali la busara sana, na ni ufunguo wa siri zote za tatizo la talaka. Kwa kusema kweli, ndoa ni uhusiano wa asili na sio uhusiano wa kimkataba. Maumbile yameweka sheria maalum kwa ajili yake. Mikataba mingine ya kijamii kama vile ya mauzo, ya ajira, rehani ya amana, ya uwakili n.k. Si lolote zaidi ya makubaliano ya kijamii. Hayana mkono wa maumbile na silika. Sheria ya maumbile haiingilii mikataba hii. Lakini kinyume chake, mkataba wa ndoa una utaratibu maalum. Umeundwa na matamanio ya asili ya pande mbili.

Kwa hiyo, haishangazi kuona kuwa mkataba wa ndoa una kanuni zake maalum ambazo ni tofauti na zile za mikataba mingine yote.

Sheria Za Maumbile Katika Ndoa Na Talaka.

Katika jamii ya kiraia, sheria za asili pekee ni sheria ya uhuru na usawa, sheria ambayo juu yake hujengwa sheria nyingine zote za kijamii. Lakini katika mkataba wa ndoa, mbali na kanuni za jumla za uhuru na usawa, maumbile yametoa sheria nyingine pia, ambazo lazima zizingatiwe katika suala la ndoa, mahari, matunzo na mwisho talaka. Hakuna faida yoyote kuyapuuza maumbile. Kama Alexis Carrel alivyoonyesha, sheria za kibaiolojia na sheria nyingine za maisha (asili) ni ngumu, katili na zisizozuiliwa kama sheria za kinajimu.

Ndoa maana yake ni kuambatana na ni muungano, na talaka maana yake ni kutengana.

Maumbile yamesanifu sheria ya maumbile katika namna ambayo mwanaume hutenda mambo kwa nia ya kumpata mwanamke, na mwanamke hujiondoa (hukataa kataa) kwa nia ya kumvutia na kumpotosha mwanaume. Mwanaume hutaka kuumiliki mwili wa mwanamke na mwanamke hutaka kuuteka moyo wa mwanaume. Msingi wa ndoa umejengwa juu ya upendo, muungano na kuhurumiana na ushirikiano na uswahiba peke yake. Katika jengo la familia, jinsia ya kike huchukua nafasi muhimu na jinsia ya kiume huchukua nafasi ya pembeni. Kutokana na yote haya ni dhahiri kuwa maumbile lazima yatakuwa yameweka kanuni maalumu kwa ajili ya uvunjaji wa maisha ya familia pia.

Hapo awali tulimnukuu msomi mmoja akisema kuwa kutafuta mwenzi maana yake ni kushambulia (kwa upande wa mwanaume) na kuteka nyara na kujifaragua kwa mwanamke kwa nia ya kumpendeza na kumdanganya. Kwa mwanaume ambaye yeye kwa asili ni kama mnyama mwindaji, vitendo vyake ni vya kichokozi na kwake mwanamke ni medali ambayo lazima aipate. Kutafuta mwenzi ni mapambano na ndoa ni kunyakua na kumiliki.

Mkataba ambao umejengwa juu ya upendo na hisia za umoja hauwezi ukashinikizwa kwa nguvu. Sheria inaweza kuwalazimisha watu wawili kuuheshimu mkataba wao kwa msingi wa kushirikiana na usawa lakini haiwezi kuwalazimisha kupendana, kuwa waaminifu kila mmoja kwa mwenzake, kila mmoja kujitolea kwa ajili ya mwenzake na kila mmoja kushiriki furaha za mwenzake.

Kama tunataka kudumisha uhusiano huu kati ya watu wawili, tunapaswa kutumia mbinu na njia nyingine tofauti na sheria.

Kwa mujibu wa mpangilio wa asili wa ndoa, ambao juu yake ndio sheria za Kiislamu zimejengwa, mke hushika nafasi ya mtu anayestahiki upendo na heshima katika familia. Ikiwa kwa sababu fulani fulani atapoteza nafasi hii na akanyimwa upendo na mapenzi ya mume wake, msingi wa jengo la familia huanguka chini na utaratibu wa asili huparanganyika.

Uislamu huiangalia hali hii kwa huzuni, lakini Uislamu hauwezi kuendelea kufikiri kuwa ndoa bado iko hai hata baada ya kusambaratika kwa msingi wake wa asili.

Uislamu umechukua hatua maalum ili kuhakikisha kuwa maisha ya familia yanabaki katika hali yake ya asili, yaani mke atabaki katika hali ya kupendwa na kuhitajika, na mume abaki na hisia za kumpenda mkewe na awe tayari kumhudumia.

Uislamu umemhimiza mwanamke ajipambe na kujiremba sana ili kumridhisha mume wake, kuonyesha utimilifu wake kwa ajili ya mumewe, kumkidhia matamanio yake ya asili na kuepuka kumkera kwa ujeuri na kiburi. Pia umemhimiza mwanaume kumpenda mke wake, kuwa mpole kwake na kushikamana naye na asiufiche upendo wake kwa mkewe. Hatua hizi zimechukuliwa ili kuifanya furaha ya ngono ibakie katika wigo wa familia na kuifanya jamii ya nje ya familia kujishughulisha na kazi na shughuli nyingine badala ya ngono (yaani ngono iwe nyumbani tu, nje ya nyumbani iwe ni sehemu ya kazi na shughuli nyingine).

Uislamu unataka mahusiano ya jimai (ngono) yawe masafi na yasiyo na uchafu. Hatua zote hizi zimechukuliwa kwa nia ya kuifanya taasisi ya familia iepukane na hatari ya kuvunjika na kusambaratika.

Nafasi Ya Asili Ya Mwanaume Katika Maisha Ya Familia.

Kwa mtazamo wa Uislamu, ni matusi kabisa kwa mwanamke kwamba sheria imlazimishe kuishi na mwanaume asiyempenda. Sheria inaweza kumlazimisha mwanamke kuishi na mwanaume fulani lakini haiwezi kumhakikishia kuwa atapata nafasi muhimu kabisa katika familia, nafasi ambayo anastahili. Sheria inaweza kumlazimisha mwanaume kumhudumia mke wake lakini haiwezi kumlazimisha kuwa mume anayejali.

Hivyo, upendo wa mwanaume unapopoa, ndoa hupoteza mwelekeo kwa mtazamo wa maumbile.

Hapa swali jingine linaibuka. Je, upendo wa mwanamke ukipoa, maisha ya familia yataathirika? Je maisha ya ndoa yataendelea kama yalivyo au yatafikia kikomo. Kama yatabaki salama, sasa inakuwaje kwamba ukosefu wa upendo kwa upande wa mume huvunja ndoa lakini ukosefu wa upendo kwa upande wa mke hauvunji ndoa?

Je, kuna tofauti yeyote kati ya mwanaume na mwanamke? Kama ukosefu wa upendo kwa upande wa

mke vile vile huvunja ndoa, basi ni dhahiri kuwa wanawake pia wanapaswa kuwa na haki ya kutoa talaka kama mwanaume.

Kwa kusema kweli, mafanikio ya maisha ya familia hutegemea maelewano na masikilizano ya wote wawili, mume na mke. Lakini kama tulivyosema hapo awali kuna tofauti ya tabia ya akili (*mentality*) ya mwanaume na ile ya mwanamke. Huko nyuma tumeshanukuu maoni ya wanasayansi juu ya hili. Maumbile yamepanga kuwa mapenzi ya kweli na ya dhati ya mwanamke huja tu kama mwitikio wa upendo wa dhati wa mwanaume. Hivyo mapenzi ya mwanamke kwa mwanaume ni matokeo ya upendo wa dhati wa mwanaume.

Maumbile yamemkabidhi mwanaume funguo za udhibiti wa mapenzi na maelewano yao. Ikiwa mwanaume anampenda mwanamke na ni mwaminifu kwake basi mwanamke pia humpenda na kubaki mwaminifu kwake, kwa kusema kweli uaminifu wa mwanamke ni mwitikio wa uaminifu wa mwanaume.

Maumbile yameweka funguo za kuvunja ndoa mikononi mwa mwanaume. Ni kutojali kwa mwanaume na kutokuwa kwake mwaminifu kunakopoozesha mapenzi ya mwanamke. Kwa upande mwingine, kutojali na kupuuzia kwa mwanamke hakumwathiri mwanaume lakini kinyume chake sio kweli.

Mwanaume kupoteza upendo ni mwisho wa ndoa, lakini kwa mwanamke sio hivyo. Ikiwa mwanaume anajali na ni mwaminifu, mara zote anaweza kurejesha upendo wa mke wake kwa kumuonyesha upendo, upole na kujali. Sio matusi kwa mwanaume kumlazimisha kipenzi chake kwa msaada wa nguvu ya sheria, kuendelea kuishi naye, na kumshawishi polepole. Lakini si jambo linalovumilika kwa mke kutumia nguvu ya sheria ili kumrejesha mlinzi na kipenzi chake.

Mambo huwa hivi inapokuwa kutojali kwa mwanamke hakutokani na ukosefu wa maadili na ukatili wa mwanaume. Hawezi kuruhusiwa kutumia vibaya nafasi yake kumtesa au kumtendea vibaya mke wake. Tutaijadili nukta hii baadaye.

Ilivyo, mwanaume anahitaji mwili wa mwanamke na mwanamke anauhitaji moyo wa mwanaume. Hiyo ndio tofauti kati ya hawa wawili. Ndoa huwa haina maana kwa mwanamke kama hapati ulinzi na mapenzi ya dhati ya mume wake.

Maoni Ya Mwanasaikolojia Wa Kike.

Hivi karibuni makala moja ilichapishwa na mwanamama mmoja mwanasaikolojia wa Kifaransa, Beatrice Maryo, ambaye ana shahada ya udaktari na anafanya kazi kama daktari wa akili katika hospitali ya Paris. Yeye mwenyewe ni mama wa watoto watatu.

Katika makala hii ameelezea vizuri sana ni jinsi gani mwanamke mwenye mimba au anayenyonyesha anavyohitaji upole na upendo wa mume wake. Anasema kwamba; “Kuanzia wakati mwanamke anapoanza kuhisi kuwa muda si mrefu atakuwa mama, huanza kuutafiti mwili wake. Huutazama kila mara na kuunusa, hasa inapokuwa ni mtoto wake wa kwanza. Huhisi udadisi mwingi juu yake

mwenyewe kana kwamba yeye ni mgeni wa mwili wake na hutaka kujijua (kujigundua) kwa mara ya kwanza.

Anapohisi kutembea kwa mtoto kidogo katika tumbo lake, huanza kusikilizia kwa uangalifu kila sauti ya mwili wake. Kuwepo kwa mtu mwingine katika mwili wake humfanya asikie furaha sana kiasi cha kutaka kujitenga na kupumzika. Hutaka abaki peke yake na kitoto chake kidogo, ambacho bado hakijaja katika ulimwengu huu.

“Wanaume, katika kipindi cha ujauzito wa wake zao, wana majukumu muhimu ya kufanya, lakini kwa bahati mbaya sana, mara nyingi huyakwepa majukumu haya. Mama mtarajiwa huhitaji kuhisi kuwa mume wake anamwelewa, anampenda, na anamlinda. Vinginevyo, anapoona tumbo lake limevimba, kuvutia kwake kumetoweka, homa za asubuhi zimeanza, na anaogopa uchungu wa uzazi, atamlaumu mume wake, aliyempa mimba na kumsababishia matatizo na taabu zote. Ni jukumu la mume kujiweka karibu zaidi na mke wake mara nyingi zaidi kuliko kipindi kingine chochote katika miezi yake ya ujauzito. Familia yote inahitaji baba mpole na anayejali ambaye mke na watoto watamweleza matatizo yao, huzuni zao na furaha zao. Hata kama maongezi yao sio ya maana bado ni muhimu baba kuyasikiliza.

“Mwanamke mjamzito hutaka sana watu wote wamuongelee mtoto wake. Mwanamke huona fahari kuwa mama. Lakini anapoona mume wake hamjali mtoto, hisia yake ya fahari hubadilika na kuwa hisia ya dharau. Huchukia kuwa mama na kuwa mjamzito, na huwa ni aina ya udhalilishaji kwake. Inafahamika kuwa akina mama hawa hupata uchungu mkubwa wakati wa kujifungua... Uhusiano kati ya mama na mtoto sio wa pande mbili. Ni uhusiano wa pande tatu; mama, mtoto na baba. Hata kama baba hayupo (ikiwa wamepeana talaka), bado ana jukumu muhimu katika maisha ya ndani ya mama yaani fikra na hisia zake pamoja na hisia ya umama (*motherhood*)...”

Haya ndiyo aliyoyasema mwanasaikolojia wa kike ambaye pia ni mama.

Jengo Lililojengwa Juu Ya Msingi Wa Hisia Za Moyoni.

Mwanamke hutegemea sana uaminifu, upole na ulinzi wa mume wake kiasi kwamba bila ya kuwepo ushirikiano wake wa dhati, basi hata mtoto mwanamke huyu huwa hamjali sana. Anaweza kuvumilia ugumu wa maisha kwa msaada wake tu (mumewe). Katika hali hii inawezekanaje kumlazimisha, kwa kutumia nguvu ya sheria kubaki ameshikamana na mwanaume ambaye hamtaki?

Je, sio kejeli kwamba kwa upande mmoja tunajenga mazingira ambayo kwayo wanaume wanawajali wake zao kidogo tu na wanamalizia ujana wao sehemu nyingine na kwa upande mwingine tunawatupa wake zao juu yao kwa nguvu ya sheria? Ukweli ni kuwa, Uislamu unataka mwanaume mwenyewe amtafute mwanamke, na ampende. Uislamu hautaki kumtupia mwanamke (yaani kumpatia mwanamke asiyempenda).

Ni kanuni ya jumla kuwa palipo na suala la mapenzi, kujitolea na uaminifu, hapawezi kuwa na

kulazimishana kwa nguvu ya sheria. Ikiwa mume hampendi mke wake, linaweza kuwa ni jambo la kusikitisha lakini hakuna nguvu inayoweza kumfanya ampende.

Hebu tutoe mfano mmoja. Kama tunavyojua, katika sala za jamaa kuna sharti kwamba kiongozi wa sala anaweza kuwa yule tu ambaye ni mchamungu na ambaye wafuasi wake wana imani juu ya uchamungu wake. Katika hali hii uhusiano kati ya kiongozi na wafuasi wake umejengwa juu ya uchamungu wa kiongozi na imani waliyonayo wafuasi wake juu yake. Ikiwa wafuasi wake watapoteza imani juu yake iwe kwa haki au kwa makosa, uhusiano huu huharibika. Sheria haiwezi kutumika kuurejesha.

Kwa vile ni suala la hisia za moyoni, hakuna yeyote anayeweza kulazimishwa kisheria kuwa na imani na mtu fulani. Hata kama kiongozi wa sala ana kiwango cha juu kabisa cha uchamungu na wema, hawezi kuwalazimisha wengine kusali nyuma yake. Itakuwa ni kichekesho sana kufungua kesi mahakamani kwa sababu watu fulani au wote hawakusali nyuma yake. Inaweza hata kuwa ni matusi kwa nafasi ya kiongozi wa sala kujaribu kuwalazimisha watu kusali nyuma yake.

Hali ni hivyo hivyo katika suala la uhusiano kati ya wapiga kura na mgombea katika uchaguzi. Watu watampigia kura mgombea yule tu ambaye wana imani naye. Wasipomchagua mgombea fulani, hata awe na sifa na anafaa kiasi gani, hawezi kuwashitaki wapiga kura.

Kitu pekee kinachoweza kufanyika katika hali hizi ni kuwaelimisha watu juu ya vigezo sahihi na kukuza kiwango chao cha uelewa ili watakapokuwa wakitekeleza jukumu lao la kidini, wampate mtu muongofu kabisa wa kumfuata na wanapotekeleza jukumu lao la kijamii wampigie kura mtu anayestahiki. Lakini ikitokea, kwa sababu yoyote iwayo, watu wakabadilisha maoni yao, linaweza kuwa ni jambo la kusikitisha tu, lakini hakuwezi kuwa na suala la kulazimishana au kuwachukulia hatua za kisheria wapiga kura.

Jukumu la kifamilia ni sawa kabisa na majukumu ya kidini na kijamii tuliyoyataja hapo juu, Uislamu huiona familia kuwa ni jamii ya asili ambayo imewekewa taratibu maalum ambazo zinapaswa kufuatwa kwa ukamilifu ili iweze kwenda vizuri.

Ni mafanikio makubwa sana kwa Uislamu kwa kuweza kuuweka utaratibu huu, kwani nchi za Magharibi bado hazijaweza kutatua matatizo yake ya kifamilia. Sio hivyo tu, bali kila siku matatizo yanazidi kuongezeka na kila siku matatizo mapya yanazidi kuongezeka juu ya matatizo ya zamani. Kwa bahati nzuri, kutokana na uchunguzi wa kisayansi, mambo yanazidi kuwa wazi pole pole. Tunashawishika kwa asilimia zote kuwa ulimwengu wa Kimagharibi pole pole utazikubali kanuni na mafundisho ya Kiislamu juu ya sheria za familia. Hata hivyo hatuamini kuwa mafundisho halisi ya Uislamu yanafanana kabisa na yale yanayofuatwa na kutekelezwa leo hii. (na waislamu – yaani mafundisho hayatekelezwi vilivyo)

Kinachoimarisha Jengo La Familia Ni Zaidi Ya Usawa.

Ulimwengu wa Kimagharibi wa leo umeleweshwa na neno usawa bila kujua kuwa suala la uhusiano kati

ya mwanaume na mwanamke lilitatuliwa na Uislamu karne 14 zilizopita. Katika suala la mfumo wa familia, kuna kitu kikubwa zaidi kuliko usawa. Kwa jamii ya kiraia, maumbile yameweka sheria ya usawa tu, lakini kwa jamii ya kifamilia maumbile yameweka sheria nyingine pia. Mahusiano ya kifamilia hayawezi kuongozwa kwa msingi wa usawa peke yake. Sheria nyingine zote za maumbile zinazoyaongoza mahusiano haya, lazima zitambuliwe na zifuatwe.

Usawa Katika Ufisadi

Kwa bahati mbaya neno 'usawa' limetumika sana na mara nyingi mno kiasi cha kuwa maana yake halisi imeshaharibika. Ni mara chache kutokea kwa yeyote kuwa neno usawa linapotumika humaanisha usawa wa haki. Kanuni ya usawa haiwezi kutumika kila sehemu bila kubagua. Inaweza kuwa dhihaka kubwa kusema kuwa kila kitu kimekuwa sawa kwa sababu huko nyuma ni wanaume tu waliowadanganya wake zao.

Je, tunaweza kufurahia na kutangaza kuwa sasa usawa umefikiwa kwa sababu huko nyuma ni 10% ya ndoa zilizokuwa zikiishia kwenye talaka na kutengana, na sasa katika baadhi ya sehemu za dunia, 40% ya ndoa zinaishia kwenye talaka, na katika 50% (nusu) ya talaka hizi zilianzishwa (ziliombwa) na wanawake? Zamani ni wanaume waliowasaliti wake zao kwa kujiingiza katika zinaa na wake zao walikuwa waaminifu sana kwa waume zao, lakini sasa hata wanawake nao wanawasaliti waume zao na hawazingatii tena usafi wa kimaadili (hawajiepushi na zinaa).

Je haya ni maendeleo? Je tunaweza kusema kuwa huu ni usawa? Zamani mara nyingi wanaume waliuonyesha ukatili na ugumu (wa hisia) kwa wake zao. Waliwatelekeza wake zao na watoto na kuwakimbilia vimada. Sasa hata akina mama wenye watoto wengi, baada ya kuwa wameolewa miaka mingi huko nyuma, wanazitelekeleza nyumba zao na kwenda kukidhi tamaa zao, kufuatia utambulisho mfupi aliopewa kwa mtu asiyejua katika hafla ya dansi. Je, hii inamaanisha kuimarika kwa usawa?

Hivyo ndivyo ambavyo badala ya kutibu maradhi ya kijamii na kuimarisha maisha ya kifamilia (ndoa), tunadhoofisha mfumo wa familia na kuitikisa misingi yake. Lakini vilevile, tunafurahia kuwa sasa usawa unazidi kuboreka. Kama hali hii itaendelea muda si mrefu mwanamke atamzidi mwanaume kwa ufisadi, upotofu na ugumu wa moyo.

Sasa ni dhahiri kuwa kwa nini Uislamu, licha ya kuichukia talaka, haujaiharamisha moja kwa moja. Ni dhahiri kuwa ni vipi kitu kinaweza kuruhusiwa na bado kikawa kinachukiza sana.

Talaka – IV

Ni dhahiri kutokana na majadiliano tuliyoyafanya kuwa Uislamu unachukia talaka na kuvunja maisha ya

ndoa. Umechukua kila hatua ya kimaadili na kijamii ili kuiokoa ndoa kutokana na hatari ya kuvunjika, lakini haukutumia mbinu ya kulazimisha wala nguvu ya sheria. Uislamu unapinga matumizi ya nguvu ya sheria ili kumzuia mwanaume asimtaliki mkewe na kumlazimisha mwanamke kuendelea kuishi na mume wake. Uislamu unaona kuwa hatua hizi haziafikiani na nafasi ya mwanamke katika familia, kwani hisia za moyoni na mihemko ndio nguzo za maisha ya familia.

Ni mwanamke anayepokea fukuto la hisia za upendo wa mume wake na yeye hulipeleka kwa watoto wake. Ikiwa mwanaume atapoteza upendo wake kwa mke wake, mazingira ya nyumbani huwa baridi na ovyo ovyo. Hata hisia za kimama kwa watoto wake hutegemea kwa kiasi kikubwa upendo wa mumewe. Kwa mujibu wa mwanasaikolojia mashuhuri, hisia za kimama sio silika kwa maana kwamba haiwi kuwa hisia hizi haziongezeki au kupungua. Upendo na kujali anakokuonyesha mwanaume kwa mkewe kuna athari kubwa kwenye hisia zake za kimama.

Kwa kifupi, mwanamke huhamasishwa na kuchochewa na hisia za ndani na upendo wa mumewe katika kuzisafirisha hisia zake kwa wanawe.

Mwanaume anaweza kulinganishwa na mlima, mwanamke kama mto na watoto kama mimea. Mto lazima upokee maji kutoka milimani ili uyafyonze na kuyatoa katika hali ya maji yanayotoa uhai kwa ajili ya umwagiliaji wa mimea na maua. Mvua isiponyesha mlimani au yakinyong'onyea ardhini, mto utakauka na mimea itanyauka.

Kama ilivyo kuwa ni muhimu kwa rutuba ya ardhi na kwa kustawi kwa mimea, hisia za ndani na upendo wa mwanaume kwa mke wake ni muhimu sana kwa maisha ya ustawi, mafanikio na furaha ya watoto na mama yao.

Inapokuwa hisia za moyoni na upendo wa mume ni muhimu kiasi hicho kwa mafanikio ya maisha ya familia, ni vipi sheria inaweza kutumika kama silaha dhidi yake?

Uislamu unapinga vitendo vya aibu na udhalilishaji vinavyofanywa na baadhi ya wale wanaowataliki wake zao wa zamani na kuoa wapya. Lakini kwa maoni ya Uislamu, sio dawa kumlazimisha mwanaume aliyepoteza mapenzi kuendelea kuishi na mkewe dhidi ya matakwa na utashi wake. Kitendo hicho hakiendani na sheria ya maumbile ya maisha ya familia.

Ikiwa mwanamke atajaribu kurudi katika nyumba ya mumewe kwa nguvu ya sheria na kwa msaada wa mamlaka za kiutawala, nafasi yake katika nyumba itakuwa sawa na utawala wa kijeshi. Katika hali hii hataweza kuwa malikia wa nyumba, wala hawezi kuwa kiunganishi cha hisia kati ya mume wake na watoto wake. Pia hataweza kukidhi hitajio lake la upendo na kutazamwa vyema.

Uislamu umechukua hatua ili kuondoa kesi za talaka, lakini Uislamu ukiwa kama mtunga sheria, hautaki kumlazimisha mwanamke ambaye ni kitovu cha mfumo wa familia, kuishi na mwanaume mkorofi asiyemtaka (yaani mwanaume asiyemtaka mwanamke huyo).

Hatua iliyochukuliwa na Uislamu ni kinyume cha kilichofanywa na kinachofanywa na ulimwengu wa Magharibi. Uislamu unapiga vita mambo yote yanayosababisha hali ya kutokuwa na uaminifu na uasherati lakini hauko tayari kumlazimisha mwanamke kuishi na mume asiyekuwa mwaminifu. Lakini kinyume chake ulimwengu wa Kimagharibi unapalilia mambo yanayosababisha kutokuwepo kwa uaminifu, na wakati huo huo unataka kumlazimisha mwanamke kuendela kuishi na mume asiyekuwa mwaminifu na mwasherati.

Uislamu umetumia rasilimali zake zote ili kutunza uhai wa roho ya ubinadamu na uchangamfu na ingawa haumlazimishi mwanaume asiye mchangamfu kwa mkewe kuendelea kuishi na mke wake, kiuhalisia umefanikiwa sana kupunguza kesi za talaka zinazotokana na kutochangamkiana. Wengine hawazingatii nukta hizi na wanataka furaha kwa nguvu na katika ncha ya sindano na hivyo hawajafanikiwa.

Mbali na kesi za talaka zinazotokea katika nchi za Magharibi kwa madai ya wanawake kwa sababu ya kutoshabihiana (*incompatibility*) na kama ilivyoelezwa na gazeti la *Newsweek*, kupenda starehe, idadi ya matukio ya talaka kwa sababu ya uasherati wa mwanaume ni kubwa mno kuliko idadi ya matukio kama hayo katika nchi za Mashariki (Asia).

Asili Ya Amani Ya Familia Ni Tofauti Na Zile Aina Nyingine Za Amani.

Hapana shaka yoyote kuwa inapaswa pawepo amani na maeleweno kati ya mume na mke, lakini amani na maelewano yanayopaswa kuwepo katika maisha ya ndoa ni tofauti sana na amani inayopaswa kuwepo kati ya marafiki wawili, wenzi wawili, majirani wawili na nchi mbili majirani.

Amani na maelewano katika maisha ya ndoa ni sawa na amani na maelewano yanayopaswa kuwepo kati ya wazazi na watoto. Yanahusisha uvumilivu, kujitolea, kujali maslahi ya mwenzako, kuvunja ukuta wa uwili (hivyo kuwa mwili mmoja) na kushiriki katika furaha na huzuni ya mwenzi wake. Lakini kinyume chake, amani na maelewano kati ya marafiki wawili, wenzi wawili, majirani wawili au nchi mbili majirani ina maana kutoingilia haki za mwenzako katika nchi mbili zinazogombana, hata amani iliyopatikana kwa mtutu inatosha. Hata dola ya tatu ikiingilia na kuweka kizuizi ili kuzuia mashambulizi ya moja kwa moja kati ya nchi hizi mbili, amani itakuwa tayari imepatikana, kwa amani ya kisiasa inamaanisha kutokuwepo vitendo vya uchokozi na migongano (kuparuana).

Lakini amani ya familia ni tofauti na amani ya kisiasa. Hapa kutoingilia haki za mwenzako hakutoshi. Amani ya mtutu wa bunduki haifai chochote. Kinachotakiwa ni muungano wa roho, jambo ambalo ni la juu zaidi na la msingi zaidi. Mambo yako hivyo hivyo katika amani na maelewano kati ya wazazi na watoto. Hapa pia panahitajika kitu kikubwa zaidi kuliko kutokuwepo kwa uchokozi peke yake. Kwa bahati mbaya, kwa sababu za kihistoria na wakati fulani za kimkoa, nchi za Magharibi hazitambui umuhimu wa hisia za moyoni. Wao hawaoni tofauti yoyote kati ya amani ya familia na amani ya kisasa au amani ya kijamii.

Watu wa Magharibi wanafikiri kuwa kwa vile amani kati ya nchi mbili inaweza kufikiwa kwa kurundika majeshi ya dola ya tatu katika mpaka wa nchi hizi mbili, halikadhalika amani kati ya mume na mke inaweza kuimarishwa kwa kuweka nguvu ya kisheria (kimahakama) katika mpaka wa maisha yao. Wanasahau kuwa mafanikio ya maisha ya familia hutegemea kutoweka au kuondolewa kwa mipaka yote (baina yao).

Watu wa Mashariki wenye akili za Kimagharibi, badala ya kujivunia mfumo wao na kuwaonyesha watu wa Magharibi ubovu na mapungufu ya mfumo wa Kimagharibi, wamebobea katika kuiga kibubusa kiasi cha kushindwa kutofautisha kati ya wema na uovu. Lakini muda si mrefu nchi za Mashariki zitaondokana kabisa na minyororo ya magharibi, zitaigundua haiba (Shaksia) yao na zitajifunza kujitegemea. Hapa ni muhimu kutaja nukta mbili.

Uislamu Unakaribisha Jambo Lolote Litakaloondosha Hatari Ya Talaka.

Kutokana na tulivyoyaandika baadhi ya watu wanaweza kwa makosa kuhitimsiha kuwa tunaunga mkono wazo la wanaume kuwataliki wake zao kwa ridhaa zao na kwa raha zao. Kwa hakika hivi sivyo. Tunachomaanisha ni kuwa Uislamu hautaki kutumia nguvu ya sheria dhidi ya mume. Uislamu unakaribisha jambo lolote litakalofanikiwa kumshawishi mume kuachana na wazo la kutoa talaka, na zaidi ya hayo talaka sio sahihi mpaka itamkwe mbele ya watu wawili waadilifu, ambao wanatarajiwa kutumia jitihada zao zote kuwapatanisha wanandoa.

Mila ya sasa ambayo mara nyingi talaka inatolewa mbele ya watu wawili waadilifu, ambao hata hawafahamu wanandoa zaidi ya kuyajua majina yao, sio ya Kiislamu kabisa.

Ulazima wa kuwepo mashahidi wawili wajuzi ni moja ya mambo yanayoweza kumshawishi mume kuachana na mpango wa kutoa talaka, ikiwa sharti hili litazingatiwa kikamilifu kwa maana iliyokusudiwa. Uislamu hauchukulii kuwepo kwa mashahidi wawili kuwa ni jambo la lazima wakati wa ndoa (ili ndoa isihi), ambayo ni mwanzo wa mkataba wa ndoa, kwa sababu hautaki kuchelewesha amali njema. Lakini unaona kuwa ni sharti la lazima kuwepo kwa mashahidi wawili waadilifu na wajuzi ili talaka iweze kusihi (kuwa sahihi), jambo ambalo ni mwisho wa mkataba wa ndoa.

Halikadhalika kwa mujibu wa Uislamu talaka sio sahihi (valid) kama itatolewa wakati mwanamke yupo hedhini ingawa hakuna kikwazo cha kufunga ndoa katika kipindi hicho. Ilivyo hedhi kwa vile ni kikwazo cha kufanyika tendo la ndoa, ilipaswa kuwa ni kikwazo cha ufungaji wa ndoa sio talaka. Lakini kwa vile Uislamu unahimiza usalama wa ndoa na unakataza utengano, umeruhusu ndoa ifungwe hata kama mwanamke yupo hedhini na umekataza talaka katika kipindi hicho. Katika baadhi ya hali, ni lazima kusubiri kwa miezi mitatu kabla ya talaka kuruhusiwa kutolewa.

Vikwazo vyote hivi vinakusudiwa kutoa muda wa kutosha wa kuruhusu hasira, iliyosababisha uamuzi wa kutoa talaka, ipoe na kuwawezesha mume na mke kurejea maisha yao ya kawaida.

Aidha, katika talaka rejea mume anaruhusiwa kumrejea mke wake ndani ya kipindi cha eda.

Uislamu umemuwekea mwanaume kikwazo kingine kwa kumtaka azikabili gharama za ndoa pamoja na matunzo ya mke na watoto katika kipindi chote cha eda. Ikiwa mwanaume anataka kumtaliki mke wake na kumuoa mwanamke mwingine, kwanza anapaswa kulipa gharama za matunzo ya mke wa kwanza, na kubeba gharama ya matunzo ya watoto na kulipa mahari ya mke mpya. Na pia anapaswa kubeba jukumu la matunzo ya mke wa pili pamoja na watoto atakaomzalia.

Mbali na jukumu la kuwalea watoto, majaaliwa yao yenye mashaka humhofisha na kumzuia mume kuchukua uamuzi wa kutoa talaka.

Pamoja na yote haya, Uislamu unaona kuwa ni lazima pindi ndoa inapovunjika mahakama ya familia yenye wasuluhishi wawili, mmoja kutoka upande wa mume na mwingine upande wa mke, hupaswa kuwasuluhisha wanandoa.

Wasuluhishi wanapaswa kufanya kila liwezekanalo kusuluhisha ugomvi baina ya mume na mke na ikibidi wanaweza kuwataka ushauri wanandoa ili kufikia lengo hili. Wanaweza tu kuvunja ndoa ikiwa wataona kuwa usuluhishi hauwezekani kabisa. Ikiwa kuna uwezekanao, wasuluhishi wanapaswa kuwa ni ndugu wa wanandoa, ikiwa upo uwezekano wa kupatikana watu wenye ujuzi miongoni mwa ndugu zao.

Qur'ani Tukufu inasema:

وَإِنْ خِفْتُمْ شِقَاقَ بَيْنِهِمَا فَابْعَثُوا حَكَمًا مِنْ أَهْلِهِ وَحَكَمًا مِنْ أَهْلِهَا إِنْ يُرِيدَا
إِصْلَاحًا يُوَفِّقِ اللَّهُ بَيْنَهُمَا ۗ إِنَّ اللَّهَ كَانَ عَلِيمًا خَبِيرًا {35}

"Ikiwa mna hofu ya kuvunjika kwa ndoa baina yenu wawili (mke na mume), chagueni msuluhishi mmoja kutoka kwa mume na mwingine kutoka kwa mke. Ikiwa wote wanataka mapatano, Mwenyezi Mungu atawawezesha. Kwa hakika Mwenyezi Mungu ni Mjuzi wa yote, Mwenye habari." (***Suratul Nisa, 4:35***).

Mwandishi wa Kashshaf, neno '**msuluhishi**' anasema kuwa ni mtu anayechaguliwa kusuluhisha anayepaswa kuwa mwaminifu, fasaha na mwenye uwezo wa kuleta maelewano na kuzitendea haki pande mbili. Anasema pia kuwa inafaa zaidi kuteuwa msuluhishi kutoka miongoni mwa ndugu zao kwa vile wanatarajiwa kujua sababu za mgogoro vizuri zaidi na pande zote zinaweza kuzungumza nao kwa uhuru zaidi na wanaweza kuwa na imani nao zaidi.

Mafakihi wanatofautiana juu ya suala la usuluhishi, iwapo usuluhishi ni wajibu au unapendekezwa tu. Wazo lililo mashuhuri zaidi ni kuwa ni jukumu la serikali kuteuwa wasuluhishi. Shaheed Thani, katika kitabu chake, *'Masalik'* ametoa rasmi rai ya kisheria kuwa usuluhishi ni wajibu na unapaswa kuratibiwa

na serikali.

Sayyid Muhammad Rashid Riza, mwandishi wa Tafsiri ya Qur'ani, *AlManar*, baada ya kutoa rai kuwa usuluhishi ni wajibu, anazungumzia khitilafu ya maoni ya mafakihi (wajuzi wa sheria za Kiislamu) juu ya suala hili na anasema kuwa, kivitendo, Waislamu hawafuati kanuni hii ya busara na hivyo wanakosa fursa ya kufaidika na faida zake nyingi. Wanavyuoni wanapoteza nguvu zao katika kubishana tu, wakati hakuna anayechukua hatua kuitekeleza. Kama kanuni haitekelezwi, kuna tofauti gani ikiwa kanuni hiyo ni wajibu au inapendekezwa tu?

Juu ya sharti ambalo wasuluhishi wanaweza kumuwekea mume ili kufanikisha usuluhishi, Shahid Thani anasema kuwa wanaweza kwa mfano, kumlazimisha mume kumweka mke wake katika mji fulani au nyumba fulani na asimuweke mama yake au mke wake mwingine katika nyumba hiyo hata kama ni kwenye chumba tofauti; kulipa malipo yote ya mahari aliyopangiwa wakati wa ndoa kwa mkupuo na kulipa mkopo wote kwa mkupuo mmoja kwa mke wake.

Kwa kifupi, hatua yoyote inayofaa kumshawihsi mume kuachana na mpango wa kutoa talaka inafaa na inakaribishwa.

Hili ni jibu kwa swali tulililoliibua awali kuwa mahakama inayoiwakilisha jamii ina haki ya kuingilia kati na kuzuia kuvunjika kwa ndoa au haina.

Mahakama inaweza kuingilia kati kwa sababu uamuzi wa mume wa kumtaliki mke si mara zote unakuwa ni dalili ya kuvunjika kabisa kwa ndoa. Anaweza kutoa uamuzi huo kwa sababu ya hasira au hali ya kutoelewana. Hatua yoyote itakayochukuliwa na jamii kuzuia utekelezaji wa uamuzi huo inakaribishwa na Uislamu.

Mahakama ya usuluhishi, ikiwa ni mwakilishi wa jamii, inaweza kuziamuru ofisi zinazohusika na utoaji wa talaka kutohitimisha kesi ya madai ya talaka, mpaka mahakama iwahakikishie kuwa imeshindwa kuwapatanisha na kuleta amani na maelewano kati ya mume na mke.

Huduma Alizotoa Mke Katika Familia

Talaka, mbali na kuvunja maisha matakatifu ya familia, husababisha matatizo mengine makubwa kwa mke, matatizo ambayo hayawezi kupuuzwa. Jaalia mke ameishi katika nyumba na mumewe kwa miaka, ameichukulia nyumba kuwa ni yake na kwa dhati na uaminifu mkubwa, anafanya bidii kubwa kuijenga na kuitengeneza. Anapunguza bajeti ya chakula na mavazi, ukiachilia mbali wanawake wa mijini (ambao hawafanyi hivi), kiasi cha kumkera hata mumewe (kwa jinsi anavyobana matumizi), na anasita hata kuajiri msaidizi wa kumsaidia kazi za ndani. Anajitolea ujana wake, nguvu zake, afya yake kwa ajili ya mumewe na nyumba yake. Sasa mume wa mke huyu, baada ya miaka ya kuishi pamoja, anataka kumtaliki mke mwingine, sio tu kuwa anataka kuziharibu jitihada zote za mke wake, bali pia anataka kujiingiza katika raha za mapenzi kwa kutumia maumivu ya mke wake (anayemuacha).

Huku sio kuvunjika tu kwa ndoa, na haiwezi ikadaiwa kuwa, kwa asili ni jambo la aibu kwa staha ya mwanamke kung'ang'ania kwa mwanaume huyu ambaye hampendi.

Hapa maswala mengine pia huibuka – suala la kutokuwa na nyumba kwa mke, suala la kuikabidhi nyumba yake kwa hasimu wake na suala la kupoteza jitihada zake zote na huduma alizozitoa huko nyuma katika nyumba yake.

Kila mwanadamu anataka kuwa na nyumba yake na huhisi kushikamana na nyumba aliyoijenga kwa mikono yake mwenyewe hasa. Ukijaribu kumfukuza ndege katika kiota alichokijenga, bila shaka atakataa na kujilinda. Kwa maoni yetu, tatizo hili linastahili kujadiliwa kwa umakini. Katika hali hizo, talaka inakuwa sio kuvunjika kwa ndoa peke yake, bali huwa ni kuangamia kabisa kwa mwanamke.

Hata hivyo, suala la nyumba ni tofauti na lile la talaka, na haya masuala mawili yanapaswa kujadiliwa tofauti tofauti. Kwa mtazamo wa Uislamu, tatizo hili halipaswi kutokea. Linatokea kutokana na kutojua kanuni za Kiislamu na taratibu zake na wanaume kuzitumia vibaya dhamira njema za wake zao.

Watu walio wengi wanadhani kuwa matunda yote ya jasho la mwanamke ni mali ya mume wake. Wanafikia hata kufikiri kuwa mume ana haki ya kumlazimisha mke wake kumfanyia kazi na kwamba anapaswa kutii amri zote kama mtumwa. Fikra hii potofu ndio chanzo cha matatizo yote. Kama tulivyosema mwanamke ana uhuru kamili kuhusiana na kazi na shughuli. Chochote anachopata huwa ni mali yake peke yake. Uislamu umempa uhuru wa kiuchumi. Na bado umemuwajibisha mume kubeba gharama zote za mke na watoto wake.

Hivyo Uislamu umempa mwanamke fursa nyingi za kujipatia fedha za kumwezesha kuishi maisha ya heshima na yasiomtegemea mwanaume (baada ya kuachika). Talaka na kutengana hakukupaswa kumhofisha kwa upande wa uchumi. Vitu vyote ambavyo anaweza kuwa amekusanya ili kuijenga nyumba yake ni mali yake na mume wake hana haki ya kuvichukua. Mwanaume kuvichukua vitu hivyo kunaweza tu kuhalalishwa na mifumo ambayo inamlazimisha kufanya kazi katika nyumba ya mumewe. Masaibu yanayowapata watu wetu huenda yanasababishwa na kutojua kwao sheria.

Sababu nyingine ya tatizo hili ni tabia ya baadhi ya wanaume kuunyonya uaminifu wa wake zao. Baadhi ya wanawake wanajitolea sio kwa sababu hawaielewi sheria ya Kiislamu, bali kwa sababu wanawaamini waume zao kupita kiasi. Hawataki kuitumia fursa waliyopewa na Uislamu. Ghafla huzinduka usingizini na kukuta kwamba wamepoteza maisha yao kwa kujitolea kwa mwanaume asiyekuwa mwaminifu na wamepoteza fursa waliyopewa na dini yao.

Ikiwa mke atasamehe haki yake ya kisheria ya kujiwekea akaunti yake tofauti ya fedha na mapato mengine, mume pia anatarajiwa kwamba, kwa kuzingatia kujitolea na huduma alizotoa mke wake atatoa zawadi na hidaya kwa mkewe. Qur'ani inasema;

وَإِذَا حُيِّيتُمْ بِتَحِيَّةٍ فَحَيُّوا بِأَحْسَنَ مِنْهَا أَوْ رُدُّوهَا ۗ

“Mnaposalimiwa kwa salamu, itikieni kwa salamu iliyo bora kuliko hiyo au angalau kama hiyo.’ (*Suratul Nisa, 4:86*).

Imekuwa ni mila ya watu wema kumpa mke zawadi za vitu vya thamani kama vile nyumba au mali nyingine kama hidaya.

Hata hivyo, tunachomaanisha ni kuwa suala la kutokuwa na nyumba(makazi) halihusiani na talaka na haliwezi kutatuliwa kwa kurekebisha sheria. Tatizo hili linahusiana na suala la uhuru wa kiuchumi wa mwanamke na tatizo hilo tayari limeshatatuliwa na Uislamu. Tatizo hili limeibuka kutokana na ujinga (kutojua) wa baadhi ya wanawake na wengine kwa sababu ya kuwaamini mno waume zao, tatizo hili litamalizika kabisa ikiwa wanawake watayajua mafundisho ya Uislamu juu ya jambo hili na kuacha kuwaamini mno waume zao.

Talaka V

Tumeshasema hapo awali kuwa kuna hali mbili za talaka zinazosababisha matatizo yote. Mojawapo ni kuwa kuna baadhi ya kesi za talaka ambazo zinatokana na tabia ya kutokuwa mwaminifu na kutochangamka kwa upande wa wanaume. Nyingine ni kuwa, hata kunapokuwa hakuna uwezekano wa kufikia maelewano kati ya mume na mke, baadhi ya wanaume hukataa kutoa talaka sio kwa nia ya kutaka kuendelea kuishi naye bali kwa nia ya kumnyanyasa.

Tumeshaeleza hapo awali kuwa Uislamu unakaribisha jambo lolote litakalozuia talaka za aibu (udhalilishaji) na umechukua hatua kuliondosha kabisa tatizo hili. Hata hivyo Uislamu haukubaliani na matumizi ya nguvu kwa lengo la kudumisha mahusiano ya ndoa.

Uislamu unaiona familia kama taasisi yenye uhai na (Uislamu) unafanya jitihada kuifanya iendelee kuwa hai. Lakini ikifa, hukumu ya Uislamu ni kuwa inapaswa kuzikwa. Uislamu hautaki familia iliyotiwa mumiani na ibakie kuwa na uhai bandia.

Tumejifunza kwamba sababu ya kwa nini mwanaume ana haki ya kutoa talaka ni kuwa mahusiano ya kinyumba (ndoa) yamejengwa juu ya uhusiano wa asili ambao una kanuni zake. Maumbile yamezikabidhi funguo za uimarishaji wake au ubomoaji wake mikononi mwa mwanaume.

Mwanaume na mwanamke, kila mmoja, kwa asili ana nafasi yake, ambayo haiwezi kubadilishwa wala nafasi zao haziwezi kuunganishwa na kufanywa kuwa nafasi moja. Hizi nafasi maalumu za kila mmoja huibua haki na majukumu maalumu, haki ya talaka ikiwa ni mojawapo. Kwa maneno mengine haki hii inatokana na jukumu na mchango mahususi na maalumu ambao mwanaume na mwanamke kila mmoja huutoa katika kutafuta mwenzi katika maisha.

Haki Ya Kutoa Talaka

Haki ya kutoa talaka inatokana na jukumu la mwanaume na Sunan Ibn Majah kwa ajili ya haki au umiliki wa mke wake. Sasa unaweza kirahisi kupima thamani ya propaganda zinazoendeshwa na wanaoupinga Uislamu. Wanadai kuwa Uislamu umempa mwanaume haki ya talaka, kwa sababu hamtambui mwanamke kuwa ni mwenye utashi huru au kuwa ana matamanio au dhamira. Wanasema kuwa Uislamu unamuweka mwanamke katika kundi la vitu visivyo na uhai, umempatia mwanaume haki ya umiliki dhidi ya mwanamke. Kiasili haki hizo zinajumuisha haki ya ukombozi.

Tumeshaonyesha kuwa sheria ya familia ya Kiislamu haikujengwa juu ya umiliki (umwinyi) wa mwanaume na utwana wa mwanamke. Falsafa ya Uislamu ni ya kina na ya juu mno kuliko uwezo wa kiakili wa waandishi hawa. Kwa kupitia muongozo wa Mwenyezi Mungu, Uislamu unaelewa asili ya msingi na muundo wa mfumo wa familia. Hivi sasa sayansi inabainisha baadhi ya mambo ya ajabu yaliyotatuliwa na Uislamu karne 14 zilizopita.

Talaka Inatolewa Kwa Namna Maalum.

Wanaoupinga Uislamu wanasema kuwa talaka inapaswa kuwa na muundo wa kimahakama na sio wa kuachia huru au kutoa nafuu. Ukweli ni kwamba talaka ina kipengele cha kuachia huru kwa sababu ndoa ina kipengele cha kutwaa. Haiwezekani kubadilisha sheria ya kumtafuta mwenzi, ambayo imetoa majukumu ya kufanya kwa mwanaume na mwanamke katika mchakato huu (wa kutafuta mwenzi), na hali ya asili ya ndoa inafanana na kutwaa (kujinyakulia). Kuhusiana na uhusiano wa ngono (jimai), maumbile yameweka majukumu tofauti kwa mwanaume na mwanamke, kwa wanaadamu na wanyama. Talaka ingeweza kunyang'anywa kipengele chake cha kuachia huru kama tu ingewezekana kubadili sheria ya maumbile.

Mkosoaji mmoja anasema kuwa kwa ujumla mafakihi wa Kishia wanautafsiri mkataba wa ndoa kuwa ni wa kudumu, lakini inaonekana kuwa kwa mujibu wa sheria ya Kiislamu, ni wa kudumu kwa mke tu, kwani mume anaweza kuubatilisha muda wowote kwa utashi na raha zake. Anaongeza kuwa ni jambo la aibu kumpa mume haki ya kutoa talaka katika zama hizi za atom, miezi bandia na demokrasia.

Inaelekea kuwa bwana huyu na wengine, wenye fikra kama zake, hawatofautishi kati ya kubatilisha ndoa na talaka. Tunaposema kuwa mkataba wa ndoa ni mkataba wa kudumu, tuna maana kuwa si mume wala mke mwenye haki ya kuubatilisha. Ikiwa ndoa imebatilishwa (kama ambavyo huwa inatokea japo mara chache sana) huchukuliwa kana kwamba haikuwahi kufungwa na hakuna mtiririko wowote wa kisheria katika hilo.

Mwanamke hawezi kudai mahari yake. Mwanaume hana jukumu la kumtunza katika kipindi cha eda. Lakini kwa upande mwingine wa talaka, mkataba wa ndoa iliyofungwa kihalali huvunjwa, lakini athari zake za kisheria hazifutwi (hazibatilishwi) kabisa. Kwa mfano, ikiwa mwanaume atamtaliki mke wake baada ya kuishi naye hata kwa siku moja, anapaswa kulipa mahari yote na anawajibika kumtunza katika

kipindi chote cha eda.

Ikiwa atampa talaka mara tatu baada ya ndoa kufungwa lakini kabla ya kuingiliana naye, anapaswa kulipa nusu ya mahari na kumtunza mke wake.

Kwa vile hapa hakuna suala la eda hivyo hakuna suala la matunzo. Hivyo ni wazi kuwa talaka haibatilishi athari zote za kisheria za mkataba wa ndoa. Ni dhahiri pia kuwa talaka ni tofauti na kubatilisha ndoa na kwamba haki ya ndoa haipingani na ukweli kwamba mkataba wa ndoa ni wa kudumu. Kuna vipengele viwili vilivyo bainishwa katika Uislamu, ubatilisho wa ndoa na talaka. Ndoa inaweza kubatilika ikiwa kuna upungufu mkubwa wa kimwili uliogundulika ama kwa mume au mke, katika hili wote wana haki sawa ya kubatilisha ndoa. Talaka tu ndiyo haki ya mume peke yake.

Ukweli kwamba kuna kanuni tofauti kwa ajili ya talaka kwa upande mmoja na kanuni tofauti za ubatilisho wa ndoa kwa upande mwingine unaonyesha kuwa Uislamu haukumpa mwanaume haki ya kutoa talaka kwa sababu ulitaka kumpa upendeleo maalum.

Adhabu Kwa Mtu Anayetoa Talaka.

Kwa nia ya kuzuia talaka, baadhi ya mifumo ya sheria imeweka adhabu kwa mtu anayempa mkewe talaka. Hatuna hakika kama sheria kama hii bado ipo sehemu yoyote ile duniani kwa sasa. Hata hivyo, wanahistoria wanasema kuwa Wafalme wa Kikristo wa Urumi waliwatoza faini wale wote ambao waliwataliki wake zao bila sababu ya maana.

Ni wazi kuwa huu ni muundo mwingine wa matumizi ya nguvu katika kudumisha maisha ya ndoa, na hivyo haiwezi ikawa na manufaa (msaada) makubwa.

Kumpa Mke Haki Ya Kutoa Talaka.

Mpaka sasa tumejadili haki ya asili ya kutoa talaka ambayo ni ya mume peke yake. Lakini anaweza kumpa mke wake haki ya kutoa talaka. Utoaji huu wa mamlaka haya kwa mke unaweza kuwa wa jumla au unaoweza kutumika katika mazingira fulani. Ili kuhakikisha kuwa haibatilishwi huingizwa katika mkataba wa ndoa kama sharti la kudumu, ambapo kwa mujibu wa sharti hilo mke hupewa mamlaka fulani ambayo tayari watakuwa wameshakubaliana.

Imekuwa ni kawaida tokea zamani kwamba wanawake wanaohisi kwa namna yoyote kuwa na shaka na mwenendo wa waume zao huhimiza kuwekwa kwa sharti hili katika mikataba yao ya ndoa na hutumia mamlaka waliyopewa, pindi kukiwa na haja ya kufanya hivyo.

Hivyo, sio sawa kusema kuwa haki ya talaka ni haki ya mtu mmoja tu na kwamba Uislamu umempa haki hiyo mwanaume tu.

Talaka Ya Kimahakama.

Talaka ya kimahakama ina maana uvunjaji wa ndoa kwa mamlaka ya jaji na si kwa mamlaka ya mume. Katika nchi nyingi ni mahakama tu yenye mamlaka ya kutoa talaka na kuvunja ndoa. Kwa mujibu wa mfumo huu, kila talaka ni talaka ya kimahakama., Tumeshabainisha hapo awali kuwa ikiwa asili ya ndoa, lengo la kuundwa kwa familia na nafasi inayoshikiliwa na mwanamke katika familia, talaka ambayo hujiendesha itakavyo haiwezi kutegemea uamuzi wa jaji.

Sasa tungependa kuona ikiwa, kwa mtazamo wa Uislamu, jaji hana mamlaka ya kutoa talaka au ikiwa kuna hali zozote ambazo, zikiwa sio za kawaida jaji anaweza kufanya hivyo.

Talaka ni haki ya asili ya mume, ikiwa uhusiano wake na mke wake ulikuwa wa kawaida. Kwa kawaida, kama anataka kuishi na mke wake anapaswa kumjali, kumpatia haki zake zote anazostahili na kuishi naye kwa wema. Kama akiona kuwa hawezi kuishi naye kwa wema anapaswa kumlipa haki zake zote na kutengana (kuachana) naye. Mbali na kumlipa haki zake anapaswa kumlipa kiasi kingine cha fedha au mali cha ziada kama shukrani kwa wema wake. Qur'ani Tukufu inasema:

وَمَتِّعُوهُنَّ عَلَى الْمُوسِعِ قَدَرُهُ وَعَلَى الْمُقْتِرِ قَدَرُهُ مَتَاعًا بِالْمَعْرُوفِ ۚ

"...Wapatieni cha kuwaliwaza, mwenye wasaa kwa kadri ya uwezo wake, na maskini kwa kadiri ya uwezo wake, riziki nzuri." (*Suratul Baqara, 2:236*).

Lakini kunaweza kuwa na hali ambapo maisha ya ndoa hayaendi kama kawaida. Kunaweza kuwa na mwanaume ambaye hataki kuishi kwa wema na mkewe wala hataki kumpa talaka.

Talaka ya asili inaweza kufananishwa na mtoto anapozaliwa kwa njia ya kawaida. Lakini talaka ya mwanaume ambaye hayuko tayari kutekeleza wajibu wake na hataki kutoa talaka, kwa hiari yake ni kama uzazi usio wa kawaida ambao huhitaji upasuaji wa daktari.

Je, Baadhi Ya Kesi Za Ndoa Hazitibiki Kama Kansa?

Katika hali hizo talaka haitegemei ridhaa na mapenzi ya mume. Ikiwa mwanaume huyo hayuko tayari kutoa talaka, mwanamke hawezi kuachwa aendelee kuvumilia maumivu bila kupata dawa. Uislamu hauwi mtazamaji mkimya katika hali hizi.

Baadhi ya watu wana fikra potofu kuwa kwa mtazamo wa Uislamu hali hizi hazitibiki. Wanafikiri kuwa ni aina ya kansa inayowatesa watu wenye bahati mbaya lakini haiwezi kutibika na hivyo mwanamke hana namna isipokuwa kustahamili hadi atakapokufa.

Kwa maoni yetu fikra hii haikubaliki katika kanuni za Uislamu. Uislamu ni dini ambayo mara zote hutetea

uadilifu. Kujenga jamii adilifu imekuwa ni lengo kuu la Mitume wote. Qur'ani Tukufu inasema;

لَقَدْ أَرْسَلْنَا رُسُلَنَا بِالْبَيِّنَاتِ وَأَنْزَلْنَا مَعَهُمُ الْكِتَابَ وَالْمِيزَانَ لِيَقُومَ النَّاسُ بِالْقِسْطِ ۖ

"**Kwa hakika Tuliwapeleka Wajumbe Wetu na dalili zilizo wazi na Tuliwateremshia pamoja nao Kitabu na Mizani, ili wanaadamu wahukumiane kwa haki (usawa)." (57:25).**

Uislamu hauwezi kuvumilia uvunjaji wa maadili wa wazi namna hii, wala ukafikiriwa kuwa utatoa sheria itakayotoa suluhisho linalofananishwa na kansa.

Inasikitisha kwamba baadhi ya watu ambao wanakiri kuwa Uislamu ni dini ya uadilifu, bado wanashikilia mtazamo huu. Ikiwa 'sheria moja nyeusi' itapachikwa kwenye Uislamu na ikakubaliwa kuwa ni kansa, hakuwezi kuwa na kizuizi cha maana cha kuzuia sheria nyingine 'za kikatili' kuitwa tetenasi, kifua kikuu, polio n.k.

Madai haya ni kinyume cha kanuni ya uadilifu ambayo ndio msingi mkuu wa sheria za Kiislamu.

Aidha, kama inawezekana kuondoa kansa kwa upasuaji mdogo. Je haitakuwa busara kuharakisha tiba na kumpa mgonjwa nafuu?

Hebu chukua mfano wa mwanamke anayekwenda kwa mwanaume kwa moyo na nia safi akijua ni mwenzi wake maishani, lakini ghafla mwanaume huyo anapoteza mapenzi naye. Ikiwa mwanaume atatumia vibaya madaraka yake, hampi talaka wala hataki kukaa naye kwa wema, kwa maneno ya Qur'ani anamning'iniza, sio kwa sababu anataka kuishi naye kama mkewe bali kwa nia ya kumzuia asitafute mume mwingine anayefaa, mwanamke huyu kwa hakika anataabishwa na kansa. Lakini kansa hii inaweza kuponyeshwa kirahisi kwa upasuaji, na baada ya upasuaji mgonjwa anatarajiwa kupona kabisa. Upasuaji huu unaweza kufanywa na jaji mwenye ujuzi tu.

Kama ilivyoelezwa awali, ni tatizo kubwa la jamii yetu kwamba baadhi ya waume wasio na huruma hukataa kutoa talaka na hivyo kufanya dhulma kubwa. Wanatumia dini kuhalalishia mienendo yao isiyokubalika kabisa. Wanaposema kuwa mwanamke avumilie kwa subira ukatili wao kama kansa isiyotibika kwa hakika wanalichafua jina la Uislamu.

Ingawa somo hili ni la kiufundi, hata hivyo tunataka kulijadili kwa kifupi ili kuondoa shaka ya watu waovu na kufafanua mafundisho ya Uislamu juu ya hili.

Kushindwa Kabisa Kufikia Maafikiano.

Baadhi ya hali za kushindwa kufikia maafikiano sio za kipekee kwenye masuala ya ndoa na talaka. Hutokea pia katika maeneo mengine pia, kama vile yanayohusiana na matatizo ya kifedha. Sasa hebu tuangalie jinsi Uislamu ulivyoshughulikia mikwamo katika maeneo haya. Je umeiondoa mikwamo hii au umeikubali kama hali zisizotibika?

Jaalia watu wawili, kwa kupitia mirathi au njia nyingine wanatokea kumiliki mali isiyogawanyika kama vile almasi, pete au gari na hawako tayari kutumia mali hiyo pamoja au kwa zamu. Pia kila mmoja wao hayuko tayari kuuza sehemu yake kwa huyu mwenzake. Pia hawakubaliani juu ya namna nyingine ya kuitumia mali hiyo. Mali hiyo inakaa bila kutumiwa, kwa sababu ni dhahiri hakuna yeyote kati yao anayeweza kuitumia bila idhini ya mwenzake. Nini kifanyike katika hali hiyo. Je tatizo hilo libakie hivyo bila kutatuliwa na mali ibaki bila kutumiwa? Je Uislamu umetafuta suluhisho la utata huu?

Ukweli ni kuwa Uislamu hauchukulii suala hili kuwa lisiloweza kutanzuliwa. Haukiri kuwa haki ya kumiliki inaweza kuzuia kutumiwa kwa mali yoyote. Unaziruhusu mahakama za sheria kuingilia kati na kuyaweka mambo sawa. Hata kama pande zinazohusika hazitaki suala hilo liamuliwe, bado mahakama inaweza kuamuru mali hiyo ikodishwe au iuzwe. Mapato yatakayopatikana yatagawiwa baina ya wamiliki, lakini mahakama inaweza kuchukua hatua kwa idhini au bila idhini yao.

Katika hali hizo, haki ya umiliki haizingatiwi kwa sababu ya kuhusika kwa kanuni nyingine, kanuni ya kuzuia kitu kukaa bila kutumika. Haki ya umiliki inapaswa kupuuzwa katika hali hii, kwa sababu inapaswa kuheshimiwa tu ikiwa haitasababisha hasara kabisa au kitu kukaa bila kutumiwa.

Jaalia watu wawili wanaolimiki almasi, jambia au kitu kinginecho. Hakuna aliye tayari kumuuzia mwenzake sehemu yake (gawio lake la mali) lakini wote wawili wanakubaliana kuikata na kila mtu kupata kipande (nusu). Ni wazi kuwa almasi, jambia au gari likikatwa vipande viwili huwa haiwezi kutumika tena na hupoteza thamani yake. Uislamu hauruhusu uharibifu huo.

Fakihi (mjuzi wa sheria za Kiislamu) mkubwa, Allamah Hilli, anasema kuwa mamlaka za kisheria hazipaswi kumruhusu yeyote kuchukua uamuzi kama huu. Ukweli kwamba wamiliki wa mali hiyo wamekubaliana juu ya uamuzi huu, hautazingatiwa wala kuheshimiwa katika hali hizi.

Mkingamo Wa Talaka.

Sasa hebu tuangalie nini kinapaswa kufanywa juu ya suala la talaka. Ikiwa mume hataki maelewano na hatekelezi majukumu yake yote au baadhi ya kifedha (matunzo), kimaadili kuishi naye kwa wema na jimai (ngono) kama ilivyoamrishwa na Uislamu na wakati huo huo hayuko tayari kumtaliki mkewe, je ni hatua gani ichukuliwe? Je kuna sababu inayotosheleza hapa kuiruhusu mamlaka ya kisheria kuingilia kati?

Maoni Ya Ayatullah Hilli.

Fakihi mkubwa wa zama hizi, Ayatullah Sheikh Husein Hilli wa Najaf Iraq, amelijadili suala hili katika tashifu (makala) yake iitwayo 'Haki za unyumba'. Huu hapa ni mukhtasari wa maoni yake:

"Ndoa ni mkataba mtakatifu na wakati huo huo ni aina fulani ya ushirika (ubia) kati ya watu wawili ambao kila mmoja anawajibika kwa mwenzake, na ambao utekelezaji wa majukumu hayo huwasababishia furaha. Huu sio mwisho. Kwa kweli, mafanikio na furaha ya jamii nzima hutegemea mafanikio ya uhusiano wao.

Haki kuu za mke ni matunzo, unyumba na kuishi naye kwa wema. Ikiwa mume ataacha kutekeleza majukumu yake na pia atakataa kumtaliki mke wake, je mwanamke afanye nini na amwelekee vipi mume wake? Hapa kuna njia mbili. Aidha mamlaka ya kisheria ya kiislamu iingilie kati na kuitangaza ndoa kuwa imevunjika au mke naye akatae kutekeleza majukumu yake.

Njia ya kwanza inaungwa mkono na Aya hizi za Qur'ani.

الطَّلَاقُ مَرَّتَانِ ۖ فَإِمْسَاكٌ بِمَعْرُوفٍ أَوْ تَسْرِيحٌ بِإِحْسَانٍ

"Talaka inaweza kutolewa mara mbili; kisha mwanamke arejeshwe na kukaa naye kwa wema au aachiliwe aende kwa wema (*Suratul Baqarah, 2:229*).

Kwa maneno mengine, haki ya talaka na kutanguliwa kwake ni mara mbili tu. Baada ya hapo kuna njia mbili tu zinazobaki, ama kukaa na mke kwa wema au kumwacha kwa wema.

Katika *Suratul Baqarah* tena (2:232), Qur'ani inasema:

وَإِذَا طَلَّقْتُمُ النِّسَاءَ فَبَلَغْنَ أَجَلَهُنَّ فَلَا تَعْضُلُوهُنَّ أَنْ يَنْكِحْنَ أَزْوَاجَهُنَّ إِذَا تَرَاضَوْا بَيْنَهُمْ بِالْمَعْرُوفِ

"Mnapokuwa mmewataliki wake zenu, na wamemaliza eda zao, ama kaeni (warejeeni) nao kwa wema au waacheni kwa wema. Msiwashikilie kwa nguvu ili muwatese, hamuwarejei wala hamuwaachi.

Kutokana na Aya hizi, tunaweza kupata kanuni ya jumla. Mume anapaswa ama kumrejea mke wake na kutekeleza majukumu yake kikamilifu au kumwacha na kukata uhusiano wa unyumba.

Kwa mtazamo wa Uislamu, hakuna njia ya tatu. Maneno 'Msiwang'ang'anie kwa nguvu ili muwatese'

yanakataa njia (suluhisho) ya tatu mbali na kuwarejea na kukaa nao kwa wema au kuwaacha kwa wema. Kwa maana ya kijumla zaidi, maneno haya yanajumlisha hali zote, kumtesa mwanamke kwa makusudi na kupuuzia haki na maslahi yake kwa kukataa kumtaliki.

Aya hizi zinaeleza wazi wazi suala la kubatilisha talaka na zinaweka wazi kuwa ubatilishaji wa talaka unapaswa kufanywa kwa nia njema ya kutaka kuendelea kuishi na mwanamke kwa wema kama mwenzi maishani na sio kwa nia ya kumtesa. Lakini kwa upana wake, Aya hizi hazizungumzi suala hili tu. Zinaweka kanuni ya jumla kutumika katika haki za mke wakati wote na katika hali zote. Kama kanuni ya jumla, mume anapaswa kuchagua moja kati ya njia mbili katika maisha yake yote ya ndoa. Hakuna njia ya tatu.

Baadhi ya mafakihi, kwa makosa wamezibana Aya hizi. Wana maoni kuwa zinawahusu wale waume tu wanaotaka kuzibatilisha talaka zao katika kipindi cha eda. Kwa kusema kweli mtazamo huu sio sahihi. Mbali na muktadha wa Aya hizi, Maimamu wa Ahlul Bait ambao maoni yao ni hukumu moja kwa moja, wamezitumia Aya hizi katika hali nyingine pia. Kwa mfano Imam Baqir (as.) amesema kuwa mume anayeapa kuwa hamtaki mke wake na kwa kufuatana na kiapo hicho akajitenga naye, ana njia mbili tu za kufanya baada ya kipindi cha miezi mine kuisha. Ama avunje kiapo chake na kutoa kafara kwa tabia yake isiyofaa au mara moja amtaliki mkewe, kwani Mwenyezi Mungu anasema;

فَإِمْسَاكٌ بِمَعْرُوفٍ أَوْ تَسْرِيحٌ بِإِحْسَانٍ

“Ama mrejeshe na kukaa naye kwa wema au muache kwa wema (*Suratul Baqara 2:229*).

Katika tukio jingine ambapo mtu mmoja alikuwa amemteuwa mtu mwingine kupanga mahari na kufunga naye ndoa kwa niaba yake, lakini baadaye alikana kuwa hakuagiza hivyo, Imam Sadiq (a.s) alisema kuwa mwanamke angejichagulia mume mwingine. Mwanaume huyo atakapojua kuwa alikuwa amemteuwa mtu na kumpa madaraka ya kupanga mahari na kufunga ndoa kwa niaba yake lakini baadaye akakana, basi ni lazima atoe talaka ili moyo wake (dhamira) uwe safi, kwa kuwa Allah amesema; **“Ama kaa na mwanamke kwa wema au muache kwa wema”** Mifano hii inaonyesha kuwa Maimamu waliamini kuwa Aya hii ilikuwa ni kanuni ya jumla.

Na iwapo mume hatekelezi jukumu lake la unyumba wala hamtaki mke wake, mahakama ya kidini inapaswa kumwita na kumtaka atoe talaka. Akikataa, mahakama yenyewe inaweza kutangaza kuwa ndoa imevunjika. Kwa mujibu wa hadith, Abu Basir amesimulia kuwa Imam Sadiq (a.s) alisema: “Ikiwa mume hamtunzi mke wake ni jukumu la mahakama kuvunja ndoa yao, kwa kulazimisha talaka.” Hii kwa kifupi ni maoni ya fakihi wa cheo cha juu wa zama hizi. Anayetaka kujua undani wake asome kitabu kiitwacho ‘*HuququzZawjiyyah’* ambacho kina maelezo marefu ya mwanazuoni huyu.

Kama ulivyoona, Aya, **“Ama kaa naye kwa wema au muache kwa wema’** ni kanuni ambayo Uislamu

umeitumia kuwajibisha haki za mke. Kwa mujibu wa kanuni hii na amri kali iliyomo katika sentensi msiwarejeshe ili kuwadhuru', Uislamu hautaki mwanaume yeyote mwovu kuyatumia madaraka yake vibaya na kumbana mwanamke asiolowe na mtu mwingine.

Mbali na hoja hizo zilizonukuliwa kutoka kwenye makala ya 'Haki za Unyumba', kuna hoja nyingine pia ambazo zinaunga mkono mtazamo kuwa Aya **"Ama kaa naye kwa wema au muache kwa wema'** kwa mtazamo wa Uislamu ni kanuni ya jumla inayohusu haki zote za mke. Kwa kadri mtu anavyozitazama pande mbali mbali za kanuni hii, ndivyo anavyozidi kuutambua ubora wa mafundisho ya Uislamu.

Katika kitabu, *alKafi*, Jalada la tano, Imam Sadiq (a.s) ameripotiwa kusema kuwa mtu anapotaka kumuoa mwanamke anatakiwa asema; "Ninakiri kiapo kilichochukuliwa na Allah'

"Ama Kaa Naye Kwa Wema Au Muache Kwa Wema'

Qur'ani Tukufu inasema;

وَكَيْفَ تَأْخُذُونَهُ وَقَدْ أَفْضَىٰ بَعْضُكُمْ إِلَىٰ بَعْضٍ وَأَخَذْنَ مِنْكُمْ مِيثَاقًا غَلِيظًا

"Vipi mnaweza kunyang'anya mahari (mliyowapa) na hali mmeshaingiliana nao, na wamechukua kwenu ahadi thabiti (ya kuwalipa mahari kamili) (*Suratul Nisaa*, 4:21).

Wafasiri wa Qur'ani, wote Shia na Sunni wanakubali kuwa hapa **'ahadi thabiti'** inazungumziwa Aya, **"Ama kaa naye kwa wema au muache kwa wema'.** Hii ndio ahadi ambayo Imam Sadiq (a.s) aliimaanisha alipowataka watu kuikubali ahadi ya Allah wakati wa ndoa.

Vyanzo vyote vya Kishia na Kisunni vinaripoti kuwa katika Hija ya mwisho Mtukufu Mtume alisema; "Muogopeni Allah juu ya wanawake kwani hiyo ni dhamana ya Allah, na mmeruhusiwa kustarehe nao kwa neno lake."

Mwanahistoria maarufu na mwanatheolojia Ibn alAthir anaandika kuwa 'neno la Allah' katika kauli hii ya Mtume linamaanisha Aya ya Qur'ani; **"Ama kaa naye kwa wema au muache kwa wema' Maoni ya Sheikh Tusi.**

Sheikh Tusi akitoa maoni yake juu ya suala la kukosa nguvu za kiume (uhanithi), anasema kuwa baada ya kuthibitika kuwa mume ni hajiwezi (kiunyumba), mke ana hiari ya kuvunja ndoa. Anasema kuwa mafakihi wote wamekubaliana juu ya hili na kwa kutetea hoja yao wanatumia Aya **"Ama kaa naye kwa wema au muache kwa wema'** Mwanaume huyu, kwa vile hana uwezo wa kutekeleza jukumu lake la unyumba, hawezi kukaa na mke wake kwa wema, hivyo anapaswa kumwacha.

Maoni yote yaliyonukuliwa hapo juu, yanathibitisha kuwa Uislamu haumruhusu mwanaume yeyote

kuitumia haki yake ya talaka vibaya na kumweka mke wake kama mfungwa. Hata hivyo, ifahamike kuwa si kila jaji ana ujuzi wa kutosha kuingilia masuala haya. Uislamu umeweka vigezo vigumu sana vya mtu kuwa kadhi.

Inafaa pia ieleweke kuwa talaka zinazotolewa na jaji zinatarajiwa kuwa chache sana, kwani Uislamu unapenda familia zidumu kwa kadri inavyowezekana, Uislamu hauwezi kuruhusu talaka ichukue sura kama ile ya Ulaya na Marekani, mambo tunayoyasoma kila siku kwenye magazeti. Kwa mfano mwanamke mmoja alidai talaka kwa kuwa mume wake hakuipenda filamu ambayo yeye alikuwa anaipenda. Mwanamke mwingine alitaka talaka kwa kuwa mume wake hakumbusu mbwa wake kipenzi, vijisababu vingine vingi vya ovyo ambavyo ni vituko vinaripotiwa kila siku. Vyote hivi vinaashiria kuporomoka kwa ubinadamu.

Katika sura hii, tumejadili nadharia tano za talaka kwa mtiririko huu:
1. Haifai kuwepo kwa vizuizi vya kimaadili na kijamii vya talaka.

2. Ndoa ni mkataba wa milele. Talaka inapaswa kupigwa marufuku kabisa (maoni ya kanisa Katoliki).

3. Ndoa inaweza kuvunjwa na mwanaume sio mwanamke.

4. Ndoa inaweza kuvunjwa na wote wawili, mume na mke lakini kwa masharti fulani. Taratibu za uvunjaji wake zinafanana bila kujali aliyeamua kuvunja ni mume au mke (maoni ya watetezi wa usawa wa haki).

5. Njia ya talaka iko wazi kwa wote mume na mke lakini taratibu zake ni tofauti (kutegemea ni nani, mume au mke, anayeamua kuvunja ndoa).

Kama tulivyosema hapo awali, Uislamu unaunga mkono nadharia ya mwisho. Kutokana na tuliyoyasema juu ya kutoa madaraka kwa mke ya kuvunja ndoa kama sharti la lazima na mkataba wa ndoa na uwezekano wa talaka ya kimahakama, ni dhahiri kuwa japo Uislamu hautambui kuwa mke ana haki ya asili ya talaka, lakini haujamfungia moja kwa moja mlango wake wa kutokea.

Suala la talaka ya kimahakama linaweza kujadiliwa zaidi, hasa kwa kurejea maoni ya mafakihi wa matapo mbali mbali ya sheria, lakini tunafikiri kuwa kwa matumizi na haja yetu ya sasa, hatuhitaji kwenda ndani zaidi.

Ndoa Ya Muda (Mut'a)

Ndoa Ya Muda – I

Moja ya sheria tukufu za Uislamu kwa mtazamo wa sheria ya Ja'fari (Shia) ni kuwa kuna aina mbili za ndoa, ndoa ya kudumu na ndoa ya muda maalumu.

Baadhi ya athari zinazotokana na aina hizi mbili za ndoa ni sawa (zinafanana) na nyingine ni tofauti. Kuna tofauti mbili za msingi tu kati ya ndoa hizi mbili. Moja ni kuwa katika ndoa ya muda, mwanaume na mwanamke huingia katika mkataba wa ndoa ya muda maalum. Muda ukiisha wanaweza kuongeza au kuachana.

Tofauti nyingine ni kuwa kuna uhuru mkubwa zaidi wa kuchagua katika ndoa ya muda. Wanaooana wanaweza kuwekeana masharti yoyote wanayopenda. Kwa mfano, katika ndoa ya kudumu mume anawajibika kumtunza mke wake na kumtimizia mahitaji yake ya kila siku. Pia anapaswa kumpatia mavazi, malazi na mahitaji mengine ya lazima kama vile matibabu. Lakini katika ndoa ya muda, kila kitu hutegemea masharti ya mkataba. Inawezekana kuwa mume anaweza kuwa hana uwezo au hayuko tayari kubeba gharana za mke wake, au mke anaweza asipende kutumia fedha za mume wake.

Katika ndoa ya kudumu mke anapaswa kumtambua mume wake kuwa ni mkuu wa familia na kumtii katika mambo ambayo yamo ndani ya mipaka ya familia, lakini katika ndoa ya muda hili linategemea masharti ya mkataba wa ndoa waliyowekeana. Katika ndoa ya kudumu, mke na mume wanarithiana, lakini katika ndoa ya muda hawarithiani.

Hata hivyo, katika ndoa ya muda, baada ya nikaha kusomwa, wanandoa hutambuliwa kuwa ni mume na mke halali na wanaweza kuingiliana lakini kabla ya hapo hawaruhusiwi kabisa kufanya hivyo (tendo la ndoa).

Tofauti kuu kati ya ndoa ya muda na ndoa ya kudumu ni kuwa ndoa ya muda huweka masharti (majukumu) machache zaidi kwa wanandoa. Masharti yake hutegemea hiari, matakwa na makubaliano yao wao wenyewe. Kwa asili aina hii ya ndoa huwapa wanandoa uhuru fulani, na huwapa wao uhuru wa kuamua ni muda gani ndoa itadumu.

Katika ndoa ya kudumu si mume wala mke anayeweza kutumia njia za kuzuia mimba bila idhini ya mwenzake, lakini katika ndoa ya muda idhini sio jambo la lazima. Hii ni aina nyingine ya uhuru waliopewa mume na mke.

Mtoto anayezaliwa katika ndoa ya muda ana hadhi sawa kisheria na mtoto aliyezaliwa ndani ya ndoa ya kudumu.

Mahari: Mahari lazima ipangwe wakati wa ndoa, lakini malipo yake halisi yanaweza kutegemea makubaliano ya wanandoa wote wawili.

Mahari ni ya lazima katika ndoa zote mbili ya muda na ya kudumu ingawa kuna tofauti kuwa kutopangwa kwa mahari katika ndoa ya muda huibatilisha ndoa hiyo, lakini kutopangwa kwa mahari katika ndoa ya kudumu hakubatilishi ndoa. Ikiwa mahari haikupangwa wakati wa kufunga ndoa, mke hustahili mahari ambayo imezoeleka eneo hilo.

Katika ndoa ya kudumu, mume amekatazwa kabisa kumuoa mama au binti wa mke wake na mke amekatazwa kuolewa na baba au mtoto wa mume wake. Hali iko hivi pia katika ndoa ya muda.

Kama ilivyokuwa hairuhusiwi kutoa pendekezo la kumuoa mke aliyeolewa ndoa ya kudumu, halikadhalika hairuhusiwi kutoa pendekezo la kumuoa mwanamke aliye ndani ya ndoa ya muda. Mtu akizini na mwanamke aliyeolewa ndoa ya kudumu hiki huwa ni kizuizi cha kudumu cha yeye kutokumuoa mwanamke huyo na halikadhalika mtu akizini na mke wa mtu aliye katika ndoa ya muda huwa amejiwekea kizuizi cha kudumu cha yeye kutokumuoa mwanamke huyo.

Baada ya kupewa talaka, katika ndoa ya kudumu mke hupaswa kukaa eda, kipindi ambacho haruhusiwi kuolewa na mwanaume mwingine, halikadhalika katika ndoa ya muda baada ya ule muda waliokubaliana kuisha, mke anapaswa kukaa eda pia. Tofauti pekee ni kuwa kwa mke wa kudumu, eda ni miezi mitatu, ambapo kwa ndoa ya muda eda ni vipindi viwili vya hedhi, au siku 45. Kuwaoa madada wawili kwa wakati mmoja hairuhusiwi katika ndoa zote mbili, ya muda na ya kudumu. Hii ndio maana ya ndoa ya muda kwa mujibu wa sheria ya Shia.

Ni wazi kuwa tunaiunga mkono sheria hii kama itazingatia masharti yake. Ikiwa baadhi ya watu waliitumia vibaya huko nyuma au bado wanaitumia vibaya, hilo ni jambo ambalo liko nje ya sheria. Kufutwa kwa sheria hii, kama inavyopendekezwa na watu wa kisasa (modernist) hakuwezi kuwa na manufaa yoyote kwani kwa kuifuta maovu hayatakoma, isipokuwa tu yatachukua sura mpya. Vile vile, kufutwa kwa sheria hii kutasababisha kuzuka kwa maovu mengine mengi. Kinachotakiwa ni kuwa badala ya kutafuta dosari za sheria hii, watu wanapaswa kusaidiwa wajirekebishe na kuelimishwa.

Sasa hebu tuangalie kwanini ni muhimu kuwa na taasisi ya ndoa ya muda sambamba na ndoa ya kudumu. Ikiwa ndoa ya muda ni muhimu je inakubaliana na hali za sasa na mawazo ya kisasa ya maadili? Tunataka kulijadili swali hili chini ya vichwa viwili.

Maisha ya sasa na ndoa ya muda. Dosari na uovu wa ndoa ya muda.

Maisha Ya Sasa Na Ndoa Ya Muda.

Kama tulivyojifunza huko nyuma, ndoa ya kudumu huwapa majukumu mazito wanandoa wote wawili, mume na mke.

Hata hivyo, hakuna mvulana au msichana ambaye wakati wa kupevuka, ambapo huwa katika shinikizo kubwa la hamu ya ngono, huwa amejiandaa kwa ndoa ya kudumu. Mahitaji ya zama hizi yameongeza urefu wa kitambo kati ya kupevuka kwa asili na kupevuka kijamii, ambapo mtu huwa na uwezo wa

kujenga familia. Katika zama za kale, ambapo maisha yalikuwa rahisi, mvulana alikuwa anaweza kuanza kufanya kazi fulani toka kipindi cha awali kabisa cha kupevuka kwake na akaendelea nayo hadi mwisho wa uhai wake. Lakini sasa hivi hili haliwezekani tena.

Mvulana humaliza hatua mbali mbali za elimu akiwa na umri wa miaka 25, ikiwa hakufeli katika hatua yoyote. Hapo ndipo anapoweza kutarajiwa kuwa na kipato chake mwenyewe. Huchukua miaka mingine mitatu au minne ya kujiandaa na kuweza kuoa. Mambo yanakuwa hivi pia kwa msichana anayependa kupata elimu bora maishani.

Mabarobaro Na Mihemko Ya Ngono.

Leo hii ukimuambia mvulana wa miaka 17, ambaye ndio anakuwa katika kilele cha hamu ya ngono, aoe, watu watakucheka. Hali itakuwa hivyo hivyo kwa msichana mwanafunzi wa miaka 16. Katika umri huu wote, wavulana na wasichana hawawezi kubeba majukumu ya ndoa ya kudumu, sio tu kwao kama mume na mke bali na kwa watoto wao pia watakaozaliwa.

Kipi Ni Bora: Utawa Wa Muda, Ukomonisti Wa Ngono, Au Ndoa Ya Muda?

Tunajua maumbile yalivyo, lakini hali hiyo ya maisha katika ulimwengu wa sasa haituruhusu kuoa tukiwa na umri wa miaka 16 au 17. Maumbile hayako tayari kuchelewesha upevukaji au hamu ya ngono hadi tutakapomaliza elimu yetu. Je vijana wetu wapo tayari kuishi maisha ya ubikra kwa muda hadi hapo watakapokuwa na uwezo wa kuoa ndoa ya kudumu? Hata kama kijana mwenyewe yuko radhi kustahamili, je, maumbile yapo tayari kumsamehe asipatwe na shinikizo na hitilafu za neva ambazo kwa kawaida matokeo yake ni kumfanya ajiepusha kutokana na tendo la kawaida la ngono, kama ilivyobainishwa na wataalamu wa kisasa wa sayansi ya akili?

Sasa tumebakiwa na njia mbili tu. Ya kwanza ni kumruhusu mvulana kushirikiana ngono na mamia ya wasichana, na msichana kushiriki katika uhusiano haramu na wavulana wengi, na kisha kutoa mimba nyingi. Hii inamaanisha kuwa kivitendo tunaruhusu Ukomonisti wa ngono. Kwa hakika, tukitoa uhuru usio na mipaka kwa wavulana na wasichana, tutakuwa tunakidhi matakwa ya Azimio la Haki za Binaadamu, kwa sababu kwa maoni ya watu wengi wenye akili finyu, Azimio linataka kuwa, ikiwa wanaume na wanawake wataenda motoni, basi waende pamoja mkono kwa mkono.

Lakini swali ni iwapo itawezekana kwa wavulana na wasichana hawa ambao watakuwa wamefanya ngono zisizo na idadi wakati wa kipindi chao cha masomo, kuishi maisha ya kawaida ya familia.

Njia ya pili ni ndoa huru ya muda. Kwa kuanzia ndoa ya muda humpa kila mume mke mmoja kwa wakati mmoja. Ikiwa kila mwanamke ana mwanaume mmoja, ni wazi kila mwanaume atakuwa na mwanamke mmoja, isipokuwa pale ambapo jinsia moja itakuwa kubwa sana kuliko nyingine. Hivyo wavulana na

wasichana wanaweza kupita katika kipindi chao cha masomo bila kupata madhara ya kuishi maisha ya utawa wa muda, au kuangukia katika lindi la Ukomonisti wa ngono.

Ndoa Ya Majaribio.

Kimsingi inawezekana kwa mwanaume na mwanamke wanaokusudia kuona ndoa ya kudumu wakawa kila mmoja hana imani ya kutosha juu ya mwenzake, hivyo wakaoana kwa majaribio kwa muda fulani. Wakiwa wameaminiana vya kutosha, huendelea kuishi maisha ya ndoa, vinginevyo wanatengana. (kwa hiyo, tofauti kati ya mtindo wa Kimagharibi wa uhusiano pamoja na mwanamke na Uislamu ni kuwa kwa Wamagharibi hakuna dhana ya mfumo wa ndoa kati ya mwanamke na mwanaume ambapo katika Uislamu wenzi huhesabiwa kuwa mke na mume hata kama ni kwa muda).

Nadharia Ya Russell Ya Ndoa Ya Muda.

Katika kitabu chake *'Matrimony and Morals'* mwanafalsafa maarufu sana wa Kiingereza, Bertrand Russell, anasema kuwa malaya wanauhifadhi usafi wa kimaadili (kutozini) wa wake zetu na binti zetu. Mtazamo huu ulipotolewa kwa mara ya kwanza na Luckey katikati ya kipindi cha utawala wa Victoria watetea maadili walikereka sana, ingawa hata wao hawakujua kwanini. Hata hivyo hawakuweza kuzivunja hoja za Luckey. Mantiki ya watetezi wa maadili ilikuwa, kama watu wangefuata maadili yao, malaya wasingekuwepo. Lakini walielewa fika kuwa hakuna aliyezingatia walichosema.

Hii ndio kanuni ya kizungu ya kukabiliana na hatari inayoletwa na wanaume na wanawake wasioweza kufunga ndoa ya kudumu, na iliyotajwa hapo juu ni kanuni iliyopendekezwa na Uislamu. Ikiwa kanuni hii ya kizungu itazingatiwa na jukumu hili likakabidhiwa kwa kundi fulani la wanawake wenye bahati mbaya, je hii itakuwa inaafikiana na heshima ya utu wa mwanadamu na staha ya mwanamke na kiini cha Azimio la haki za Binadamu?

Bertrand Rusell, katika kitabu chake, ameingiza sura ya ndoa ya majaribio pia. Anasema kuwa Lindsay, ambaye kwa miaka mingi alikuwa jaji wa Denver, na kwa nafasi yake hiyo alikuwa na nafasi ya kutosha ya kuchunguza ukweli wa mwenendo wa maisha, alipendekeza kuwa iwepo 'ndoa ya wenzi' (companionship marriage). Lakini kwa bahati mbaya jaji huyu alilazimika kupoteza kazi yake kwa kuwa alikuwa anajali maslahi ya vijana mno kuliko kuwajengea ndani yao hisia ya dhambi. Ili kuhakikisha anafukuzwa, mengi yalisemwa na kanisa Katoliki na Ku Klux Klan, (chama cha siri cha watu ambao hawataki watu weusi kushirikiana na watu weupe – wabaguzi wa rangi nchini Marikani).

Ndoa ya wenzi ilipendekezwa na msomi anayependelea kuhifadhi mila za kale kwa nia ya kuweka jambo litakaloleta uimara katika mahusiano ya ngono. Lindsay alibaini kuwa tatizo kubwa la ndoa lilikuwa ni ukosefu wa fedha. Fedha haihitajiki kwa ajili ya watoto watakaozaliwa tu, lakini pia kwa sababu haimuwajibikii mwanamke kubeba gharama za matunzo ya familia. Anafikia hitimisho kuwa vijana wanapasa kufunga ndoa za wenzi (muda) ambazo ni tofauti na ndoa za kawaida katika njia tatu. Kwanza nia ya ndoa hii sio kuzaa watoto.

Pili kwa vile mwanamke huwa hajazaa mtoto, kuachana muda unapokwisha huwa jambo rahisi. Tatu, katika suala la talaka, mwanamke hustahili kulipwa masurufu baada ya kuwa ameachwa. Hapana shaka kwamba mapendekezo ya Lindsay yanafaa na yanatekelezeka, kama yangekuwa yamekubaliwa kuwa sheria, yengetarajiwa kuwa na matokeo mazuri kwa maadili.

Ambacho Lindsay na Russell wanakiita ndoa ya wenzi ni tofauti kidogo tu na ndoa ya muda katika Uislamu, lakini pendekezo hili linaonyesha kuwa wanafalsafa wa fani hii wamebaini kuwa ndoa ya kawaida ya kudumu haikidhi mahitaji yote ya jamii.

Ndoa Ya Muda II

Tayari tumeshaeleza tabia ya ndoa ya muda, ulazima wa kuwepo kwake na ndoa ya kudumu kushindwa kukidhi mahitaji yote ya wanaadamu. Sasa hebu tuangalie upande wa pili wa shilingi na kuona hasara na dosari zake. Kabla ya kujadili hilo hebu tuangalie kitu kimoja.

Historia Ya Imani.

Katika masomo yote ambayo watu mbali mbali wameyatolea maoni, hakuna lililo tata na gumu kama historia ya mawazo, imani, mila na desturi za mwanadamu. Hii ndio sababu kuwa japo mada hii ni maarufu sana, maoni yaliyo mengi yanayotolewa juu ya hili yamekuwa ni upuuzi.

Mtu yeyote mwenye elimu juu ya falsafa, mafundisho ya kumfikia Mungu kwa tafkira, irifan (*mysticism*) na falsafa ya uanazuoni (*schalasticim*) wa Kiislamu, na akasoma maandishi ya hivi karibuni katika nchi yetu juu ya masuala yanayohusiana na mada hii ataona kuwa mengi yanaazimwa kutoka kwa wageni au wananukuu na kuiga kila neno lao, pia anaweza kuelewa ninachomaanisha. Waandishi wetu wa zama hizi wanarudia au kuziegemeza kazi zao na mustashirik, wakati inaonekana kuwa mustashirik hawa na vibaraka wao hawafanyi lolote katika kuyachambua masuala haya kwa kina.

Kwa mfano, suala linalofahamika katika mafunzo ya Kiislamu ya irifan (*mytcism*) kama *wahadat alWujud* (Umoja wa Mwenyezi Mungu) limejadiliwa kutoka katika kila pembe, lakini hakuna jitihada ya maana iliyoelekezwa kufafanua maana halisi ya dhana (neno) hiyo wala kuelezea maoni ya vinara wa mafunzo haya ya irifan (Islamic Mysticism) kama vile Muhyiuddin ibn Arabi na Sadrul Muta'llihin Shiraz. Hivi karibuni maoni yaliyotolewa juu ya ndoa ya muda katika gazeti la Iran *'ZaneImruz'* au "mwanamke wa leo" yamenikumbusha mada ya *'Wahdat alWujud'*

Katika makala haya kila kitu kilizungumzwa juu ya ndoa ya muda, lakini nia hasa ya sheria hii iliachwa. Watu hawajali sheria hii kwa kuwa ni sehemu ya urithi wa Mashariki. Ingekuwa ni zawadi kutoka Magharibi mambo yangekuwa tofauti kabisa.

Kama sheria hii ingekuwa inatoka Magharibi bila shaka makongamano na semina yangekuwa yanafanyika kutetea wazo kuwa ndoa ya kudumu haikidhi hali ya maisha ya karne hii na kwamba kizazi hiki hakiko tayari kubeba majukumu mazito ya ndoa ya kudumu. Kizazi hiki kinataka kuwa huru. Kinataka kuishi maisha ya uhuru. Kinataka ndoa huru ambayo masharti yake yataamuliwa na wanandoa wenyewe.

Sasa kwa kuwa tayari sauti zimeanza kupazwa huko Ulaya kuteteta ndoa ya muda na watu mashuhuri kama Bertrand Russel wanaihubiri kwa jina la ndoa ya wenzi inatarajiwa kuwa baada ya muda si mrefu ndoa ya muda itakuwa mashuhuri mno kiasi cha kuwa tutalazimika kuzindua kampeni za kutetea ndoa ya kudumu.

Pingamizi

Yafuatayo ndiyo yanayosemwa kuwa ni ubaya na mapungufu ya ndoa ya muda.

Msingi wa ndoa unapaswa kuwa wa kudumu tokea mwanzo wa mahusiano ya unyumba, mume na mke wanapaswa kujua kuwa kila mmoja ni mali ya mwenzake kwa kudumu. Wazo la kutengana halipaswi kuingi akilini mwao. Ndoa ya muda sio mkataba wa kudumu kati ya mume na mke.

Ni kweli kuwa msingi wa ndoa unapaswa kuwa wa kudumu. Hata hivyo, pingamizi hili linaweza kuwa sahihi tu kama tutaipinga ndoa ya kudumu na kuhimiza kuwa nafasi yake ichukuliwe na ndoa ya muda.

Kama pande mbili zinaweza kuimudu ndoa ya kudumu na kila mmoja ana imani ya kutosha na mwenzake na wakaamua kuwa kwa kudumu kila mmoja awe mali ya mwenzake hapana shaka kuwa wanapaswa kufunga ndoa ya kudumu.

Sheria ya ndoa ya muda imewekwa tu kwa vile ndoa ya kudumu peke yake haiwezi kukidhi mahitaji yote ya wanaadamu katika hali zote. Kuruhusu ndoa ya kudumu peke yake kutasababisha tu Ukomonisti wa ngono. Ni wazi kuwa hakuna mvulana au msichana ambaye ana rasilimali za kutosha kwa ajili ya ndoa ya kudumu anaweza kujiingiza katika mahusiano ya muda.

Wanawake na wasichana wa Kiirani, licha ya kuwa Shia, hawalipendi wazo la ndoa ya muda. Wanaliona kama tusi kwao. Hivyo maoni ya jumla ya Shia wenyewe yamelikataa.

Tunaweza kujibu kuwa kulichukia wazo hilo kijumla kunatokana na wanaume waasherati kulitumia vibaya. Ni jukumu la serikali kuzuia kutumiwa kwake vibaya. Pili sio jambo la maana kutarajia ndoa ya muda kuwa mashuhuri kama ndoa ya kudumu, kwa sababu ndoa ya muda inakusudiwa kukidhi mahitaji ya wahusika ikiwa wote au mmoja wao hayuko tayari kufunga ndoa ya kudumu.

Ndoa ya muda inashusha hadhi na utu wa mwanamke. Ni sawa sawa na kuukodi mwili wa mtu, na hata kuhalalisha uuzaji wa watu. Ni kinyume na staha ya mwanamke kumuweka kwa ajili ya mwanaume yeyote kwa kubadilishana na fedha.

Hili ni pingamizi linalostaajabisha zaidi. Kwanza ndoa ya muda, kama tulivyoeleza hapo awali, haina uhusiano wowote na uuzaji au ukodishaji. Je inaweza kuwa uuzaji au ukodoshaji kwa vile tu muda wa ndoa ni maalum? Je inakuwa ni kukodisha kwa kuwa mahari inapaswa kupangwa? Tunataka kulijadili suala la mahari tofauti.

Mafakihi wamekubaliana kuwa, kwa asili ya mkataba, hakuna tofauti kati ya ndoa ya kudumu na ndoa ya muda. Ni miundo miwili ya ndoa na mikataba yake inaweza kusihi tu kwa kuzingatia kanuni ya ndoa. Ikiwa mkataba wa ndoa ya muda utachukua sura ya uuzaji au ununuaji, basi itakuwa ni batili.

Pili, tangu lini ada ya kukodi (kuajiri) watu ilipigwa marufuku? Mafundi cherehani, vionyozi, wapishi, hata wataalamu mabingwa, waajiriwa wote wa serikali kuanzia kwa Waziri Mkuu hadi kwa afisa wa cheo cha chini kabisa na wafanyakazi wote wa viwandani wote ni wa kukodiwa.

Mwanamke ambaye kwa hiari yake anaingia mkataba wa ndoa ya muda na mwanaume fulani sio mwanamke aliyekodishwa na hafanyi jambo la aibu kwa staha yake. Kama unataka kuona wanawake waliokodishwa na waliofanywa watumwa na unataka kujua maana halisi ya mwanamke aliyeajiriwa (kodiwa), unapaswa kwenda Ulaya na Marekani na utembelee makampuni ya filamu. Huko utaona miondoko ya viungo vya mwanamke, ishara zake na mikao ya kingono ikiuzwa.

Tiketi za sinema na kumbi za starehe unazonunua ndiyo mishahara ya wanawake waliokodiwa. Unatambua ni kiasi gani mwanamke anajidhalilisha ili kupata fedha? Analazimika kujifunza kwa miaka mingi sanaa ya kuamsha na kuchochea hamu ya ngono chini ya usimamizi wa wataalamu bingwa wa fani hiyo na wenye uzoefu. Analazimika kuuweka mwili wake, roho yake na haiba yake rehani kwenye makampuni ya biashara ili kuvutia wateja zaidi na zaidi. Ukitembelea mikahawa na mahoteli, unaweza kuona ni heshima gani mwanamke aliyopata, ni jinsi gani analazimika kuuza heshima na utu wake kwa ajili ya fedha kidogo ili kujaza masanduku ya fedha ya mabepari na jinsi gani analazimika kujiuza mbele ya wageni.

Wanawake waliokodiwa ni wale wasichana wa mauzo katika maduka makubwa ambao wanaitoa mhanga heshima na staha yao ili kukidhi tamaa ya waajiri wao.

Wanawake waliokodiwa ni wale wasichana wanamitindo wanaoonekana katika TV wakitangaza bidhaa na wanaotumia mbinu zote kuwavutia wateja kwao.

Nani asiyejua kuwa leo hii huko Magharibi uzuri wa mwanamke, mvuto wake wa kingono, sauti yake, sanaa yake, mwili wake, roho yake na zaidi ya yote, haiba yake vinatumika kama njia nyenyekevu za kutumikia maslahi ya ubepari wa Ulaya na Marekani?

Ninashangaa ni vipi mwanamke aliyeolewa na mwanaume fulani kwa hiari yake lakini kwa muda maalum anachukuliwa kuwa mwanamke aliyekodiwa (kufanya ngono) wakati mwanamke ambaye katika sherehe ya harusi au kwenye hafla ya jioni, mbele ya maelfu ya macho yenye tamaa ya wanaume, anaimba mpaka koo lake linauma, haonekani kuwa ni mwanamke aliyekodiwa (kufanya mambo

machafu).

Kwa kuruhusu ndoa ya muda, Uislamu umemkinga mwanamke dhidi ya kunyonywa na mwanaume. Pia Uislamu umemkataza kutumia njia dhalili ili kujipatia riziki. Je, ni Uislamu uliomdhalilisha mwanamke au Ulaya ya karne hii?

Ikiwa siku moja mwanamke atagundua mitego yote ambayo mwanaume wa karne hii ameiweka katika njia yake, bila shaka atapinga kwa nguvu zote uongo na udanganyifu huu. Hapo tu ndipo atakapobaini kuwa mlinzi pekee mwaminifu kwake na kimbilio lake ni Qur'ani. Siku hiyo haiko mbali sana!

Aidha, ndoa ya muda inahalalisha ndoa za mitala, ambazo ni mila mbaya. Kwa hiyo ndoa ya muda haifai. Mwisho wa sura hii tutaeleza ni kwa ajili ya nani sheria hii imewekwa. Na kuhusiana na ndoa za mitala, tutajadili hilo katika sura inayofuata.

Ndoa ya muda haidumu. Huwaacha watoto watakaozaliwa wakiwa hawana makazi. Wanakuwa hawana mtu anayewajibika kwao. Wananyimwa uangalizi wa baba na upendo wa mama.

Katika ndoa ya kudumu hakuna mwanandoa anayeweza kukwepa jukumu la kuzaa watoto, lakini katika ndoa ya muda, pande zote mbili ziko huru. Ni kweli kuwa mke hapaswi kumzuia mume wake kufurahia jimai, lakini anaweza kuchukua hatua za kuzuia mimba. Tatizo hili limetatuliwa kabisa kutokana na maendeleo ya njia za kisasa za kuzuia mimba.

Hivyo katika ndoa ya muda, ikiwa wote wawili, mume na mke wanapenda wanaweza kuzaa watoto, ikiwa wanalikubali jukumu la kuwalea. Ni wazi kuwa, kwa upande wa upendo wa asili, hakuna tofauti kati ya mtoto aliyezaliwa ndani ya ndoa ya kudumu na yule wa ndoa ya muda. Ikiwa baba au mama watakataa kutekeleza jukumu lao, ni jukumu la mahakama kuwalazimisha kama vile tu inavyoingilia katika suala la talaka. Ikiwa mume na mke hawataki kuzaa watoto na nia yao ni kukidhi haja zao tu, wanapaswa wajiepushe kuzaa watoto.

Kama tunavyojua, Kanisa haliruhusu njia za kuzuia mimba. Lakini kwa maoni ya Uislamu mume na mke wako huru kutumia njia za kuzuia mimba. Hata hivyo mimba ikishaingia hairuhusiwi kuitoa au kuiharibu.

Hili ndilo wanalolimaanisha mafakihi wa Kishia wanaposema kuwa lengo la ndoa ya kudumu ni kupata watoto na la ndoa ya muda ni kukidhi haja ya asili ya jimai.

Ndoa Ya Muda Maalum Na Nyumba Ya Wake Wa Mtu

Moja ya mada, ambazo nchi za magharibi zinaitumia kama silaha ya kuonyesha uovu wa nchi za Mashariki na ambayo nchi za magharibi zimeandaa filamu na tamthilia kwa ajili yake ni suala la uundaji wa nyumba za wake (harems). Kwa bahati mbaya, mifano hii ni ukweli uliopata kuwepo katika historia.

Maisha ya baadhi ya makhalifa na masultani yanatoa mfano kamili wa muundo wa 'nyumba za

wanawake' wao, ambazo huelezewa kuwa ni alama mashuhuri ya uasherati wa mwanaume wa Mashariki.

Inadaiwa kuwa uhalali wa ndoa ya muda unafanana tu na uhalali wa nyumba ya wake, ambayo ni nukta dhaifu kwa upande wa nchi za Masharikii na imeleta aibu kwayo. Sio hivyo tu, bali pia ni sawa na kuhalalisha uasherati, miundo yote ambayo inakwenda kinyume na maadili na husababisha kuporomoka na kuangamia.

Kitu hicho pia kimesemwa juu ya ndoa za mitala na zimetafsiriwa kuwa ni uhalalishaji wa nyumba za wanawake wengi (walio chini ya mwanaume mmoja). Tutalijadili suala la ndoa za mitala peke yake. Hivi sasa tunabakia kwenye ndoa ya muda.

Suala hili linapaswa kujadiliwa katika pembe mbili:

Ni sababu gani za kijamii zilizosababisha uundwaji wa nyumba za wake (wa mtu mmoja) huko nyuma? Je, sheria ya ndoa ya muda ilikuwa na ushawishi katika hali hii?

Je sheria ya ndoa ya muda inakusudia kutoa fursa kwa wanaume waasherati kuunda nyumba za wanawake wao?

Sababu Za Kijamii Za Uundwaji Wa Nyumba Za Wake Wa Mtu (Harems).

Kulikuwa na sababu mbili zilizosababisha kuwepo kwa nyumba hizi. Ya kwanza ilikuwa ni uchamungu na staha ya mwanamke. Nyumba hizi zinaweza kuundwa tu katika mazingira ambayo mwanamke hawezi kufanya tendo la ndoa na mwanaume zaidi ya mmoja. Katika hali hiyo mwanaume muasherati hana namna ila kuwakusanya wanawake wengi na kuunda 'nyumba ya wakeze' (harem).

Ni wazi kuwa katika mazingira ambayo umuhimu hauwekwi katika staha na wanawake wapo wengi na bure hakuna anayeweza kuchukua taabu ya kuunda 'nyumba ya wake' kubwa kwa gharama kubwa na vifaa vingi.

Sababu ya pili ilikuwa ni kutokuwepo kwa uadilifu wa kijamii. Mazingira yanayofaa kwa uundaji wa 'nyumba za wake' ni kuwa wachache wamebobea katika kila aina ya starehe na raha, ambapo wengine hawawezi hata kupata mlo wa siku, na ambamo kuna wengi ambao hawawezi kumudu kuoa na kuwa na familia. Katika mazingira hayo, idadi ya wanawake ambao hawajaolewa huongezeka na hutengeneza mazingira mazuri ya uundwaji wa nyumba za wake.

Kwa upande mwingine, ikiwa kuna uadilifu wa kijamii na kuna uwezo wa kuunda familia na kuchagua mke/mume kwa wote, basi ni wazi kuwa kila mwanamke ataambatana na mume mmoja na kunakuwa hakuna fursa ya ufisadi na uundaji wa nyumba hizi.

Ikiwa kila mtu mzima ana nafasi ya kuwa na mume/mke, ni wazi kuwa hapatakuwa na idadi kubwa ya wanawake wanaobaki kwa ajili ya matajiri kuunda nyumba za wake, kwani idadi ya wanawake kwa kawaida huwa sawa, huzidi au kupungua kidogo kuliko idadi ya wanaume.

Imekuwa ni mila kuwa historia inasimulia hadithi za nyumba hizi za makhalifa na masultani na kuelezea fahari na utajiri wa vitala (makazi na ofisi) vyao lakini hupuuzia kueleza dhiki, shida na taabu ya wale waliokufa katika tawala hizo na ambao hali zao hazikuwa zikiwaruhusu kuwa na mke.

Mamia ya wanawake waliomalizia maisha yao katika nyumba hizi walikuwa ni haki ya asili ya wanaume hawa fukara waliolazimika kubakia bila kuoa mpaka walipokufa.

Bila shaka katika jamii ambayo staha na usafi wa kimaadili upo na ambapo tendo la ngono haliwezekani isipokuwa ndani ya mipaka ya ndoa, zikiwemo zote mbili, ya muda na ya kudumu, uundaji wa nyumba za wake hauwezekani, hasa inapokuwa matabaka ya kijamii na kiuchumi yameondolewa na haki ya ndoa inapowekwa wazi kwa kila mtu mzima.

Tukiitazama historia kwa haraka haraka tutaona kuwa sheria ya ndoa ya muda haikuwa na ushawishi wowote katika uundwaji wa ‘nyumba za wake’ hata kidogo.

Hakuna khalifa yeyote wa ukoo wa Abbas na masultani wa himaya ya Ottoman ambao hawa ndio walikuwa mashuhuri kwa kuwa na ‘nyumba za wake’ kubwa, aliyekuwa mfuasi wa Theolojia ya Shia na hivyo haitarajiwi kuwa yeyote kati yao angeweza kuwa alitumia fursa ya sheria ya ndoa ya muda.

Masultani wa Kishia, japo wangeweza kuwa waliitumia sheria hii kama kisingizio kamwe hawakupata kufanya hivi kama makhalifa wa Ibn Abbasi na masultani wa himaya ya Ottomani. Hii inaonyesha wazi kuwa nyumba hizi zilisababishwa na sababu nyingine maalum za kijamii.

Je Ndoa Ya Muda Imehalalishwa Ili Kukidhi Tamaa Ya Mwili?

Hapana shaka kwamba dini zote za kimungu zinazuia kabisa uasherati na ukosefu wa maadili, kiasi cha kufikia baadhi ya wafuasi wake kuamua kuishi maisha ya utawa.

Moja ya kanuni za wazi za Uislamu na zinazokubalika ni kupiga vita uzinifu, ambao umelinganishwa na shirki (kwa maneno ya Qur’ani). Uislamu umemuelezea ‘muonjaji’ yaani anayetaka kufaidi kila aina ya wanawake, kuwa anashutumiwa na kuchukiwa na Allah. Tulipokuwa tukijadili suala la talaka, tulilizungumzia hili.

Moja ya sifa (tabia) za Uislamu ni kuwa unapinga utawa na useja (kutooa) lakini hauruhusu uzinifu, kwa mujibu wa Uislamu, matamanio ya haja zote za asili, ikiwa ni pamoja na haja ya ngono yanatakiwa kukidhiwa ndani ya mipaka ya kisheria tu kwa kiasi cha mahitaji ya asili. Uislamu hauruhusu kuwasha moto wa matamanio na kuubadili kuwa kiu isiyokatika. Uislamu unapinga mambo yote yenye sura ya uasherati na dhulma.

Ni ukweli usio na shaka kuwa kamwe haikuwa nia ya Mtungaji wa sheria hii ya ndoa ya muda kutoa njia kwa washerati ya kukidhi matamanio yao yasiyokatika ya ngono na kuleta maafa na maangamizi kwa mwanamke na watoto wake wasio na hatia. Utiaji moyo mkubwa uliowekwa kwenye wazo la ndoa ya muda maalumu na Maimamu (wa Ahlul Bait) una falsafa maalumu, ambayo tutaieleza kwa kifupi.

‘Nyumba Za Wake’ Na Ulimwengu Wa Kisasa.

Sasa hebu tuangalie jinsi ulimwengu wa kisasa ulivyolishughulikia suala la nyumba hizi. Ulimwengu wa kisasa unazitazana nyumba hizi kwa chuki na mila hii imeshaachwa. Moja ya vipengele viwili vilivyosababisha kuwepo kwa nyumba hizo kimeshaondolewa. Lakini ni sababu ipi hiyo? Sio ile ya matabaka ya kijamii bali ile ya staha na uchamungu wa wanawake ndiyo imeondolewa.

Mwanaume mzinifu wa zama hizi hahitaji tena kutaabika kuunda ‘nyumba ya wake’ na kubeba gharama kubwa za kuihudumia. Shukrani kwa utamaduni wa Kimagharibi kwamba kwa mwanaume wa karne hii ‘nyumba ya wake’ ipo katika kila sehemu. Ili kuwafaidi wanawake wa rangi na mataifa mbali mbali, mwanaume wa sasa hahitaji kuwa na madaraka makubwa na fedha nyingi kama Harun alRashid au Fazl Ibn Yahya Barmaki. Anachohitaji ni gari tu na kipato cha elfu kiasi kila mwezi ili kuweza kufaidi ngono kwa kiasi ambacho hata Harun alRashid hakupata kuota. Hoteli za kisasa, migahawa, na mikahawa mara zote zipo tayari kuhudumia (kutumiwa) kama nyumba za wanawake kwa wanaume.

Wakati fulani uliopita kijana wa Kiiran, Adil Kutwali, wazi wazi alikiri kuwa na mabibi (mahawara) 22 wa maumbo na sura mbali mbali kwa wakati mmoja. Shukrani kwa utamaduni wa Kimagharibi kwamba mwanaume wa sasa anafurahia raha zote za nyumba hizi (harem) bila kuwa na hofu ya gharama kubwa ya kuihudumia.

Kama shujaa wa ‘Alfu Lela Ulela’ (masiku elfu moja na moja) angenyanyua kichwa chake kutoka mavumbini na kuona fursa tele za kufaidi ngono na urahisi wa bei pamoja na uwingi wa wanawake, asingefikiri tena haja ya kuwa na nyumba ya wake, na kubeba gharama zote za kuihudumia. Angewashukuru watu wa magharibi kwa kumuokoa na gharama zote za kuunda nyumba ya wanawake na hapo hapo angetangaza kufutwa kwa ndoa za mitala na ndoa za muda, kwa sababu zinawapa wanaume mzigo wa majukumu juu ya wanawake. Ukiuliza ni nani aliyepoteza katika mchezo huu, kwa kuwa mshindi anajulikana toka zamani, tutasema kuwa kwa bahati mbaya mwanamke ndiye mara zote amekuwa mpotezaji. Kwa sababu ya kuamini kirahisi na kuwa rahisi, alipoteza jana na amepoteza leo.

Khalifa Apiga Marufuku Ndoa Ya Muda Maalum.

Ndoa ya muda inaruhusiwa na sheria ya Shia (Jafaria) peke yake. Madhehebu mengine ya Kiislamu hayaruhusu. Sikusudii kuingia katika ubishani wa Shia na Sunni. Napenda tu hapa kutaja kwa kifupi usuli wa kihistoria wa suala hili.

Waislamu wote wanakubaliana kuwa katika kipindi cha awali cha Uislamu Mtukufu Mtume wakati akiwa

safarini na ikawa Waislamu walikuwa mbali na wake zao na hivyo wakawa wanapata ugumu, aliwaruhusu kufunga ndoa za muda. Inakubaliwa pia na Waislamu wote kuwa Khalifa wa pili, katika kipindi cha ukhalifa wake, aliipiga marufuku ndoa ya Mut'a kwa mujibu wa taarifa mashuhuri, alisema kuwa: "Leo ninapiga marufuku vitu viwili ambavyo vilikuwa halali wakati wa Mtume. Ni ndoa ya muda na kuhiji 'Hajj' na Umra kwa ihram mbili tofauti."

Baadhi ya Sunni wanaamini kuwa Mtume mwenyewe aliipiga marufuku ndoa ya muda katika kipindi cha mwisho cha uhai wake na Khalifa wa pili alirudia kupiga marufuku ambayo tayari imeshawekwa na Mtume. Lakini maneno ya Khalifa ambayo yamekuja kwetu yanaonyesha kitu tofauti na hiki.

Maelezo sahihi juu ya hili ni yale yaliyotolewa na Allamah Kashif alGhita. Khalifa alipiga marufuku ndoa ya muda kwa sababu alifikiri kuwa jambo hili lilikuwa ndani ya mamlaka yake kikatiba kama Mkuu wa Dola, ambaye angeweza kutumia mamlaka yake maalum kutokana na mahitaji ya wakati. Kwa maneno mengine zuio la Khalifa lilikuwa ni la kisiasa sio la kisheria. Khalifa kamwe alikuwa hafichi wasi wasi wake juu ya kusambaa kwa masahaba wa Mtume katika nchi mpya zilizotekwa na kuchanganyika kwao na Waislamu wapya waliosilimu. Katika muda wote wa uhai wake, alipinga vikali suala la Waislamu (masahaba) kuhama kutoka Madina.

Pia hakutaka damu zao zichanganyike na Waislamu wapya waliosilimu, ambao imani yao ilikuwa bado haijawa kubwa. Ni wazi kuwa hii ilikuwa ni rai ya muda. Waislamu wa wakati ule waliikubali amri yake bila kuonyesha chuki, kwa sababu tu walijua kuwa ilikuwa ni ulazima wa kisiasa na sio sheria ya kudumu. Vinginevyo hailekei kwamba watu wangeridhika, kama wangeona Mtume aliamrisha hivi na Khalifa anaamrisha vinginevyo. Lakini baadaye ambapo kama matokeo ya maendeleo fulani, maisha ya makhalifa wa mwanzo, hususan makhalifa wawili wa mwanzo, yalichukuliwa kama kiigizo, amri zao zilichukua sura ya sheria ya kudumu.

Hivyo ndugu zetu wa kisunni wanapaswa kulaumiwa zaidi kuliko khalifa ambaye aliweka zuio la muda dhidi ya ndoa ya muda kwa sababu za kisiasa (kama ilivyokuwa kwa zuio la tumbaku nchini Iran katika mwanzo wa karne hii) Wengine wasingepaswa kulipa zuio hili sura ya sheria ya kudumu.

Ni dhahiri kuwa Allamah Kashif alGhita hakutoa maoni yoyote juu ya kitendo cha khalifa kama kilikuwa kinakubalika au la. Alieleza tu asili ya zuio hili na kwa nini halikupingwa na Waislamu.

Hata hivyo ni kutokana na ushawishi huu na haiba (shaksia) ya Khalifa, kwamba watu waliacha kuifuata sheria hii na kwa sababu mila ya Uislamu ya ndoa ya kudumu ilidhaniwa ingeachwa basi ikawa ndoa ya muda imeachwa.

Ni katika hali hii kwamba kwa nia ya kuhakikisha kuwa desturi ya Kiislamu haisahauliki kabisa, Maimamu watukufu wa Ahlul Bait, ambao ni watetezi na walinzi wa imani walihimiza na kuitetea sana. Imam Jafar Sadiq (a.s) alikuwa akisema kuwa ndoa ya muda ni nukta ambayo hawezi kuificha kamwe.

Mbali na faida nyingi za ndoa ya muda, jitihada ya kufufua desturi zilizokufa ilikuwa ni sababu nyingine

ya Maimamu kuihubiri. Kwa maoni yetu, Maimamu walipowakataza watu kuoa kwa ndoa ya muda, walitaka iwe wazi kuwa ndoa hii haikuwa kwa wale wasioihitaji.

Imam Kadhim (as) alimwambia Ali ibn Yaqtin, 'Unataka ndoa ya muda ya nini? Allah amekuepusha na tatizo la kuihitaji."

Alimwambia mtu mwingine kuwa 'ndoa ya muda, ni kwa yule asiye na mke au mwenye mke lakini mke wake yuko mbali."

Muongozo na uhimizaji wa umma katika kuoa ndoa za muda ni hatua moja mbele katika "ufufuaji wa mila zilizoachwa" au desturi lakini uhimizaji peke yake kwa wale waliokuwa wakiihitaji haukuwa unatosha kuihuisha tena mila hii tuliyoruhusiwa na Mtume, kama inavyoonyeshwa wazi katika maandiko ya Kishia na vitabu vya hadithi.

Hata hivyo ni ukweli ulio wazi kuwa maana na lengo la Mtunzi wa sheria hii katika kuikuza (kuitetea) na maelezo ya sheria hii na lengo la Maimamu Maasumin la kuihimiza halikuwa na nia ya kuruhusu majaribio ya ngono, matamanio maovu na ujenzi wa nyumba za wake kwa ajili ya watu wenye tabia za wanyama wala kuwakandamiza na kuwatesa wanawake wasio na uwezo na waliokandamizwa pamoja na watoto yatima kwa wakati wowote.

Mwandishi wa kimisri, Sheikh Muhammad Abu Zuhra, katika kitabu chake, *'AlAhwal alShakhsiya,* amemnukuu Amirul Muuminina Ali (a.s) kuwa amesema, "Kama nikipata habari kwamba mtu mmoja mwenye mke amefunga ndoa ya muda, nitampiga mawe mpaka afe."

Hadith hii haina sanad (nyororo) ya wasimuliaji inayoeleweka. Hata hivyo usahihi wake unakubalika, inaunga mkono wazo kuwa ndoa ya muda inaruhusiwa tu kwa yule asiye na mke au ambaye mke wake yuko mbali.

Kwa kifupi kwa nini tushikilie hadith hii moja ya mwanazuoni wa Kisunni (ambayo chanzo chake hakieleweki) na kuziacha hadithi nyingine nyingi za Amirul Muuminina Ali (a.s) zilizoripotiwa katika vitabu vyote vya kisunni na Kishia katika sura ya Mut'ah.

Katika kauli zake nyingi za thamani Imam Ali (a.s), Amiri wa walioamini anasema, "Kama Umar asingeifuta ndoa ya muda, hakuna mtu ambaye angezini, isipokuwa wachache wenye maradhi ya ngono." Hii ni kuwa kama ndoa ya muda isingekuwa imepigwa marufuku, hakuna mtu ambaye angejenga tabia ya kuzini, ni wale tu ambao mara zote wanapenda kufanya mambo yaliyoharamishwa ndio wangefanya hivyo.

Ndoa Ya Mitala (Mke Zaidi Ya Mmoja)

Ndoa ya mke mmoja ndio muundo wa asili zaidi wa ndoa. Hali ya kumiliki kitu peke yako, au uhusiano ambao wewe tu ndio unashikilia nafasi hiyo na umiliki binafsi umejikita katika aina hii ya ndoa, japo umiliki huu ni tofauti na umiliki wa mali au utajiri. Katika mfumo huu mume na mke, kila mmoja huhisi hisia za moyoni na faida za ngono za mwenzake kuwa ni zake peke yake.

Kinyume na ndoa ya mke mmoja ni ndoa ya mke zaidi ya mmoja (mitala) kwa wakati mmoja na Ukomonisti wa ngono. Jimai ya ngono, kimaana pia inaweza kuitwa mitala.

Ukomonisti Wa Ngono.

Ujimai wa ngono maana yake hakuna kuwa peke yako. Kwa mujibu wa nadharia hii, hakuna mwanaume ambaye anapasa kuwa mali ya mwanamke mmoja tu wala mwanamke kuwa mali ya mume mmoja tu. Maana yake ni kupinga (kuikana) kuwepo maisha ya familia.

Historia na nadharia zinazohusiana na zama za kale kabla ya kuanza kuandikwa kwa historia haionyeshi kipindi chochote ambapo mwanadamu hakuwa na familia na ambapo Ukomonisti wa ngono ulikuwa umestawi. Kinachodaiwa kuwepo katika baadhi ya makabila ya kishenzi (yasiyo na ustaarabu na utamaduni) ilikuwa ni hali ya kati na kati, kati ya maisha ya familia (yaani kila mtu na mke wake au mume wake) na Ukomonisti wa ngono. Inasemekana kwamba katika baadhi ya makabila ilikuwa ni jambo la kawaida kwamba wavulana kadhaa kwa pamoja waliwaoa wasichana kadhaa, au wanaume kadhaa wa ukoo mmoja waliwaoa kwa ushirikiano wanawake kadhaa wa ukoo mwingine.

Will Durant katika kitabu chake, '*History of Culture'* Jalada la 1, anaandika kwamba katika baadhi ya maeneo ndoa za ushirikiano zilikuwa mashuhuri kwa maana kuwa wanaume kadhaa wa ukoo mmoja walishirikiana kuwaoa wanawake kadhaa wa ukoo mwingine, kwa mfano imekuwa ni mila huko Tibet kwamba ndugu kadhaa wa kiume wana idadi sawa ya madada (ambao ni ndugu) kama wake zao. Kila kijana huingiliana na yeyote katika wale akina dada anayempenda. Hapa kuna aina fulani ya Ukomonisti wa ngono.

Mila kama hii ilipata kuwepo huko Uingereza enzi za kale. Mila ambayo ilikuwa maarufu miongoni mwa Wayahudi na makabila mengine ya zamani na ambapo kwa mujibu wa mila hiyo, baada ya kufa ndugu mmoja wa kiume, ndugu yake mwingine wa marehemu alimuoa mjane wake, ilikuwa ni masazo ya mila ya kale.

Maoni Ya Plato

Inaelekea kwamba wakati akiitangaza nadharia yake ya 'wanafalsafa watawala' Plato amependekeza

katika kitabu cha '*The Republic,'* aina fulani ya ujamaa wa kifamilia kwa tabaka hili. Viongozi kadhaa wa kikomunisti wa karne ya 19 pia walitoa pendekezo kama hilo, lakini kama ilivyoripotiwa na mwandishi wa kitabu, '*Freud and the Prohibition of Consanguineuous Marriage,'* baada ya machungu mengi, dola nyingi za kikomunisti zenye nguvu, zilitangaza rasmi kuitambua sheria ya mke mmoja mume mmoja mwaka 1938.

Kuwa Na Mume Zaidi Ya Mmoja (Polyandry).

Muundo mwingine wa mitala ni hali ya mke kuwa na mume zaidi ya mmoja (*polyandry*) kwa wakati mmoja. Kwa mujibu wa Will Durant mila hii inapatikana miongoni mwa makabila fulani ya Tibet na kwingineko.

AlBukhari katika mkusanyiko wake maarufu wa hadithi, *asSahihi*, anamripoti Aisha kuwa alisema kuwa miongoni mwa Waarabu wa kabla ya Uislamu kulikuwa aina nne za mahusiano ya ngono. Mojawapo ni ndoa sahihi ambayo bado ipo hadi sasa. Katika muundo huu mwanaume hutoa pendekezo kwa msichana kupitia kwa baba yake na baada ya kupanga mahari, humbeba mke wake. Hapawezi kuwa na utata juu ya watoto waliozaliwa katika ndoa hii.

Kulikuwa na aina nyingine ya ndoa, ambayo ilikuwa ikiitwa *Istibza.* Ili kuzaa (kupata) kizazi kizuri, mume alimchagua mwanaume na kumuomba mke wake aingiliwe na huyo mwanaume kwa muda fulani. Yeye mwenywe alijitenga na mke wake hadi mwanamke alipopata mimba. Ilikuwa ni ndoa ndani ya ndoa iliyofanywa ili kuboresha kizazi.

Kwa mujibu wa mila nyingine, kundi la wanaume kumi au pungufu ya hapo, walishirikiana kufanya mapenzi na mwanamke mmoja. Baada ya kuwa mjamzito, mke aliwaita wote, na kwa mujibu wa mila ya enzi hizo, wote walipaswa kwenda. Hapo alimteua mwanaume mmoja kuwa baba wa mtoto wake na kuwaacha wale wengine ambao nao pia walikuwa tayari kukubali jukumu hilo. Mwanaume huyo baada ya kuchaguliwa, hakuwa na hiari ya kukubali au kukataa kuwa baba wa mtoto.

Aina ya nne ya mahusiano ya unyumba ni umalaya. Malaya walikuwa na bendera juu ya nyumba zao. Hii ilitumika kama alama ya kuwatambulisha. Mwanaume yeyote alikuwa anaweza kuwaingilia wanawake hawa. Mwanamke yule alipozaa, aliwaita wanaume wote waliomwingilia, na kwa msaada wa mtaalamu wa kutambua tabia kwa kuangalia uso, alimteua baba wa mtoto. Mwanaume mhusika alipaswa kukubali uamuzi wa mtaalamu huyu na kummiliki mtoto.

Hizi ni aina za mahusiano ya kinyumba zilizokuwepo Arabuni kabla ya Uislamu. Mtume alizipiga marufuku zote na kubakiza moja iliyopo sasa. Hii inaonyesha kuwa mila ya mke kuwa na mume zaidi ya mmoja ilikuwepo miongoni mwa Waarabu wa kabla ya Uislamu pia.

Montesquieu anaripoti kuwa Mwarabu mtembeaji wa dunia nzima, Abu Zahir alHassan, aliikuta mila hii China na India alipozitembelea nchi hizi katika karne ya 19 na aliichukulia kama aina ya ufisadi. Pia

anaandika: “Katika Pwani ya Malabar kuna kabila liitwalo Nair. Waume wa kabila hili hawawezi kuwa na mke zaidi ya mmoja lakini wanawake wanaruhusiwa kuchagua waume wengi. Labda sababu ni kuwa Wanair ni jamii ya wapiganaji na wawindaji. Kama tunavyowazuia kuoa askari wetu wa Ulaya ili ndoa isiingiliane na kazi zao za kupigana, makabila ya Malabar pia yameamua kuwa, wanaume wa Nair wajitahidi kadri wawezavyo kuepukana na majukumu ya familia. Kutokuwa na hali na tabia ya kitropiki ya eneo hili, haiwezekani kuzuia ndoa kabisa, imeamuliwa kuwa wanaume wengi wawe na mke mmoja ili wasielemewe na majukumu ya kifamilia na hivyo kuathiri ufanisi wao.”

Kasoro Za Mke Mmoja Kuwa Na Waume Zaidi Ya Mmoja.

Kasoro kubwa na ya msingi ya mfumo huu wa mke kuwa na mume zaidi ya mmoja ni kuwa ukoo wa baba wa mtoto hubakia haujulikani kwa uhakika (yaani baba halisi wa mtoto huwa hajulikani). Katika mfumo huu uhusiano kati ya baba na mtoto haueleweki na hii ndio sababu mfumo huu hau jafanikiwa kama ilivyo Ukomonisti wa ngono haujaweza kujikita sehemu yeyote, mfumo huu pia haujakubalika katika jamii yoyote ya maana. Kama tulivyosema awali, maisha ya familia, ujenzi wa nyumba (makazi) ya kizazi kijacho na muunganiko maalumu kati ya vizazi vya zamani na vijavyo ni moja ya mahitaji ya silika za binadamu.

Kuwepo kwa mifano michache ya mke kuwa na waume wengi katika baadhi ya jamii hakuthibitishi kuwa uundaji wa familia sio silika ya mwanadamu. Halikadhalika utawa na useja kabisa (kuepuka kufanya tendo la ndoa), kama inavyofanywa na wanaume na wanawake kadhaa, pia ni aina ya upotofu. Mfumo huu si tu kwamba hauafikiani na asili ya mwanaume ya kuhodhi na upendo wake wa mfumo dume, bali pia unapingana na maumbile ya mwanamke pia. Uchunguzi wa kisaikolojia umebaini kuwa mwanamke anapenda zaidi kuwa na mume mmoja kuliko mwanaume anavyopenda kuwa na mke zaidi ya mmoja.

Mitala (Mke Zaidi Ya Mmoja).

Muundo mwingine wa mitala ni mtu kuwa na mke zaidi ya mmoja. Mfumo huu umezoeleka na kuwa na mafanikio zaidi kuliko ule wa mke kuwa na waume wengi na ujima wa ngono. Sio tu kwamba umekuwepo miongoni mwa makabila ya kishenzi, bali pia umetumiwa na watu wengi wastaarabu. Mbali na Waarabu, umetumiwa pia na Wayahudi, Wairani wa zama za Sasania na jamii nyinginezo. Montesquieu anasema kuwa huko Malaya ilikuwa inaruhusiwa kuwa na wake watatu. Pia anasema kuwa mfalme wa Urumi, Valentinian II aliwaruhusu watu wake kuoa wake wengi, lakini kwa sababu sheria hii ilikuwa haiafikiani na hali ya hewa (tabia) ya Ulaya, ilifutwa na wafalme wengine kama Theodore n.k.

Uislamu Na Mitala.

Tofauti na ilivyokuwa kwa mfumo wa mke kuwa na mume zaidi ya mmoja, Uislamu haukukataza moja kwa moja ndoa ya mke zaidi ya mmoja (mitala). Badala yake uliweka idadi maalumu, pia umeweka masharti mengine pia na haukumruhusu kila mtu kujiingiza katika kuoa wake wengi. Tutaeleza baadaye masharti yaliyowekwa na Uislamu na tutaeleza kwa nini Uislamu haukupiga marufuku ndoa za mitala moja kwa moja.

Inashangaza kwamba katika zama za kati, ambapo propaganda za kuupinga Uislamu zilikuwa katika kilele chake, wapinzani wa Uislamu walikuwa wakisema kuwa ni Mtume wa Uislamu ambaye kwa mara ya kwanza alianzisha ndoa ya mitala. Walidai kuwa mila hii ilikuwa msingi wa Uislamu na kwamba kuenea kwa Uislamu kwa haraka haraka sehemu mbalimbali duniani kulitokana na mila hii. Wakati huo huo walidai kuwa mitala hii ilikuwa ndio sababu ya kuporomoka kwa watu wa Mashariki.

Will Durant katika kitabu chake "*History of Culture" juz. 1,* anasema kuwa mapadri na makasisi wa zama za kati waliamini kuwa ndoa za mitala zilianzishwa na Mtume wa Uislamu, ambapo sio kweli. Kama tunavyojua maisha ya ndoa katika jamii nyingi za kijima yalifuata utaratibu huu wa mitala. Kuna sababu nyingi za kuzuka kwa mfumo huu. Katika jamii za kijima, sehemu kubwa ya wanaume walikuwa zaidi wakijishughulisha na uwindaji na upiganaji, hivyo kiwango chao cha vifo kilikuwa juu miongoni mwao. Kwa vile idadi ya wanawake ilizidi ya wanaume, hivyo ilikuwa ni lazima kutumia mfumo huu. Haikuwa inawezekana kuwaacha baadhi ya wanawake bila kuolewa, hasa ikizingatiwa kuwa, kwa vile idadi ya vifo katika jamii za kijima ilikuwa juu, kila mwanamke alitarajiwa kuzaa watoto.

Hapana shaka kwamba mfumo huu ulizifaa jamii hizo, sio tu kwa sababu ya uwingi wa wanawake kuliko wanaume, bali pia mfumo huu uliongeza idadi yao na kuwafanya kuwa na nguvu. Katika zama hizi wanaume wengi wenye nguvu na afya huchelewa kuoa na huzaa watoto kidogo tu. Lakini zamani wanaume wenye nguvu walikuwa na nafasi ya kuoa wake bora kabisa na walikuwa wakizaa idadi kubwa ya watoto. Hii ndio sababu desturi hii iliendelea kwa muda mrefu sana si tu miongoni mwa jamii za kijima bali hata katika jami zilizoendelea. Ni hivi karibuni tu kuwa pole pole desturi hii imeanza kutoweka katika nchi za Mashariki. Kilimo kimeimarisha maisha ya wanaume na kimepunguza ugumu wa taabu za kale, ambapo matokeo yake ni kuwa na idadi ya wanaume na wanawake imeanza kulingana. Hivi sasa mitala imekuwa ni fahari ya kundi dogo la matajiri, hata katika jamii za kijima, na walio wengi wanalazimika kuridhika na mke mmoja, na kwa burudani ya ziada, wanaweza kujiingiza katika zinaa, kila inapowezekana.

Gustav Leabeon katika kitabu chake, '*History of Culture*' anasema kuwa hakuna mila isiyopendwa Ulaya kama ndoa za mitala, wala Ulaya haijaihukumu kimakosa mila nyingine yoyote kama ilivyofanya kwa ndoa hii. Waandishi wa kizungu wameamini kuwa ndoa za mitala ni msingi wa Uislamu na ndio sababu kubwa ya kuenea kwake. Pia wanashikilia kuwa mila hii ndio sababu ya kuanguka kwa watu wa mashariki. Pingamizi nyingine mbali na hizi, zinazoonyesha huruma kwa wanawake wa Mashariki,

zinadai kuwa wanawake hawa walionenepeana wanafungiwa ndani ya kuta nne za nyumba zao chini ya matowashi (wanaume waliohasiwa) wenye mioyo migumu.

Pia wanadai kuwa kosa dogo ambalo wanaweza kumuudhi mkuu wa familia linaweza kuwafanya waadhibiwe adhabu ya kifo. Fikra kama hizi hazina msingi wowote. Wazungu wasio na upendeleo wanapaswa kujua kuwa ni mila ya ndoa ya mitala ambayo imeyapa nguvu mahusiano ya kifamilia na kuinua maadili ya watu hawa. Ni kutokana na mila hii kwamba mwanamke wa Mashariki anaheshimika zaidi kuliko wa ulaya. Kabla ya kuthibitisha nukta hii, lazima tuweke wazi kuwa mila hii haihusiani na Uislamu.

Hata kabla ya Uislamu, mila hii ilikuwa inafuatwa na watu wa Mashariki wakiwamo Wayahudi, Wairani, Waarabu n.k. Watu waliosilimu huko Mashariki hawakunufaika na lolote katika mila hii. Juu ya hayo, hakuna dini yoyote yenye nguvu kama hii iliyobuni au kuzuia mila hii ya mitala. Mila hii haikuanzishwa na dini yoyote. Ilitokana na hali ya hewa na sababu nyingine zilizohusiana na mfumo wa maisha ya Mashariki.

Hata Magharibi, ambako hali ya hewa haiendani na kuweko kwa desturi kama hiyo, lakini ndoa ya mke mmoja inapatikana katika vitabu vya sheria tu. Katika maisha halisi hakuna dalili ya ndoa ya mke mmoja. Haifahamiki ni kwa namna gani mitala ya halali ya Mashariki ni ya hadhi ya chini kuliko ndoa za mitala ya siri za watu wa Magharibi. Watu wa mashariki, wanapotembelea nchi za Ulaya na kukumbana na shutuma kali za Wazungu dhidi ya mila zao hushangazwa na kuona wameonewa.

Ni ukweli kwamba Uislamu haukuanzisha ndoa za mitala. Ulichokifanya ni kuidhibiti tu. Umepanga idadi ya mwisho. Umeweka masharti magumu juu yake. Mila tayari ilikuwepo katika jamii nyingi ambazo zilikuja baadaye kusilimu. Walilazimika tu kufuata masharti yale yaliyowekwa na Uislamu.

Katika kitabu chake '*Iran During the Sassanian Period*,' Christenson ameandika: "Ndoa za mitala zilichukuliwa kuwa ni msingi wa familia. Kimsingi, idadi ya wake ambao mtu angependa kuwa nao ilitegemea na uwezo wake. Watu maskini hawakuwa wanamudu kuwa na mke zaidi ya mmoja. Mkuu wa familia alikuwa na haki maalum. Mmoja wa wake alichukuliwa kuwa ni mke kipenzi na alipata haki zote.

Wake wengine waliwatendea kama wafanyakazi tu. Haki za kisheria kati ya makundi haya mawili zilitofautiana sana. Watumwa wa kike (masuria) walijumuishwa katika kundi la wake wafanyakazi. Haifahamiki ni wake vipenzi wangapi mume angeweza kuwa nao. Lakini limetajwa suala la wake wawili vipenzi katika maandishi ya kisheria. Kila mmoja wao aliitwa malkia wa nyumba (mama mwenye nyumba). Waliishi katika nyumba tofauti. Mume alipaswa kumhudumia mke wake kipenzi katika maisha yake yote. Kila mtoto wa kiume hadi anapobalehe na kila mtoto wa kike hadi alipoolewa walikuwa na haki sawa. Lakini ni watoto wa kiume tu (wa wake wafanyakazi) walioingizwa katika ukoo wa baba."

Katika kitabu, "*Social History of Iran from tha fall of the Sassanians to the fall of Umayads",* marehemu Sa'id Nafisi anaandika kuwa, "Idadi ya wanawake ambao mwanaume angeoa haikuwa na mpaka na wakati fulani inavyoonekana katika kumbukumbu za Kigiriki mwanaume alikuwa anaweza kuwa na

mamia ya wanawake katika nyumba yake.”

Montesquieu, akimnukuu mwanahistoria wa Kirumi, anasema kuwa wanafalsafa wengi wa Kirumi ambao walikuwa wanateswa na Wakristo kwa sababu walikataa kuwa wakristo walikimbia Roma na kwenda kwa Mfalme wa Iran, Khusro Parviz. Walishangazwa kuona kwamba huko si tu kwamba ndoa za mitala zilikuwa zinaruhusiwa bali pia wanaume wa Kifarsi walikuwa wakiingiliana na wake za watu wengine pia.

Lazima ieleweke hapa kwamba wanafalsafa wa Kirumi walikimbilia kwenye kasri la Mfalme wa Iran, Anushirwan na sio kwenye kasiri la Khusro Parviz. Montesquieu amechanganya majina kutokana na kutoelewa vizuri.

Kabla ya Uislamu, Waarabu walikuwa na uwezo wa kuwa na idadi isiyo na mipaka ya wake. Ni Uislamu ulioweka mipaka. Hii bila shaka iliwasababishia usumbufu wale waliokuwa na wake zaidi ya wanne. Kuna baadhi walikuwa na wake kumi. Walilazimika kuwaacha sita.

Kutokana na haya ni wazi kuwa si Uislamu ulioanzisha ndoa za mitala. Uislamu uliziwekea udhibiti tu. Hata hivyo haukuzipiga marufuku kabisa, katika sura zinazofuatia tutataja sababu zilizosababisha mila hii, na tutaelezea sababu ambazo zimewafanya wanaume na wanawake wa zama hizi walazimike kuipiga vita mila hii.

Sababu Za Kihistoria Za Mitala.

Ni sababu zipi za kihistoria na kijamii zilizosababisha mitala? Kwa nini mataifa mengi ya ulimwengu, hasa mataifa ya mashariki yamekubali mila hii na kwa nini mataifa ya Magharibi, kamwe hayakupata kuitumia mila hii? Imekuwaje kwamba katika miundo mitatu ya mitala ni huu muundo mmoja tu wa mume kuwa na wake wengi ndio uliopata umaarufu? Mke kuwa na waume wengi na Ukomonisti wa ngono ama hazikupata kutumiwa kabisa, au zimetumika kidogo sana na katika maeneo machache sana.

Mpaka tuyajadili maswali haya ndio tutaweza kulijadili suala la ndoa za mitala katika Uislamu na kwa mujibu wa mahitaji ya sasa ya mwanadamu.

Tusipoyatumia na kuyazingatia matokeo ya uchunguzi wa kijamii na kisaikolojia yaliyopatikana juu ya mada hii, sisi pia, kama walivyokuwa waandishi wengine wa juu juu, tunaweza kuangukia na kuanza kuimba nyimbo za zamani za kudai kuwa sababu za mitala ziko wazi. Yaani, mila hii imetokana na ukatili wa mwanaume na utawala wake kwa mwanamke. Ni matokeo ya mfumo dume. Kwa kuwa mwanaume amemtawala mwanamke, ametunga sheria na mila ambazo zitamnufaisha yeye. Hivi ndivyo alivyoipa nguvu mila hii yenye manufaa kwake na madhara kwa mwanamke, na amekuwa akiitumia kwa karne nyingi. Mwanamke alikandamizwa, hakuweza kuutekeleza mfumo wa yeye kuwa na waume wengi. Na sasa muda wa uonevu wa mwanaume umekwisha, mila ya ndoa za mitala lazima iondoke kama ilivyokuwa kwa fursa nyingine za uongo ili kuleta haki sawa kwa wanaume na wanawake.

Kufikiri kwa namna hii ni kwa kitoto na kwa juu juu sana. Sababu ya mitala sio ukandamizaji wa

mwanaume kwa mwanamke wala kushindwa kwa mfumo wa mke kuwa na waume wengi sio ukandamizaji wa mwanamke. Kama kivitendo mfumo huu umekufa, hii sio kwa sababu muda wa uonevu wa mwanaume umefikia kikomo. Mwanaume hajapoteza fursa yoyote, kimsingi amepata fursa juu ya mwanamke.

Hatukatai kuwa ukandamizaji ni moja ya mambo yaliyobadilisha historia. Pia hatukatai kuwa katika kipindi chote cha historia mwanaume ameyatumia vibaya madaraka yake dhidi ya mwanamke. Lakini tunaamini kuwa ni mawazo finyu kuyaelezea mawazo ya kifamilia kwa kigezo cha dhulma peke yake.

Tukikubali mtazamo huu, lazima pia tukubali kuwa katika kipindi ambacho ndoa za mke kuwa na wanaume wengi zilikuwa maarufu miongoni mwa Waarabu wa kabla ya Uislamu, au kama alivyoripoti Montesquieu, miongoni mwa Wanair katika pwani ya Malabar mwanamke alipata fursa ya kumtawala mwanaume na akawa anakaa na wanaume wengi. Lazima ikubaliwe pia kuwa kipindi hicho kilikuwa ni cha dhahabu kwa mwanamke. Awali tulimnukuu Montesquieu akisema kuwa mila ya mke kuwa na waume wengi miongoni mwa Wanair haikutokana na utawala wa mwanamke au heshima aliyokuwa akipewa, bali ilikuwa ni uamuzi wa jamii wa kuwaepusha askari dhidi ya mzigo wa majukumu ya familia.

Aidha, kama Mfumo dume ndio ulisababisha mitala, kwa nini mfumo huu haukupata umaarufu Ulaya (Magharibi)? Hata hivyo, mfumo dume haukuwepo Mashariki peke yake. Je, watu wa Magharibi tokea awali wamekuwa Wakristo wachamungu wanaoamini juu ya usawa kati ya mwanaume na mwanamke? Je, kigezo cha kumiliki kimemnufaisha mwanaume wa mashariki na kukuza uadilifu huko Magharibi?

Mpaka kufikia nusu karne iliyopita mwanamke wa Magharibi alikuwa miongoni mwa wenye bahati mbaya kabisa duniani. Hata mali yake ilidhibitiwa na mume wake. Wazungu wenyewe wanakiri kuwa katika zama za kati, nafasi ya mwanamke wa mashariki ilikuwa bora sana ikilinganishwa na mwanamke wa Magharibi. Gustav Leabeon anasema kuwa Uislamu, katika kipindi cha mwanzo kabisa, ulimpa mwanamke nafasi (hadhi) ambayo mwanamke wa kizungu alipata baada ya muda mrefu sana, yaani baada ya uungwana na ustaarabu wa Waarabu wa Andolusia kuingia Ulaya.

Tabia njema kwa mwanamke ni sehemu kubwa ya uungwana ambao Wazungu walijifunza kutoka kwa Waislamu. Ilikuwa ni Uislamu (na sio dini ya Kikristo kama inavyoaminiwa na watu wengi wa kawaida), ulioinyanyua hadhi ya mwanamke. Katika zama za kati machifu wa makabila, licha ya kuwa Wakristo kamwe hawakumpa mwanamke heshima anayostahili. Uchambuzi wa historia ya kale unaonyesha kuwa tabia ya wafalme na viongozi wengine wa Ulaya ilikuwa ni ya kishenzi sana.

Waandishi wengine wa Kizungu, pia wametoa maelezo kama haya kuhusiana na nafasi ya mwanamke katika zama za kati. Japo mfumo dume ulikuwa umeenea sana Ulaya katika kipindi hiki, bado ndoa za mitala hazikuweza kuwa ni desturi.

Ukweli ni kuwa ni mfumo wa mke kuwa na waume wengi (popote ulikotumika) hautokani na utawala au nguvu ya mwanamke juu ya mwanaume wala kushindwa kwa mfumo huu hakukutokana na udhaifu wa mwanamke wala ukandamizaji wa mwanaume dhidi yake. Halikadhalika mitala katika nchi za Mashariki

haikusababishwa na udikteta na uonevu wa mwanaume wala si kwamba haujaenea huko magharibi kwa sababu ya kuwepo usawa kati ya mwanaume na mwanamke.

Sababu Za Kushindwa Kwa Mfumo Wa Mke Kuwa Na Waume Wengi

Sababu kubwa ya kushindwa kwa mfumo huu ni kuwa ulikuwa haufai kwa maumbile ya mwanaume wala ya mwanamke. Haufai kwa maumbile ya mwanaume, kwa sababu, kwanza hauafikiani na asili yake ya kupenda umiliki pekee (yaani awe wake peke yake) na pili kwa sababu haukubaliani na kanuni ya kwamba baba aweze kujiamini juu ya ubaba wake. Ni maumbile ya mwanadamu kuwa na mafungamano maalumu na wanawe.

Kila mwanadamu kwa asili anatamani kuzaa watoto na anataka uhusiano na kizazi chake kilichopita na kijacho uwe unaeleweka na wa uhakika. Anataka kujua yeye ni mtoto wa nani na ni baba wa nani. Mfumo wa mke kuwa na waume wengi haukubaliani na silika hii ya mwanadamu. Kwa upande mwingine mfumo wa mume kuwa na wake wengi (mitala) hausababishi matatizo haya, si kwa mwanaume, wala mwanamke. Imeelezwa kuwa wakati fulani wanawake wapatao arobaini walimwendea Imam Ali (a.s.) na kumuuliza kwa nini Uislamu umewaruhusu wanaume kuoa wake wengi lakini haujaruhusu wanawake kuwa na waume wengi. Wakamuuliza kama huu sio ubaguzi wa wazi.

Imam Ali (a.s.) aliagiza viletwe vikombe vya maji na akampa kila mwanamke kikombe kimoja cha maji. Kisha akawaamuru wamwagie maji yote yale katika chombo kimoja kikubwa kilichokuwa katikati yao. Baada ya kutekeleza agizo hilo, Imam Ali (a.s.) aliwaamuru kila mmoja wao achukue maji yale tu yaliyokuwa kwenye kikombe chake. Wanawake wote walisema kuwa hilo lilikuwa haliwezekani kutokana na ukweli kwamba maji yote yalikuwa yamechanganyika. Imam Ali (a.s.) alisema kuwa kama mwanamke mmoja angeolewa na wanaume wengi, ni wazi kuwa angeingiliana nao. Akipata mimba na kuzaa, haitafahamika mtoto yule ni wa baba yupi.

Kwa upande wa mwanamke, mfumo huu pia hauafikiani na maumbile yake. Mwanamke hamhitaji mume kwa ajili ya kukidhi silika yake ya ngono tu. Ingekuwa hivyo tungesema kuwa ‘Wanaume wengi zaidi, raha zaidi’. Mwanamke anataka mwanamume ambaye yeye mwanamke ataudhibiti moyo wake, atakayekuwa mlinzi na mwangalizi wake, atakayejitoa mhanga kwa ajili ya mkewe na atakayefanya kazi kwa bidii na kumletea fedha. Fedha anazojitafutia mwanamke huwa hazitoshi kukidhi mahitaji yake wala huwa hazina thamani sawa na zile alizopewa na mwanaume anayempenda. Mume hukidhi mahitaji ya kifedha ya mke wake kwa moyo wa kujitolea. Mke na watoto ni hamasa kubwa na bora kabisa kumhamasisha mwanaume kufanya kazi.

Katika mfumo wa mke kuwa na waume wengi mwanamke hawezi akadai na kupata mapenzi ya kweli na kujitolea kutoka kwa yeyote kati ya wanaume hawa. Hii ndiyo sababu, kama ilivyo tu kwa umalaya, huu umekuwa ni mfumo unaochukiza kwa mwanamke. Hivyo mfumo huu wa mke kuwa na waume wengi

haukidhi wala kukubaliana na asili na mahitaji ya mwanaume wala mwanamke.

Kushindwa Kwa Ukomonisti Wa Ngono

Katika mfumo huu si mwanaume wala mwanamke anayeweza kudai au kujinasibisha na mke au mume maalumu kuwa ni wake na hii ndiyo sababu mfumo huu kamwe haukupata kuwa maarufu sehemu yoyote ile. Ilipendekezwa na Plato ambaye aliliruhusu jambo hili kwa tabaka la watawala au 'wanafalsafa watawala.' Lakini pendekezo lake halikuwa kama la wengine na yeye mwenyewe baadaye ilibidi abadilishe maoni yake.

Katika karne iliyopita, Frederick Engels, baba wa pili wa ukomunisti alitoa wazo hili na akalitetea kwa nguvu. Lakini halikukubaliwa hata katika ulimwengu wa kikomunisti. Inasemekana kuwa Urusi ilijaribu kutekeleza nadharia ya familia ya Engels, lakini kufuatia machungu waliyayopata yaliyotokana na mfumo huu walilazimika kuutambua mfumo wa mume mmoja mke mmoja kuwa ndio sera rasmi.

Mitala inaweza kuonekana kuwa ni jambo la fahari kwa mwanaume lakini kamwe suala la mke kuwa na waume wengi halijawahi na halitapata kuwa ni jambo la fahari kwa mwanamke. Sababu ni kuwa mwanaume anataka mwili wa mwanamke na mwanamke anataka moyo wa mwanaume. Mwanaume anachojali ni kuumiliki mwili wa mwanamke, haijalishi hata kama haumiliki moyo wake. Hii ndio sababu mwanaume huwa hajali hata kama mmoja wa wake zake atapunguza upendo kwake, lakini kwa mwanamke, kitu muhimu kabisa ni moyo wa mwanaume na hisia zake za moyoni. Akivipoteza hivyo, huwa amepoteza kila kitu.

Kwa maneno mengine, kuna vitu viwili katika maisha ya unyumba, mwili na hisia za moyoni. Mwili unahusiana na ngono, ambayo hamu yake huwa kileleni katika kipindi cha ujana na baadaye hupungua polepole. Hisia za moyoni huhusiana na hisia za upendo, upole na kujitoa. Hisia hizi hukua na kukomaa kwa kadri muda unavyokwenda. Kwa vile maumbile ya mwanamke ni tofauti na ya mwanaume, mwanamke hujali zaidi hisia za moyoni katika maisha yake ya ndoa. Lakini kwa mwanaume, ama mwili ndio muhimu zaidi au vyote viwili, mwili na hisia za moyoni vina umuhimu sawa.

Huko nyuma, tulimnukuu mwanasaikolojia wa kike ambaye ana maoni kuwa mwanamke ana tabia za kipekee za akili. Mtoto hukua katika tumbo lake na kunyonyeshwa na kulelewa katika mapaja yake. Anahitaji sana kujitolea na upendo wa dhati wa mumewe kama baba wa mtoto. Hata kiasi cha upendo kwa wanawe kinategemeana na kiasi cha upendo anachokipata kutoka kwa baba yao. Ni ndoa ya mume mmoja tu ndiyo inaweza kukidhi mahitaji haya.

Ni kosa kubwa sana kulinganisha ndoa ya mke mmoja kuwa na waume wengi na ndoa ya mume mmoja kuwa na wake wengi na kudai kuwa hakuna tofauti yoyote kati ya aina hizi mbili za ndoa.

Pia ni makosa kusema kuwa ndoa za mitala zilikuwa mashuhuri katika baadhi ya sehemu za dunia kwa sababu mwanaume ana nguvu zaidi, na kwamba ndoa za mke kuwa na waume wengi zilishindwa

kutokana na mke kuwa ni jinsia dhaifu.

Mwandishi wa zama hizi, ambaye ni mwanamke anasema: “Tunaweza kusema kuwa kwa vile mwanaume anaweza kuwa na wake wanne, basi mke pia anapaswa kuwa na haki hiyo kwani wote ni binadamu. Hitimisho hili la kimantiki ni la kuudhi, zaidi kwa wanaume. Wanakasirishwa kusikia hoja hii na wanapiga kelele: ‘Inawezekanaje mwanamke akawa na waume zaidi ya mmoja?’ Kujibu hilo sisi kwa sauti ndogo tunasema: Inawezakanaje mwanaume akawa na mke zaidi ya mmoja?”

Pia anasema: “Hatukusudii kupalilia ufisadi au kupuuzia umuhimu wa maisha ya usafi wa kimaadili. Tunataka tu wanaume waelewe kuwa maoni yao juu ya wanawake hayakujengwa juu ya hoja za maana. Mwanaume na mwanamke ni sawa kama wanaadamu. Kama mwanaume ana haki ya kuwa na wake wanne, basi mwanamke pia lazima awe na haki kama hiyo. Hata kama tukichukulia kwamba mwanamke kiakili sio bora kuliko mwanaume, lakini ni hakika kwamba kiroho mwanamke sio dhaifu kuliko mwanaume.”

Kama ambavyo utakuwa umebaini kauli hiyo haioneshi tofauti yeyote kati ya mitala na ndoa za mke kuwa na waume wengi, isipokuwa kwamba kwa kuwa mwanaume ni wa jinsia yenye nguvu zaidi basi amechukuwa mfumo wa mitala kwa manufaa yake, na mwanamke kwa kuwa ni wa jinsia dhaifu hakuweza kuutumia utaratibu huo.

Mwandishi huyo pia anasema kuwa mwanaume anamuona mwanamke kuwa ni mali yake, na ndio maana anataka kuwa na wake wengi. Kwa maneno mengine ni kuwa mwanaume anataka kujikusanyia mali nyingi kwa kadri inavyowezekana. Kwa vile mwanamke yupo katika nafasi ya mtumwa, hawezi kuwa anamilikiwa na bwana zaidi ya mmoja.

Kinyume na maoni ya mwandishi huyu, ukweli kwamba mfumo wa mke kuwa na waume wengi haujawahi kukubaliwa na idadi yoyote kubwa ya watu popote pale duniani unathibitisha kuwa mwanaume hamchukulii mke wake kuwa ni mali yake, kwani katika mali, ni mashuhuri duniani kote kuwa mali humilikiwa kwa ubia na wamiliki wote hunufaika na mali hiyo kwa ubia. Kama mwanaume angekuwa anamchukulia mwanamke kuwa ni mali, ni wazi kuwa asingekuwa na pingamiza katika kuichangia na wengine. Hakuna sheria duniani inayolazimisha kuwa mali imilikiwe na mtu mmoja tu.

Inasemwa kwamba mume ni mtu mmoja na mke ni mtu mmoja. Wanapaswa kuwa na haki sawa. Kwa nini mume awe na haki ya kufurahia mitala na mke anyimwe haki hiyo ya kuwa na waume wengi? Tunasema kuwa hapa ndio kuna makosa. Unadhania kwamba mitala ni sehemu ya haki za mume, na mke kuwa na waume wengi ni sehemu ya haki za mke. Ukweli ni kwamba mitala ni sehemu ya haki za mwanamke, na ndoa ya mke kuwa na waume wengi sio sehemu ya haki za mwanaume wala mwanamke. Ni mfumo usio na faida kwa wote wawili, mwanamke na mwanaume. Tutathibitisha baadaye kuwa mfumo wa mitala umewekwa na Uislamu kwa nia ya kulinda maslahi ya mwanamke. Kama nia ingekuwa kumpendelea mwanaume, Uislamu ungemruhusu mwanaume kufanya mapenzi na mwanamke mwingine mbali na mke wake na usingeweka uwajibikaji juu yake kuhusiana na mke wake

wa halali na watoto wake wa halali.

Mfumo wa mke kuwa na waume wengi kamwe haujapata kuwa na maslahi yoyote kwa mwanamke. Sio haki aliyonyimwa.

Mwandishi ambaye tumenukuu maoni yake anasema: “Tunataka wanaume waelewe kuwa maoni yao juu ya wanawake hayajajengwa juu ya hoja ya maana.”

Kwa bahati sisi pia hicho ndicho tunachokusudia kukifanya. Katika sura zinazofuata tutaeleza msingi wa mtazamo wa Uislamu juu ya mitala.

Tunawaalika watu wote wanaofikiri kuutazama na kuona kama mtazamo wa Uislamu umejengwa au haukujengwa juu ya hoja zozote za maana. Tunaahidi kuwa tutayabatilisha yale yote, tuliyoyasema ikiwa mtu yeyote atathibitisha kuwa msingi wa mtazamo wa Uislamu ni mbovu.

Sababu Za Kihistoria Za Mitala II

Tamaa ya mwanaume katika ngono na utawala wake wa kibabe peke yake sio sababu tosha za kuibuka kwa mitala. Lazima ziwepo sababu nyingine zilizochangia katika mwanaume muasherati kukidhi hamu yake ya kuwa na wanawake wa aina mbalimbali. Ni rahisi zaidi kujiingiza katika ngono holela kuliko kuwa na mwanamke wa chaguo lake kama mke wake wa halali na kujitwisha jukuma la kutunza watoto wake wa baadaye. Mitala huwa mashuhuri katika jamii zile tu ambazo zinajali maadili na zinazuia ngono holela na mwenye kiu ya uasherati hulazimika kulipa gharama ya kutaka aina mbalimbali za wanawake kwa kumkubali mwanamke anayehusika kuwa mke wake wa halali na kubeba jukumu la kuwa baba wa watoto wa mwanamke huyo.

Sasa hebu tuangalie kama kuna sababu zozote za kijografia, kiuchumi au kijamii zilizochangia kuibuka na kuwepo kwa ndoa za mitala.

Sababu Za Kijiografia

Montesquieu na Gustav Leobeon wanasisitiza kuwa hali ya hewa na tabia za nchi ndio sababu kuu za maendeleo ya mitala. Wasomi hawa wanaamini kuwa tabia ya nchi na hali ya hewa ya nchi za Mashariki zinaifanya mila hii isiepukike huko. Katika nchi za Mashariki, wanawake hupevuka na kuzeeka haraka zaidi, hivyo mwanaume huoa mke wa pili na wa tatu. Pia wanafikiri kuwa mwanamke mmoja hawezi kukidhi kiu ya ngono ya mwanaume aliyekulia katika tabia ya nchi za Mashariki.

Gustav Leobeon katika kitabu chake “*History of Islamic and Arab Culture*” (Historia ya utamaduni wa Kiislamu na kiarabu) anasema: “Mila ya ndoa za mitala haikuanzishwa na dini. Ni matokeo ya tabia za

nchi, tabia ya watu wa huko na sababu nyingine zinazohusiana na maisha ya Mashariki. Haihitajiki kusisitiza sana kuwa hizi ni sababu zenye nguvu sana. Pia tabia zao za kimwili na kimhemko, unyoyeshaji wao wa watoto na magonjwa yao mara nyingi huwalazimisha wanawake wa Mashariki kujitenga na waume zao. Kwa kuzingatia tabia za nchi za Mashariki (Hali ya Hewa) pamoja na tabia za kitaifa za wanaume wa Mashariki, huwa haiwezekani kwa wanaume kustahamili kutengana na wake zao japo kwa muda mfupi, hivyo ndoa za mitala zimekuwa ni mila."

Montesquieu katika kitabu chake, "*The Spirit of Law*" anasema: "Katika nchi za kitropiki wanawake hupevuka wakiwa na umri wa miaka nane, tisa au kumi na baada ya kuolewa punde huwa wajawazito. Tunaweza tukasema kuwa katika nchi za kitropiki, mimba hushika mara moja tu baada ya ndoa."

Predo, alipokuwa anayaelezea maisha ya Mtume wa Uislamu, anasema kuwa alimuoa Khadija akiwa na umri wa miaka mitano na alianza kumwingilia akiwa na umri wa miaka nane. Kwa sababu ya ndoa za mapema, wanawake katika nchi za kitropiki huzeeka wakiwa na umri wa miaka ishirini. Anasema kuwa huanza kuzeeka hata kabla ya kupevuka.

Katika nchi zenye tabia ya vuguvugu, wanawake hubaki na ujana na uzuri wao kwa muda mrefu zaidi. Huchelewa kupevuka na huwa wamekomaa zaidi na wanakuwa na uzoefu zaidi wakati wanapoolewa. Hupata watoto katika umri mkubwa zaidi, na mume na mke huzeeka takribani kwa wakati mmoja. Hivyo ndivyo usawa kati ya mwanamke na mwanaume unavyopatikana na wanaume huwa hawahitaji kuwa na mke zaidi ya mmoja.

Hivyo ni kwa sababu ya tabia ya nchi ndio maana sheria imekataza mitala huko Ulaya lakini ikairuhusu huko Asia.

Maelezo haya sio sahihi. Mila ya mitala haiko katika nchi za kitropiki tu huko Asia. Katika kipindi cha kabla ya Uislamu mila hii ilikuwa mashuhuri sana nchini Iran, ambapo tabia ya nchi ni ya vuguvugu. Ni uzushi kabisa kusema kuwa katika nchi za Mashariki wanawake huzeeka wakiwa na umri wa miaka ishirini, kama ilivyodaiwa na Montesquieu. Inashangaza pia kusikia kuwa Mtume wa Uislamu, alimuoa Khadija akiwa na umri wa miaka mitano na kwamba alianza kumwingilia akiwa na umri wa miaka nane. Kila mtu anaelewa kuwa Mtume alimuoa Khadija, wakati yeye Mtume, alikuwa na umri wa miaka ishirini na tano na Bibi Khadija alikuwa na umri wa miaka ishirini na nane, ingawa baadhi ya vyanzo vya kihistoria vyenye makosa vinasema kuwa Khadija wakati huo alikuwa na umri wa miaka arobaini.

Pili, ikikubaliwa kuwa kuwahi kwa umri wa uzee kwa wanawake na nguvu nyingi za urijali kwa wanaume ndizo sababu ya mila hii, kwa nini watu wa Mashariki hawakujiingiza katika ngono holela na ufuska kama wenzao wa Magharibi ambao walifanya ngono holela na ufuska katika zama za kati na za sasa. Kama alivyoonyesha Gustav Leabeon, suala la mume kuwa na mke mmoja limebakia katika vitabu vya sheria lakini halionekani katika maisha halisi ya kila siku.

Tena, katika nchi za Mashariki, mitala ipo katika muundo wake wa Kisheria. Mwanamume humkubali mwanamke mhusika kama mke wake wa kisheria na halali na anapaswa kubeba jukumu la kuwa baba

wa watoto wa mwanamke huyo. Mitala iliyopo Ulaya ni ile haramu na isiyokuwa ya kisheria pamoja na ndoa za siri. Mwanaume wa Magharibi hujiingiza katika ngono holela na hukwepa majukumu yanayohusiana na ndoa.

Mitala Huko Magharibi

Tunaona kuwa ni muhimu kutoa maelezo mafupi ya mitala huko Ulaya katika zama za kati kama yalivyoelezewa na mwana historia mashuhuri wa kimagharibi. Maelezo haya yanapasa kuwafunua shuka jeusi wale wanaozikosoa nchi za mashariki kwa mitala kwamba licha ya dosari zinazodaiwa, mitala zilikuwa ni ndoa zenye heshima zaidi kuliko kile kilichokuwepo Ulaya.

Will Durant katika kitabu chake, *History of Civilization,* Juz.17*,* anatoa maelezo ya kuvutia juu ya hali ya maadili nchini Italia katika kipindi cha uamsho. Hapa chini tunatoa muhtasari wa yale aliyosema chini ya kichwa *“Morals in Sexual Relations”.*

Katika utangulizi wake mfupi anasema kuwa kabla ya kuelezea maadili ya Italia, tunaweza kusema kuwa kwa asili mwanamume ni mwenye asili ya kuoa wake wengi. Ni vikwazo vikali vya kimaadili, kazi nyingi ngumu na umaskini na uwajibikaji wa hali ya juu wa mke, kwa pamoja ndio vinaweza kumlazimisha kubaki na mke mmoja.

Kisha anasema kuwa uzinifu haukuwa jambo geni katika zama za kati kabla ya zama za uamsho. Kama ilivyokuwa kwamba katika zama za kati dhambi ya zinaa ilishutumiwa na watu walihimizwa kuishi maisha ya usafi, halikadhalika katika kipindi cha uamsho (*Renaissance*), vijana, wasomi walifundishwa kuwa na tabia njema na kutunza ubikra kwa wanawake.

Wasichana waliokuwa wanatoka katika familia zinazoheshimika walikuwa kwa kiasi fulani wakitengwa na wanaume wasiokuwa na familia yao na walifundishwa faida za kutunza ubikra wao hadi watakapoolewa. Wakati fulani mafundisho haya yalikuwa yanawaingia kichwani na kusaidia. Inaripotiwa kuwa ilikuwa kwamba ikitokea msichana akinajisiwa alikuwa akijizamisha majini na kufa. Haya lazima yatakuwa ni matukio haba sana, kwa sababu askofu alikuwa akichukua taabu ya kujenga mnara baada ya kifo chake ili kukumbuka usafi wake wa kimaadili.

Idadi ya waliokuwa wakifanya mapenzi kabla ya ndoa lazima itakuwa ilikuwa kubwa, kwa sababu kulikuwa na idadi kubwa ya watoto waliozaliwa nje ya ndoa katika kila mji wa Italia. Lilikuwa ni jambo la fahari kwamba mtu alikuwa hana mtoto wa nje ya ndoa, lakini kuwa naye mmoja halikuwa ni jambo la aibu. Kwa kawaida mume alimshawishi mke wake wakati wa ndoa kuja kwa mumewe pamoja na mtoto wake (wa huyo mwanamke) aliyemzaa nje ya ndoa. Ili alelewa pamoja na watoto wa ndani ya ndoa. Kuzaliwa nje ya ndoa halikuwa ni doa katika utukufu wa yeyote. Isitoshe cheti cha uthibitisho kuwa mtoto husika ni wa ndani ya ndoa kilikuwa kinaweza kupatikana kirahisi kwa kumpa rushwa kiongozi wa kanisa.

Iwapo watoto wa ndani ya ndoa wenye haki ya kurithi walikuwa hawapo, basi watoto wa nje ya ndoa walikuwa wakirithi mali na hata kiti cha ufalme kama ilivyokuwa kwa Frante I ambaye, alimrithi Alfonso I, Mfalme wa Naples. Pius – II alipokuja Bavaria mwaka 1459, alipokelewa na wana wa mfalme saba, ambapo wote walikuwa ni watoto wa nje ya ndoa. Uhasama na uadui kati ya watoto wa nje ya ndoa na wale wa ndani ya ndoa ndio ilikuwa sababu muhimu ya migogoro katika zama za uamsho. Liwati nayo ilikuwa ni kufufuliwa tu kwa desturi ya kale ya kigiriki.

San Bernardino aliikuta aina hii ya upotofu na uchafu ikiwa imeenea sana huko Naples akahisi kuwa hali hiyo inahatarisha kutokea kwa adhabu waliyopewa watu wa Sodoma. Artino aliikuta hali hii chafu huko Roma pia. Umalaya pia ulikuwa katika kiwango cha juu. Mwaka 1490, kati ya wtu wote 90,000 wa Roma, wanawake 6,800 walikuwa wamesajiliwa kama malaya. Idadi hii haihusishi mahawara na malaya ambao hawajasajiliwa. Kwa mujibu wa takwimu za mwaka 1509, kati ya watu laki tatu wa mji huo, kulikuwa malaya 11,654. Katika karne ya 15, msichana ambaye alikuwa amefikisha umri wa miaka 15 hali ya kuwa hana mume alionekana kama doa katika jina zuri la familia.

Katika karne ya 16 “umri wa mkosi” ulisogezwa mbele hadi miaka 17, ili kumuwezesha msichana kupata elimu ya juu. Wanaume, ambao walikuwa wanafurahia huduma za malaya waliokuwa wameenea kila sehemu, walikuwa wanavutiwa kuoa ikiwa tu mwanamke mhusika aliahidi kumpatia mahari ya kuvutia. Kwa mujibu wa mfumo wa zama za kati, mke na mume walitarajiwa kupendana na kushirikiana katika huzuni na furaha. Inavyoonekana matarajio haya kwa kiasi fulani yalifikiwa, lakini bado uzinifu ulikuwa umejikita mizizi. Ndoa nyingi za watu wa tabaka la juu zilikuwa ni za kidiplomasia zilizofungwa kwa maslahi ya kisiasa na kiuchumi. Waume wengi waliona kuwa ni haki yao kuwa na bibi pembeni. Mke alikuwa anakasirika sana lakini alikuwa analazimika kuizoea hali hiyo.

Miongoni mwa watu wa tabaka la kati uzinifu ulionekana kuwa ni mila halali. Machiavelli, na rafiki zake inaonekana hawakujisikia vibaya juu ya hadithi za kutokuwa kwao waaminifu ambapo walikuwa wakibadilishana wake. Ilikuwa mke naye akifuata nyendo za mumewe za kutokuwa mwaminifu, kwa kawaida alikuwa anaipuuzia tabia yake wala hakuona wivu wala kukereka.

Hii ndio hali ya maisha ya watu ambao wanaona kuwa mitala ni uhalifu usiosameheka wa watu wa Mashariki na wakati mwingine wamekuwa wakiilaumu hali ya hewa (tabia ya nchi) kwa kusababisha mila hii isiyokuwa ya kibinadamu. Lakini hali ya hewa ya huko kwao haiwaruhusu kutokuwa waaminifu kwa wake zao na kuvuka mipaka ya mke mmoja!

Pia inafaa ieleweke kuwa kutokuwepo kwa mitala ya halali miongoni mwa wazungu, iwe mizuri au mibaya, hakutokani na dini ya Kristo, ambaye kamwe hakuikataza. Kinyume chake, dini ya Kristo inazithibitisha kanuni za Agano la kale ambalo waziwazi linazitambua ndoa za mitala. Hivyo tunaweza kusema kuwa dini ya Kristo inaruhusu mitala na Wakristo wa kale walikuwa wakioa na kuolewa mitala. Hivyo kujiepusha kwa wazungu kisheria na mitala lazima kutakuwa kumetokana na sababu nyinginezo, sio dini.

Hedhi

Baadhi wanasema kuwa ndoa za mitala zimetokana na hedhi za mwanamke na mchoko anaoupata baada ya kuzaa na kutopenda kwake kufanya ngono wakati wa kunyonyesha.

Will Durant anasema kuwa katika jamii za kijima wanawake huzeeka haraka. Hiyo ndiyo sababu kwamba ili wawanyonyeshe watoto wao kwa muda mrefu na ili warefushe tofauti ya umri kati ya mtoto mmoja na mwingine bila kuziziba kiu za wanaume zao za kupata watoto, na ili kuwawezesha waume zao kukidhi hamu yao ya ngono huwahimiza waume zao kuoa mke mpya. Mara nyingi imeonekana kuwa mke wa kwanza, kwa nia ya kupunguza uzito wa majukumu yake, humshawishi mume wake kuoa mke wa pili ili apate watoto zaidi na mali zaidi.

Hapana shaka kwamba hedhi ya mwanamke na uchovu wake baada ya kuzaa, kijimai, huwaweka mwanaume na mwanamke katika nafasi tofauti.

Sababu hizi humfanya mwanaume amgeukie mwanamke mwingine, lakini hizi peke yake haziwezi kuwa sababu ya mitala isipokuwa tu kama kuna vikwazo vya kijamii na kimaadili vinavyozuia ngono holela, sababu hizo zinaweza kuwa na nguvu tu ikiwa mwanaume hayuko huru kufanya ngono holela.

Kikomo Cha Kipindi Cha Kuzaa Kwa Wanawake

Baadhi wanaamini kuwa kikomo cha kipindi cha kuzaa kwa wanawake ni moja ya sababu zilizoibua ndoa za mitala kwani inaweza kutokea kwamba mwanamke anafikia umri huu kabla hajazaa watoto wa kutosha. Inawezekana pia kwamba watoto wameshakufa.

Katika hali hizo, kama mume hataki kumtaliki mke wake wa kwanza na wakati huo huo anataka watoto zaidi, basi anakuwa hana namna isipokuwa kuongeza mke wa pili, au wakati fulani hata mke wa tatu. Halikadhalika utasa wa mke wa kwanza unaweza kuwa ni sababu ya mume kuoa mke wa pili.

Sababu Za Kiuchumi

Sababu za kiuchumi zimetajwa pia kuwa ni sababu ya mitala. Inasemekana kuwa katika zama za kale wake wengi na idadi kubwa ya watoto vilikuwa vinachukuliwa kuwa ni rasilimali ya kiuchumi. Alikuwa akiwatumikisha wake na watoto wake na wakati mwingine alikuwa akiwatendea kama watumwa. Wakati mwingine aliamua hata kuwauza. Wengi wa watumwa hawakutekwa vitani bali waliuzwa na baba zao.

Hii inaweza kuwa sababu ya mitala. Kwa sababu mwanaume anaweza kupata watoto tu kwa kumkubali mwanamke kuwa ni mke wake wa halali. Ngono holela haiwezi kufanikisha jambo hili. Hata hivyo hii sio sababu ya ndoa zote za mitala.

Baadhi ya jamii za kijima zilikuwa zikioa wake wengi zikiwa na wazo hili kichwani. Lakini si watu wote

walioa wake wengi kwa lengo hili. Katika zama za kale, mitala ilikuwa ni mila iliyozoeleka katika matabaka mbalimbali. Wafalme, wana wa wafalme, machifu, mitume na wafanya biashara walikuwa na wake wengi.

Kama tunavyojua, matabaka haya, kamwe hayakuwanyonya kiuchumi wake zao wala watoto wao.

Idadi Ya Wanafamilia

Kupenda idadi kubwa ya watoto na kupanuka kwa familia, kumekuwa ni moja ya sababu za mitala. Mitazamo ya mwanamke na mwanaume juu ya idadi ya watoto wanayoihitaji inaweza kutofautiana. Idadi ya watoto ambayo mwanamke anaweza kuzaa ni ndogo sana, awe na mume mmoja au waume wengi.

Lakini idadi ya watoto ambayo mwanaume anaweza kuzaa inategemeana na idadi ya wanawake alionao. Kinadharia inawezekana mwanaume akawa na maelfu ya watoto kwa kupitia mamia ya wanawake alionao. Tofauti na ulimwengu wa sasa, katika ulimwengu wa kale idadi ya wanafamilia iilikuwa inahesabika kuwa ni sifa muhimu ya kijamii. Makabila na koo zilifanya kila linalowezekana kuongeza idadi yao, ilikuwa ni fahari ya ukoo kuwa na kabila kubwa. Ni wazi kuwa ndoa za mitala ndio ilikuwa ni njia pekee ya kufikia lengo hili.

Uwingi Wa Wanawake

Sababu ya mwisho na muhimu zaidi ambayo ilichangia kuibuka kwa ndoa za mitala ni kuwa mara zote wanawake huwa ni wengi kuliko wanaume. Sio kwamba idadi ya wanawake wanaozaliwa ni kubwa kuliko ya wanaume. Ikitokea katika sehemu fulani wanawake zaidi wamezaliwa katika sehemu nyingine wanaume zaidi watazaliwa. Lakini bado idadi ya wanawake wanaofaa kuolewa ni kubwa kuliko idadi ya wanaume wanaofaa kuoa. Sababu ni kuwa idadi ya vifo vya wanaume mara zote imekuwa kubwa kuliko wanawake. Inawezekana kwamba ikiwa ndoa ya mke mmoja mume mmoja itazingatiwa kikamilifu, idadi kubwa ya wanawake itabaki bila waume wa halali, watoto wa ndani ya ndoa na maisha ya familia.

Hakuna shaka kwamba kwa uchache hii ndio ilikuwa hali ya mambo katika jamii za kijima. Tayari tumeshanukuu maoni ya Will Durant anayesema kuwa katika jamii za kijima, uhai wa mwanaume mara zote ulikuwa hatarini kwa sababu mara zote alikuwa akishughulika katika kuwinda na kupigana na hii ndio sababu kwamba idadi ya vifo vya wanaume ilikuwa kubwa kuliko wanawake. Kwa kadri idadi ya wanawake ilivyozidi kuongezeka, kulikuwa na mambo mawili tu ya kuchagua ama kuruhusu mitala au kuilazimisha idadi kubwa ya wanawake kuishi maisha yao yote bila kuolewa.

Hitimisho

Hapo juu tumejadili sababu zote ambazo zinaweza kudhaniwa kuwa ndio chanzo cha mitala. Kama ambavyo tumeona, baadhi ya sababu hizi kama vile tabia ya nchi (hali ya hewa) ilivyo sio sababu halisi. Hivyo tunazipuuza. Sababu nyingine zinaweza kuwa zile zenye nguvu ya kumshawishi mwanaume kuoa wake wengi lakini hazitoi uhalali juu ya kitendo chake. Zina sura ya ukandamizaji, ubabe na ukatili. Sababu za kiuchumi zinaingia katika kundi hili.

Ni dhahiri kuwa uuzaji wa watoto ni moja ya vitendo vya kikatili na kishenzi kabisa. Kuamua kuoa wake wengi kwa ajili ya lengo hili ni haramu kama kitendo chenyewe kilivyo haramu.

Kundi la pili linajumuisha sababu ambazo zinaweza kuonekana kuwa ni sababu thabiti kwa upande wa mume au jamii. Ugumba wa mke wa kwanza, kufikia kikomo cha uzazi wakati bado mume anahitaji watoto au kama kabila au taifa linahitaji idadi kubwa ya watu. Kama kanuni ya jumla, sababu zote ambazo zinatokana na kutofautiana kati ya mume na mke kuwiana na mahitaji ya jimai na nguvu ya uzazi, zina uthabiti.

Kundi la tatu linajumuisha sababu ambazo kama ikikubaliwa kuwa zilikuwepo au bado zipo, sio tu kwamba huruhusu mitala bali pia huzifanya kuwa ni wajibu. Katika hali hii, mitala ni haki ya mwanamke ambayo mwanaume na jamii wanapaswa kuitoa. Sababu hii ni uwingi wa wanawake kuwazidi wanaume, ikiwa idadi ya wanawake wanaopaswa kuolewa ni kubwa kuliko idadi ya wanaume wanaofaa kuoa, mitala huwa ni wajibu wa wanaume na haki ya mwanamke, kwani ikiwa itaamuriwa kuwa mume mmoja akae na mke mmoja tu, idadi fulani ya wanawake itakuwa imenyimwa haki ya kuishi maisha ya kifamilia.

Haki ya ndoa ni haki ya msingi ya binadamu na hakuna anayepaswa kunyimwa haki hii kwa kisingizio chochote. Jamii haiwezi ikachukua hatua yoyote ambayo inaweza ikawanyima baadhi ya watu haki hii.

Haki ya ndoa ni haki ya asili kama ilivyo kwa haki ya uhuru, haki ya kufanya kazi na haki ya kupata chakula, malazi na elimu. Hivyo, sheria ya kuwa na mke mmoja inapingana na haki za binadamu pindi inapokuwa wanawake wanaopaswa kuolewa ni wengi kuliko wanaume wanaofaa kuoa.

Kwa uchache, hii ndiyo imekuwa ni hali ya mambo huko nyuma. Katika sura zifuatayo tutaangalia ikiwa bado kuna mazingira ambayo sio tu kwamba yanahalalisha mitala bali pia yanaijenga haki hii kwa ajili ya mwanamke. Na kama mazingira haya bado yapo, sasa ni nini nafasi ya haki hii dhidi ya haki ya mke wa kwanza.

Haki Ya Mwanamke Katika Ndoa Ya Wake Wengi

Tumeshaelezea sababu za kushindwa kwa ndoa za mke mmoja kuwa na waume wengi na kufanikiwa kwa mitala na tumeelezea sababu mbalimbali zilizosababisha kuibuka kwa mitala. Baadhi ya sababu

zilitokana na moyo wa ukandamizaji na ubabe wa mwanaume na nyingine zilitokana na kutofautiana kwa mwanamke na mwanaume kuhusiana na kudumu kwa uwezo wao wa kuzaa na idadi ya watoto ambayo kila mmoja wao anaweza kuzaa. Hizi sababu za pili zinaweza kuchukuliwa kuwa ni sababu thabiti za mitala. Lakini sababu yake kuu katika kipindi chote cha historia imekuwa ni idadi ya wanawake inayozidi ya wanaume wanaofaa kuolewa na kuoa sawia. Sababu hii husababisha kuzaliwa kwa haki ya mwanamke na jukumu la mwanaume.

Ili kuepuka mjadala mrefu, tunaziruka sababu hizi ambazo zinaweza kuchukuliwa kuwa ni uhalalishaji tu wa mitala, na kushughulikia tu sababu yake kubwa, ambayo kama ikiwepo hubadilika kuwa haki ya jinsia dhaifu.

Ili kuthibitisha hili, nukta mbili za utangulizi zinapaswa kuwekwa sawa. Kwanza ni kuthibitisha kuwa kwa mujibu wa takwimu za kuaminika, idadi ya wanawake wanaopwaswa kuolewa ni kubwa kuliko idadi ya wanaume wanaofaa kuoa. Nukta ya pili tunayotaka kuithibitisha ni kuwepo kwa mazingira halisi yanayounda wajibu kwa wanaume waliooa na wanawake walioolewa juu ya wanawake walionyimwa haki ya kuwa na ndoa. Kuhusiana na nukta ya kwanza, kwa bahati nzuri takwimu zote thabiti zipo duniani. Sensa huchukuliwa katika kila nchi katika kila baada ya muda fulani. Katika nchi zilizoendelea, sio tu kwamba idadi wa wanaume na wanawake hukusanywa bali pia idadi ya wanaume na wanawake katika umri mbalimbali huonyeshwa. Takwimu hizi huchapishwa na Umoja wa Mataifa katika ripoti zake za kila mwaka juu ya idadi ya watu.1

Inaweza kuonyeshwa kwamba kwa madhumuni yetu, haitoshelezi kujua idadi ya wanaume na wanawake katika kila nchi, tunahitaji pia kujua uwiano wa idadi ya wanaume na wanawake wanaofaa kuoa na kuolewa sawia. Mara nyingi uwiano huu unatofautiana na uwiano wa jumla wa wanaume na wanawake. Kuna sababu mbili za tofauti hii. Moja ni kuwa wanawake hupevuka mapema zaidi. Hii ndio sababu katika nchi zilizo nyingi umri unaoruhusiwa wasichana kuolewa upo chini kuliko umri wa wavulana wanaoruhusiwa kuoa. Kwa wastani, umri wa mume huwa ni miaka mitano zaidi kuliko mkewe.

Sababu nyingine na muhimu zaidi ni kuwa idadi ya vifo vya wavulana ni kubwa kuliko wasichana, na matokeo yake ni kuwa katika umri wao wa ndoa, wasichana huwa ni wengi kuliko wavulana. Wakati fulani tofauti huwa kubwa. Inaweza kutokea kuwa idadi ya wanaume na wanawake katika nchi inalingana au hata wanaume wakawa wengi kuliko wanawake, lakini bado idadi ya wasichana wanaofaa kuolewa ikawa kubwa kuliko idadi ya wavulana wanaoweza kuoa, tena kwa idadi kubwa.

Ripoti ya Umoja wa Mataifa ya Uwingi wa watu kwa mwaka 1964, inashuhudia ukweli huu.

Kwa mfano, kwa mujibu wa ripoti hii, jumla ya watu katika Jamhuri ya Korea ni 26,277,635. Kati ya hawa wanaume ni 13,145,289 na 13,132,326 ni wanawake. Hivyo idadi ya wanaume ni zaidi ya wanawake kwa 12,943. Uwiano huu unabaki hivi katika umri wa miaka 14, 59, 1214 na 1519.

Takwimu zinaonyesha kuwa katika makundi yote haya ya umri idadi ya wanaume ni kubwa kuliko ya wanawake. Lakini katika kundi la umri la miaka,2024, uwiano unabadilika. Katika kundi hili la umri idadi

ya wanaume ni 1,083,364, na idadi ya wanawake ni 1,110,051. Katika makundi yote ya umri wa juu, ambayo ni makundi ya wanayoweza kuoa na kuolewa idadi ya wanawake ni kubwa zaidi.

Hata hivyo, Jamhuri ya Korea ni mfano wa pekee ambapo idadi ya wanaume ni kubwa kuliko idadi ya wanawake. Takribani, katika nchi nyingine zote, sio tu kwamba idadi ya wanawake wanaofaa kuolewa ni kubwa kuliko ya wanaume, bali hata katika idadi ya jumla, wanawake ni wengi kuliiko wanaume. Kwa mfano idadi ya watu nchini Urusi ni 216,101,000 na wanawake ni 118,261,000, na tofauti hii inaendelea katika makundi yote ya umri, yale ambayo hayajafikia umri wa kuingia katika ndoa na yale yaliyofikia umri huo, hii ni kuanzia 2024, 2529, 3034 na hata 8084.

Hali iko hivi hivi katika nchi nyingine pia kama vile Uingereza, Ufaransa, Ujerumani ya Magharibi, Ujerumani wa Mashariki, Czechoslavakia, Poland, Romania, Hungary, Marekani, Japan n.k. Katika baadhi ya sehemu kama vile Berlin Magharibi na Berlin Mashariki, tofauti ya idadi kati ya wanaume na wanawake ni kubwa mno.

Nchini India, katika makundi ya umri ambapo watu wanaweza kuingia katika ndoa, idadi ya wanaume ni kubwa kuliko ya wanawake. Idadi ya wanawake ni kubwa tu kuanzia katika umri wa miaka 50 na kuendelea. Inavyoonekana uchache wa wanawake unatokana na ukweli kwamba watu wengi nchini India hawapendi kutaja majina ya wake zao vijana au binti zao wadogo, wakati wa sensa.

Kwa mujibu wa takwimu za sensa iliyopita, Iran ni moja ya nchi ya pekee ambapo, idadi ya wanawake inaizidi ile ya wanaume.

Inashangaza kwamba baadhi ya wakosoaji wanasisitiza kuwa sheria inayoruhusu mitala ipigwe marufuku angalau katika nchi ambazo idadi ya wanaume ni kubwa kuliko ya wanawake. Katika hatua ya kwanza, sheria hii ni ya wote, sio ya nchi maalumu. Pili, haitoshi kujua uwiano wa wanaume na wanawake peke yake. Tumeona kuwa katika Jamhuri ya Korea, idadi ya wanaume ni kubwa kuliko ya wanawake, lakini idadi ya wanawake wanaofaa kuolewa ikawa kubwa kuliko idadi ya wanaume wanofaa kuoa. Aidha, takwimu za sensa, sio za kuaminika sana katika nchi zilizo nyingi. Kwa mfano, tunajua kuwa ingawa mitala ni mila iliyozoeleka nchini Iran, mijini na vijijini, lakini haijawahi kutokea upungufu wa mabibi harusi watarajiwa. Ukweli huu peke yake unaongea vizuri zaidi kuliko takwimu za sensa.

Ashley Montaque, katika kitabu chake, *“Woman The Superior Sex”,* anakiri kwamba duniani kote, idadi ya wanawake wanaofaa kuolewa ni kubwa kuliko ile ya wanaume wanaofaa kuoa.

Takwimu za mwaka 1950, zinaonyesha kuwa idadi ya wanawake waliofikia umri wa kuolewa nchini Marekani inaizidi ile ya wanume takriban kwa 1,430,000.

Bertrand Russel katika kitabu chake, *“Marriage and Morality”,* anasema kwamba katika Uingereza ya leo, wanawake wanazidi idadi ya wanaume kwa zaidi ya milioni mbili. Kwa mujibu wa mila yao, wanapaswa wabakie bila kupata watoto, jambo ambalo ni dhulma kubwa kwa upande wao.

Miaka kadhaa iliyopita, ilitangazwa kwenye vyombo vya habari kwamba, kufuatia shinikizo kubwa la wanawake wa Kijerumani ambao hawakuweza kupata waume na maisha ya kifamilia, kufuatia vifo vingi vya wanaume katika vita vya Pili vya Dunia, serikali ya Ujerumani imekiomba chuo kikuu cha AlAzhar kiipatie mwongozo wa mitala. Baadaye ilifahamika kuwa kufuatia upinzani mkali wa kanisa, pendekezo hilo ilibidi liachwe. Kanisa liliona bora wanawake wakae bila kuolewa wala kuzaa wala kuishi maisha ya kifamilia, na ni bora uzinifu na ufuska kuliko kuukubali mfumo wa wanaume kuoa mke zaidi ya mmoja. Kwa vile tu mfumo huu ni wa Mashariki na wa Kiislamu.

Kwa Nini Kuna Wanawake Wengi Wa Umri Wa Ndoa Kuliko Wanaume?

Ingawa idadi ya wasichana wanaozaliwa sio kubwa kuliko ile ya wavulana, lakini bado kuna idadi kubwa ya wanawake wengi wa umri wa kuolewa kuliko idadi ya wanaume. Sababu iko wazi. Kiasi cha vifo vya wanaume ni kikubwa. Vifo hutokea katika kipindi ambapo mwanamume alipaswa kwa kawaida kuwa mkuu wa familia. Tukizingatia vifo vinavyotokea katika ajali, vita, kufa majini, kuanguka, kugongana kwa magari n.k. tutakuta kwamba wengi wa waathirika ni wanaume.

Ni mara chache sana kukutwa kwamba mwanamke ni moja wa waathirika. Iwe ni migongano (ajali) kati ya wanaadamu au kati ya mwanadamu na maumbile, wengi wa waathirika huwa ni wanaume watu wazima. Ili kujua kwa nini idadi ya wanawake wanaopaswa kuolewa ni kubwa kuliko idadi ya wanaume wanaofaa kuoa, inatosha kufahamu kuwa tokea mwanzo wa historia ya mwanadamu hakuna hata siku moja ambayo imewahi kupita bila kupigana vita na wanaume kupoteza uhai.

Vifo vinavyotokea kutokana na vita katika hizi zama za viwanda ni vingi mara mia kuliko vile vilivyokuwa vinatokea katika zama za uwindaji na zama za kilimo. Katika vita vya Pili vya Dunia, idadi ya vifo vilivyotokea inafikia milioni saba. Utakubaliana na sisi ukihesabu vifo vinavyotokea katika vita vya kimkoa huko Mashariki ya Mbali, Mashariki ya Kati na Afrika katika miongo miwili iliyopita.

Will Durant anasema kwamba sababu nyingi zimechangia kudondoka kwa mila hii ya mitala. Maisha thabiti ya kilimo yamepunguza ugumu na hatari za maisha ya wanaume, ambapo matokeo yake ni kuwa idadi za wanawake na wanume zinakaribia kulingana.

Anachosema Will Durant kinashangaza sana. Kama ingekuwa kupotea kwa maisha ya watu kunatokana na mapambano ya wanaume dhidi ya muambile tu, kungekuwa kuna tofauti kati ya zama za uwindaji na zama za kilimo. Lakini kadri muda unavyokwenda, vita vimeendelea kuchukua idadi kubwa zaidi ya uhai wa wanaume na idadi ya vifo vinavyotokana na vita haijapata kupungua katika zama zozote. Pia sababu kubwa kwa nini wanawake hawajakumbwa na ajali nyingi ni kwamba wakati wote wanaume wamekuwa wakiwalinda, na wao wanaume ndio wamekuwa wakifanya kazi za hatari zaidi. Hivyo kama ilivyokuwa katika zama za uwindaji, uwiano usio sawa wa idadi ya wanaume na wanawake umeendelea pia katika zama za kilimo.

Will Durant hajasema lolote juu ya zama za viwanda, ingawa hiki ndio kipindi ambacho kimeshuhudia mauaji makubwa zaidi ya wanaume na kipindi ambacho uwiano kati ya idadi ya wanaume na wanawake umepishana mno.

Mwanamke Ana Uwezo Zaidi Wa Kujikinga Dhidi Ya Maradhi.

Imegunduliwa hivi karibuni kuwa mwanaume ana uwezo mdogo zaidi wa kujikinga dhidi ya maradhi kuliko wanawake. Hii ni sababu nyingine kwa nini idadi ya vifo vya wanaume ni kubwa zaidi.

Miaka kadha iliyopita, Tume ya Takwimu ya Ufaransa iliripoti kuwa nchini Ufaransa, wavulana 105 huzaliwa dhidi ya wasichana 100 lakini cha ajabu idadi ya wanawake ilikuwa ni kubwa kuliko wanaume kwa 1,758,000 (milioni moja na laki saba na elfu hamsini na nane). Inaaminika kwamba tofauti hii inatokana na uwezo mkubwa wa mwanamke wa kujilinda dhidi ya magonjwa.

Si muda mrefu umepita, makala moja ilichapishwa kwenye jaria la UNESCO liitwalo *Courier*. Kwa mujibu wa makala hii, mwanamke ana uwezo mkubwa zaidi wa akili kuliko mwanamume. Wastani wa kinga yake ni kubwa zaidi. Kwa kawaida, ana afya nzuri zaidi kuliko mwanaume na ana uwezo zaidi wa kustahamili maradhi. Hupona haraka kuliko mwanaume. Katika kila mwanamke mmoja mwenye kigugumizi, kuna wanaume watano wenye kigugumizi.

Katika kila mwanamke mmoja asiyeweza kutofautisha rangi, kuna wanaume kumi na sita wasioweza kutofautisha rangi. Na kwa kawaida ni ugonjwa wa wanaume tu. Wanawake wana mfumo bora zaidi wa kinga ya ajali. Wakati wa vita vya Pili vya Dunia ilithibitika kuwa katika mazingira ya aina moja, mwanamke alikuwa na uwezo zaidi wa kustahamili ugumu wa vizuizi, magereza, na kambi za wafungwa wa vita kuliko wanaume. Takribani katika nchi zote, idadi ya kesi za wanaume kujinyonga ni kubwa mara tatu zaidi kuliko wanawake.

Ashley Montague ameitaja nadharia yake ya uwezo mkubwa zaidi wa mwanamke kustahamili maradhi, katika kitabu chake kiitwacho, *“Woman, the Superior Sex.”*

Ikiwa siku moja itatokea mwanaume ataamua kumpeleka mwanamke katika kazi za hatari na za kifo au kama atamsukumia katika uwanja wa vita kukabiliana na bunduki na mabomu, bado idadi ya wanawake itaendelea kuwa kubwa kwa sababu yeye ana uwezo zaidi wa kustahamili maradhi.

Haya tuliyoyasema yanahusiana tu na uwingi wa wanawake wanaofaa kuolewa dhidi ya wanaume wanaofaa kuoa. Tunajua kwamba uwingi huu ni ukweli halisi. Pia tunajua sababu zake. Na sababu zake, zile zilizokuwepo tokea mwanzo wa historia ya mwanadamu bado zipo mpaka sasa.

---

1. Tunayo mbele yetu ripoti ya 1964, iliyochapishwa tena 1965

Haki Ya Mwanamke Katika Mitala

Nukta ya pili ni kuwa uwingi wa idadi ya wanawake wanaofaa kuolewa sio tu kwamba hufanya haki kwa ajili yao, bali pia na wajibu kwa ajili ya mwanaume na mwanamke aliyeolewa.

Hapana shaka kwamba ndoa ni moja ya haki za asili na ni moja ya haki za msingi za binadamu. Kila mtu awe mwanaume au mwanamke, ana haki ya kuishi maisha ya familia na kupata watoto. Haki hii ni sawa na haki ya kufanya kazi, kuwa na nyumba, kupata elimu na huduma za afya na haki ya kufurahia uhuru na usalama.

Ni jukumu la jamii kuhakikisha kwamba hakuna kizuizi kinachowekwa katika upatikanaji wa haki ya asili na ya msingi ya binadamu. Badala yake, jamii inapaswa kutoa ushirikiano wa kutosha katika kufanikisha lengo hili.

Ni maoni yetu kuwa moja ya dosari kubwa za Amizio la Haki za Binadamu kwa wote ni kutoipa umuhimu wowote haki hii. Azimio limeitambua haki ya uhuru na usalama, haki ya kupata huduma bora za kimahakama, haki ya kuwa na uraia na kuubadili, haki ya kuoa au kuolewa bila vipingamizi vya rangi au dini, haki ya kumiliki mali, haki ya kukusanyika na haki ya kupumzika na kupumbaa, lakini azimio hili halijaitaja haki ya mtu kuishi maisha ya ndoa halali.

Kwa mwanamke, haki hii ni yenye umuhimu mkubwa sana, kwani anayahitaji maisha ya kifamilia zaidi kuliko mwanaume. Kwa mwanaume kilicho muhimu zaidi, katika ndoa ni ngono na kwa mwanamke kilicho muhimu zaidi ni hisia za moyoni na roho. Kama mwanaume hana familia, angalau anaweza kukidhi sehemu ya mahitaji yake kwa kujiingiza katika ngono holela na ufuska. Lakini kwa mwanamke, familia ina umuhimu mkubwa zaidi. Ufuska hauwezi kukidhi japo sehemu tu ya mahitaji yake ya kimwili na kimhemko (hisia ya moyoni).

Kwa mwanaume, haki ya kuwa na familia ina maana kukidhi tamaa zake za ngono, haki ya kuwa na mwenzi maishani na haki ya kuwa na watoto halali. Lakini kwa mwanamke, ndoa inamaanisha pia kuwa na mlinzi na mwangalizi na ambaye anaweza kumpa msaada wa kimaadili.

Baada ya kuzielezea nukta hizi mbili, kwamba kwanza idadi ya wanawake wanaofaa kuolewa ni wengi kuliko idadi ya wanaume wanaofaa kuoa, na pili kwamba ni haki ya asili ya binadamu kuwa na familia, ni rahisi kutoa hitimisho kwamba ikiwa ndoa ya mume kuwa na mke mmoja itafanywa kuwa ndio ndoa pekee iliyo halali, idadi kubwa ya wanawake itakuwa katika hatari ya kunyimwa haki yao ya asili, na hivyo ni ndoa za mitala tu ndio zinaweza kuwarejeshea wanawake hao haki hii iliyo hatarini.

Ni jukumu la wanawake wa Kiislamu, kwamba kama njia ya kutetea haki za wanawake, waitake na kuishinikiza tume ya Umoja wa Mataifa ya Haki za Binadamu kuutambua rasmi mfumo wa ndoa za Kiislamu wa kuwa na wake wengi kama haki ya binadamu, na hii itakuwa ni neema kubwa kwa

mwanamke na maadili. Ukweli kwamba kanuni hii imetoka Mashariki na nchi za Magharibi zinapaswa kufuata usionekane kuwa ni dhambi.

Nadharia Ya Russel

Kama ilivyoonyeshwa hapo awali, Bertrand Russel alikuwa anaufahamu ukweli kwamba ndoa za kuoa mke mmoja kufanywa kuwa ndio ndoa pekee zilizo halali kungewanyima wanawake wengi haki ya kuolewa. Amependekeza suluhisho rahisi sana la tatizo hili. Alitaka wanawake waruhusiwe kuwashawishi wanaume na kuzaa watoto wasio na baba. Kama ambavyo baba huwa anasaidia katika matunzo ya watoto, serikali inapaswa kuchukua nafasi ya baba na watoe ruzuku kwa wanawake ambao hawajaolewa.

Russell anasema kwamba hivi sasa nchini Uingereza kuna zaidi ya wanawake milioni mbili waliozidi idadi ya wanaume ambao kamwe hawatarajii kuolewa na kupata watoto kutokana na sheria iliyopo inayotaka mwanaume awe na mke mmoja tu. Hii ni dhulma kubwa. Anasema kwamba mfumo wa mume mmoja mke mmoja umejengwa juu dhana kwamba idadi ya wanaume inalingana na idadi ya wanawake, lakini pindi idadi hizi hazilingani, hawa wanawake waliozidi huwa hatarini kubakia bila kuolewa katika umri wao wote. Aidha, ikitokea haja ya kuongeza, idadi ya watu, aina hii ya ndoa sio tu kwamba haina maslahi na umma, achilia mbali maslahi ya mtu mmoja mmoja.

Hili ni suluhisho la tatizo hili la kijamii, kama lilivyopendekezwa na mwanafalsafa mkubwa wa karne ya 20. Lakini kwa mujibu wa Uislamu, tatizo lote hutatuliwa ikiwa idadi ya kutosha ya wanaume wenye uwezo wa kifedha, wa kimaadili na kimwili watakubali kuoa mke zaidi ya mmoja na kuwatendea uadilifu na kutoonyesha upendeleo baina ya watoto wa wake hawa wawili. Mke wa kwanza anapaswa kumpokea na kumkubali kwa ukunjufu mke wa pili kwa nia na lengo la kutekeleza jukumu la kijamii ambalo ni muhimu sana na ni namna bora ya maadili.

Kinyume na kifra za Uislamu, mwanafalsafa huyu anawashauri wanawake walionyimwa haki ya kuolewa, wawaibe waume wa wanawake wengine na anatoa wito kwa serikali kuwasaidia na kuwatunza watoto hawa waliozaliwa katika mahusiano haramu.

Inaonekana kwamba mwanafalsafa huyu wa karne ya 20 anadhani kuwa mwanamke anahitaji ndoa kwa sababu tatu: kukidhi tamaa zake za ngono, kupata watoto na kukidhi mahitaji yake ya kiuchumi. Haja mbili za mwanzo zinaweza kukidhiwa kwa ulaghai na haja ya tatu itekelezwe na serikali. Anasahau kwamba mwanamke ana haja za hisia za moyoni pia. Anataka awe chini ya uangalizi wa mume anayempenda na kwamba mkataba wake na mwanaume huyo usiwe ni wa kingono peke yake.

Nukta nyingine ambayo mwanafalsafa huyu hajaipa umuhimu ni hadhi ya watoto waliozaliwa katika mahusiano haramu. Kila mtoto huhitaji wazazi wanaoeleweka vizuri na upendo wao wa dhati. Uzoefu unaonyesha kuwa mara nyingi mwanamke huwa haonyeshi upendo kwa mtoto wake ambaye baba yake hajulikani. Ni vipi ukosefu wa upendo huu unaweza kufidiwa? Je serikali inaweza kufanya chochote

katika hili?

Bertrand Russell anasikitika kwamba wanawake wengi watabaki bila watoto mpaka pendekezo lake lipewe sura ya kisheria. Lakini anapaswa kujua kuwa wanawake wa kiingereza hawawezi wakasubiri sheria yoyote. Wao wenyewe tayari wameshatatua tatizo hili, wanaiba waume za watu na wanapata watoto wasio na baba.

Katika ripoti ya mwaka ya 1958, iliyoandaliwa na Dr. Z.A. Scott, Mkuu wa Idara ya Utabibu ya Halmashauri ya London, ilionekana kwamba katika watoto kumi waliozaliwa mwaka uliopita, mtoto mmoja ni wa nje ya ndoa. Ripoti hiyo pia ilisema kuwa idadi ya watoto wanaozaliwa nje ya ndoa inazidi kuongezeka. Idadi ya watoto waliozaliwa nje ya ndoa ilipaa kutoka watoto 33,838 mwaka 1957 hadi 54,433 katika mwaka uliofuata.

Inaonekana kwamba Waingereza wameamua kutatua tatizo lao bila kuwa na haja ya kusubiri kupitishwa kwa pendekezo la Bertrand Russell kuwa sheria.

Mitala Yakatazwa, Liwati Yaruhusiwa

Serikali ya Uingereza, badala ya kuufanyia kazi ushauri wa Russell na kutatua tatizo la wanawake ambao hawajaolewa, imechukua hatua katika mwelekeo kinyume na huu. Imezidi kumnyima zaidi mwanamke haki ya kuwa na mume kwa kuhalalisha liwati. Kwa sasa mitala hairuhusiwi nchini Uingereza lakini liwati (ya wanaume kwa wanaume) inaruhusiwa. Mbele ya macho ya Waingereza sio jambo la ubinadamu kuwa na mke wa pili.

Lakini ikitokea kuwa “mke” wa pili ni mwanaume, basi hapo inakuwa sio tatizo. Wanaiona liwati kuwa ni kitendo kitukufu kinachoafikiana na mahitaji ya karne ya 20. Kwa mujibu wa sheria ya mamlaka ya Uingereza, kuwa na wake wengi hakukatazwi ili mradi tu wake watakaoolewa baada ya mke wa kwanza wawe na ndevu (yaani wanaume). Inasemekana kwamba nchi za kimagharibi zimetatua matatizo ya masuala ya ndoa na familia, na kwamba sisi tunapaswa kuiga mfano wao.

Kitendo hiki cha kimagharibi hahishangazi kwani ni matokeo ya mantiki ya jinsi nchi za kimagharibi zinavyokwenda.

Kinachoshangaza ni kwamba watu wetu, hasa vijana wasomi, wamepoteza uwezo wao wa kufikiri kwa uhuru na kuchambua mambo. Wamepoteza haiba zao. Wanawaamini wamagharibi kirahisi mno. Kama wana almasi mikononi mwao na watu kutoka upande mwingine wa dunia wakisema kuwa hiyo sio almasi ni ubao wa fomaika basi huitupa almasi yao. Lakini wakiona ubao wa fomaika mikononi mwa mgeni na wakiambiwa kuwa hiyo ni almasi, wao huamini kirahisi kabisa.

Je Mwanaume Ana Asili Yakuoa Wake Wengi?

Utashangaa ukiambiwa kuwa wanasaikolojia na wanafalsafa wa huko Magharibi wanaamini kuwa mwanaume ni mwenye asili ya kuoa wake wengi na kwamba ndoa za mke mmoja ni kinyume cha maumbile yake.

Will Durant, akielezea vurugu za kimaadili leo, anasema kuwa sehemu kubwa ya matatizo haya ya kimaadili yanatokana na hamu isiyotibika ya kupenda kuwa na wanawake wa aina mbalimbali. Mwanume kwa asili, hawezi kuridhika na mke mmoja.

Anasema kwamba kwa asili mwanaume hupenda kuwa na wake wengi. Ni vikwazo vikali tu vya kimaadili, kiasi cha kutosha cha umasikini na ukakamavu wa mke wa kwanza ndio vinaweza kumlazimisha kubaki na mke mmoja.

Profesa wa Kijerumani, Schmidt, anasema kuwa katika kipindi chote cha historia, mwanaume amekuwa sio mwaminifu kwa mkewe. Kuna viashirio kuwa hata katika zama za kati, vijana wa kiume walikuwa wakibadili wapenzi wao kila mara, na nusu ya wanaume walioowa hawakuwa waaminifu kwa wake zao.

Robert Kinsey katika ripoti yake inayojulikana kama ‘Ripoti ya Kinsey’, anasema kwamba wanaume na wanawake wa Kimarekani wanawazidi watu wa mataifa mengine yote kwa kutokuwa waaminifu katika ndoa. Katika sehemu nyingine ya ripoti anasema kwamba, tofauti na mwanaume, mwanamke huwa hapendi kubadili wanaume na ndio maana mara nyingi huwa anakataa ofa za wanaume wa nje, lakini mwanamume huona kubadili wanawake kama kujifunza mambo mapya.

Kilicho muhimu zaidi kwa mwanaume ni kufurahia ngono kuliko hisia za moyoni na kiroho. Mwanaume hujifanya kuwa ana hisia za moyoni na za kiroho kabla tu hajapata ngono. Daktari mashuhuri alimwambia Kinsey kuwa ni dhahiri kuwa mwanaume ni mwenye asili ya kuwa na wanawake wengi wakati mwanamke ni mwenye asili ya kuwa na mume mmoja, kwa sababu mamilioni ya manii (mbegu za kiume) hutengenezwa kwa mwanaume wakati kwa mwanamke ni yai moja tu ambalo huzalishwa katika mwezi mzima. Mbali na nadharia ya Kinsey, itakuwa si vibaya kama tutajiuliza sisi wenyewe kama ni vigumu kwa mwanaume kuwa mwaminifu au la.

Mwanasosholojia wa Kifaransa akijibu swali hili anasema kuwa mwanaume kuwa mwaminifu katika ndoa sio tu kwamba ni vigumu bali haiwezekani kabisa. Mwanamke mmoja huzaliwa kwa ajili ya mwanaume mmoja, lakini mwanaume mmoja huzaliwa kwa ajili ya wanawake wote. Mwanaume akiwa sio mwaminifu na akimsaliti mke wake, asilaumiwe. Ni kosa la maumbile, ambayo yamemuwekea nguvu zote hizi za kutokuwa mwaminifu ndani yake.

Gazeti moja la Kifaransa lenye kichwa cha habari “Mwenendo wa Mapenzi na Ndoa wa Kifaransa”, limeandika kuwa wanandoa wa Kifaransa wameshatatua tatizo hili. Wanajua kanuni za mchezo huo. Ilimradi mwanaume havuki mipaka, mahusiano yake ya mara moja moja na wanawake wengine sio

tatizo. Kama kanuni, mwanaume hawezi akaendelea kuwa mwaminifu kwa mke wake baada ya miaka miwili ya ndoa yake. Kwa kiasi fulani hali ni tofauti kwa wanawake na ni bahati kwamba wao pia wanajua tofauti hii. Nchini Ufaransa, mke huwa haoni kuwa ametendewa ubaya kama mume wake amezini.

Hujifariji kwa kusema kwamba anaweza kuwa ameupeleka mwili wake kwa mwanamke mwingine lakini roho na hisia zake za moyoni zinaendelea kuwa zake (huyu mke mwenye mume).

Miaka kadhaa iliyopita kulikuwa ubishani juu ya maoni yaliyotolewa na mwanabailojia aitwaye Dr. Russel Lee. Alikuwa na maoni kwamba kitendo cha mwanaume kuridhika na mke mmoja hudhoofisha uzao wake hivyo kitendo hiki huwa ni uhalifu dhidi ya ubinadamu. Alifikiri kwamba mfumo wa yeye kuwa na wake wengi ulikuwa unawafanya watoto wake kuwa na afya na nguvu.

Tunaamini kwamba maelezo haya yaliyotolewa juu ya maumbile ya mwanadamu sio sahihi hata kidogo. Wasomi hawa wanaonekana kuwa wamehamasishwa na hali ya mazingira ya kimaadili katika sehemu yao ya dunia.

Hata hivyo, tunaamini kwamba kibaiolojia na kisaikolojia mwanamke na mwananume wanatofautiana na maumbile yamewafanya hivyo kwa makusudi na kwa malengo maalumu. Hivyo usawa wa haki zao usitumike kama kisingizio cha kuzifanya haki zao kuwa sawiya. Hata kwa maoni ya wale wanaounga mkono ndoa za mke mmoja, wanakiri kuwa tabia ya kisaikolojia ya mwanaume ni tofauti na ya mwanamke. Kwa asili mwanamke anapaswa kuolewa na mume mmoja tu. Yeye kuolewa na waume wengi ni kinyume na asili yake na hakuafikiani na matarajio yake kwa mumewe. Lakini mwanaume sio mwenye asili ya kuwa na mke mmoja, kwa maana kwamba kwake kuwa na wake wengi sio kinyume na tabia yake pamoja na matarajio yake kwa mkewe.

Lakini hatukubaliani na maoni kuwa ndoa za mke mmoja haziafikiani na asili ya mwanaume. Sio sahihi kabisa kusema kwamba tabia ya mwanaume ya kupenda kubadili wanawake haitibiki. Pia hatuamini kuwa mwanaume hawezi kuwa mwaminifu, au kwamba mwanamke mmoja ni wa mwanume mmoja lakini mwanaume mmoja ni wa wanawake wote.

Kwa imani yetu, sababu za kutokuwa mwaminifu kwa mwanaume zinahusiana na mazingira ya kijamii na sio maumbile ya mwanaume. Mambo yaanayosababisha kutokuwa mwaminifu yanatokana na mazingira ambayo yanamhimiza mwanamke atumie aina zote za visahwishi ili kumvuta na kumpotosha mwanaume, kwa upande mmoja na kwa upande wa pili sheria ya kuoa mke mmoja tu huwanyima mamilioni ya wanawake fursa ya kuolewa.

Katika ulimwengu wa Kiislamu, kabla ya kuja kwa mila na tabia za kimagharibi, 90% ya wanaume walikuwa wanakaa na mke mmoja tu. Hawakuwa na mke zaidi ya mmoja wala hawakuwa wakijiingiza katika uzinifu na ufuska.

Mitala Kama Njia Ya Kuokoa Ndoa Ya Mke Mmoja

Utashangaa tukisema kuwa mitala ni kipengele muhimu sana kilichohudumia ndoa za mke mmoja katika nchi za Mashariki. Uhalali wake kwa hakika ni kipengele kikubwa mno cha kuokoa, pale ambapo idadi ya wanawake wanaopaswa kuolewa inakuwa kubwa kuliko ya wanaume wanaofaa kuoa, kwa sababu kama haki ya kuolewa ya wanawake waliozidi haitatambuliwa na kama wanaume wenye maadili, uwezo wa fedha na afya njema hawataruhusiwa kuwa na mke zaidi ya moja, ngono holela na vimada lazima itajikitia mizizi, na hivyo kuharibu msingi halisi wa ndoa ya mke mmoja.

Katika ulimwengu wa Kiislamu wa Mashariki, mitala ilikuwa inaruhusiwa kwa upande mmoja na kwa upande wa pili vishawishi vya vitendo visivyo vya maadili mema havikuwepo. Kwa hiyo, ndoa halisi za mke mmoja zilistawi na kushitadi katika familia zilizo nyingi. Tabia ya kuwa na vimada kamwe haikupata nafasi. Katika nchi za Mashariki, kamwe haikupata kudaiwa kuwa mwanaume ana asili ya kuwa na wake wengi na kwamba hawezi kukaa na mke mmoja.

Tunaweza tukauliza, mwanaume afanye nini wakati mitala imezuiwa kisheria na kama wasomi wanavyosema, mwanaume ni mwenye asili ya kuwa na wake wengi.

Kwa mujibu wa mawazo ya hawa mabwana jibu liko wazi, kisheria mwanaume awe na mke mmoja lakini kiuhalisia awe na wake wengi. Asiwe na mke zaidi ya mmoja wa halali lakini anaweze akazini na idadi yoyote ya wanawake anaotaka. Vimada ni haki ya asili ya mwanaume. Sio vizuri kumzuia mwanaume kuwa na mwanamke zaidi ya mmoja.

Tunaamini kuwa muda umefika ambapo wasomaji watakuwa wameelewa tatizo. Swali sio kwamba ndoa ipi ni bora, ya mke mmoja au wake wengi. Hapana shaka kwamba ndoa ya mke mmoja ndio ndoa inayochaguliwa na wengi, kwani ndoa ya mke mmoja ina maana maishi ya wawili tu. Utu haupaswi kuchagua kati ya ndoa ya mke mmoja na ya wake wengi.

Tatizo pekee ni kuwa ndoa ya mke mmoja tu, wakati fulani haitekelezeki katika baadhi ya hali za kijamii hasa inapokuwa idadi ya wanawake wanaohitaji kuolewa ni kubwa kuliko idadi ya wanaume wanaoweza kuoa. Ndoa za mke mmoja kutumika kama ndoa pekee ni jambo la kufikirika tu.

Kuna mambo mawili tu ya kuchagua: ama kuitambua rasmi ndoa ya wake wengi au kuhimiza wanaume kuwa na vimada. Katika chaguo la kwanza ni asilimia isiyozidi kumi tu ndio watakaokuwa na mke zaidi ya mmoja na wanawake wote wanaohitaji kuolewa watapata fursa ya kuolewa na kuwa na familia. Katika chaguo la pili, kila mwanamke asiyekuwa na mume wa halali ataweza kufanya ngono na wanaume wengi, na hivyo takribani wanaume wote walioowa kiuhalisia watakuwa na wake wengi.

Hii ndio picha sahihi ya mitala. Lakini wafuasi wa mwenendo wa kizungu hawako tayari kuielezea picha halisi ya tatizo hili. Hawataki kueleza ukweli waziwazi. Kiuhalisia wanatetea utaratibu wa kuwa na vimada. Wanamuona mke wa halali kuwa ni mzigo na kizuizi katika njia yao. Kwao hata mke mmoja ni

mwingi mno, achilia mbali wawili, watatu au wanne. Wanajifanya kuwa ni watetezi wa ndoa za mke mmoja, lakini kiuhalisia wanataka ndoa zisiwepo kabisa.

Hila Za Mwanamume Wa Karne Hii

Mwanaume wa karne hii amefanikiwa kumpumbaza mwanamke katika masuala mengi yanayohusiana na haki za kifamilia. Hutumia maneno matamu matamu ya usawa, na uhuru ili kujipunguzia majukumu na kujiogezea fursa za starehe. Lakini kuna masuala machache ambayo ameyafanikisha sana ikiwa ni pamoja na kuingiza imani katika fikra za watu kwamba ndoa za mitala ni mila duni na isiyofaa.

Wakati fulani huwa tunakutana na vitabu vinavyotufanya tushangae ikiwa waandishi wake ni wapumbavu au ni wahuni. Mwandishi mmoja, anasema: Kwa sasa, katika nchi zilizoendelea uhusiano kati ya mume na mke umejengwa juu ya msingi wa haki na majukumu yanayofanana, na kwa sababu hiyo ni vigumu kwa mwanamke kukubali ndoa za mitala za muundo wowote kama ilivyo vigumu kwa mwanaume kuwavumilia waume wenza.

Hatufahamu iwapo hivi ndivyo wanavyolielewa tatizo hili au hawaelewi kuwa tatizo hili limetokana na tatizo la kijamii, ambalo huwatwisha mzigo mkubwa wanaume walioowa na wanawake walioolewa, tatizo ambalo halijapatiwa suluhisho jingine lolote zaidi ya mitala. Kulifumbia macho tatizo halisi na kuanzisha kauli mbiu za: ‘Idumu ndoa ya mke mmoja’ na “Ipotelee mbali ndoa ya wake wengi’ hakuwezi kusaidia chochote.

Je hawajui kwamba mwanamke kuolewa na wanaume wengi si sehemu ya haki za mwanamke wala za mwanaume? Ndoa ya aina hii haishabihiani kwa namna yoyote na mitala.

Ni dhihaka kusema kwamba ni vigumu kwa mwanamke kukubaliana na mitala kama ilivyo vigumu kwa mwanaume kuvumilia waume wenza. Mbali na ukweli kwamba ulinganishaji huu ni wa makosa, inaelekea kwamba mabwana hawa hawajui hali halisi ya ulimwengu wa mwanamke wa leo, kutokana na kumeremeta ambako kumewatia ushamba sana kiasi kwamba mume hutakiwa kuheshimu mapenzi ya nje ya ndoa ya mke wake na pia humtaka astahamili umewenza. Mfumo wa kimagharibi huondoa uingiliaji wowote wa mume katika masuala ya kimapenzi ya mkewe, yaani hutakiwa kutokuwa na wivu. Tunatamani kwamba vijana wetu wangekuwa na elimu kubwa zaidi juu ya kile kinachoendelea katika nchi za Magharibi.

Kwa vile mitala ni matokeo ya tatizo la kijamii na sio silika ya mwanaume, ni wazi kwamba katika jamii ambayo idadi ya wanawake ni sawa na wanume inatarajiwa kuwa mitala haitakuwepo au itakuwa kidogo sana. Lakini haitakuwa sawa hata katika hali hizo kuipiga marufuku mitala. Katazo la kisheria la mitala sio tu kwamba halitoshelezi bali pia sio jambo sahihi.

Kuna baadhi ya mambo ambayo lazima yawepo ili lengo hili liweze kufikiwa. Kwanza, uadilifu wa kijamii lazima uwepo na kila mwanaume awe na hakikisho la kupata ajira ili kila mwanaume anayefaa kuoa

aweze kuoa. Sharti la pili ni kuwa kila mwanamke anapaswa kuwa huru kuchagua mume wake na asishinikizwe na walezi au wazazi wake. Ni wazi kuwa mwanamke mwenye fursa ya kuolewa na mwanaume asiyekuwa na mke hataridhia kuolewa na mume mwenye mke. Ni walezi wao ambao huwauza kwa wanaume wenye fedha kwa ajili ya fedha.

Sharti la tatu ni kuwa inapaswa pasiwepo na vishawishi vingi ambavyo huwashawishi hata wanawake wenye waume achilia mbali wasio na waume.

Kama jamii inataka kuleta mageuzi na kubakiza ndoa ya mke mmoja tu inapaswa kuyafikia masharti yote hayo matatu. Vingenevyo katazo la kisheria la kuzuia mitala litachochea tu kuporomoka kwa maadili.

Matatizo Yanayotokana Na Baadhi Ya Wanawake Kukosa Waume.

Kama wanawake wanaohitaji ndoa ni wengi kuliko wanaume wanaohitaji kuoa, katazo la mitala ni hila dhidi ya wanawake na ubinadamu. Sio suala tu la kukandamiza haki za baadhi ya wanawake. Kama ingekuwa hivyo, lingekuwa lilivumiliwa kwa kisasi fulani. Matatizo ambayo jamii inakabiliana nayo kama matokeo ya ulazimishaji wa kisheria wa ndoa ya mke mmoja, ni tishio la hatari kubwa kuliko tatizo jingine lolote, kwani taasisi ya familia ni taasisi takatifu kuliko taasisi nyingine yoyote.

Mwanamke aliyenyimwa haki yake ya asili ni kiumbe mzoefu kwenye hisia zote za viumbe hai kama vile katika hali ya ufukara. ni kiumbe ambaye ana matatizo ya kisaikolojia na hisia. Ni Eva (Hawa) aliye sheheni silaha za kumrubuni mwanaume.

Yeye sio ngano au shayiri ambayo inayozidi humwagwa baharini au kuhifadhiwa stoo kwa ajili ya matumizi ya dharura, ya baadaye. Yeye sio nyumba au chumba ambacho kisipopata mpangaji kinaweza kufungwa. Ni mtu anayeishi. Ni mwanadamu. Ni mwanamke. Ana vipaji vya ajabu.

Akipuuzwa anaweza kuiangamiza jamii. Hawezi kuwa mtazamaji tu wakati wengine wanafurahia maisha. Kunyimwa kwake haki ya ndoa kunaweza kuibua athari mbaya na uovu. Uovu na silika vikiungana pamoja, madhara yake yanaweza kuwa mabaya sana.

Wanawake walionyimwa haki ya kuwa na maisha ya kifamilia, watafanya kila waliwezalo kuwanasa wanaume na kuutumia vyema udhaifu wa wanaume katika jambo hili. Wake watakaowaona waume zao kutokuwa waaminifu watafikiria kulipiza kisasi hivyo nao watapoteza uaminifu wao. Na matokeo yake hayasemeki.

Matokea ya mwisho yamefupishwa katika ripoti mashuhuri ya Kinsey, katika sentensi moja “Wanaume na wanawake wa Kimarekani wamewazidi watu wa mataifa mengine yote kwa kutokuwa waaminifu.”

Tunaweza tukaona kwamba suala haliishii katika ufisadi na upotofu wa wanaume peke yao. Moto huu

hatimaye huwakumba hata wanawake wenye waume na familia.

Matokeo Ya Kuwepo Idadi Kubwa Ya Wanawake Wasio Na Waume.

Hali ya kuwepo kwa idadi kubwa ya wanawake wasio na waume imekuwepo katika kipindi chote cha historia ya mwanadamu, lakini matokeo mabaya ya hali hii ambayo huisababishia ugumu jamii, hayajapata kuwa na ukubwa sawa katika jamii mbalimbali. Watu ambao walikuwa wameshikamana zaidi na uchamungu na usafi wa kutozini na ambao walikuwa wanaongozwa na dini tukufu zilizoletwa na mitume walilitatua tatizo hili kwa kutumia mfumo wa ndoa za mitala. Watu wengine ambao hawakuwa wachamungu sana waliitumia hali hii kama fursa ya kujiingiza katika ufuska.

Katika nchi za mashariki, mitala haikuanzishwa na Uislamu na wala kuzuiliwa kwa mitala katika nchi za Magharibi hakukutokana na dini ya Kristo. Kwani hakuna palipoandikwa katika Biblia kuwa hairuhusiwi kuwa na mke zaidi ya mmoja, wala Kristo hakuwahi kutamka kwa kinywa chake kuwa hairuhusiwi kuwa na mke zaidi ya mmoja. Mila hii ilikuwepo katika nchi za Mashariki hata kabla ya Uislamu na ikaja kuruhusiwa na dini za Mashariki. Kwenye Biblia pia kuna mifano tele ya Mitume waliokuwa wakioa mke zaidi ya mmoja.

Ndoa za mke mmoja zimepigwa pigo kubwa na mataifa yaliyoamua kuruhusu ufuska kuliko yale yaliyoruhusu ndoa za wake wengi.

Dk. Muhammad Husayn Haikal, mwandishi wa kitabu, *“Life of Muhammad”,* baada ya kunukuu Aya kadhaa za Qur’ani juu ya mitala, anasema: Aya hizi zinasaidia na kuimarisha ndoa za mke mmoja. Zinasema kwamba kama una hofu kwamba hutaweza kufanya uadilifu ukiwa na mke zaidi ya mmoja, basi oa mke mmoja tu. Hata hivyo Aya hizi zinahimiza kuwa kufanya uadilifu kwa ukamilifu haiwezekani. Vyoyote vile kwa mtazamo wa ukweli huu, kuna baadhi ya wakati ambapo mitala huwa haiepukiki.

Mtume mwenyewe alioa wake wengi, katika kipindi ambacho idadi kubwa ya wanawake wa Kiislamu ilipoteza waume zao katika vita vya awali vya Uislamu. Je inawezekana kusema kwamba, kufuatia vita, magonjwa ya milipuko na dharura nyinginezo ambazo husababisha vifo vya maelfu na wakati fulani mamilioni ya watu, ni bora kubaki na ndoa ya mke mmoja kuliko mitala kama hali pekee pamoja na sharti la kufanya uadilifu baina ya wake? Je watu wa Magharibi wanaweza wakadai kuwa baada ya vita vya dunia, sheria ya ndoa ya mke mmoja imeongezwa nguvu katika njia ile ile ambayo kwamba kwa sasa imebakia jina tu?

Dosari Na Kasoro Za Mitala

Maisha ya ndoa yenye furaha hutegemea, uaminifu, uvumilivu, kujitolea na umoja. Mambo yote haya huhatarishwa na ndoa za wake wengi (mitala). Mbali na mazingira ya wivu kati ya wake na watoto katika

ndoa za mitala, majukumu ya mume huwa ni mazito sana na yanayovunja mgongo kiasi kwamba sio burudani kuyabeba.

Wanaume walio wengi ambao wana furaha na wameridhika na mitala, ni wale ambao katika hali halisi hukwepa majukumu yao ya kisheria na kimaadili. Humjali mke mmoja tu na huwapuuza wengine, ambao kwa mujibu wa Qur'ani huachwa wamening'inia. Kile ambacho watu wa aina hii wanakiita mitala, kiuhalisia ni ndoa za mke mmoja zilizochanganyika na ubabe, ukatili na dhulma ya jinai. Kuna methali iliyoenea sana miongoni mwa watu wa kawaida isemayo: "Mungu Mmoja, Mke Mmoja".

Kilichosemwa ni imani ya watu walio wengi na tukilipima tatizo kwa kutumia furaha ya mtu mmoja mmoja, ni sahihi. Kanuni ya mke mmoja, hata kama haitekelezwi na wanaume wote lakini ndiyo inayotumiwa na wanaume walio wengi.

Kama mtu anafikiri kuwa mitala, pamoja na majukumu yake yote ya kisheria na kiuchumi, ni kitanda cha maua waridi, basi amekosea sana. Kwa upande wa furaha na starehe binafsi, ndoa za mke mmoja ndio zinafaa zaidi.

Tathmini Sahihi

Hata hivyo, tathmini sahihi ya mfumo wa mitala, ambao unatokana na mahitaji binafsi na ya kijamii, haiwezi ikafanywa kwa kulinganisha na ndoa za mke mmoja. Namna sahihi ya kutathmini mfumo huu ni kuzingatia sababu zinazousababisha, ili kuangalia ni madhara gani mabaya yatafuatia, na wakati huo huo tutazame dosari na kasoro za mfumo wa mitala. Ni baada tu ya kupima faida na hasara zote za mfumo huu ndio tutafikia kwenye hitimisho sahihi. Ili kufafanua nukta hii, hebu tuutazame mfano huu.

Tukiitazama sheria ya kulazimisha watu kwenda jeshini, ni wazi kwamba kwa upande wa maslahi binafsi, sheria hii sio nzuri. Ingekuwa vizuri zaidi kama sheria hii isingekuwepo, na hakuna mpendwa wa familia ambaye angeondolewa kwenye familia yake (na kupelekwa jeshini) na wakati fulani kupelekwa vitani.

Lakini hii sio tathmini sahihi ya jambo hili pamoja na ubaya wa mtoto kutenganishwa na familia yake, tunapaswa pia kutazama mahitaji ya kiulinzi ya nchi. Tukifanya hivyo tutaona kwamba ni jambo la maana kabisa kuweka idadi ya kutosha ya raia iwekwe tayari kwa ajili ya ulinzi wa nchi na familia zao zinapaswa kustahamili usumbufu na matatizo yanayosababishwa na sheria ya kulazimisha watu kuingia jeshini.

Awali tulielezea mahitaji ya mtu mmoja mmoja na ya kijamii ambayo wakati fulani huhalalisha mitala. Sasa kuandaa mazingira ya hukumu ya jumla, hebu tujadili dosari na kasoro za mfumo huu. Tunakubali kwamba mfumo huu una dosari fulani fulani, lakini hatuamini kwamba yote yaliyosemwa dhidi ya mitala ni sahihi. Tunapendekeza kwamba tuzijadili dosari zake katika mitazamo mbalimbali.

Katika Mtazamo Wa Kisaikolojia

Mahusiano ya unyumba hayaishii katika ushirikiano wa kimwili na kifedha. Kama ingekuwa hivyo, ingekuwa rahisi kuhalalisha mitala, kwani fedha na matendo ya ndoa yanagawanyika baina ya watu wengi, kila mmoja anapata gawio lake.

Msingi wa mahusiano ya unyumba ni wa kimhemko na kisaikolojia. Yamejengwa juu ya vitu kama upendo, mihemko na hisia. Maisha ya ndoa yana maana ya muungano wa mioyo. Kama ilivyo kwa vitu vyote dhahania (visivyoonekana), upendo na hisia havigawanyiki. Haviwezi kugawiwa miongoni, mwa watu wengi wala haiwezekani kila anayehitaji akapewa kijisehemu maalumu cha upendo na hisia hizo. Moyo hauwezi ukagawanywa baina ya watu wawili. Upendo na ibada vinakwenda pamoja. Havikubali mpinzani. Upendo hauwezi ukapimwa wala kugawiwa kama ngano au shayiri. Aidha, hisia haziwezi kudhibitiwa. Moyo humtawala mwanaume, mwanaume hautawali moyo. Roho ya ndoa, yaani, kipengele chake cha kibinadamu ambacho hutofautisha mahusiano kati ya wanaadamu na wanyama haigawanyiki wala haiwezi kudhibitiwa. Kwa hiyo, mitala haipaswi kuruhusiwa.

Kwa imani yetu, maelezo haya yametiwa chumvi. Ni kweli kwamba mihemko na hisia ni roho ya ndoa. Pia ni kweli kwamba hisia hazidhibitiki. Lakini ni mawazo halisi ya kindoto, bali pia ni hoja ya uwongo kusema hisia hazigawanyiki.

Sio suala la kugawanya hisia kama vile mali au fedha. Ni suala la uwezo wa kiakili wa mwanaume, ambao ni mdogo kiasi cha kushindwa kumudu mahusiano ya watu wawili. Baba mwenye watoto kumi huwapenda wote na hujitolea mhanga kwa ajili yao.

Lakini suala moja liko wazi. Upendo hauwezi kuwa mkubwa sana katika wake wengi kama ndoa ya mke mmoja. Upendo mkubwa, haukubaliani na wingi, lakini pia haukubaliani na hoja za kiakili.

Russel katika kitabu chake, *“Marriage and Morality”* anasema kwamba watu wengi leo hii wanayaona mapenzi kama ubadilishanaji mzuri wa hisia. Hoja hii peke yake, bila kujali hoja nyingine zote, inatosheleza kuzishutumu ndoa za mitala.

Kama ni suala la ubadilishanaji mzuri wa hisia tu, tunashangaa kwa nini ubadilishanaji huu uhodhiwe. Baba mwenye watoto huwapenda wanaye wote nao wote humpenda. Je huu sio ubadilishanaji wa haki wa hisia? Hata baba anapokuwa na watoto wengi, upendo wa baba kwa kila mtoto, mara zote huwa ni mkubwa kuliko upendo wa kila mtoto kwa baba yao.

Sehemu inayoshangaza zaidi katika kauli hiyo ni kwamba, imetengenezwa na mtu ambaye anawashauri wanaume kuyaheshimu mapenzi ya nje ya wake zao na kwamba wasiwaingilie.

Pia anawapa ushauri kama huo wanawake walioolewa. Je bado anaamini kuwa ubadilishanaji wa hisia kati ya mume na mke utakuwa wa haki?

Kutoka Katika Mtazamo Wa Tabia

Katika ndoa za mitala, mahusiano baina ya wake wenza huwa ni balaa tupu. Kwa kawaida mwanamke humuona mke mwenzake kama adui yake mkubwa kuliko wote. Kuwa na wake wengi mara nyingi husababisha magomvi baina yao na wakati fulani dhidi ya mume wao. Huzusha uovu na huibadili hali ya hewa ya familia, kutoka katika hali ya uaminifu na utulivu iliyotarajiwa na kuwa uwanja halisi wa vita. Uadui na uhasama ambao huwepo baina ya akina mama huhamia mpaka kwa watoto na kambi mbili au zaidi huundwa. Hali ya hewa ya familia, badala ya kuwa shule ya awali ya kuwafundisha watoto maadili, hubadilika na kuwa shule ya magomvi na tabia zisizo za kibinadamu.

Hapana shaka kwamba ndoa za mitala zina athari hizi zote mbovu. Lakini nukta moja haipaswi kusahaulika. Tunapaswa kuona kama hizi ni athari za asili za mitala au zinatokana na tabia isiyofaa ya mume na mke wa pili. Tunaamini kwamba athari mbaya zilizo nyingi hazitokani na matokeo ya moja kwa moja ya mitala, bali zinatokana na utekelezaji usiofaa wa mitala.

Jaalia mume na mke wanaishi pamoja na wanaishi maisha ya kawaida. Kisha mume anakuja na mwanamke mwingine ambaye anahamishia upendo wote kwake. Baada ya maelewano ya siri baina ya wawili, mke wa pili huvamia nyumba na huutumia vibaya upendo wa mume, na huyatishia mamlaka ya mke wa kwanza. Tunaweza tukaelewa atakachokifanya mke wa kwanza. Hakuna kitu ambacho huwa kinamuudhi na kumkera mwanamke kama kitendo cha kudharauliwa na mume wake. Kushindwa kuurejesha upendo wa mume wake ni kufeli kukubwa kabisa kwa upande wa mke. Mume anapofanya jeuri na uasherati na mke wa pili ndio hubaki mwenye mamlaka pekee, hapa haitarajiwi mke wa kwanza awe na subira.

Lakini mambo yatakuwa tofauti na migogoro ya ndani itapungua sana ikiwa mke wa kwanza anajua kuwa mume wake ana haki ya kuwa na mke wa pili na kwamba hajamchoka. Mume hapaswi kuonyesha jeuri wala kujishughulisha na ngono na mke wa pili zaidi kuliko kujali hisia za mke wa kwanza. Baada ya kuwa na mke wa pili anafaa kuwa mpole zaidi kwa mke wake wa kwanza na kujali hisia zake. Mke wa pili anapaswa pia kujua kuwa mke wa kwanza pia ana haki zinazopaswa kuheshimiwa. Kwa kifupi pande zote zinazohusika, zinapaswa kukumbuka kuwa zimechukua hatua katika kutatua tatizo la kijamii.

Sheria ya mitala ni suluhisho endelevu la tatizo la kijamii na imezingatia maslahi makubwa na mapana zaidi ya jamii. Wale wanaoitekeleza wanapaswa kuwa na uwezo mkubwa wa kufikiri na wawe wamefundishwa vizuri mwenendo wa Kiislamu. Uzoefu unaonyesha kwamba ikiwa mume sio muasheati na sio mjeuri na mke wake akishawishika kuwa mume wake anahitaji mke wa pili, yeye mwenyewe mke wa kwanza hufanya maadalizi ya ndoa ya mke wa pili. Katika hali hii matatizo huwa hayaibuki, kwani matatizo mengi hutokana na tabia mbaya za wanaume.

Kutoka Katika Mtazamo Wa Kimaadili.

Inadaiwa kwamba mitala maana yake ni kupenda sana ngono. Maadili hutaka vitendo vya ngono vipunguzwe, kwani maumbile ya mwanaume yapo katika hali ambayo kwa kadri anavyofanya ngono ndivyo hamu ya kufanya ngono zaidi inavyoongezeka.

Montague katika kitabu chake, *"Spirit of Laws",* alipokuwa akijadili suala la mitala, anasema: "Mfalme wa Morocco, katika kasri yake ana wake wa rangi zote, weupe, wa njano na weusi. Hata kama mwanaume huyu angekuwa na wanawake mara mbili ya hawa alionao bado angetaka wake zaidi. Kama ukusanyaji wa dhahabu na fedha zaidi na zaidi unavyoongeza tamaa zaidi, hali kadhalika kuoa wake wengi hukuza tabia mbaya, na zisizo za asili za kufanya mapenzi, kwani katika suala la ngono, kila kitendo kinachovuka mipaka huhimiza upotofu. Fujo zilipoibuka Istanbul, hakuna hata mwanamke mmoja aliyekutwa katika kasri la mtawala kwa sababu alijihusisha na mapenzi yasiyo ya asili (liwati).

Pingamizi hili linaweza kutazamwa katika pande mbili. Kwanza imedaiwa kuwa tendo la ndoa ni makruhu (linachukiza) mbele ya maadili safi na kwamba matamanio ya ngono yanapaswa kudhibitiwa kwa kadri inavyowezekana. Pili imedaiwa kuwa maumbile ya mwanamume ni kwamba kadri anavyofanya mapenzi zaidi ndivyo anavyopata hamu ya ngono zaidi.

Kuhusiana na hoja ya kwanza, tunaweza kusema kuwa inawakilisha fikra potofu. Inahubiriwa sana miongoni mwa wakristo, wahindu, budha na wengineo kuwa maadili maana yake ni kukaa bila kuoa au kuolewa. Kwa mtazamo wa Uislamu sio sahihi kusema kwamba kwa kadri mtu anavyofanya mapenzi kidogo (katika ndoa) ndivyo anavyokuwa na maadili safi zaidi. (Pengine kwa mujibu wa nadharia hii, maadili timilifu zaidi ina maana ni kutofanya mapenzi kabisa). Ni ngono zilizovuka mipaka tu, ndizo zinazochukiza mbele ya maadili ya Kiislamu.

Ili kuyakinisha kama ndoa za mitala maana yake ni kufanya ngono kupita kiasi, hebu tuangalie kama kwa maumbile mwanaume ni mwenye asili ya kuoa mke mmoja au la.

Kama ilivyoelezwa huko nyuma hakuna anayeamini kuwa mwanaume ni mwenye asili ya kuwa na mke mmoja kwa asilimia zote wala kwamba mitala ni kitendo cha upotofu. Kinyume chake wanasosholojia wengi wana maoni kwamba mwanaume ni mwenye asili ya kuwa na wake wengi na kwamba ndoa za mke mmoja ni kinyume na maumbile yake kama tu ilivyo kwa useja (kuishi bila kuoa wala kuolewa).

Ingawa hatuamini kuwa mwanaume ni mwenye asili ya kuwa na wake wengi, pia hatuamini kuwa ana asili ya kuwa na mke mmoja na kwamba mitala sio mwenendo wa asili na kwamba ni aina ya upotofu kama liwati.

Watu wa aina ya Montesquieu, ambao wanaziona ndoa za mitala kuwa ni sawa na uasherati, wana fikra ya 'nyumba za wake' – *harems* – vichwani mwao. Wanafikiri kwamba Uislamu, kwa kuruhusu ndoa za wake wengi, unataka kutoa kisingizio cha kuyalinda majumba ya wake ya makhalifa wa Bani Abbas na

masultani wa Ottoman. Lakini, kwa kusema ukweli, Uislamu unapingana na jambo hilo kabisa. Masharti yaliyowekwa na Uislamu juu ya suala la wake wengi ni magumu kiasi kwamba uwezekano wa kuwepo na uasherati huondolewa kabisa.

Kuhusiana na nukta ya pili kwamba tamaa ya ngono huongezeka kwa kadri tamaa hizo zinavyokidhiwa, na kwamba kwa kadri zinavyokandamizwa ndivyo zinavyotulia, hoja hii inapingana moja kwa moja na nadharia mashuhuri ya Freudi.

Kwa mujibu wa wafuasi wa Freud, tamaa za kisilika hutulia zikikidhiwa, lakini zikikandamizwa, hulipuka. Hii ndio sababu wafuasi wa nadharia hii wanatetea kuwepo kwa uhuru kamili na kuondolewa kwa vikwazo vyote katika suala la ngono. Natamani Montesquieu angekuwa hai leo hii ili aone jinsi nadharia yake inavyokejeliwa na wafuasi wa nadharia ya Freud.

Kwa maoni ya Uislamu, nadharia zote ni potofu. Maumbile ya mwanadamu yamejiwekea sheria na mipaka yake ambayo lazima itambuliwe. Huwa na hisia kali katika hali zote kwa matokeo ya ufukura na halikadhalika uhru usio na mipaka.

Muhimu ni kuwa, ndoa za mitala sio kinyume na maadili wala haziharibu amani ya kiroho, kama Montesquuieu na wenzake wanavyodai, wala sio kinyume na maumbile ya mwanadamu, kuridhika na mke mmoja au wake zaidi ya mmoja wa halali kama inavyodaiwa na wafuasi wa nadharia ya Freud.

Kutoka Katika Mtazamo Wa Kisheria

Kwa asili ya mkataba wa ndoa, mume na mke kila mmoja ni mali ya mwenzake na kila mmoja wao ana haki ya kumfurahia mwenzake. Kutokana na faida za kiunyumba, mkataba wa ndoa huunda kitu kama haki miliki. Katika mitala ni mke wa kwanza ambaye ana stahili ya awali kwenye manufaa ya unyumba, na hivyo mkataba wowote na mwanamke mwingine ni batili, kwani mali zilizoko chini ya mkataba, kama manufaa ya unyumba yanavyoweza kuitwa, tayari yameshauzwa kwa mke wa kwanza. Hivyo hakuna makubaliano yoyote ya faida hizo za unyumba yanayoweza kufanywa bila idhini ya mke wa kwanza. Hivyo, kama mitala inaruhusiwa, lazima iwe ni kwa idhini ya mke wa kwanza. Anapaswa kuwa na haki ya kuamua iwapo mume wake ana haki au hana haki ya kuoa mke mwingine.

Hii ina maana kuwa kuoa mke wa pili, wa tatu au wa nne ni kana kwamba mtu alimuuzia mtu mwingine mali yake na kisha akaiuza tena kwa mteja wa pili, wa tatu na wa nne. Uhalali wa makubaliano unategemeana na idhini ya mnunuzi wa kwanza, wa pili na wa tatu sawia. Mchuuzi akiwauzia wanunuzi wengine bila idhini hiyo, anastahili kushitakiwa.

Pingamizi hili lemewekwa juu ya dhana kwamba asili ya kisheria ya ndoa ni ile ya kubadilishana faida, na kwamba mume na mke kila mmoja anamiliki faida za unyumba zinazotokana na mwenzake, ingawa dhana hii haifai, kwa sasa hatutaki kuibishia. Tujaalie kuwa ilivyoelezwa ndio hivyo hivyo ilivyo. Lakini pingamizi hili linaweza kuwa halali tu ikiwa mume atachukua mke mwingine kwa burudani tu.

Ni wazi kwamba kama ikikubaliwa kuwa asili ya kisheria ya ndoa ni ile ya kubadilishana faida za unyumba, ndoa za wake wengi (mitala) hazitakubalika tu ikiwa mke anakidhi mahitaji yote ya halali ya mume wake. Lakini ikiwa kutakuwa na sababu yoyote inayokwamisha upatikanaji wa mahitaji ya mume kutoka kwa mkewe basi pingamizi hilo huwa batili. Kwa mfano ikiwa mke ni tasa au amefikia umri wa kuacha kuzaa na mume anahitaji mtoto au mke ni mgonjwa na hawezi kumudu kujamiiana, haki ya mke haitakuwa kizuizi cha mume kuoa mke au wake wengine.

Hukumu inakuwa hivi kama mitala ni mahitaji binafsi ya mume. Lakini kama ni mahitajio ya jamii, kwa mfano ikiwa wanawake ni wengi kuliko wanaume au kama jamii inahitaji watu wengi, zaidi, basi hapa mambo huwa tofauti. Katika hali hiyo, ndoa za wake wengi huwa ni wajibu unaopaswa kutekelezwa na idadi ya kutosha ya wanaume.

Ni jukumu linalopaswa kutekelezwa ili kuiokoa jamii dhidi ya ufisadi na umalaya au ili kuongeza idadi ya watu katika jamii. Linapokuwa ni suala la jukumu la kijamii, ni wazi kwamba hapa ruhusa ya mke huwa haitajiki. Jaalia katika jamii idadi ya wanawake ni kubwa kuliko ya wanaume au jamii inahitaji idadi kubwa zaidi ya watu, basi hapa jukumu la kijamii huenda kwa wanaume na wanawake wote walio na ndoa, jukumu ambalo linapaswa kufanywa na idadi yao ya kutosha kwa moyo wa kujitolea. Hii inafanana sana na sheria ya kuingizwa jeshini kwa nguvu. Ulinzi wa nchi hupeleka jukumu kwa familia zote ili ziwapeleke wapendwa wao vitani kwa ajili ya jamii. Katika hali hizi huwa hakuna suala la idihini kutoka katika pande zinazohusika, wale wanaoshikilia kuwa uadilifu unataka mitala itegemee idhini ya mke wa kwanza wanaliangalia suala hili kwa mtazamo finyu.

Wanafikiri kwamba kila mume anapoongeza mke huwa anafanya hivyo kwa ajili ya raha zake na kutaka kubadilibadili wanawake. Wanasahau kwamba kunaweza kuwepo matatizo mengine ya mtu mmoja na jamii pia. Kimsingi ndoa za wake wengi hazipaswi kukubaliwa hata kwa idhini ya mke wa kwanza, ikiwa hakuna mahitaji ya mtu mmoja mmoja au ya kijamii.

Kwa Mtazamo Wa Kifalsafa

Sheria ya mitala inachukiza mbele ya kanuni ya usawa kati ya mwanaume na mwanamke kama wanaadamu. Kwa kuwa mwanaume na mwanamke wote wana haki sawa, ama wote waruhusiwe kuwa na mwenzi zaidi ya mmoja au wote wakatazwe. Ni ubaguzi wa wazi kumruhusu mwanaume kuwa na wake wengi huku wanawake wakizuiwa kuwa na waume wengi. Kumruhusu mwanaume kuwa na wake mpaka wanne. Kunamaanisha kuwa thamani ya mwanamke ni robo ya thamani ya mwanaume. Hili ni tusi kubwa kwa mwanamke. Hali iko hivi hivi hata katika mfumo wa Uislamu wa mirathi na ushahidi. Katika suala la kutoa ushahidi, wanawake wawili wanahesabiwa kuwa ni sawa na mwanaume mmoja.

Hili ni pingamizi lilichoka kuliko yote. Inaelekea kwamba wakosoaji hawa hawajazingatia mahitaji ya mtu mmoja mmoja na yale ya kijamii yanayosababisha mitala. Wanafikiri kuwa ni suala la mvuto wa kimapenzi tu. Hivyo mwanaume na mwanamke wanapaswa kutendewa kwa usawa. Tayari tumeshaeleza mazingira ambayo yakiwepo kunakuwa na uhalali wa mitala. Pia tumeonyesha hali

ambazo zikiwepo jukumu la wanawake wasio na waume huenda kwa wanaume waliooa na wanawake walioolewa. Hivyo hakuna haja ya kulirudia swali hili tena.

Inatosha kusema kwamba mafundisho ya Uislamu katika masuala ya mitala, mirathi na ushahidi hayajamfanyia ukatili wala dharau yoyote mwanamke katika haki zake, na kwamba Uislamu ungekuwa unawabagua wanaume na wanawake kama wanaadamu, ungekuwa na mitazamo sare sare katika masuala yoyote.

Katika suala la mirathi, Uislamu usingekuwa umeamuru nusu ya gawio katika baadhi ya hali, na gawio kamili katika baadhi ya hali. Halikadhalika katika suala la ushahidi kusingekuwa na kanuni tofauti katika masuala tofauti. Yote hii inaonyesha kwamba Uislamu una falsafa nyingine, sio kumbagua au kumdhulumu mwanamke.

Tayari tumeshajadili suala, la mirathi katika sura zilizopita. Pia katika maeneo mengine tumeonyesha kuwa kwa mtazamo wa Uislamu, usawa kati ya mwanaume na mwanamke kama binadamu ni sehemu ya haki za msingi za binadamu. Hata hivyo, tunapojadili haki za kifamilia, Uislamu umezingatia mambo mengine pia ambayo ni muhimu kuliko usawa.

Mchango Wa Uislamu Katika Uboreshaji Wa Mitala.

Uislamu imma haukuanzisha ndoa za mitala (kwani zilikuwepo kabla ya Uislamu), wala Uislamu haukuzipiga marufuku, kwani hapakuwepo suluhisho mbadala kwa baadhi ya matatizo ya kijamii. Uislamu ulichokifanya ilikuwa ni kuiboresha tu hii desturi ya kale.

Mipaka (Ya Idadi).

Kabla ya Uislamu mtu alikuwa na uwezo wa kuwa na idadi isiyo na mipaka ya wake na aliweza kuunda (*harem*) 'nyumba ya wake.' Uislamu uliweka kikomo. Haukumruhusu yeyote kuwa na wake zaidi ya wanne. Wale waliokuwa na wake zaidi ya wanne waliposilimu walipaswa kuwaacha wale waliozidi.

Tunakutana na majina ya watu wengi wa aina hii katika historia ya Uislamu. Mtu mmoja aliyeitwa Ghaylan bin Aslmah alikuwa na wake kumi. Mtu mwingine aliyeitwa Nawfal bin Muawiyah alikuwa na wake watano. Mtume aliwaamuru kuwaacha wake zao waliozidi ile idadi iliyoruhusiwa.

Hadithi za Kishia zinasimulia kuwa katika enzi za Imam Sadiq (as) Mzoroastria alisilimu. Alikuwa na wake saba. Imam aliulizwa yule mtu afanye nini na hiyo idadi iliyozidi? Imam akasema lazima awaache watatu.

Uadilifu Na Kuwatendea Kwa Usawa.

Mageuzi mengine yaliyoletwa na Uislamu ilikuwa ni sharti la kuwatendea kwa usawa wake wote.

Uislamu hauruhusu ubaguzi wowote baina ya wake au watoto wao. Qur'ani Tukufu wazi wazi inasema,

فَإِنْ خِفْتُمْ أَلَّا تَعْدِلُوا فَوَاحِدَةً

"Ikiwa mna hofu kuwa hamtatenda uadilifu basi oeni mmoja tu." (***Suratul Nisaa, 4:3***).

Kabla ya Uislamu watu walikuwa hawatendi uadilifu kwa wake zao wala watoto wao. Tumeshanukuu maoni ya Christenson na wengine ambao wamesema kwamba katika kipindi cha Sassania, mitala ilikuwa ni mila iliyozoeleka nchini Iran. Mke mmoja au zaidi waliitwa wake vipenzi na walipata haki zote na wengine walijulikana kama wake wafanyakazi na walikuwa na haki chache zaidi za kisheria. Ni watoto wa kiume tu wa wake wafanyakazi walioingizwa katika ukoo wa baba.

Uislamu ulipiga marufuku mila na desturi zote hizi. Hauruhusu mke yeyote au watoto wake kuonekana kuwa ni wa cheo cha chini kuliko wa mke mwingine au watoto wengine wa mume wake.

Will Durant katika kitabu chake, *History of Culture*, juz. 1 amesema, "Mtu alipokusanya mali alihofu kuwa ikiwa itagawiwa kwa watoto wake wote, kila mmoja angepata sehemu ndogo tu. Hivyo alihisi kuwa aweke tofauti kati ya mke wake kipenzi na wale wengine ili kuwawezesha watoto wa mke kipenzi tu ndio warithi mali yake."

Hii inaonyesha kuwa enzi za kale ubaguzi kati ya wake na kati ya watoto wao ulikuwa jambo la kawaida. Hata hivyo cha kushangaza ni kuwa Will Durant anaongeza kwa kusema, "Mpaka hivi karibuni hali imekuwa hivi huko Asia. Popepole mke halisi alichukua nafasi ya mke pekee. Wake wengine ama walitoweka au walikuwa wake wa siri".

Will Durant hakuujuwa ukweli au hakutaka kufanya hivyo, kuwa karne 14 zilizopita Uislamu ulitokomeza ubaguzi kati ya watoto, kuwa na mke mmoja halisi na vimada wengine wengi wa siri ni mila ya Kizungu sio ya Kiasia. Ni hivi karibuni tu imeanza kujipenyeza Asia.

Hata hivyo mageuzi ya pili ambayo Uislamu uliyaleta katika ndoa za mitala ilikuwa ni kupiga marufuku ubaguzi baina ya wake na watoto wao. Upendeleo wa aina yoyote hauruhusiwi. Mafakihi wote wanakubaliana juu ya hili. Ni matapo machache tu ya kifakihi ambayo yamezitafsiri haki za wanawake katika namna ambayo inaashiria upendeleo. Lakini ni ukweli usiopingika kuwa tafsiri hii inapingana na tafsiri sahihi ya Qur'ani.

Mtukufu Mtume ameripotiwa na wote, Shia na Sunni kuwa amesema: "Yule mwenye wake wawili lakini akawa hawatendei kwa usawa na akaonyesha kumpendelea mmoja wao atafufuliwa siku ya kiama hali ya kuwa upande mmoja wa mwili wake unamvutia chini. Hatimaye atapelekwa Motoni."

Haki ni sifa kubwa kuliko zote za maadili. Kuweka sharti la haki na kuwatendea sawa inamaanisha kuwa

mume anapaswa kuwa na sifa za juu kabisa za uadilifu. Kwa kuwa hisia za mwanaume kwa wake zake haziko sawa, kuzingatia uadilifu na kujiepusha na ubaguzi ni moja ya majukumu yanayohitaji jitihada kubwa.

Wote tunajua kuwa Mtukufu Mtume, katika miaka kumi ya mwisho ya uhai wake, yaani katika kipindi alipokuwa akiishi Madina alioa wake wengi. Hiki kilikuwa ni kipindi cha vita vya Kiislamu (Jihad) na wakati huo idadi ya wanawake ambao hawakuwa na watu wa kuwatazama ilikuwa kubwa kabisa. Wengi wa wake za Mtume walikuwa wazee na wajane. Wengi wao walikuwa na watoto wa waume zao wa zamani.1

Mwanamwali pekee aliyemuoa na Aisha, ambaye alikuwa akisema mara kwa mara kwa kujivuna kwamba yeye ndiye mwanamke pekee ambaye hakuna mume mwingine mbali na Mtume aliyewahi kumgusa kwamwe.

Mtukufu Mtume mara zote alikuwa akiwatendea wake zake kwa usawa na uadilifu na hakubagua kati yao. Urwah bin Zubayr alikuwa ni mtoto wa dada yake na Aisha. Alimuuliza mama yake mdogo juu ya jinsi Mtume alivyokuwa akiwatendea wake zake. Aisha alisema kuwa alikuwa akiwatendea kwa uadilifu na usawa kabisa. Kamwe hakuwa akimpendelea yeyote miongoni mwao. Kila siku alikuwa akimtembelea kila mke na kumuuliza juu ya afya yake n.k. Kila siku moja alilala kwa mke mmoja. Ikiwa alitaka kulala kwa mke ambaye sio zamu yake alikuwa akimuomba ruhusa yule mke ambaye ndiyo zamu yake (mwenye zamu). Alikuwa akienda kama akiruhusiwa vinginevyo asiporuhusiwa alikuwa haendi. Aisha mwenyewe anasema kuwa alikuwa anakataa kutoa ruhusa pindi alipokuwa akiombwa.

Hata katika maradhi yake ya mwisho yaliyosababisha kifo chake na alipokuwa dhaifu kiasi cha kushindwa kutembea, bado Mtume alikuwa anazingatia uadilifu kwa kuwatendea kwa usawa wake zake wote. Kitanda chake kilihamishwa kutoka chumba kimoja kwenda kingine kila siku. Hatimaye, siku moja aliwaita wake zake wote na kuwaomba akae kwenye chumba kimoja. Baada ya kumruhusu alikaa kwenye chumba cha Aisha kwa vile chumba chake kilikuwa karibu zaidi na msikiti.

Wakati alipokuwa na wake wawili, Imam Ali (a.s) alikuwa anazingatia uadilifu kwa kiasi kuwa hata udhu alikuwa anachukulia kwa yule mke mwenye zamu.

Uislamu umeweka umuhimu mkubwa kwenye uadilifu na usawa katika kuwatendea wake kiasi kwamba haumruhusu mwanaume kuingia mkataba wa ndoa na mke wa pili kwa sharti kuwa mume atampa mke wa pili upendeleo katika maisha yao. Hii ina maana kuwa ni wajibu wa lazima kwa mume kuwatendea kwa usawa na uadilifu wake zake na kwamba hawezi kulikwepa jukumu hili kwa kuingia mkataba kabla na mke yeyote kuwa yeye atapendelewa (kama sharti la lazima la ndoa).

Mke wa pili anachoweza kukifanya ni kwa hiari kusamehe baadhi ya haki zake akipenda kufanya hivyo kwa sababu za msingi alizonazo. Lakini sharti hili haliwezi kuwekwa kwenye mkataba wa ndoa. Halikadhalika mke wa kwanza anaweza kusamehe baadhi ya haki zake kwa hiari yake na kwa sababu maalum, lakini hawezi kuzikataa moja kwa moja.

Wakati fulani Imam Baqir (a.s) aliulizwa kuwa inawezekana kuamriwa kwa makubaliano na mmoja wa wake kuwa mume angemtembelea mmoja wa wake zake (huyo aliyetoa ruhusa) mara moja kwa wiki au mara moja kwa mwezi au kwamba gharama za matunzo za mmoja wake huyo aliyetoa ruhusa zitakuwa pungufu za zile anazopata mwenzake. Imam alisema kuwa hilo halikubaliki hata kwa ridhaa ya huyo mke anayataka kusamehe haki zake. Kwa asili ya ndoa kila mke anastahili haki zote za unyumba. Anachoweza kukifanya ni kusamehe baadhi au haki zake zote iwe kwa kumridhisha mume wake au ka sababu nyinginezo.

Kwa masharti haya magumu mitala huwa ni jukumu badala ya raha na burudani. Raha na uasherati vinawezekana tu katika mazingira ya uhuru kamili wa kukidhi matamanio yao. Lakini panapokuwa panahitajika nidhamu, uadilifu na majukumu (wajibu), hapawezi kuwa na nafasi ya uzinifu.

Wale wanaojiingiza katika uasherati kwa kisingizio cha mitala wanaitumia vibaya sheria ya Kiislamu na jamii ina kila haki ya kuwaita wajieleze na kuwaadhibu.

Wasiwasi Wa Kutotenda Uadilifu.

Kuwa wakweli, lazima tukiri kuwa idadi ya wale wanaotenda uadilifu na kuzingatia masharti yote yaliyowekwa na Uislamu juu ya mitala ni ndogo sana. Kwa mujibu wa sheria ya Kiislamu, ikiwa mtu atahofia kuwa akitumia maji yatamdhuru basi hatakiwi kutawadha kwa maji, na kama atakuwa na wasiwasi kuwa akifunga (Saumu) atadhurika basi anapaswa asifunge. Unakutana na watu wengi wanaouliza kama wachukue au wasichukue udhu (kwa maji), au kama wafunge au wasifunge, kwani wana wasiwasi kuwa kutawadha (kwa maji) na kufunga saumu kutawadhuru. Maswali kama haya ni sawa kabisa. Watu kama hao hawapaswi kutawadha wala kufunga.

Lakini Qur'ani Tukufu inaeleza wazi wazi kuwa kama mnahofu kuwa hamtatenda uadilifu basi mnapaswa kuoa mke mmoja tu. Lakini bado hakuna mtu hata mmoja anaweza kusema kuwa ana wasiwasi kuwa hawezi kuwatendea wake zake wawili kwa usawa, na anaweza kuuliza kuwa katika hali hii awe na mke wa pili au asiwe naye. Ni dhahiri kuwa baadhi ya watu wanajua fika kuwa hawataweza kufanya uadilifu, lakini bado wana wake wengi. Wanafanya hivyo chini ya kivuli cha sheria ya Kiislamu. Hawa ndio watu wanaochafua jina la Uislamu kwa matendo yao yasiyofaa.

Nyumba Za Wake (Harem).

Sababu nyingine inayofanya Uislamu ushutumiwe kwa mitala ni mfumo wa mwanaume kumiliki nyumba ya wake uliokuwa ukitumiwa na makhalifa na masultani waliopita. Baadhi ya waandishi wa Kikristo na Wamisionari wamezielezea ndoa za mitala katika Uislamu kuwa ni sawa na mfumo wa 'nyumba ya wake' ambao umejaa mambo ya aibu na ukatili.

Kwa bahati mbaya baadhi ya waandishi wetu, kama kasuku, wanarudia yale yale mawazo yaliyoelezwa na wazungu, bila ulazima wanahusisha ndoa za mitala na nyumba hizi. Hawana uwezo wa kutosha wa

kufikiri wenyewe kwa uhuru ili kutofautisha mambo haya mawili.

Masharti Mengine.

Mbali na sharti la uadilifu na usawa kuna masharti mengine pia ambayo mume anapaswa kuyatimiza. Wote tunajua kuwa mke ana haki nyingi za kifedha na nyinginezo ambazo mume anapaswa kuzitekeleza. Mume ana haki ya kuwa na mke zaidi ya mmoja ikiwa uwezo wa kifedha unamruhusu kufanya hivyo. Uwezo wa kifedha ni sharti la msingi hata kwa ndoa ya mke mmoja. hata hivyo hatutalijadili zaidi hili kwa sasa.

Uwezo wa kiafya na urijali ni sharti jingine la msingi. Imesimuliwa katika *Alkafi* na *AlWasail* kuwa Imam Sadiq amesema kuwa ikiwa mtu atakusanya wake wengi, wakati hana uwezo wa kuwaridhisha (kimapenzi) wote, atabeba jukumu la madhambi yoyote watakayofanya.

Historia ya 'nyumba za wanawake' inasimulia visa vya wanawake vijana, ambao kwa kuelemewa na hamu ya ngono, walilazimika kutenda madhambi (kuzini) na wakati fulani ilisababisha uhalifu na mauaji.

Mpaka sasa wasomaji wanapaswa kuwa wamefahamu sababu zilizosababisha mitala na kwa nini Uislamu haukuipiga marufuku mila hii. Wanapaswa pia kuwa wamefahamu masharti na mipaka iliyowekwa na Uislamu juu ya mitala. Uislamu haujamshushia hadhi mwanamke kwa kuruhusu mfumo huu, bali umewasaidia. Ikiwa mitala haitaruhusiwa, hata pale ambapo idadi ya wanawake wanaostahili kuolewa inazidi ya wanaume, wanawake wanaweza kuwa ni midoli isiyo na thamani mikononi mwa wanaume. Wanaweza kutendewa vibaya zaidi kuliko wasichana watumwa, kwa vile mwanaume anajua kuwa mtoto wa msichana mtumwa ni wake humthamnini, lakini hawaheshimu hawa vimada wake au mahawara.

Mwanaume Wa Sasa Na Mitala.

Mwanaume wa sasa hapendi mitala, sio kwa sababu anataka kuridhika na mke mmoja, bali kwa sababu anataka kuridhisha hamu yake ya kuwa na aina mbali mbali za wanawake kwa kujiingiza katika uzinifu na wanawake wasio na idadi, njia ambayo ni rahisi zaidi na kuna mazingira mazuri zaidi kwa hilo. Dhambi na sio uaminifu, imechukua nafasi ya mitala. Hii ndio sababu mwanaume wa sasa anachukia mitala ambayo humtwisha majukumu mengi ya kifedha na vinginevyo.

Zamani, hata kwa mwasherati, fursa za kufanya hivyo hazikuwa nyingi. Hii ndio sababu aliamua kuoa wake wengi na licha ya kukwepa majukumu mengi bado alilazimika kubeba majukumu fulani kwa ajili ya wake na watoto wake. Mwanaume wa sasa ambaye ana fursa nyingi za kufurahi na wanawake, haoni haja yoyote ya kuwajibika hata kidogo. Na kwa hiyo anakirihika kabisa na mitala.

Mwanaume wa sasa anaajiri wanawake kama makatibu muhtasi, wapiga chapa, nk. kwa ajili ya raha zake, na gharama zake hulipwa na serikali, kampuni yake au mashirika mengine anapofanyia kazi, bila

yeye kuwa na haja ya kulipa hata shilingi kutoka mfukoni mwake.

Mwanaume wa leo anaweza kubadili wanawake kila baada ya siku chache bila kuwa na shida ya kufuata taratibu za mahari, matunzo na talaka. M.Tshombe alikuwa anapinga vikali sana mitala lakini alikuwa na katibu muhtasi wa kike kijana na aliyeumbika vizuri pembeni yake na ambaye alikuwa akimbadilisha (akiajiri mwingine) kila mwaka. Kwa kuwepo fursa hizi ni dhahiri kuwa mwanaume hana haja ya kuoa wake wengi.

Tunasoma katika historia ya Bertrand Russell ambaye alikuwa ni mpinzani mkubwa wa mitala, kuwa wanawake wawili, pembeni kwa bibi yake, walikuwa na mchango mkubwa katika maisha yake. Mmoja alikuwa ni mke wake, Alice, na mwingine alikuwa ni mpenzi wake, Morrel. Morrel ambaye alikuwa mmoja wa wanawake mashuhuri wa wakati ule alikuwa na mahusiano ya kimapenzi na waandishi wengi wa karne ya 20. Ni wazi kuwa mwanaume wa aina hii asingeunga mkono wazo la mitala.

Inavyoonekana ni kuwa ilikuwa ni mapenzi ya nje ya ndoa ya Russel yaliyovunja ndoa yake na Alice. Yeye mwenyewe anaandika kuwa siku moja alasiri akiwa anaendesha baiskeli yake kwenda kwenye migahawa nje ya mji, ghafla alihisi kuwa hampendi Alice tena.

---

1. Wake aliowaoa wakiwa hawana watoto ni Bibi Khadija, Aisha na Hafsa. Japo kwa makosa ya kihistoria inadaiwa kuwa Bibi Khadija alipata kuolewa na waume wengine na akazaa watoto, lakini ukweli ni kuwa Mtume ndio alikuwa mume wa kwanza wa Bibi Khadija na wale watoto wanaodaiwa kuwa Bibi Khadija alizaa na wanaume wengine walikuwa ni watoto wa dada yake aliokuwa anawalea baada ya dada yake kufariki.

Orodha Ya Vitabu Vilivyo Chapishwa Na Alitrah Foundation

1. Qur'an AlKariim Tafsir AlKashif Juzuu ya kwanza mpaka kumi na Nne
2. Uharamisho wa Riba
3. Uharamisho wa uwongo Juzuu ya kwanza
4. Uharamisho wa uwongo Juzuu ya pili
5. Hekaya za Bahlul
6. Muhanga wa Imamu Husein (A.S.)
7. Mikingamo iliyomzunguka Imamu Ali (A.S.)
8. Hijab vazi Bora
9. Ukweli wa Shia Ithnaashari
10. Madhambi Makuu

11. Mbingu imenikirimu
12. Abdallah Ibn Saba
13. Khadijatul Kubra
14. Utumwa
15. Umakini katika Swala
16. Misingi ya Maarifa
17. Kanuni za Ndoa na maadili ya Familia
18. Bilal wa Afrika
19. Abudharr
20. Usahihi wa Historia ya Uislamu na Waislamu
21. Salman Farsi
22. Ammar Yasir
23. Qur'an na Hadithi
24. Elimu ya Nafsi
25. Yajue Madhehebu ya Shia
26. Ukusanyaji na Uhifadhi wa Qur'an Tukufu
27. AlWahda
28. Ponyo kutoka katika Qur'an.
29. Mashukio ya Akhera
30. Nafasi ya Ahlul Bayt
31. Uislamu mfumo wa maisha
32. Mwenyeezi Mungu na sifa zake
33. Adhana
34. Amateka
35. Udhuu kwa mujibu wa kitabu na sunna
36. AlAmali
37. Nyuma yaho naje Kuyoboka
38. Amavu namavuko by ubushiya
39. Dua Kwa Mujibu Wa Ahlulbayt (as)

Back Cover

Mahitaji ya zama zetu hizi yanalazimisha kutathmini maswali mengi yenye umuhimu na sio kuridhika na tathmini zake za awali. Mfumo wa haki za ndoa na majukumu ya kifamilia ni miongoni mwa masuala haya.

Suala la msingi kabisa juu ya haki za kifamilia, ni iwapo mfumo wa ndoa unajitegemea na hautangamani

na mifumo mingine yote ya kijamii na una vigezo na mantiki yake maalum, au ni moja tu ya mifumo mingi ya kijamii na kuwa vigezo na falsafa zile zile ndizo zinazotumika kulishughulikia suala hili kama ilivyo kwa mifumo mingine ya kijamii.

Tatizo la mahusiano ya kifamilia katika zama zetu sio rahisi sana kiasi kwamba mtu anaweza kulitatua kwa kuandaa kura za maoni ya vijana wa kike na wa kiume, au kwa kuendesha semina. Sio tatizo la nchi wala hakuna nchi iliyodai kulitatua kabisa.

Inakubaliwa na kila rafiki na adui kuwa Qur'ani Tukufu ilifufua haki za wanawake. Hata maadui wanakiri angalau kwamba Qur'ani wakati wa kuteremshwa kwake ilichukua hatua kubwa katika kuboresha hali ya mwanamke na kurejesha haki zake za kibinadamu. Qur'ani ilifufua haki za mwanamke kama mwanadamu na kama mwenzi wa mwanaume katika utu na haki za binadamu lakini haikupuuza jinsia yake wala jinsia ya mwanaume.

Kwa maneno mengine Qur'ani haikupuuza maumbile ya mwanamke. Ndio maana kuna kuwafikiana kikamilifu kati ya kanuni za maumbile na kanuni za Qur'ani. Mwanamke katika Qur'ani ni sawa na mwanaume katika maumbile. Vitabu hivi viwili vikubwa vya kimungu (Qur'ani na maumbile), kimoja kikiwa kimeumbwa na kingine kikiwa kimekusanywa, vinakubaliana na kuafikiana kabisa. Nia ya kitabu hiki ni kuangazia na kuelezea kuafikiana huku.

Kimetolewa na kuchapishwa na:
Alitrah Foundation
P.O. Box 19701
Dar es Salaam, Tanzania
Simu:+255 22 2110640
Fax: +255 22 2131036

Source URL: https://www.al-islam.org/node/23282

Links
[1] https://www.al-islam.org/user/login?destination=node/23282%23comment-form
[2] https://www.al-islam.org/user/register?destination=node/23282%23comment-form
[3] https://www.al-islam.org/person/ustadh-shahid-murtadha-mutahhari
[4] https://www.al-islam.org/organization/al-itrah-foundation-0
[5] https://www.al-islam.org/person/aziz-njozi
[6] https://www.al-islam.org/library/women
[7] https://www.al-islam.org/tags/haki
[8] https://www.al-islam.org/tags/wanawake
[9] https://www.al-islam.org/tags/historia

[10] https://www.al-islam.org/tags/kifamilia

[11] https://www.al-islam.org/person/imam-khomein

[12] https://www.al-islam.org/person/bibi-fatima-0

[13] https://www.al-islam.org/person/imam-ali